# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### Kikao cha Kumi – Tarehe 12 Februari, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

### TAARIFA YA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Spika, chini ya Kanuni ya 39(2) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge ya Toleo la Februari, 2023.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo Tarehe 10 Februari, 2024, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, alitangaza kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, ambaye umauti ulimkuta Saa Nane Mchana, akiwa anapatiwa matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Jijini Dar es Salaam.

Katika taarifa hiyo, Makamu wa Rais alieleza kuwa, Hayati Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, ameugua kwa muda mrefu na amekuwa akipatiwa matibabu tangu Tarehe 14 Januari, 2022 katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Jijini Dar es Salaam na

baadaye akapelekwa kwenye matibabu nchini Afrika Kusini na kurejeshwa tena *JKCI*.

Aidha, kutokana na msiba huu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mbali na kutoa pole kwa ndugu jamaa na marafiki, alitangaza siku tano za maombolezo ambazo bendera zitapepea nusu mlingoti kuanzia Tarehe ya Msiba ambayo ni Tarehe 10 Februari, 2024. Katika siku tano hizo za maombolezo, Taifa tutaendelea na shughuli za umma na za kijamii.

Hayati Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, ameitumikia nchi yetu katika nafasi mbalimbali kwa zaidi ya miaka 35. Akianza ushiriki wake katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Chama Cha Mapinduzi, Ubunge, Uwaziri katika Wizara mbalimbali na hatimaye alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Akiwa Mbunge, amewahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuanzia mwaka 2011 – 2013. Baadaye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, mwaka 2013 – 2015.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Taarifa iliyotolewa na Serikali, Mwili wa Hayati Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, unatarajiwa kuagwa siku ya Jumanne tarehe 13 Februari, 2024 katika Viwanja vya Karimjee Jijini Dar es Salaam. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anatarajiwa kuongoza maziko yanayotarajiwa kufanyika Wilayani Monduli, Mkoani Arusha Siku ya Jumamosi tarehe 17 Februari, 2024.

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu natoa pole kwa mjane Mama Regina Lowassa, watoto wa marehemu wakiongozwa na Mheshimiwa Fredrick Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli, ndugu, jamaa na marafiki na Watanzania wote kwa msiba huu. Kwa kauli hiyo, Bunge sasa limeshatoa pole rasmi kwa mfiwa na ndugu wa marehemu Hayati Lowassa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na upendo wetu naomba sasa tusimame kwa dakika moja ili tumkumbuke na

kumuombea kwa Mwenyezi Mungu ampokee na ampumzishe kwa amani. Bwana ametoa, Bwana ametwaa, Jina la Bwana lihimidiwe, Amina. Hii ni taarifa ya Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Spika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kwa ajili ya kumkumbuka Marehemu Hayati Mhe. Edward N. Lowassa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni, Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaenda kwenye maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jonas Mbunda.

Na.156

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Utiri Mbinga Mjini**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Utiri iliyopo Jimbo la Mbinga Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mahitaji ya vituo vya afya katika Kata za kimkakati ikiwemo Kata ya Utiri. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali inakusudia kutenga bajeti kwa kila Jimbo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya. Hivyo, Serikali itaipa kipaumbele Kata ya Utiri katika Jimbo la Mbinga Mjini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwanza, naomba nitoe shukrani kwa Serikali kuhakikisha kwamba, inaweka mikakati ya kutenga fedha kwa ajili ya kujenga ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Utiri. *(Makofi)*

Swali la kwanza, Serikali katika kipindi cha mwaka 2022/2023 ilitenga fedha na kujenga Kituo cha Afya Myangayanga ilitenga shilingi milioni 250. Nataka nijue ni lini sasa Serikali itapeleka kiasi kilichobaki kwa ajili ya kukamilisha kituo hicho cha afya kilichobaki? *(Makofi)*

Swali la pili, Serikali ilitoa shilingi milioni 500 kujenga Kituo cha Afya Mbangamao. Kituo hicho kimejengwa na kimekamilika, naishukuru Serikali kwa jitihada hizo. Nataka nijue sasa, ni lini kituo hicho kitaanza kufanya kazi na kutoa huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jonas William Mbunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipokee pongezi zake kwa Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo imefanyika ujenzi wa vituo vya afya, ikiwemo Kituo hiki cha Afya cha Myangayanga. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tulianza na shilingi milioni 250, katika mwaka wa fedha 2022/2023. Tutapeleka shilingi milioni 250 iliyobaki, ili kuhakikisha kituo hicho kinakamilika. Kwa hiyo, nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, ipo kwenye mpango na fedha inatafutwa, mapema iwezekanavyo fedha hiyo itapelekwa kukamilisha majengo yaliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusiana na kituo cha afya, ambacho Serikali imeshapeleka Milioni 500 na kimekamilika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumeshatoa maelekezo kwa Wakurugenzi na nitumie nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga, kuhakikisha kwamba, anaanza kutoa huduma za awali (huduma za *OPD)* kwenye hiki kituo cha afya wakati tunasubiri vifaatiba kwa ajili ya majengo ya upasuaji, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mahitaji ya muda mrefu sana ya Kituo cha Afya katika Kata ya Mtunda. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Mtunda, kwenye Jimbo la Kibiti? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mpembenwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Kata hii ya Mtunda aliyotaja Mheshimiwa Mbunge ni moja ya Kata za Kimkakati katika Jimbo la Kibiti ina idadi kubwa ya wananchi na tayari tumeshaainisha kwenye Mpango wa Kata za kimkakati kwa ajili ya kutafuta fedha na kujenga Kituo cha Afya. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa Wizara ilishatoa ahadi ya ku-*upgrade* Zahanati ya Solwa kuwa kituo cha afya na humu ndani ukaagiza Mkoa ufanye tathmini na imeshafanyika.

Je, ni lini kituo hicho kitaanza kufanya kazi kama kituo cha afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mnzava, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ambao tumeuweka katika upandishaji wa hadhi ya zahanati kuwa vituo vya afya. Kwanza, tunafanya tathmini ya ukubwa wa eneo, ambayo imeshafanyika. Pili, tunatafuta fedha kwa ajili ya kupandisha

hadhi kwa maana ya kujenga majengo yanayoendana na hadhi ya kituo cha afya. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sababu tathmini imeshafanyika na tayari tumeshapata ripoti hiyo, Serikali inatafuta fedha kupitia mapato ya ndani lakini pia kupitia Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo pia kuanza kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani kwenye asilimia 60 ya miradi ili tuanze kujenga Kituo cha Afya na kupandisha hadhi Zahanati ya Solwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, kwa niaba Mheshimiwa Hokororo.

Na. 157

**Kuanzisha Tarafa mpya Mtwara**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha Tarafa mpya Mtwara kwa kuwa Halmashauri ya Mtwara ilipogawanywa ilijitokeza changamoto ya mipaka ya Tarafa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji Nanyamba ina Tarafa za Nanyamba, Kitaya na Dihimba. Tarafa mbili za Kitaya na Dihimba zinaingiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Mchakato wa kugawa tarafa hizo ulishaanza ambapo Baraza la

Madiwani la tarehe 10 Novemba, 2023 liliidhinisha mapendekezo ya kuanzishwa Tarafa za Njengwa na Namtumbuka. Mapendekezo hayo yanasuburi Vikao vya Kisheria vya Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)* na Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)* na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo, ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadae kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa. Hivyo, maombi ya kuanzisha Tarafa katika Halmashauri ya Mtwara, yatafanyiwa kazi na Serikali itakapoanza kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba huo mchakato utafanyika, lakini nimkumbushe kwamba haya siyo maombi ya kupata maeneo mapya ya kiutawala, kwa sababu kilichofanyika ni mkanganyiko katika ugawaji ndiyo maana kuna Kata zinaingia kwenye halmashauri mbili mpaka sasa.

Je, kwa kuwa Kata za Chawi, Nanyamba na Njengwa ambazo maombi yake yamepitishwa kwenye ngazi zote lakini bado mgawanyo wa kiutawala haujafanyika, ni lini, Serikali itafanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuzingatia mkanganyiko wa mgawanyo wa Halmashauri hiyo mpya, kuna vijiji bado ni vikubwa na maombi yake yameshapitishwa kwenye ngazi zote.

Je, ni lini majibu kutoka TAMISEMI yatapatikana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu

Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hokororo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la msingi ilikuwa ni lini Tarafa mpya itaanzishwa na majibu ya swali la msingi ilikuwa ni baada ya kukamilisha taratibu za *DCC* na *RCC* basi Halmashauri ya Nanyamba iwasilishe Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taratibu zitafuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kata hizi za Chawi, Njengwa na nyingine ambazo umezitaja kwamba, lini mgawanyo utafanyika? Nimhakikishie tu Mheshimiwa Hokororo kwamba, Serikali inatambua mkanganyiko wa mipaka katika Kata hizo na tarafa hizo na nimhakikishie ni dhamira ya Serikali kuhakikisha tunaondoa mkanganyiko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo baada ya kukamilisha uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya utawala yaliyopo, tutahakikisha tunalipa kipaumbele suala hilo na kulitatua mara moja ikiwa ni pamoja na suala lile la pili, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mbulu Vijijini tuliomba Tarafa ya Yaeda Chini; je, ni lini mtatusaidia kutugawanyia ile Tarafa ya Yaeda Chini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba Halmashauri ya Mbulu Vijijini, wana ombi la kuanzisha Tarafa mpya lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara tutakapokuwa tumekamilisha taratibu hizi za ukamilishaji wa miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo,

tutahakikisha tunafanyia kazi ombi la Halmashauri ya Mbulu kwa ajili ya hii Tarafa mpya, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa tunaendelea. *Oh,* Mzee wa "ma - bi" umeingia? Karibu swali la nyongeza, haya uliza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa Jimbo la Makambako lina Kata 12 na Jimbo la Lupembe katika Tarafa ya Makambako lina Kata tano; Tarafa hiyo ina Kata 17 zenye muingiliano; ni lini Serikali sasa itagawa utawala wa Jimbo la Makambako na Lupembe ili kila Jimbo liwe na Tarafa zake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Tarafa ya Makambako ambayo iko ndani ya Jimbo la Makambako pia ipo ndani ya Jimbo la Lupembe kuna muingiliano. Majimbo mawili yana-*share* Tarafa moja na Kata zipo ambazo zipo upande wa Jimbo la Lupembe lakini zipo Kata ambazo zipo upande wa Jimbo la Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Deo Sanga kwamba, tumechukua hoja hiyo tunaifanyia kazi kwa ajili ya urekebishaji wa mipaka ya Kata hizo, ili kata ambazo ziko Makambako zisomeke upande wa Makambako, pia zile ambazo ziko upande wa Lupembe zisomeke katika Tarafa ambazo ziko upande wa Lupembe, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kitabu cha Maombolezo cha Hayati Mheshimiwa Lowassa kipo kwenye

mlango mkuu huu wa kuingilia ukumbini, kwa wale ambao watakuwa na nafasi tunaomba muende mkakipitie kitabu hicho.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais Utumishi, Mheshimiwa Issaay.

Na. 158

**Ujenzi Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Mbulu utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya Serikali, hasa ile ya ujenzi wa miundombinu ya majengo, unategemea mipango ya kibajeti. Katika kutekeleza hitaji la ujenzi wa Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Mbulu, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa jengo hilo katika mwaka ujao wa fedha yaani 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali na ninaomba yawe ya ukweli. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya TAKUKURU katika maeneo mengi hapa nchini inakabiliwa na upungufu wa

watumishi. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kupunguza upungufu huu wa watumishi kwa nchi nzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Wilaya ya Mbulu ina jiografia ngumu na gari la TAKUKURU tulilonalo Wilaya ya Mbulu ni gari lisiloweza kufika kwenye maeneo magumu kama yenye milima. Je, Serikali ina mpango gani wa kutupatia gari linaloweza kustahimili jiografia ya Wilaya ya Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza juu ya shida ya watumishi, katika mwaka huu wa fedha na hapa tulipo taasisi yako ya TAKUKURU imeshatangaza nafasi za ajira 250, ambapo hili ni ongezeko la nafasi nyingine 320 ambazo zilitangazwa mapema Mwezi wa Kumi na Moja mwaka 2023. Hivyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako kwamba Serikali inatambua upungufu wa watumishi uliopo katika Idara yetu hii ya TAKUKURU. Pia, nataka kumhakikishia kwamba Serikali inaendelea kuiwezesha idara hii ili iweze kufikia malengo ya kutoa huduma nzuri kwa wananchi likiwemo lengo kubwa la kupambana na rushwa ambayo inaonekana kuota mizizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili juu ya jambo la gari, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge maana tunaongea mara kwa mara kwamba kilio chake cha magari tumeshakipata, lakini nataka nimwambie kwamba katika mwaka huu wa fedha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya kuiwezesha TAKUKURU ikiwemo katika miundombinu ya majengo na magari. Tutakapokuwa tumepata gari, tutalipeleka Mbulu ili wananchi wetu waende wakapate huduma kama ambavyo malengo ya uanzishwaji wa TAKUKURU yanavyoelezea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua, ajiandae Mheshimiwa Monni.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi ilianzishwa mwaka 2002, takribani miaka 22 sasa, lakini Ofisi ya TAKUKURU wamepanga; je, nini mpango mkakati kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kilindi pia inakuwa na Ofisi ya TAKUKURU? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Issaay, ni kwamba Serikali inaendelea na mikakati ya kuwezesha taasisi yetu hii ya TAKUKURU ili nayo iweze kujenga uwezo siyo tu wa ufanyaji kazi, lakini pia wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unakumbuka, wakati wa Bunge lako hapa tulikuja na maoni ya kuomba kuongezewa bajeti ili tuweze kujenga ofisi katika maeneo mbalimbali ikiwemo mahitaji ya Mikoa tisa ambayo mpaka sasa haina ofisi, pia Wilaya 79 na vituo maalum sita ambavyo tulikuwa tumevitengea bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, furaha yangu, mpaka sasa Serikali imeshaipatia TAKUKURU shilingi bilioni 2.5 ambapo tumeanza katika baadhi ya Wilaya na baadhi ya Mikoa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapokuwa tumepata bajeti yote ya shilingi bilioni 4.5 ambayo tuliitenga katika bajeti ya Bunge hili, basi tutafika Kilindi na kuweka mambo yake vizuri Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; Wilaya ya Chemba kama ilivyo Wilaya ya Mbulu haina jengo la Ofisi ya TAKUKURU.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo hilo katika Wilaya ya Chemba? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza wakati najibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kilindi, ni maelezo yale yale ambayo pia nataka niyapeleke kwa wenzetu wa Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga katika mwaka huu wa bajeti kwamba tutatumia shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya majengo pamoja na ununuzi wa vifaa mbalimbali. Katika ununuzi huo au ujenzi huo, moja ya maeneo ambayo tunayo hapa katika orodha ni pamoja na Wilaya yake ya Chemba ambayo tunatambua kwamba haina jengo linalofaa kwa ajili ya kazi zetu za kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie wewe pamoja na Bunge lako kwamba Wilaya zote 79 ambazo hazina ofisi ni malengo ya Serikali kuhakikisha kwamba tunazijenga, na pia Mikoa yote tisa ambayo haina ofisi nayo pia tutahakikisha tunajenga ofisi hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Tanganyika haina jengo la TAKUKURU, na haina jengo la *DSO,* je, ni lini mtapeleka huduma hiyo kwenye Wilaya ya Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lililoulizwa na Mheshimiwa Kakoso, naweza kulifananisha pia na maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Chemba na Mbunge wa Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulihakikishia Bunge lako kwamba Serikali itakapokuwa imetupatia ofisi yetu shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa majengo yote ya ofisi, ni malengo ya

Serikali kuhakikisha kwamba tunaenda kupambana na rushwa kwa nguvu zaidi hasa ukiwa na ofisi. Nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba unajua unapokuwa umepanga kwa mtu, wakati mwingine uhuru pia wa kufanya hizi kazi nao unapungua, lakini utakapokuwa una jengo lako, ufanisi, usiri wa utekelezaji wa majukumu nao pia unaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nilihakikishie Bunge lako, siyo tu kwa Wabunge hawa watatu waliouliza juu ya uhitaji wa majengo, lakini Bunge zima kwa jumla, kwamba tutakapokuwa tumepata fedha hizi ambazo tuliziomba kwenye bajeti ambayo mpaka sasa hivi kwa kweli, zinakwenda vizuri sana kwa sababu, Serikali imeshatupatia shilingi bilioni 2.5. Tutakapopata shilingi bilioni 4.5 nataka kuwahakikishia Wabunge na Bunge lako Mheshimiwa kwamba kazi ya ujenzi itakwenda kufanyika kwa nguvu kubwa zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Cherehani.

Na. 159

**Kauli juu ya wanaume kutelekeza familia**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wanaume wanaozitelekeza familia zao baada ya mke kujifungua watoto mapacha kuanzia watatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo miongozo ya kisheria ambayo ndiyo msingi wa maelekezo na msimamo wa kiserikali kuhusu wanaume wanaozitelekeza familia zao baada ya mke kujifungua watoto mapacha kuanzia watatu. Kwa kuzingatia Sheria ya Mtoto Sura Na.13, kifungu cha 7, 8 na 9 kinawapa wazazi wajibu wa kumlea mtoto katika mazingira salama na kuwapa mahitaji muhimu. Aidha, kifungu cha 14 cha sheria hiyo kinatoa adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo cha miezi isiyozidi sita au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matakwa hayo ya kisheria, bado wapo baadhi ya wazazi, hususan wanaume ambao hutelekeza wenza wao pale wanapojifungua watoto watatu au zaidi. Hivyo, natoa wito kwa wazazi wanaokabiliwa na changamoto ya kushindwa kuhudumia watoto hao kutoa taarifa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii ili waweze kupata msaada badala ya kutelekeza familia zao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa sheria hizi kweli zipo lakini utekelezaji wake umekuwa ni mgumu na kundi hili la akinamama linakuwa linateseka sana hasa wenza wao wanapowakimbia baada ya kujifungua watoto zaidi ya mmoja; je, Serikali kwa nini isitenge bajeti ya kuweza kulisaidia kundi hili ili kuondokana na kero ya watoto ambao wengi wanakuwa ombaomba mitaani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa nini sasa Serikali inapotoa asilimia kumi ya mikopo ya akinamama, walemavu pamoja na vijana, kuna kundi hili la wanaume wanaozidi miaka 35 linasahaulika? Serikali ina mkakati gani wa kuwafanya akinababa hawa nao waweze kupata mikopo waweze kuendelea kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cherehani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la mwanzo, Serikali imeelekeza Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia Halmashauri, kuweka bajeti ya kuhudumia watoto ambao wana mahitaji maalum wakiwemo waliozidi zaidi ya watatu, lakini pia wenye ulemavu ili kuwapatia huduma hizo pale zinapohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili. Kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Serikali inatoa asilimia kumi ya Halmashauri ya mapato ya ndani. Katika asilimia hizo, asilimia nne inawalenga vijana ambao ni wanawake na wanaume na asilimia mbili ili waweze kujiwezesha kiuchumi pale inapohitajika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Ally Mhata, kwa niaba Mheshimiwa Tunza.

Na. 160

**Hitaji la kiwanda cha kuchakata mazao – Nanyumbu**

**MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani kuhakikisha kiwanda cha kuchakata mazao ya karanga, ufuta na alizeti kinajengwa Kata ya Likokona, Nanyumbu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mahitaji ya viwanda vya kuchakata mazao ya karanga, ufuta na alizeti katika Wilaya ya Nanyumbu, hususan katika Kata ya Likokona, Serikali kupitia *SIDO, TEMDO* na *CARMATEC* inaendelea kubuni mashine za bei nafuu za kuchakata mazao hayo. Aidha, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* inaendelea kutangaza fursa za uanzishaji wa viwanda, vituo vya kuchakata mazao ikiwemo mazao ya karanga, ufuta na alizeti yanayopatikana katika Kata ya Likokona, Nanyumbu, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, wananchi hawa wa maeneo haya wanapata changamoto kubwa ya soko la uhakika, hasa soko la karanga kwa sababu wanazalisha kwa kiasi kikubwa, ndiyo maana kilio chao kikubwa wapate viwanda kwa ajili ya kuchakata.

Naomba jibu la Serikali la dhati kabisa, kuna mkakati gani wa makusudi kuhakikisha kiwanda kinapatikana ili soko la uhakika la karanga lipatikane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, nataka kujua katika mazao ya korosho pamoja na ufuta, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa uwekezaji wa kongani ya viwanda pale Maranje, Nanyamba? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Tunza kwamba moja ya changamoto tuliyonayo sasa baada ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongeza fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo, ni uzalishaji mkubwa katika mazao ya kilimo ikiwemo karanga, ufuta na mazao mengine ambayo sasa yanahitaji soko na soko kubwa ni viwanda ambavyo ndiyo vinavyochakata kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali kama nilivyosema ni kuona kwanza, tunaendelea kuzalisha teknolojia ya mashine nafuu na rahisi, ambayo ni teknolojia rahisi kupitia Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogovidogo *(SIDO)*. Hii itasaidia wananchi wa kawaida kuwa na viwanda hivyo vidogo ambavyo vitaongeza thamani, lakini zaidi tunaendelea kutangaza fursa au uwepo wa mazao haya ambayo ni malighafi kwa viwanda vya kuchakata mazao katika Kata ya Likokona, Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanda vinne, ingawa kimoja hakifanyi kazi, lakini tutahakikisha na hiki kingine ambacho kimesimama kuzalisha kitafufuliwa na kuongeza vingine, lakini zaidi tupate viwanda vikubwa zaidi ambavyo tunadhani vitatibu changamoto ya soko la mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kongani la korosho pale, Serikali tunaendelea kufanya jitihada kuhakikisha tunapata eneo ambalo litawekwa kongani hili la viwanda na Wizara kupitia taasisi mbalimbali kuwavutia wawekezaji kutoka nje ili waweze kujenga viwanda vingi zaidi na kupunguza kuuza nje korosho ghafi, kwa kuwa ndiyo lengo la Serikali kwa mazao yote, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Serikali iliahidi kufanya ukarabati Kiwanda cha Losaa kilichoko pale Masama Magharibi kwa muda mrefu; je, ni lini Serikali itaanza ukarabati wa kiwanda hiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ni kweli ndugu yangu Mheshimiwa Saashisha Mafuwe anafuatilia sana kiwanda hiki cha Losaa ambacho Serikali tuliahidi kwamba tutaweka bajeti katika mwaka huu wa fedha kupitia *SIDO* na tulikubaliana, walishaenda kufanya tathmini pale. Kwa hiyo, mwaka huu tutaweka kwenye bajeti yetu na *SIDO* watakarabati kiwanda hicho ili kiweze kufanya kazi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, kwa niaba yake Mheshimiwa Justin.

Na. 161

**Kuanzisha kiwanda cha kutengeneza pikipiki nchini**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y. MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kuanzisha kiwanda cha kutengeneza pikipiki nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha viwanda vingi vinaanzishwa hapa nchini, ikiwemo viwanda vya kutengeneza pikipiki. Mikakati hiyo ni pamoja na kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji na kujenga miundombinu wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na hasa ikiwemo upatikanaji wa nishati nafuu na ya uhakika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kutokana na matumizi makubwa ya pikipiki ambayo yanafanyika nchini, ni dhahiri upo umuhimu wa kuwa na kiwanda cha pikipiki. Serikali haioni umuhimu wa kuvutia wawekezaji kwa kufanya juhudi maalum ili mwekezaji aweke hapa na kuweza kupunguza bei za pikipiki ili vijana waweze kumudu? Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa ununuzi wa pikipiki ni mkubwa, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia vijana kwa viwanda vinavyozalisha pikipiki, ili zinapoingia nchini ziwe na bei mdogo na vijana waweze kumudu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kweli matumizi ya pikipiki hapa nchini ni makubwa na sote ni mashahidi. Tayari Serikali imeshaanza kuchukua hatua mbalimbali ili kuweka vivutio kwa ajili ya uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kwa taarifa yako na Waheshimiwa Wabunge, tayari kuna unafuu wa kodi kwa wafanyabiashara na baadhi ya watengenezaji ambao wanaleta pikipiki ambazo hazijaunganishwa na kuja kuunganisha hapa nchini, tofauti na yule ambaye analeta pikipiki kutoka nje. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, hii inasaidia vijana wetu kwanza, kupata ajira; pili, kupata ujuzi *(technology transfer)* ili hata badaye tukiwa na viwanda wawe wameshajua tayari kuunganisha pikipiki. Kwa hiyo, wale ambao wanaunganisha pikipiki nchini wanapata unafuu wa kodi na vivutio mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa pili kama nilivyosema, tunaendelea kuvutia kwamba wale watakaoanzisha viwanda vya kutengeneza pikipiki nchini maana yake kodi zote ambazo hawa sasa hivi wanalipia, hazitakuwepo. Kwa hiyo, lengo litakuwa ndiyo hilo kwamba, bei itakuwa ni ndogo na pia ajira zaidi na kodi zaidi kwa nchi yetu, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* tayari wameanza kutengeneza vipuri kwa ajili ya pikipiki na bajaji.

Je, Serikali inaona umuhimu upi katika kupeleka bajeti kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ili waanze kuunda pikipiki kamili nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ni kweli *DIT* ni chuo ambacho ni cha kuendeleza vijana katika teknolojia mbalimbali na si tu wanatengeneza au wanaona vipuri vya pikipiki lakini pia hata na magari ya umeme na vitu vingine. Serikali kupitia Wizara husika wanaendelea kuweka bajeti kwa ajili ya kusaidia wabunifu kwa sababu wale ni vijana ambao wanabuni, halafu teknolojia hiyo itahaulishwa ili kupelekwa kwa wazalishaji wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishafikia hatua hiyo, Wizara ya Viwanda na Biashara tutachukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwasaidia wale wazalishaji wa kibiashara *(Commercialization)* ili waweze kuzalisha kibiashara na kuweza kuwauzia wananchi. Kwa hiyo, tunaendelea kushirikiana kuhakikisha tunawawezesha wale wabunifu, *DIT* na vyuo vingine ili wazalishe teknolojia hizo muhimu, ikiwemo vipuri vya pikipiki na mashine nyingine, nakushukuru sana.

**NAIBIU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Margaret Sitta. *(Makofi)*

Na. 162

**Madai ya malipo ya Wakulima wa Tumbaku Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza: -

Je, Serikali inawasaidiaje Wakulima wa Tumbaku Urambo ambao hawajalipwa fedha kwa muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika misimu ya 2019/2020 na 2020/2021, sekta ya tumbaku ilikumbwa na changamoto kuu mbili zilizosababisha kuzorota kwa soko la tumbaku nchini. Sababu hizo ni kuondoka kwa Kampuni ya *TLTC* na kuzuka kwa ugonjwa wa UVIKO 19. Hali hiyo ilisababisha kampuni za kizawa zikiwemo *Naile Leaf, Jespan, Grand Tobacco, Pachtec* na *ENV Services* kujitokeza kununua tumbaku za wakulima na kushindwa kuuza katika masoko waliyoyatarajia. Hivyo kushindwa kuwalipa wakulima wakiwemo wa Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jitihada zilizofanywa na Serikali, jumla ya shilingi bilioni 324.7, sawa na 98.2% ya deni la shilingi bilioni 330.4 zimelipwa kwa wakulima. Jitihada za kuhakikisha wakulima wote wanalipwa stahiki zao ikiwemo deni la wakulima wa Urambo la shilingi 539,000,000 zinaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, naongea kwa uchungu, wakulima wa Urambo wanategemea zao la tumbaku ili kuendesha maisha yao. Ni kipindi kirefu kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri, wanadai shilingi milioni 539. Naomba watoe tamko hapa kwamba, ni lini watalipa ili wawape matumaini wakulima wa tumbaku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, sasa hivi kuna uhaba mkubwa wa kamba za kufungia majani ya tumbaku ambayo yanajulikana kama *jut twine* na kuwasababishia kero kuwa sana. Hata jana ilitokea kwenye *TBC* wakulima walikuwa wanahojiwa shida hiyo; je, ni lini tutawapelekea kamba za kufungia majani ya tumbaku sasa hivi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kitu cha kwanza nimpongeze Mama Mheshimiwa Sitta kwa kufuatilia kwa karibu kuhusu madeni ya wananchi wake wa Jimbo

la Urambo; la pili ambalo na Mama Mheshimiwa Sitta anatambua, madeni haya yako kwa kampuni ambazo zilinunua tumbaku. Sisi wajibu wetu kama Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku ni kuwafuatailia kuhakikisha deni hili linamalizika na linalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokea maelekezo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Waziri Mkuu mwenyewe kwamba, watu hawa ambao hawajalipa madeni wapelekwe Mahakamani. Wote tumekwishawapeleka Mahakamani. Tunachofuatilia ni kesi ili kumaliza hili deni la wananchi wote ambao hawajalipwa. Kwa sababu mpaka sasa wameshalipa 98.2%, bado 1.8% ikiwemo deni la Wananchi wa Urambo la shilingi milioni 539. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, tutahakikisha kesi inakwenda kwa haraka. Vilevile, tutaendelea kukaa na hizi kampuni ili kuhakikisha hili deni linalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *jute twine*, nimthibitishie tu kwamba, nimezungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku pamoja na Waziri, kwamba jambo hili wanalifuatilia ili kuhakikisha kabla ya msimu wa tumbaku haujaisha na kwa sababu sasa hivi wananchi wako katika kipindi cha mavuno, wanaweza kupata. Jitihada za kati tunazozifanya, tumezungumza na watu wa Bodi ya Pamba kupitia kampuni za uzalishaji nyuzi ili tuweze kutengeneza kamba ambazo zinaweza kutusaidia katika wakati wa sasa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiendelea kuahidi kusaidia wakulima wa *vanilla* Mkoani Kagera, je, Serikali ipo tayari kutoa tamko ni kwa namna gani itasaidia wakulima wa *vanilla* Mkoa wa Kagera kupata soko la uhakika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge anahitaji tamko la Serikali kuhusu soko la uhakika la zao la *vanilla*. Nimwondoe shaka tu, sasa hivi Wizara ya Kilimo tunaendesha mchakato wa kuhakikisha

kwamba tunawasaidia wakulima wote hususan wa zao la *vanilla*, kuanzia kule Kyela ambako kuna changamoto nyingi, pamoja na Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hofu ambayo naweza nikakuondoa tu ni kwamba, tutakapomaliza huu mchakato, maana yake utazingatia maeneo yote, tutaeleza na mkakati wa soko la uhakika jinsi ya kuwasaidia wakulima wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dkt. Ntara.

Na. 163

**Kuhusu *Sayana Press* kama njia ya uzazi wa mpango**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuruhusu *Sayana Press* kama njia ya uzazi wa mpango badala ya kutumia *P2* bila utaratibu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, *Sayana Press* imesajiliwa na *TMDA* na inapatikana kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa wateja wanaohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *P2* ni njia ya dharura ya vidonge vya uzazi wa mpango ambayo hutumika kuzuia mimba kwa mwanamke aliyefanya tendo la kujamiiana bila kinga. Kwa mfano aliyebakwa au aliyetumia kondomu ikapasuka na anadhani anaweza kupata mimba asiyoitarajiwa, wakati *Sayana*

*Press* ni njia ya kuzuia kupata ujauzito kwa muda mrefu. Hivyo, matumizi ya kuzuia mimba kwa *Sayana Press* na *P2* ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa majibu yake. Hili suala sasa hivi linatisha, mabinti wanatumia hizo *P2* kama unavyotumia *panadol*, yaani hakuna utaratibu. Tutafika wakati mabinti hawa hawataweza kupata watoto. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa hao mabinti ili wajue matumizi haya ya *P2*? Tena pamoja na hiyo *Mo Energy* nasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kuna tatizo gani linalosababisha *Sayana Press* zisipatikane kwenye vituo vyote vya afya ili wanawake hasa wa vijijini wawe huru kuzitumia? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kwa kweli swali lake la kwanza halina kipingamizi, ni kama alivyosema kwamba matumizi ya hovyo kwa dawa hii ya *P2* inaleta madhara mengi. Inasababisha masuala ya wakinamama kupata hedhi ambayo haina mpangilio na wakati mwingine hata kupata matatizo ya mifupa, kwa sababu ile *density* ya mifupa inasababisha mifupa inapoteza na ni nyingi. Kwa hiyo, unakuwa na mifupa laini. Kwa hiyo, kwa kweli sisi wote kwa pamoja tushirikiane kuendelea kuhamasisha matumizi mazuri ya *P2* yanayozingatia ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kuna shida gani ya kwamba *Sayana Press* haiko kwenye vituo. Nikwambie tu, kuna *Sayana Press* na kuna *depot*. *Depot* ni dawa za aina moja, zote ni dawa za aina moja lakini tofauti ni moja, moja unachomwa kwenye misuli lakini nyingine unaweza ukajichoma kwenye ngozi. Wakati mwingine hii ambayo unayoisema *Sayana Press*, ukiiruhusu hovyo hovyo ndiyo tunaingia kwenye matatizo sawa na ya *P2*. Ndio maana tumesema, hii ambayo watu wanaweza hata

wakatumia wenyewe kujidunga ina madhara mengi pamoja na kupata maambukizi yasiyotarajiwa, lakini kukutana na madhara makubwa kuliko hata haya ya *P2*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunasisitiza hiyo *depot* ambayo wataenda hospitalini na nesi anamchoma sindano kwa kufuata utaratibu wote ambao utalinda afya ya watu wetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itaanza matibabu kwa watu wenye seli mundu au *sickle cell* kwa kutumia *genetic edit by CRISPR-cas9 Technology? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sijui kwa sababu naona Wabunge wengi wameshtuka alichosema Mheshimiwa Gwajima lakini niseme *CRISPR-cas9 Technology*, ni teknolojia ambayo wanasayansi wamejifunza kwa kuangalia ugomvi wa bakteria na *virus* wakagundua bakteria anajilinda kwa kutengeneza kitu kama mkasi, *virus* akishaingia anajikata anawaondoa wale *virus* ndani ya mwili wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanasayansi wakaja wakasema, je, hii tiba kwa magonjwa yanayotokana na watu kurithi, haiwezekani kutusaidia? Wakaona kwamba ukitumia kwa mfano magonjwa ambayo sasa, mfano kuna magonjwa ya kurithi na mengine, unaweza ukatumia hiyo *CRISPR-cas9 Technology* halafu likaondolewa lile eneo ambalo linasababisha matatizo haya yatokee na ikarudishiwa kitu ambacho kinasaidia hayo matatizo yasiendelee au wakati mwingine ukafanya ku-*fix*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tumeanza kwa maana ya pale Mheshimiwa Waziri wa Afya juzi alikuwa na vyuo vikuu vya Marekani kwa ajili ya kuanza

pale Benjamin Mkapa, lakini sasa hivi tuko kwenye *cancer*, lakini pale *Ocean Road* tumeshanza kwa ku-*treat* baadhi ya *cancer* kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gwajima Serikali iko vizuri. Mheshimiwa Tarimba. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia ametupatia shilingi bilioni 60 kuanza hiyo kazi. *(Makofi)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba matumizi ya *P2* yana madhara kwa kinamama, ni kwa nini basi Serikali inaendelea kuruhusu dawa hii kuendele kutumika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani dawa ya *P2* siyo kwamba, tena hata *amoxcillin* ina madhara isipotumiwa kwa kufuata taratibu. Hata *Paracetamol* ina madhara isipotumiwa kwa kufuata taratibu. Tatizo la *P2* ni pale inapotumika hovyo bila kufuata taratibu na kutumika wakati wote kwa muda mrefu. Kila wakati wewe ukishajihisi unafanya haya mambo bila kufuata utaratibu halafu unameza *P2*. Unafanya bila kufuata utaratibu unameza *P2*, hayo ndiyo yanayotuletea shida. Tunataka watu waanze kufuata taratibu ambazo zinatakiwa. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Suma Fyandomo. *(Makofi)*

Na. 164

**Ahadi ya kupeleka umeme wa *REA* Mbeya**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza: -

Je, ni lini ahadi ya kupeleka umeme wa *REA* kwenye Wilaya za Mkoa wa Mbeya itakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kampuni ya *ETDCO* ambayo ni Kampuni Tanzu ya *TANESCO*, inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Mbeya ambapo hadi kufikia Februari 2024, jumla ya vijiji 109 kati ya vijiji 139 vilivyopo katika mradi vimefikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kufikisha umeme katika vijiji 30 vilivyobaki inaendelea na mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2024. Aidha, Serikali kupitia *REA* imetenga fedha shilingi bilioni 377.05 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya kupeleka umeme katika vitongoji 15 vya kila jimbo nchini, vikiwemo vitongoji vya Majimbo ya Mkoa wa Mbeya. Maandalizi ya kutekeleza mradi huu yanaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Wilaya ya Chunya, Rungwe, Mbarali, Mbeya Jiji na *Mbeya DC*, baadhi ya vijiji havijafikiwa na umeme. Sasa je, ni nini mkakati wa Serikali wa kukamilisha mradi huo ili hali ahadi yake ilikuwa ukamilike mwaka 2023? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika

majibu yangu ya msingi, kwa Mkoa wa Mbeya tulikuwa na vijiji 139 na mpaka sasa tumepeleka umeme kwenye vijiji 109, vimebaki vijiji 30. Serikali inakusudia kuhakikisha ikifika mwezi Juni mwaka huu, vijiji hivyo vyote viwe vimepatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani kwa sababu kazi kubwa ya kupeleka umeme vijijini imefanyika. Kama mnavyofahamu, nchi nzima tuna vijiji 12,318 hivi na mpaka sasa tumekwishapeleka umeme kwenye vijiji vyetu takribani 11,720. Hii ikiwa ni sawa na 95%. Naomba Waheshimiwa Wabunge wawe na imani na Serikali. Tutakamilisha upelekaji wa umeme vijijini kwa wakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Mji wa Kasulu lipo tatizo la umeme kukatikakatika mara kwa mara. Zipo nyumba ambazo umeme haukatiki na nyumba nyingine umeme unakatika, inapofika saa tano usiku, umeme unakatika unarudi asubuhi; je, ni lini Serikali itamaliza tatizo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Genzabuke swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea *concern* yake na mimi nitumie jukwaa hili kumwagiza Meneja wetu wa Mkoa wa Kigoma kushughulikia tatizo hilo haraka sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati. *(Makofi)*

Na. 165

**Malipo kwa wazabuni wenye madai**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza: -

Je, Serikali imeshalipa wazabuni wangapi wanaodai katika taasisi mbalimbali nchini na kiasi gani kimeshalipwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, madeni ya wazabuni yaliyohakikiwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na kukidhi vigezo ni shilingi trilioni 1.41. Kati ya kiasi hicho, Serikali imelipa jumla ya shilingi trilioni 1.03 sawa na 73%. Idadi ya wazabuni waliolipwa ni 8,830 ambao walikuwa wakidai taasisi mbalimbali za Serikali. Ulipaji huo ni hatua ya Serikali katika kuchochea uchumi na kukuza sekta binafsi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nawapongeza Serikali kwa kuweza kuwalipa wazabuni kiasi hicho cha fedha lakini kwa kuwa sasa wapo wazabuni waliokuwa wamehakikiwa muda mrefu sana na hawajalipwa; je, Serikali ipo tayari sasa kutoa orodha kamili ya wazabuni waliohakikiwa na ambao hawajalipwa kupitia Mfumo wa TEHAMA ili wasiendelee kusumbuka kwenda Hazina kufuatilia hayo malipo kila siku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna wazabuni wanaoidai Serikali, wapo wengine ambao walikuwa wamekopa benki na benki zinaendelea kuwatoza riba na *TRA* pia wanaendelea kutoza kodi; je, Serikali sasa ipo tayari kuwasaidia wazabuni hao wasiendelee kupewa hiyo adhabu, kwa sababu

wengine sasa hivi wamefilisika na wengine hawakopesheki? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kabla ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kabati, naomba nimpongeze sana kwa ufuatiliaji wa karibu katika masuala haya. Serikali ipo tayari lakini suala hili ni la kimkataba ambalo lazima tuzingatie sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali ipo tayari na imesikia na imechukua na naomba baada ya kipindi hiki cha mchana huu wa Bunge tukutane na Mheshimiwa Mbunge, tuone namna gani tutawasaidia wazabuni hao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida iliyopo Iringa ndiyo changamoto iliyopo Sumbawanga Mjini, wazabuni wengi hawajalipwa wanadai wengine wana miaka saba, wengine miaka mitano, wengine miaka sita, sasa wanakuja huku wanazungushwa, wanarudi Sumbawanga wanazungushwa na orodha ninayo, naomba kama utaniruhusu niikabidhi orodha hii ya wazabuni waliyodai muda mrefu. *(Makofi)*

Je, ni lini Serikali itawalipa wazabuni hawa ili kuondokana na changamoto za kudaiwa kwenye benki, wengine wanauziwa nyumba. Naomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza dogo kama lilivyoulizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba wapo baadhi ya wazabuni hawajalipwa fedha yao, lakini nikuhakikishie kadri ya upatikanaji wa fedha zitakapopatikana wazabuni hawa watalipwa fedha zao, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Habari, Mheshimiwa Magessa.

Na. 166

**Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano Kata za Busanda**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, lini minara ya mawasiliano itajengwa katika Kijiji cha Msasa, Kata ya Busanda na Kijiji cha Nyakagomba, Kata ya Nyakagomba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imeingia mkataba na mtoa huduma Kampuni ya Honora *(Tigo)* ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika Kijiji cha Msasa Kata ya Busanda na Kijiji cha Nyakagomba, Kata ya Nyakagomba kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidigitali. Ujenzi wa Minara kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali utakamilika Mei, 2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwa vijiji hivyo viwili nilivyovitaja Msasa na Nyakagomba, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile, yapo maeneo kadhaa Jimboni Busanda ambayo yana mawasiliano hafifu na sehemu zingine hakuna mawasiliano kabisa. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu uboreshaji wa mawasiliano kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha huduma ya mawasiliano nchini na maeneo ambayo yanabainika kuwa hayana kabisa huduma ya mawasiliano tunawatuma wataalam wetu ili kuchukua hatua ya kuhakikisha kwamba tunajenga minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo tunagundua kuna tatizo la mawasiliano kuwa hafifu tunaelekeza *TCRA* kuhakikisha kwamba wanafika katika maeneo hayo kuangalia *quality of service* na ili tuangalie namna gani tunaweza tukatatua changamoto hiyo kulingana na tatizo litakapobainika. Ahsante. *(Makofi)*

**MAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, unakumbuka katika ile minara 750 ulituahidi kwenda kutuboreshea katika Kata Tano za Wilaya ya Nyang'hwale kuweza kutujengea minara hiyo ya mawasiliano ili kupunguza kero ya mawasiliano iliyopo ikiwa ni kwenye Kata ya Nyamtukuza, Bukwimba, Nyijundu, Nyabulanda na Shabaka.

Je, ni lini sasa ujenzi huo wa minara utaenda kuanza na kukamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Serikali iliahidi kwenda kujenga minara katika Jimbo la Nyang'hwale lakini nikiri kabisa kwamba Kata hizi tano ambazo amezitaja hazikuwepo kwenye orodha ya minara 758 lakini baada ya kuwasilisha na Serikali ikatafuta fedha zikapatikana, sasa tunaenda kujenga minara 636 na hivyo basi Kata hizo tano za Jimbo la Nyang'hwale tunaenda kuziingiza kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo hilo wapate huduma ya mawasiliano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Florent.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Niipongeze Serikali kwa Wilaya ya Missenyi imejenga minara zaidi ya minne lakini bado katika Kata za Mutukula, Kassambya, Nsunga, Kitobo, Bugandika na Buyango bado mawasiliano ni duni.

Je, ni lini sasa minara hiyo itakamilika katika Kata hizo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Missenyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, Kata ya Mutukula, bahati nzuri nilifanya ziara pale nikiwa na Mheshimiwa Mbunge, tulitembelea maeneo yote ambayo yana changamoto na ndipo Serikali ilianzisha Mradi wa *Special Zone and Borders* ambapo sasa kuna minara ambayo ipo katika hatua ya utekelezaji. Itakapokamilika naamini kabisa

changamoto katika mpaka wa Mutukula utakuwa umeisha, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kumekuwepo na changamoto ya mawasiliano kwa Kata na Vijiji vyote vya Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Rorya ambavyo vinapakana na nchi jirani ya Kenya, kwa wananchi wale simu zao kukamata *network* ya *Safaricom* na hivyo kusababisha kutokuwepo na mawasiliano kabisa.

Je, ni lini Serikali itahakikisha inapeleka minara kwa dharura ili wananchi hawa waweze kupata haki yao ya kuwasiliana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya mawasiliano katika mipaka, upande wa Rorya kwa Mheshimiwa Chege na upande wa Tarime ni kweli nilishafika maeneo hayo yana changamoto kubwa. Kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amelileta tena na Bunge hili ndilo ambalo linapitisha bajeti, nimuombe Mheshimiwa Mbunge wakati tutakapoomba bajeti ya dharura basi awe tayari kuunga mkono kwa sababu hatuna sehemu nyingine ya kutoa fedha zaidi ya kupitisha katika Bunge lako hili Tukufu, lakini Serikali ipo makini kuhakikisha kwamba maeneo yote yenye changamoto inaenda kuyafanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Zeeland.

Na. 167

**Usambazaji wa maji Tarafa ya Turiani**

**MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha mradi wa kusambaza maji katika Tarafa ya Turiani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji katika Tarafa ya Turiani toka mwezi Desemba, 2022 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.905. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji Kijiji cha Luamba lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita 150,000, ujenzi wa madakio matatu ya maji katika Vijiji vya Ubiri, Mlaguzi na Luamba, ujenzi wa mtambo wa kutibu maji *(treatment plant)*, ujenzi wa vituo 15 vya kuchotea maji pamoja na uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 45 ambapo kwa mujibu wa mkataba unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2024. Kukamilika kwa mradi huo kunatarajia kunufaisha wananchi wapatao 40,786 waishio kwenye Mji wa Turiani pamoja na Vijiji Tisa vya Kigugu, Mlaguzi, Mbogo, Lukenge, Mlumbilo, Luamba, Ubiri, Kwelikweji na Mafuta. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Kata ya Mziha ni miongoni mwa Kata ambazo zina changamoto kubwa sana ya maji, tarehe 30 Machi, 2023 mlisaini mkataba na mkandarasi kwa ajili ya kusambaza maji kwenye vijiji vinne: Kijiji cha Njeula, Bwage, Kibatula na Mziha lakini mpaka sasa ni zaidi ya miezi 10 kazi haijaanza kwa sababu hamjamlipa mlichokubaliana - *advance payment*. Je, ni lini mtamlipa ili kazi hii iweze kuanza? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa baadhi ya miradi ni kichefuchefu katika Wilaya yetu ya Mvomero, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari kuongozana na mimi baada ya Bunge hili kwenda kuikagua hii miradi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake kuhusu ni lini tutamlipa Mkandarasi, tumshukuru Mheshimiwa Rais, kuanzia mwezi Julai mpaka Desemba tumeweza kupatiwa shilingi bilioni 23 ambazo tunaendelea kupunguza madeni ya wakandarasi mbalimbali nchini pamoja na mkandarasi huyu ambaye anafanya kazi Eneo la Turiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi kichefuchefu kuongozana na Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo tulishakubaliana lakini nitumie Bunge lako Tukufu nipo tayari baada ya Bunge hili tutapanga ratiba nzuri kwenda kufanya ziara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi kubwa za Serikali za kuweka matenki katika Kata ya Msigani, Halmashauri ya Ubungo lakini kuna changamoto kubwa ya usambazaji wa maji hayo, bado hayajawafikia wananchi katika maeneo mbalimbali.

Je, Serikali ni lini itasambaza maji katika Kata ya Msigani, Wilaya ya Ubungo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Ubungo wasambazaji maji katika Kata aliyoitaja Mheshimiwa Kisangi, tayari jitihada kubwa sana inafanyika na uongozi wa *DAWASA*. *CEO* Kikula anafanya kazi nzuri pamoja na timu yake niwatoe hofu, wakazi wa eneo hili katika Halmashauri ya Ubungo na wenyewe haraka mapema iwezekanavyo watahakikisha wanafikishiwa huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na Ilala na maeneo mengi sana mjini kuna shida maji, kwa hiyo jitihada najua zinafanyika lakini muendelee kweli wananchi ili wapate maji safi na salama. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, ni lini kazi ya kusambaza maji yanayotokana na mradi mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 520 utakamilika katika Mkoa wa Arusha, hususan kwenye Wilaya ambazo mradi huu unapita, Wilaya ya Arusha Mjini na Wilaya ya Arumeru? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kusambaza maji kutokana na mradi mkubwa wa shilingi bilioni 500 pale Arusha; kwa asilimia kubwa mradi huu ni umekamilika na tayari wananchi wananufaika, maeneo machache ambayo mtandao bado

haujawafikia. Kwa sababu Mheshimiwa Zaytun umekuwa ukifuatilia suala hili, nikuhakikishie tupo katika mkakati maalum kuhakikisha kila kona ambayo inatakiwa kupatiwa maji kutoka mradi huu inapatiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali mna mkakati gani wa kutengeneza mabomba ambayo ni ya zamani sana na kuna upotevu mkubwa wa maji hasa Jijini Dar es Salaam pamoja na Jimbo la Temeke.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutengeneza mabomba hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy Kilave, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa miundombinu chakavu tayari *DAWASA* wameanza baadhi ya maeneo. Katika eneo lako la Temeke Mheshimiwa Mbunge unafahamu kuna ule mradi mkubwa ambao tunaleta maji kule, kwa hiyo tayari pia mabomba yale chakavu tutayaondosha kwa sababu maji yanayokuja sasa kutokana na mradi ule ambao upo kwenye utekelezaji wake, kwa sasa maji yatakuwa ni mengi. Kwa hiyo utekelezaji wa ukarabati eneo lote la Temeke unafuata. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naomba niulize swali moja.

Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya maji kwenye Kata ya Mwika Kusini na Mwika Kaskazini ambayo inaendelea kwa zaidi ya miaka mitatu sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kimei, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ambayo ilianza ni lazima ikamilike, ninakuomba Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili tukutane ili tuweze kuona ratiba nzuri ya kwenda ziara ambayo itakuwa ni chachu ya miradi hii kukamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa mkutane wapi?

Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Pallangyo. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 168

**Serikali kujenga upya Uwanja wa Mpira Chuo cha Patandi**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga upya uwanja wa mpira katika Chuo cha Ualimu Patandi, kufuatia kujengwa mabweni ya shule kwenye uwanja uliokuwepo?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikamilisha ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Maalum ya Patandi mwaka 2021 ambapo baadhi ya miundombinu ya majengo ilijengwa katika eneo lililokuwa na uwanja wa mpira wa miguu wa chuo. Lengo la ujenzi wa shule hiyo ilikuwa ni kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu bora kwa wanafunzi wote hasa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imeanza hatua za awali za ujenzi wa uwanja wa mpira katika Chuo cha Ualimu Patandi yanayohusisha maandalizi ya tathmini ya gharama za

ujenzi wa uwanja kwa kushirikiana na Wahandisi wa Manispaa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii tena ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ni sehemu ya elimu ambayo inatolewa kwa kuanzia elimu ya awali hadi chuoni mpaka maishani pia ni ajira lakini pia ni burudani muhimu sana kwa afya zetu. Mimi naishi karibu sana na hicho chuo na wananihusisha sana kwenye masuala yao kila tukio linavyokuwa pale wananiita. Mwaka jana nilikuwa mgeni rasmi ndiyo nikapata hii changamoto, nilikuwa jimboni sijasikia chochote kuhusu maandalizi ya ujenzi wa huu uwanja.

Je, Mheshimiwa Waziri, unaniambia kwamba huu uwanja utaanza kujengwa lini?

Pili, je, upo tayari tuambatane tukitoka hapa tupitie pale chuoni tuweze kuzungumza na walimu na wanafunzi kwa ajili ya suala hili maana ni muhimu sana? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli michezo ni jambo muhimu sana kwa shule na tunajua siyo kwamba tu inawasaidia vijana wetu kwa maendeleo yao katika *dimension* zote lakini wakati mwingine inavutia wanafunzi kukaa shuleni kwa sababu ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Serikali inaelewa baada ya ujenzi na upanuzi wa Chuo cha Patandi kwamba tuna haja ya kuhakikisha kwamba sasa hivi wanafunzi

wale wanaweza wakafanya michezo na kama nilivyosema tayari hatua za awali zimeweza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafurahi sana kuongozana na Mheshimiwa Pallangyo, kwenda kutembelea shule hii kwa sababu kwa kweli nilimtuma Naibu Waziri kuweka jiwe la msingi lakini makusudio yangu ni kwenda kupaangalia pale vilevile kuangalia maendeleo ya shule hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Dkt. Mathayo.

Na. 169

**Kupitia Sheria na Kanuni za Madhara yanayosababishwa na Wanyamapori**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Fidia kwa waathirika wa wanyamapori ili kulipa fidia ya gharama halisi tofauti na sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikilipa kifuta jasho na kifuta machozi kama mkono wa pole au faraja kwa wananchi wanaopata madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu. Malipo hayo yamekuwa yakifanyika kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho au Kifuta Machozi za mwaka 2011 na kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha mapitio ya Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi na kuiwasilisha Wizara ya

Fedha kupitia barua yenye Kumb. Na. BA/267/297/01/14 ya tarehe 16 Julai, mwaka 2023 ili kuona uwezekano wa kuongeza viwango hivyo. Kwa sasa Wizara ya Fedha inafanya tathmini ili kuona athari za kiuchumi na uwezo wa nchi kutekeleza suala hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mathayo.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa Serikali kuchelewa kubadilisha Kanuni hizi kunawatia wananchi umaskini kwa sababu *rate* zilizopo za laki moja wa ekari siyo halisia, siyo hali ya soko na inaathiri uchumi wao na hawawezi tena hata kulima tena msimu unaofuata. *(Makofi)*

Je, Serikali itakamilisha kuzibadilisha Kanuni hizi lini?

Swali la pili, sasa hivi hata kwa kutumia Kanuni tulizo nazo sasa hivi Serikali inachelewa sana kuwalipa fidia wananchi wanaopata athari hizi za Wanyamapori.

Je, ni kitu gani hasa kinasababisha kuchelewa kulipa fidia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na ucheleweshaji wa kumalisha utoaji wa malipo jambo ambalo kwa wakati mwingine ni kweli linaweza kusababisha athari kwa wananchi. Kama tunavyofahamu, ili uweze kuwa na uhakika wa kulipa, ni lazima tathmini ya kina ifanyike. Tathmini hii inachukua muda ili kujiridhisha. Watathmini wetu wanaporudi uwandani huandaa taarifa na hatimaye Wizara iwasiliane na Wizara ya Fedha ili fedha ziweze kutoka. Tunaahidi kwamba tutajitahidi kwa

kadri inavyowezekana kuhakikisha mchakato huu unachukua muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake ya pili, kama nilivyosema ni kwamba mchakato wa kufanya tathmini ndani ya Wizara umekamilika. Kwa takribani maombi tuliyokuwa tumepata tathmini inaonesha tunahitajika kulipa zaidi ya shilingi bilioni 1.6. Hizi tayari zimekamilika na tumewasilisha Wizara ya Fedha. Hata juzi wakati tunapokea Taarifa ya Kamati ya Maliasili, jambo hili lilizungumziwa. Tunalichukua kwa umuhimu mkubwa na kwa uzito mkubwa kuhakikisha kwamba ndani ya Wizara, wenzetu wa Wizara ya Fedha nao wakamilishe sehemu yao ili tuweze kuwalipa wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mtaturu kwa niaba Mheshimiwa Aysharose.

Na. 170

**Kujenga majosho Jimbo la Singida Mashariki**

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE K.n.y. MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga majosho kwenye vijiji vya Jimbo la Singida Mashariki ili kulinda afya za mifugo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa majosho nchini ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe na wadudu wengine. Katika mwaka wa fedha 2023/2024

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo imetenga jumla ya shilingi bilioni 5.7 kwa ajili ya ujenzi wa majosho 246 katika Halmashauri 63 nchini.

Mheshimiwa Naibu Sipika, katika Jimbo la Singida Mashariki mwaka 2022/2023 Serikali ilijenga majosho manne ambayo ujenzi wake ulikamilika na yanafanya kazi. Pia, katika mwaka 2023/2024, majosho manne yanajengwa katika vijiji vya Ndughamunga, Unyampanda, Ughandi na Ngamu vilivyopo katika Kata za Mughunga, Ughandi na Mwasauya.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote zilizotengewa fedha za ujenzi wa majosho kuwasilisha nyaraka za maombi ya fedha hizo Wizara ya Fedha mapema kama walivyoelekezwa ili waweze kupatiwa fedha hizi za ujenzi wa majosho, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali katika mwaka huu wa fedha iliahidi kujenga majosho katika Vijiji vya Siuyu, Ulyampiti, Isuna na Misule, lakini hadi sasa majosho haya hayajajengwa na hata *tender* haijatangazwa, je, ni lini Serikali itajenga majosho hayo katika vijiji hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Wananchi wa Mkoa wa Singida ni wafugaji wazuri wa mifugo ya aina mbalimbali lakini hawana elimu ya kutosha ya kufuga mifugo hiyo: Je, nini mkakati wa Serikali wa kutoa elimu bora ya ufugaji ili kuongeza mazao ya ufugaji kwa wananchi hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza na hili la kwanza kwamba ni lini majosho hayo yatajengwa? Wizara imeshatoa maelekezo kwa Wakurugenzi

wote nchini ambao walitengewa bajeti ya ujenzi wa majosho, kwamba fedha zipo tayari, sasa wanapaswa kuomba Wizara ya Fedha ili waweze kupatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa majosho haya. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wanapokuwa kwenye vikao vyao vya Kamati ya Fedha na Mipango kule Halmashauri, wawe wakali kuwasukuma Wakurugenzi kuomba hizi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake Wakurugenzi wengine ni wavivu, wanashindwa kuziomba fedha hizi na fedha zipo tayari. Tumeshasema sana jambo hili kwamba fedha zipo tayari Wizara ya Fedha, Wakurugenzi waombe na Wakurungenzi walio *sharp* wameshaomba na wameshapewa fedha na majosho yamejengwa. Wale Wakurugenzi wavivu hawataki kuomba hizi fedha kwa sababu wanakuwa na mrundikano wa fedha nyingi kule Halmashauri, wanashindwa kutimiza maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusu elimu ya ufugaji, Wizara imeshaanza kutoa elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji ulio bora, kwamba sasa tunaachana na ufugaji wa kizamani wa kufuga ng'ombe wengi wasiokuwa na tija. Sasa tunatoa elimu ya ufugaji wa kisasa na tayari elimu hii imeshaanza kutolewa katika mikoa mbalimbali na wafugaji wamekuwa wakipokea elimu hii kwa namna hiyo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kulingana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Wilaya ya Nkasi, tulishaomba toka mwaka 2022, lakini mpaka sasa hatujapata fedha kwa ajili ya majosho. Ni lini mtatupa hizo fedha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wilaya ya Nkasi wameshaomba, baada ya kikao hiki naomba tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge tufuatilie fedha hizo zimekwama wapi kwa sababu taarifa zilizopo ni kwamba fedha

za ujenzi wa majosho kwa mwaka wa fedha huu ambao Halmashauri zote walishaomba, fedha zipo tayari. Kwa hiyo, nawaomba sana Wakurugenzi ambao walitengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa majosho waendelee kuomba Wizara ya Fedha na watapatiwa fedha hizo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Ndulane.

Na. 171

**Kukomesha migogoro ya wakulima na wafugaji - Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kukomesha migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji Wilayani Kilwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na migogoro inayohusisha wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Kilwa yenye jumla ya vijiji 90. Migogoro hii imekuwa katika maeneo ya vijiji yasiyokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, imeshaandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji 56 kati ya vijiji 90. Hivyo, Wizara kupitia Mradi wa *LTIP* inatekeleza mipango ya matumizi bora katika vijiji 34 vilivyobaki

vikiwemo vile vyenye migogoro mikubwa ya wafugaji na wakulima vya Naking'ombe na Zingakibaoni vilivyopo katika Kata ya Miguruwe pamoja na Kijiji cha Nainokwe kilichopo Kata ya Likawage. Mradi huo utakamilika ifikapo Juni, 2024. Aidha, kwa sasa watumishi wa Wizara wapo uwandani katika Kata ya Miguruwe na Likawage wakiendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali kupitia Wizara ya Ardhi ikiendelea kutekeleza uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, maana tunaamini itakuwa ndiyo mwarobaini wa migogoro hiyo katika Wilaya ya Kilwa na maeneo mengine hapa nchini ambapo miradi hii inatekelezwa. Natoa rai kwa wananchi kuendelea kuheshimu mipango itakayoandaliwa ili kuthibiti migogoro hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba nikiri kwamba kwa mara ya kwanza swali langu l imejibiwa kwa utoshelevu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Kilwa ina miji mingi inayokua kwa kasi sana; na moja kati ya maeneo ambayo vijiji vinakua kwa kasi sana na kuwa na sura ya kimiji ni pamoja na Kijiji cha Somanga Kusini, pamoja na Kijiji cha Njianne, kuna mgogoro mkubwa sana pale wa mpaka.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuleta *component* ya urasimishaji ili kutatua changamoto za namna hii katika Wilaya ya Kilwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza, je, kupitia mradi ambao ameueleza Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali ina mkakati gani wa kutoa hati za kimila kwenye mradi huo ili kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika na hati hizo kiuchumi katika Wilaya ya Kilwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nianze na swali lake la kwanza la kurasimisha miji inayokua kwa kasi hapa nchini, naomba tu kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tumechukua hili eneo la miji ambayo inakua katika eneo lake, wataalam wataenda kupitia na kuona namna ya kuanza zoezi la urasimishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu hati za kimila, ni sehemu ya *package* ya zoezi zima la maandalizi ya matumizi bora ya ardhi. Tunapokamilisha ile kazi, kimsingi wanavijiji wale wanatakiwa kupewa hati. Kwa hiyo, hili tunalichukua na kulitolea maagizo kwa Tume kuhakikisha kwamba kila watakapokamilisha upimaji kwenye kijiji, wahakikishe wale wananchi wanapata hati kwa sababu lengo la msingi la upimaji ule ni kuwasaidia wanavijiji vilevile kutumia zile hati zao kwanza kuboresha maisha yao kama kuchukua mikopo benki na dhamana mbalimbali ambazo zingehitaji ushahidi wa uhakika wakati wanapofikiwa wa masuala haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kumekuwa na ahadi ya Serikali hapa ya kutatua changamoto ya urasimishaji ndani ya Jimbo la Kibamba kwa kupata Fedha ya Mfuko wa Dunia shilingi bilioni 345 na shughuli hiyo ingeanza mwezi Agosti, 2024, lakini mpaka sasa wananchi wanashagaa hakuna kinachoendelea; je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya ahadi ile? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi labda ninachoweza kusema ni kwamba baada ya Bunge hili tutakutana na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kumpa mipangilio ya jinsi utekelezaji unavyokwenda kuanza mara moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo ina migogoro mingi na mikubwa ya ardhi; je, ni lini Kliniki ya Ardhi itafika Tabora ili kuweza kutatua changamoto na migogoro iliyopo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hawa, Tabora tayari tulishaanza na kliniki ndogo ndogo zilizokuwa chini ya Makamishna. Kwa sasa kwa sababu mwelekeo wako ni kuomba kliniki ambayo Mawaziri na Makatibu Wakuu tutapita pale, nikuahidi tu, baada ya Bunge letu hili utaona kinachokwenda kuwaka pale Tabora. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 12 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji, Kikundi cha *Sisterhood* kutoka Jijini Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa *Engineer* Andrea Mathew Kundo, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Bariadi, Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga, Katibu Mkuu wa *Diaspora* wanaoishi China na mfanyabiashara mwekezaji mzawa wa vifaa vya umeme majumbani kupitia Kampuni ya *KODTEC*. *(Makofi)*

Wapo pia wageni kumi wa Mheshimiwa Tarimba Abbas ambao ni wapigakura wake kutoka Kinondoni, Jijiji Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate ambaye ni rafiki yake kutoka Kyerwa, Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 140 wa Mheshimiwa Husna Sekiboko, Wajumbe wa UWT kutoka Wilaya ya Kilindi, Jijini Tanga. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Profesa Shukrani Manya, Ndugu Esther Shaduo kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman, wapiga kura wake kutoka Zanzibar, karibuni. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava, ambaye ni rafiki yake, Ndugu Richard Laizer, kutoka Jijini Arusha. Yupo mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara, ambaye ni Mpigakura wake kutoka Tarime Mkoa wa Mara. Karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambao ni viongozi wa CCM kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Adam Ngayawa, Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam na Ndugu Bananga, Katibu Mwenezi, Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hawa, mbona mikono imekuwa inapigwa sana leo? *(Makofi/Kicheko)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 45 wa *Bachelor of Science in Mathematics and Statistics* kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. Mjitahidi ninyi ndio Taifa linawategemea sasa. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 70 wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati pamoja na Ndani ya Uhandisi, kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Nestory Enyasi, Afisa Muuguzi na Mwandishi wa Vitabu vinavyotoa elimu ya kupambana na magonjwa yasiyoambukizwa kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili akiambatana na Ndugu Emmanuel Bazili, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam watakuwa na kikao kitakachofanyika kwenye chumba namba 9 Jengo la Utawala mara baada ya kipindi cha maswali na majibu.

Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam wa CCM; Wabunge wote wa Dar es Salaam ni wa CCM. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Najma aje kuendelea na ratiba.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI.**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023**
**na**
**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ili aweze kuja kuleta taarifa yake na hoja za Kamati, karibu Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Madhumuni yake ni kubainisha masuala

mbalimbali yanayojitokeza kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024 wakati wa shughuli za Kamati. Masuala hayo yalihusu sekta ya afya na masuala mtambuka ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa imegawanyika katika sehemu tatu kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Bunge; sehemu ya kwanza inahusu utangulizi, ikiwemo maelezo kuhusu muundo na madhumuni ya taarifa. Aidha, sehemu hii inafafanua msingi wa shughuli za Kamati na njia au mbinu zilizotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inatoa maelezo kuhusu shughuli zilizotekelezwa na lengo la shughuli hizo. Ufafanuzi huo, unahusu shughuli ya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Afya na ile ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Shughuli nyingine ni uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na uchambuzi wa Hoja ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sehemu hii inabainisha mambo yaliyotokana na shughuli za Kamati zilizolenga kusimamia na kufuatilia Wizara ya Afya na Taasisi zake. Sehemu hii pia inaonesha mambo yaliyobainika kuhusu masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu na ya mwisho ya Taarifa hii inatoa maoni ya jumla na mapendekezo. Kwa ujumla Sehemu hii, inaonesha kuwa kutokana na kushughulikiwa kwa masuala yaliobainishwa, kunaweza kuathiri ustawi wa wananchi kutokana na shughuli za umma katika Sekta ya Afya kuwa na tija ndogo. Aidha, sehemu hii inapendekeza mambo mbalimbali ya utatuzi wa changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi na mambo yaliyobainika; maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa mwaka 2022 yaliwasilishwa Bungeni tarehe 01 Novemba, 2023 wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5)(b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa tarehe 01 Novemba, 2023 Mheshimiwa Spika alitoa maelekezo Bungeni kwa

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kufanyia kazi maeneo mawili ya Muswada huo. Eneo la kwanza lilihusu Ibara ya 22(a) katika Jedwali la Marekebisho la Serikali kuhusu kuwagharamia watu wasio na uwezo. Jambo kuu ni kuona iwapo viwango katika vyanzo vya fedha za mfuko zinahitaji kufafanuliwa na Sheria au laa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili lilihusu huduma ambazo zitatolewa katika Kitita cha Bima ya Afya ya Jamii. Suala kuu katika eneo hili ni uwiano na upatikanaji wa huduma za Kibingwa na Ubingwa bobezi kati ya kitita cha Bima ya Afya ya Jamii na kitita cha huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa maelekezo hayo na matokeo yake. Tarehe 16 na 17 Januari, 2024, Kamati ilikutana na Waziri wa Afya ili kupata ufumbuzi wa masuala mawili niliyoyataja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kikao hicho yalibainisha mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kuhusu viwango vya fedha vinahitajika kubainishwa kwenye sheria. Kamati ilifanya mapitio ya mifuko minne iliyoanzishwa kwa Sheria nne tofauti. Moja, ulikuwa ni mfuko wa Nishati vijijini ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Nishati Vijijini *(Rural and Energy Act 2005)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili ilikuwa ni Mfuko wa Elimu ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Sura Namba 353; na tatu ni Mfuko wa Taifa wa Maji ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Namba 5 ya mwaka 2019. Mwisho ilikuwa ni Mfuko wa Barabara ulioanzishwa kwa Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta *(Road Fuel Act)* Sura Namba 220 umewekewa vyanzo vya fedha bila kutaja viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, iwapo mifuko ambayo vyanzo vyao vimebainishwa kwa kutajwa na mifuko mingine vyanzo vyake vimebainishwa bila kutaja viwango. Kwa ulinganisho huo, mfuko wa kugharamia wasio na uwezo ulianzishwa na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote

ya mwaka 2023 unafafanua na mifuko mingine ambayo vyanzo vyake vya mapato havina viwango kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, suala la kugharamia wasio na uwezo katika utaratibu wa Bima ya Afya kwa Wote linatofautiana uzito na masuala ya maji, mazingira au barabara katika uhai wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Waziri wa Afya ilionesha kuwa Serikali inajipanga kuwa na vyanzo kama ifuatavyo: -

(i) Fedha zote zinazokusanywa kutoka vyanzo vya miamala ya kielektroniki;

(ii) Kuongeza asilimia mbili ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vinywaji vyenye kaboni (*Carbonated drinks)*;

(iii) Kuongeza asilimia mbili ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vinywaji vikali;

(iv) Kuongeza asilimia tatu ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vipodozi;

(v) Kuongeza asilimia mbili ya kodi inayotozwa kwenye michezo ya kubahatisha; na

(vi) Kuongeza asilimia tano kwenye ada ya bima za vyombo vya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Waziri, vyanzo hivi vitawezesha mapato ya shilingi bilioni 273.25 kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji. Kwa makadirio ya Serikali mahitaji katika kipindi hicho ni shilingi bilioni 266.96. Ufafanuzi wa Waziri unaonesha kuwa Serikali inapendekeza vyanzo na viwango vilivyotajwa vibainishwe katika Sheria ya Fedha ya kila Mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwiano wa upatikanaji wa huduma za vitita vya Bima ya Afya; kifungu cha 15(2) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kinataka mtu yeyote awe na angalau Kitita cha Bima ya Afya ya Jamii. Katika hali halisi mbali na watu wasiokuwa na uwezo wanaotakiwa kusaidiwa na Serikali, watu

wenye uwezo wa chini watajikuta wanalazimika kuwa na Kitita hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri wa Afya yalionesha kuwa Serikali inathamini wazo la kuangalia uwiano kati ya Kitita cha Bima ya Afya cha Jamii. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Januari 2024 tathmini haikuwa imekamilika. Maelezo ya Serikali yanabainisha kuwa zoezi hilo linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya shughuli za Kamati kuhusu Wizara ya Afya na Tume ya Kuthibiti UKIMWI Tanzania. Hali ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zimeonesha kuwa, baadhi ya maazimio yametekelezwa na mengine yanaendelea. Mfano wa Maazimio yanayoendelea kufanyiwa kazi ni pamoja na uwekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba, kulipa ama kupunguza madeni ya Bohari Kuu ya Dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji ulibainisha maazimio ambayo hayajatekelezwa kikamilifu. Mfano wa maazimio hayo ni pamoja na maazimio kuhusu udhibiti wa chakula na vipodozi kurejeshwa kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba *(TMDA);* na fedha zilizoidhinishwa na Bunge hususan fedha za miradi ya maendeleo kutolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS),* taarifa zinaonesha kwamba, sehemu kubwa ya maazimio imefanyiwa kazi. Hata hivyo baadhi ya maazimio yanaendelea kufanyiwa kazi. Maazimio hayo ni muhimu kutekelezwa na ufuatiliaji unapaswa kuendelea. Mfano wake ni pamoja na azimio kuhusu mkakati wa kupata vyanzo vingine vya ndani vya mapato kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya. Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ulifanyika ili kujiridhisha na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa bajeti. Taarifa zilizowasilishwa zilibainisha masuala yafuatayo:-

(i) Ni hali ya makusanyo ya maduhuli ni ya wastani. Hadi mwezi Disemba 2023 imekusanywa asilimia 48 tu ya lengo. Mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli tumeyaweka kwenye kielelezo namba moja.

(ii) Ni upatikanaji wa kiasi kidogo cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Uchambuzi umebaini kuwa, hali ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo si ya kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2023 kiasi kilichotolewa ni asilimia 25.5 tu ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kielelezo tumekiweka namba 2. Ni muhimu Serikali ikatoa fedha za miradi ya maendeleo ya Sekta ya Afya mapema ili miradi itekelezwe na kukamilika ndani ya muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti Tume ya Kuthibiti UKIMWI; hali ya utoaji wa fedha ni ya wastani ambapo, uchambuzi unaonesha kuwa fedha za maendeleo ndani zimepokelewa kwa asilimia 26 na fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimepokelea kwa asilimia 6 tu. Hali inadhihirisha kuwa ni lazima Serikali kufikiri na kujipanga kuwa na fedha za ndani kwa wingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yanayohusu shughuli za Wizara ya Afya; tukianza na suala la Bohari Kuu ya Dawa. Kumekuwa na ongezeko la mapato ya Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* kwa mwaka 2023 na 2024 ambapo yalipatikana mapato ya shilingi bilioni 373.4 sawa na asilimia 83. Mapato haya ni ongezeko la shilingi bilioni 53.5 kutoka shilingi bilioni 320.9 ya mwaka 2021/2022. Vilevile upatikanaji wa bidhaa za ndani umeimarika kufikia asilimia 80 hadi mwezi Juni, 2023 kutoka asilimia 57 mwezi Julai, 2022. Kwa upande wa bidhaa za afya yaani bidhaa 290 imefikia asilimia 64 hadi mwezi Juni, 2023 kutoka asilimia 52 mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayoikabili Bohari Kuu ya Dawa ni ukosefu wa mtaji ambapo, katika mwaka

wa fedha 2022/2023, kupitia Wizara ya Afya iliwasilisha maombi ya mtaji utakaowezesha kufanya shughuli za uzalishaji, ununuzi na utunzaji wa bidhaa za afya kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaji ulioombwa ni shilingi bilioni 561.5 kwa mchanganuo kuwa, shilingi bilioni 204 zinahitajika kuwezesha ununuzi wa bidhaa za afya, shilingi bilioni 66.9 kwa ajili ya ujenzi wa maghala, shilingi bilioni 100.46 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na shilingi bilioni 191 kwa ajili ya malipo ya madeni ya washitiri na vituo vya kutolea huduma. Uwiano wa mahitaji hayo unaonekana katika kielelezo namba 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kiasi hiki cha mtaji kitapatikana, kitaiwezesha Bohari ya Dawa kununua mahitaji yote ya bidhaa za afya bila kusubiri fedha kutoka kwa mtoa huduma. Naomba hili nisisitize na Serikali inasikia fedha hizi Bunge limeridhia *MSD* ipewe mtaji mpaka leo haijapata hata shilingi moja. Waziri wa Fedha tunakuomba sana, fedha hizi muwapatie *MSD* ili Watanzania waweze kupata huduma kama anavyozitoa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyowekeza kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Kamati imebaini uwepo wa changamoto nyingine inayokabili uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hivi karibuni kumekuwa na mvutano mkali kati ya Sekta Binafsi ya Afya jambo lililosababisha Waziri wa Afya kuunda tume kwa ajili ya kuchunguza na kuja na mapendekezo yatakayosaidia kuondoa mvutano uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee na kwa niaba ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, tunatoa shukrani za dhati kwa kutoa kibali na kuruhusu Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kuitisha vikao ambavyo vilihusisha Wizara ya Afya, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya pamoja na wawakilishi wa sekta binafsi ya Afya ambao ni Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Chama cha Wamiliki wa Vituo vya Afya Binafsi *(APHFTA)* na Tume ya Huduma za Jamii za Kikristo *(CSSC)*. Lengo la vikao hivyo ni kupata uelewa kuhusu changamoto iliyopo na hatimaye Kamati iweze kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hiyo, Kamati imebaini ushirikiano kati ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* na Sekta Binafsi ya Afya umekuwa ukisuasua kutokana na mambo yafuatayo: -

(i) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura Namba 395 kutokutambua uwepo wa Sekta binafsi ya Afya kama mnufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;

(ii) Kutoruhusu sekta binafsi za afya kutumia mfumo wa kuchangia huduma za Afya *(Co-payment)* kwa wanufaika wa *NHIF*, wakati mfumo huo unaruhusiwa kwa hospitali za umma tu; na

(iii) Kukosekana kwa chombo huru na cha kudumu kinachoratibu na kusimamia bei za huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia changamoto hizo, Kamati inaona ipo haja ya Serikali kutafuta ufumbuzi wa mvutano huu kwa haraka ili wananchi waweze kuendelea kupata huduma za afya bora katika vituo vya afya wanavyopendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC);* chimbuko la kuanzishwa kwa Taasisi ya Chakula na Lishe lilikuwa ni kuunda chombo mahususi cha Taifa cha kuwaunganisha wataalam wa shughuli za ugani na wanasayansi, pamoja na viongozi wa Kitaifa katika mapambano dhidi ya utapiamlo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwezi Disemba, 2023 Serikali kwa kupitia Msajili wa Hazina ilitangaza nia ya kufuta taasisi hii; Kamati inaona ikiwa taasisi hii itafutwa kunaweza kusababisha nchi kukosa chombo mahsusi kitakachojikita katika tafiti za lishe na hivyo kusababisha jamii isiyo na lishe bora ikiwa ni pamoja na kuchochea ongezeko la magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifo vya mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya siku 28; malengo ya dunia ya

mwaka 2030 ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 70 kwa kila vizazi hai 100,000 na vifo vya watoto wachanga kufikia 12 kwa kila vizazi hai 1,000. Hali ya vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano, takwimu zinaonesha kuendelea kupungua kwa kiasi kikubwa kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1000 mwaka 2015/2016, na kufika vifo 43 kwa kila vizazi 1000 katika mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa taarifa za utendaji wa Tume ya Kuthibiti UKIMWI *(TACAIDS);* Taarifa za Utendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania zilibainisha mambo mbalimbali kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI. Uchambuzi wa Taarifa hizo umebainisha yafuatayo: -

(i) Kuvuka lengo kwenye utekelezaji wa shabaha ya pili ya asilimia 95 ya WAVIU waliotambua hali zao ambapo tafiti inaonesha imefika asilimia 97 ya WAVIU wapo kwenye tiba. Kwa hili tunatoa pongezi kubwa sana kwa Serikali hasa kupitia *TACAIDS* kwa kazi kubwa nzuri walioifanya wameanza kuvuka malengo ya asilimia 95 sasa wameanza kwenda asilimia 97;

(ii) Shabaha ya tatu inayohusu kufubaza virusi vya WAVIU wanaoendelea na tiba. Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 94 ya WAVIU wapo kwenye tiba ya kufubaza. Ina maana wamebakiza asilimia moja tu. Hilo nalo tunawapongeza sana;

(iii) Kuhusu shabaha ya kwanza Taifa linatakiwa kuongeza nguvu na jitihada zaidi katika kufikia shabaha hii inayohusu watu wote wanaoishi na maambukizi yaani VVU kupima na kujua hali zao za maambuzi ambapo, matokeo yanaonesha kufikia asilimia 82;

(iv) Kupungua kwa kiwango cha ushamiri wa VVU kutoka asilimia 4.7 mwaka 2016 hadi 2017 hadi asilimia 4.4 mwaka 2022/ 2023; na

(v) Kupungua kwa maambukizi mapya kutoka watu 87,013 mwaka 2016/2017 hadi hivi sasa ni watu 60,000 tu

ambao wamepata maambukizi ya UKIMWI yaani mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kutoa sasa mapendekezo na maoni ya Kamati; Taarifa hii imeeleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati pamoja na kubainisha mafanikio na changamoto kama zilivyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Msingi wa Taarifa hii pamoja na ushauri unaotolewa umezingatia vyazo muhimu kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Sera ya Afya ya mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi wa mwaka 2020/2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026; na Malengo ya Maendeleo Endelevu (Lengo Namba 3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya nchini; hata hivyo, zipo changamoto mbalimbali zilizobainika ambazo utatuzi wake utasaidia kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za afya. Kwa sababu hiyo, naomba kutoa mapendekezo ambayo Bunge lako Tukufu litayaazimia kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na mapendekezo kuhusu Wizara ya Afya; kuhusu kutokutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo:-

Kwa kuwa, fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 zimetolewa kwa kiwango kidogo ambapo hadi mwezi Disemba 2023, imetolewa asilimia 26 tu;

Na kwa kuwa, kiasi hicho kidogo cha fedha pasipokuzingatia wakati kitaathiri utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo itakayokusudiwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itenge fedha za kutosha na pia kuhakikisha fedha hizo zinatolewa zote na kwa wakati ili miradi ya maendeleo itekelezwe katika muda uliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa watumishi:-

Kwa kuwa, sekta ya afya inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kiwango cha asilimia 64, jambo ambalo ni kinyume kabisa na tamko la Sera ya Afya ya mwaka 2007 inayotaka kuwepo kwa watumishi wa kutosha wenye ujuzi katika taaluma mbalimbali katika ngazi zote za kutolea huduma;

Na kwa kuwa, upungufu huu wa watumishi umekuwa ukiathiri utoaji wa huduma bora za afya;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazima kwamba: -

(i) Serikali itoe kipaumbele cha ajira kwenye sekta hii muhimu ili huduma za afya katika ngazi mbalimbali ziweze kupatikana kwa wakati na katika ubora unaostahili; na

(ii) Kipaumbele cha ajira kitolewe kwa wanaojitolea kutoa huduma za afya katika hospitali mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na vituo vya afya na zahanati zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ukosefu wa Mtaji Bohari Kuu ya Dawa:-

Kwa kuwa, Bohari Kuu ya Dawa imekuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa mtaji kiasi cha shilingi bilioni 561.5;

Na kwa kuwa, kutokupatikana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na pia kushindwa kununua mahitaji yote ya bidhaa za afya, hivyo kuendelea kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za afya; na

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itoe mtaji wa shilingi bilioni 561.5 kwa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya, kusaidia uwekezaji

kwenye viwanda na kuongeza uwezo wa kuhifadhi kwa kujenga maghala ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwekezaji Mdogo wa Viwanda vya Dawa na Vifaatiba:-

Kwa kuwa, kumekuwa na uchache wa viwanda vya kuzalisha vifaatiba pamoja na dawa nchini;

Na kwa kuwa, kutokuwa na viwanda vya kutosha vya uzalishaji wa vifaa tiba na dawa kunasababisha gharama ya bidhaa hizo kuwa ghali na changamoto ya upatikanaji wa dawa muhimu;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye yafuatayo: -

(i) Kuweka mikakati thabiti ya kushirikisha sekta binafsi *(Public Private Partnership)* na kurahisisha uwekezaji wa viwanda vya dawa pamoja na vifaatiba nchini ili kukidhi soko la ndani na nje;

(ii) Kufufua Kiwanda cha Dawa cha Arusha *(Tanzania Pharmaceutical Industries)* na kuongeza uzalishaji katika Kiwanda cha Dawa cha Keko *(Keko Pharmaceutical)* ambacho Serikali imewekeza kwa asilimia 70; na

(iii) Bohari Kuu ya Dawa ifanye mchakato wa haraka wa uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na pamba ili kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi kwa kuwa malighafi ya bidhaa hizo yaani zao la pamba inapatikana hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kurejesha Jukumu ya Udhibiti wa Chakula na Vipodozi *TMDA*:-

Kwa kuwa, mnamo mwaka 2019 Serikali ilipeleka jukumu ya udhibiti wa chakula na vipodozi katika Shirika la Viwango Tanzania *(Tanzania Bureau of Standards - TBS)* kupitia marekebisho ya Sheria Sura Namba 219;

Na kwa kuwa, chakula, dawa na vipodozi vinauhusiano mkubwa hivyo, kupelekwa kwa jukumu hilo chini ya *TBS* ambayo ni Taasisi isiyohusiana na masuala ya afya kunaondoa dhana ya udhibiti unaozingatia athari za kiafya;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali irejeshee *TMDA* udhibiti wa chakula na vipodozi kutoka Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* kwani bidhaa hizo zinahusiana moja kwa moja na afya ya jamii na endapo udhibiti wake hautazingatia usalama wa afya ya jamii itasababisha athari mbaya kwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto za Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya:-

Kwa kuwa, imebainika kuwepo kwa upungufu katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;

Na kwa kuwa, upungufu huo unasababisha athari kubwa katika uratibu na usimamizi wa sekta binafsi ya afya, kwani Sheria ya *NHIF* ilitungwa mahsusi kwa ajili ya kuhudumia sekta ya umma; na

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ianze mchakato wa kurekebisha Sheria ya *NHIF*, Sura ya Namba 395 ili kuitambua sekta binafsi ya afya ambayo ni mdau muhimu wa afya; *(Makofi)*

(ii) Serikali ianzishe chombo huru mahsusi na cha kudumu kitakachoratibu na kusimamia bei za huduma za afya ambacho kitajumuisha wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta binafsi;

(iii) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)* iwezeshwe kisheria kwa kuwekewa Kanuni chini ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuipa mamlaka ya kudhibiti utoaji wa huduma za Bima ya Afya nchini;

(iv) Vituo vya afya binafsi viruhusiwe kuwa na utaratibu wa mgonjwa kuchangia huduma *(co-payment)* ambapo wamiliki wa kadi za *NHIF* watatakiwa kulipa kwa pesa taslimu gharama zinazozidi kiwango cha kitita kinachochangiwa na *NHIF;*

(v) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uimarishe mifumo ya TEHAMA ili kukabiliana na changamoto ya ucheleweshaji wa malipo na kudhibiti udanganyifu;

(vi) Kitita cha bei kinachotumika sasa kiendelee kutumika katika kipindi cha mpito, mpaka kitita kipya cha bei kitakachozingatia maoni ya wadau wote wa sekta ya afya kutoka sekta ya umma na sekta binafsi;

(vii) *NHIF* ianzishe Kamati ya wataalam ambao watakuwa wanapitia malalamiko ya kitaalum yanayowasilishwa na vituo vya kutolea huduma au wataalam kuhusu bima ya afya; na

(viii) Serikali ikamilishe mchakato wa kufanya tathmini ya vyanzo na viwango vya fedha kwa ajili ya mfuko wa kugharamia watu wasio na uwezo kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa Watu Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kukosekana kwa Mwongozo wa Bima ya Afya kwa Watoto Shuleni:-

Kwa kuwa, hakuna mwongozo wa kufanikisha usajili wa watoto katika huduma za bima ya afya shuleni kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF);*

Na kwa kuwa, kukosekana kwa mwongozo huo kunadhoofisha mwitikio wa usajili wa watoto katika huduma za bima ya Afya, hili lilitokea wakati wa *Toto Afya Card;*

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu iweke mwongozo wa ulazima kwa wanafunzi wote

kusajiliwa katika huduma za bima ya afya kupitia shule; na *(Makofi)*

(ii) Serikali iweke mfumo na utaratibu wezeshi wa bima kwa watoto ambao wapo chini ya miaka mitano ambao hawajaanza shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nia ya Kufutwa kwa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania *(TFNC)*:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Msajili wa Hazina ilitangaza nia ya kuifuta Taasisi ya Chakula na Lishe ambayo kimsingi iliundwa kwa lengo la kusaidia Serikali kutatua changamoto ya lishe duni katika jamii na kuwa na mfumo wa kitaifa wa taarifa kuhusu tafiti mbalimbali za lishe;

Na kwa kuwa, endepo kufutwa kwa taasisi hii, kunasababisha nchi kukosa chombo muhimu mahsusi kinachojikita katika kusimamia tafiti za masuala ya lishe jambo ambalo linaweza kusababisha kuwa na jamii isiyo na lishe bora;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali kuona umuhimu wa kutoifuta Taasisi ya Chakula na Lishe kwani ni chombo mahsusi kinachoshughulikia na kusimamia masuala yote ya lishe nchini; na

(ii) Tafiti zaidi zifanyike kujua sababu za udumavu uliokithiri katika Mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula kama Iringa, Njombe na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya ugunduzi wa Kifua Kikuu:-

Kwa kuwa, takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi thelathini zenye maambukizi makubwa ya ugonjwa wa Kifua Kikuu *(TB)* na nchi hizi huchangia asilimia 87 ya wagonjwa wote duniani;

Na kwa kuwa, ugonjwa huu huathiri Taifa kwa kupunguza nguvu kazi kwani takwimu za Mwaka 2022 zilizotolewa na Shirika la Afya duniani *(WHO)* zinaonesha Tanzania ilikadiriwa kuwa na idadi ya vifo 25,800 vilivyosababishwa na ugonjwa Kifua Kikuu;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iimarishe mfumo wa ugunduzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu katika jamii kwa kushirikisha wahudumu wa afya ngazi zote ikiwemo ngazi ya jamii;

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa uhakika wa vitendanishi kwa ajili ya kufanyia uchunguzi sampuli za makohozi kwa wahisiwa wa ugonjwa wa Kifua Kikuu katika Hospitali za Halmashauri kwani imeonekana sampuli zinakaa zaidi ya siku saba bila kufanyiwa uchunguzi kutokana na ukosefu wa vitendanishi; na

(iii) Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusu maambukizi, athari na matibabu ya Kifua Kikuu kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutengwa kwa kiasi kiasi kidogo cha fedha za ndani kwa ajili ya tafiti. Tumetoa maagizo na maazimio yamo katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutokutekelezwa vema kwa Sera ya Matibabu Bure kwa Mama na Mtoto:-

Kwa kuwa, wananchi wameendelea kulalamikia baadhi ya vituo vya afya kutoza fedha za huduma za afya kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kwamba utaratibu huo ni jambo ambalo ni kinyume na tamko la Sera ya Afya mwaka 2007 Kifungu Na. 5, 3 na 4, kipengele (c) sehemu ya (i);

Na kwa kuwa, kutozwa fedha ili kupata huduma za afya ya kwa wajawazito na watoto kunasababisha wasio na uwezo

kushindwa kupata huduma stahiki, hivyo kusababisha vifo vya wajawazito na watoto wachanga;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali isimamie kikamilifu Sera ya Utoaji wa Huduma bila malipo kwa akina Mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na kutengwa kwa kiasi kidogo cha fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI:-

Kwa kuwa, kiasi kinachotengwa kwa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Afua za UKIMWI ni kidogo, hivyo kufanya utekelezaji wa Afua za UKIMWI nchini kutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za wafadhili;

Na kwa kuwa, kutegemea fedha za wafadhili kwa kiasi kikubwa kunaliweka Taifa katika sintofahamu ikiwa wafadhili wataacha kutoa fedha hizo na hivyo Taifa kukosa uhakika wa fedha za mapambano endelevu dhidi ya VVU na ugonjwa wa UKIMWI;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ione umuhimu wa kuwa na mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutenga na kutoa fedha za ndani na kuzitoa kwa wakati; na

(ii) Kuimarisha Mfuko wa Mapambano dhidi ya UKIMWI na kuweka mipango madhubuti ya kupata vyanzo mahsusi vya mapato ya ndani vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya miradi inayolenga kudhibiti VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha. Kwanza kabisa nitoe shukurani, napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mbunge – Waziri wa Afya, ambaye ni Mbunge kutoka katika Jimbo la Tanga Mjini. Mama huyu anatosha sana, ubarikiwe sana na ametupa ushirikiano mkubwa katika Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, naye ni Mbunge, najua watu wa Siha wanamfahamu ni Mbunge mahiri na amefanya kazi yake vizuri na kwa kweli hata leo mmemuona jinsi anavyojibu maswali kwa uhakika, anafanya kazi vizuri sana. Hawa ni Waheshimiwa Wabunge ambao kwa kweli wanatupa ushirikiano mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kutoa shukrani kwa kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, ni Mbunge wa Kudumu huyu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa, naomba majina yao yaingie kwenye *Hansard* na yakumbukwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu mahiri kabisa wa Bunge Ndugu yangu, Dada Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja naye namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, tunawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John Mvunta na Ndugu Jairo Joseph Odero pamoja na msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Gwivaha kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo taarifa hii ambayo leo tumeiwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI na likubali maoni na mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, hoja imeungwa mkono, vizuri sana. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI KWA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYYOWASILISHWA MEZANI**

[*Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023*]

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Mwezi Februari 2023 hadi Januari 2024.

**1.2 Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza, inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati na njia iliyotumika;

(ii) Sehemu ya Pili, inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto;

(iii) Sehemu ya Tatu, inatoa maoni ya jumla na mapendekezo kwa ajili ya uamuzi wa Bunge, hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

**1.3 Njia zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 naomba kutaja njia zilizotumika wakati wa utekelezaji. Njia hizo ni:-

(i) Kutafakari hali ya shughuli za Wizara na Taasisi zake na kuibua ajenda;

(ii) Kuomba Taarifa Maalumu za Wizara na kuzijadili;

(iii) Kufanya uchambuzi wa Taarifa zinazowasilishwa kwenye Kamati;

(iv) Kufanya majadiliano na Wizara ili kupata undani wa hali halisi; na

(v) Kufanya majumuisho ya masuala yaliyojitokeza ili kuwa na maoni ya jumla kuhusu masuala hayo na kuandaa mapendekezo.

**1.4 Madhumuni ya Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge. Madhumuni ya Taarifa hii ni kubainisha mambo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024. Lengo ni kuonesha mambo yanayohitaji kuboreshwa ili Bunge liyajadili kwa kuzingatia madaraka yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba.

**1.5 Msingi wa Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa shughuli za Kamati ni madaraka ya Bunge kwa mujibu ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara hiyo, inalitambua Bunge kuwa chombo chenye madaraka kwa niaba ya wananchi ya

kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba inaweka msingi wa Bunge kuunda Kamati za Bunge kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Vilevile, Kanuni ya 137 ya Kanuni za Bunge ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge imeanzisha Kamati za Kudumu za Bunge na kufafanua majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 5 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaainisha Kamati Kumi na Moja za Kudumu za Bunge katika kundi la Kamati za Kisekta. Miongoni mwa Kamati hizo, ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Majukumu ya jumla ya Kamati hizo yamebainishwa kwenye kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Majukumu hayo ni:-

(i) Kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja Taasisi zilizo chini yake; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (9) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia shughuli za –

(i) Wizara ya Afya; na

(ii) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-(TACAIDS).

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inahusu shughuli za Kamati ya Kisekta na maudhui yake yanagusa Sekta ya Afya na mambo mtambuka yanayohusu masuala ya UKIMWI. Sehemu hii ya Taarifa inafafanua shughuli za Kamati na uchambuzi wa mambo yaliyobainika. Mambo hayo yanajenga msingi wa maoni na mapendekezo yanayohitaji uamuzi wa Bunge.

### 2.2 Ufafanuzi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Kamati zililenga kubainisha iwapo utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara na Taasisi zake, unawezesha Maisha bora kama ilivyokusudiwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025. Aidha, Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali kuhusu shughuli za umma katika sekta ya Afya ilizingatiwa ili kukamilisha azma ya Bunge kuwa sauti ya watu na chombo halisi cha uwakilishi wa Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Ufafanuzi wa shughuli hizo ni kama ifuatavyo: -

#### 2.2.1 Ziara za Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, Ziara za ukaguzi ni miongoni mwa shughuli muhimu za Kamati zinazofanikisha utekelezaji wa Madaraka ya Bunge. Shughuli hii ilihusisha kubaini na kutambua miradi inayostahili kutembelewa. Katika ziara hizo, Kamati ilitembelea miradi saba ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2022/2023, inayotekelezwa na Wizara ya Afya katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe.

**Mheshimiwa Spika**, Maoni na mapendekezo kutokana na shughuli hii yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge. Ni matumaini ya Kamati kuwa, Serikali inaendelea kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa wakati huo.

#### 2.2.2 Kushughulikia Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli hii ilihusu uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Mambo hayo yalifanyika tarehe 21 hadi 30 Machi, 2023 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge.

Naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa maoni na ushauri wa Kamati uliotokana na shughuli hiyo yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

**2.2.3 Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba iliyopendekezwa Kuridhiwa na Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli hii ilihusisha kufanyia kazi Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022 na Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019 *(Treaty for the Establishement of the African Medicines Agency, 2019)*. Utekelezaji wake ulifanyika kwa pamoja na mambo mengine, kupokea maelezo ya Serikali na Maoni ya Wadau kwa Mujibu wa Kanuni ya 97 (2), 136 (9) na 108 (2) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022 yaliwasilishwa Bungeni tarehe 1 Novemba, 2023 wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge kwa Mujibu wa Kanuni ya 99 (5) (b). Aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisaini Muswada huo kuwa Sheria tarehe 19 Novemba, 2023. Sheria hiyo, ilitangazwa rasmi katika gazeti la Serikali Toleo Namba 48 la tarehe 1 Desemba, 2023 kuwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Namba 13 ya Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Itakumbukwa kuwa tarehe 1 Novemba, 2023 ulitoa maelekezo Bungeni kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masula ya UKIMWI kufanyia kazi maeneo mawili ya Muswada. Eneo la kwanza lilihusu Ibara ya 22 A katika jedwali la marekebisho la Serikali kuhusu kuwagharamia watu wasio na uwezo. Jambo kuu ni kuona iwapo viwango katika vyanzo vya fedha za Mfuko vinahitaji kufafanuliwa na Sheria au laa.

**Mheshimiwa Spika**, Eneo la pili linahusu huduma ambazo zitatolewa katika Kitita cha Bima ya Afya ya Jamii. Suala kuu katika eneo hili ni uwiano wa upatikanaji wa huduma za Kibingwa na Ubingwa bobezi kati ya kitita cha Bima ya Afya ya Jamii na kitita cha huduma muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa maelekezo hayo na matokeo yake. Tarehe 16 na 17 Januari 2024,

Kamati ilikutana na Waziri wa Afya ili kupata ufumbuzi wa masuala mawili niliyoyataja hapo juu. Matokeo ya Kikao hicho yalibainisha mambo yafuatayo: -

**(a) Iwapo Viwango vya Fedha Vinahitaji Kubainishwa kwenye Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Mapitio ya Mifuko Minne iliyoanzishwa kwa Sheria nne tofauti yanaonesha kuwa ipo mifuko ambayo vyanzo vyake vimebainishwa kwa kutajwa na viwango na mifuko mingine vyanzo vyake vimebainishwa bila kutajwa viwango. Kwa Mfano, Mfuko wa Nishati Vijijini ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Nishati Vijijini *(Rural and Energy Act)* ya Mwaka 2005 vyanzo vyake vimeainishwa katika Kifungu cha 19 ambacho kimeweka asilimia ya viwango kwa vyanzo viwili kati ya vyanzo vitano vilivyotajwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Elimu ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Sura ya 353 vyanzo vyake vimetajwa kwa kubainisha viwango katika asilimia. Mifuko hiyo miwili inatofautiana ambapo Mfuko wa Nishati vijijini una vyanzo vilivyotajwa kwa viwango na visivyo na viwango na Mfuko wa Elimu hauna vyanzo visivyo na viwango.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Maji ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Namba 5 ya 2019 una vyanzo vya fedha bila viwango. Aidha, Mfuko wa Barabara ulioanzishwa kwa Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta *(Road and Fuel Act)* Sura ya 220 umewekewa vyanzo vya fedha bila kutaja viwango.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ulinganisho huo, Mfuko wa kugharamia Wasio na Uwezo ulioanzishwa na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2023 unafanana na Mifuko mingine ambayo vyanzo vyake vya mapato havina viwango kwa mujibu wa Sheria. Hata hivyo, suala la kugharamia wasio na uwezo katika utaratibu wa Bima ya Afya kwa Wote linatofautiana uzito na masuala ya maji, mazingira au barabara katika uhai wa watu.

**Mheshimwa Spika**, Taarifa ya Waziri wa Afya ilionesha kuwa Serikali inajipanga kuwa na vyanzo kama ifuatavyo: -

(i) Fedha zote zinazokusanywa kutoka chanzo cha miamala ya kielektroniki;

(ii) Kuongeza asilimia 2 ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vinywaji vyenye kaboni (*Carbonated drinks)*;

(iii) Kuongeza asilimia 2 ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vinywaji vikali;

(iv) Kuongeza asilimia 3 ya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vipodozi;

(v) Kuongeza asilimia 2 ya kodi inayotozwa kwenye michezo ya kubahatisha; na

(vi) Kuongeza asilimia 5 kwenye ada ya bima za vyombo vya moto.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa maelezo ya Waziri, vyanzo hivi vitawezesha mapato ya **shilingi bilioni 273.25** kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji. Kwa makadirio ya Serikali mahitaji katika kipindi hicho ni **shilingi bilioni 266.96**. Ufafanuzi wa Waziri unaonesha kuwa Serikali inapendekeza vyanzo na viwango vilivyotajwa vibainishwe katika Sheria ya Fedha ya kila Mwaka.

**(b) Uwiano wa Upatikanaji wa Huduma za Vitita vya Bima ya Afya**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 15 (2) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kinataka mtu yeyote awe na angalau Kitita cha Bima ya Afya ya Jamii. Katika hali halisi mbali na watu wasiokuwa na uwezo wanaotakiwa kusaidiwa na Serikali, watu wenye uwezo wa chini watajikuta wanalazimika kuwa na Kitita hicho. Kundi hilo lina idadi kubwa ya Watu hivyo, huduma wanayoweza kupata kwa utaratibu wa Sheria hii inapaswa kuangaliwa vizuri. Vinginevyo inaweza kuwa changamoto kwa Serikali kufikia lengo la Ustawi wa Wananchi kwa Mujibu wa Ibara 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, Maelezo ya Waziri wa Afya yalionesha kuwa Serikali inathamini wazo la kuangalia uwiano kati ya Kitita cha Bima ya Afya cha Jamii, hata hivyo, hadi kufikia mwezi Januari

2024 tathmini haikuwa imekamilika. Maelezo ya Serikali yanabainisha kuwa zoezi hilo linaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Mkataba wa kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu Mkataba huo Bungeni. Kumbukumbu za Bunge zinaonesha kuwa Bunge lilipitisha Azimio la Kuridhia Mkataba huu tarehe 31 Oktoba 2023 wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge.

### 2.2.4 Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa Mkutano wa Kumi wa Bunge tarehe 31 hadi 10 Februari 2023, Bunge lilipitisha Maazimio yaliyotokana na Taarifa za Kamati za Bunge. Miongoni mwa Taarifa hizo ni Taarifa ya iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo na Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2022/2023. Taarifa hiyo, pamoja na mambo mengine ilipendekeza mambo ya kufanyiwa kazi katika Sekta ya Afya.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ilitoa Taarifa na Mapendekezo kuhusu masuala mtambuka ya UKIMWI. Mapendekezo hayo yalipitishwa na kuwa sehemu ya Maazimio ya Bunge.

### 2.2.5 Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai 2023 – Disemba, 2023

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli hii ililenga kubainisha iwapo mwenendo wa utekelezaji wa bajeti unalingana na matarajio ya Bunge. Matokeo yake ni kuonesha mapendekezo kuhusu mwenendo huo. Kwa sababu hiyo, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai - Disemba 2023) kutoka Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Mambo makuu katika taarifa hizo yalihusu makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo la makusanyo pamoja na upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa. Uchambuzi wa mambo yaliyobainika unabainishwa katika taarifa hii sambamba na maoni ya Kamati kuhusu matokeo hayo.

### 2.2.6 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utendaji

**Mheshimiwa Spika**, Kupokea na kujadili taarifa za utendaji ni mojawapo ya njia za kufuatilia shughuli za umma katika sekta ya Afya na juhudi za kupambana dhidi ya janga la UKIMWI. Taarifa hizo, zilijadiliwa kwa kuoanishwa na msingi, madhumuni na majukumu ya Taasisi hizo ili kuona hatua mbalimbali za kufanikisha ustawi wa wananchi. Taarifa zilizopokelewa na kujadiliwa zilijumuisha: -

(i) Taarifa ya Utendaji Bohari Kuu ya Dawa (MSD);

(ii) Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA);

(iii) Taarifa ya Utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF);

(iv) Taarifa ya Utendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC);

(v) Taarifa ya Utendaji wa Baraza la Tiba Asili/Mbadala;

(vi) Taarifa ya Utekelezaji wa azma ya Serikali katika kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya siku ishirini na nane (28);

(vii) Taarifa ya Hali ya ugonjwa wa Kifua Kikuu nchini;

(viii) Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Magonjwa yasiyo ya kuambukiza;

(ix) Taarifa ya Uimarishaji wa miundombinu ya vituo vya damu salama nchini;

(x) Taarifa ya Uimarishaji wa huduma za matibabu ya Kibingwa na Ubingwa bobezi kwa kipindi cha Mwaka 2021 hadi 2023;

(xi) Taarifa kuhusu Tafiti za kimkakati za Afya zilizofanyika kwa ajili ya kupata suluhisho la matatizo ya kiAfya kwa kipindi cha Mwaka 2021 hadi 2023;

(xii) Taarifa kuhusu Taasisi ya Taifa ya Magonjwa ya Akili-Mirembe,

(xiii) Taarifa kuhusu Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma; na
(xiv) Taarifa kuhusu Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kati - Benjamin Mkapa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali zinazohusu uratibu wa maambukizi ya VVU na UKIMWI. Taarifa hizo ni pamoja na:-

(i) Taarifa kuhusu Hali ya maambukizi ya VVU na UKIMWI;

(ii) Taarifa kuhusu Programu ya Wasichana Balehe na Wanawake Vijana;

(iii) Taarifa kuhusu Mkakati wa kutokomeza unyanyapaa kwa WAVIU;

(iv) Taarifa kuhusu Vituo vya maarifa katika vituo vya malori ya masafa marefu *(Roadside Wellness Centers)*; na

(v) Taarifa kuhusu Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania (NACOPHA).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa hizo ulilenga kuliwezesha Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali inavyostaili kuhusu Sekta ya Afya pamoja na mapambano dhidi ya UKIMWI. Lengo hilo linatimizwa kwa Kamati kuripoti Bungeni matokeo ya shughuli hiyo kwa kubainisha masuala yaliyojitokeza, maoni na mapendekezo kuhusu mambo hayo chini ya Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

### 2.3 Matokeo ya Shughuli za Kamati kuhusu Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyobainishwa katika taarifa hii, lengo la utaratibu wa Kamati kuripoti Bungeni wakati huu ni kuliwezesha Bunge kupitisha mapendekezo yanayoweza kufanyiwa kazi katika mchakato wa Bajeti. Ili kufanikisha hilo, masuala yaliyojitokeza

wakati wa shughuli za Kamati yanabainishwa kwa kila sekta. Kwa upande wa sekta ya Afya chini ya Wizara ya Afya, uchambuzi unabainisha mambo mbalimbali ikiwemo changamoto. Ufafanuzi wa Matokeo hayo ni kama ifuatavyo: -

**2.3.1 Hali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zimeonesha kuwa, baadhi ya maazimio yametekelezwa na mengine yanaendelea kutekelezwa. Mfano wa Maazimio yaliyoripotiwa kutekelezwa ni Azimio linalohusu Serikali kutenga fedha kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya kufanya tafiti. Taarifa ya Utekelezaji imeonesha kuwa, **Shilingi Bilioni 3.37** zilitengwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo, uchambuzi umebainisha kwamba, hadi kufika mwezi Disemba 2023, shughuli za utafiti hazikuwa zimepata kiasi chochote cha fedha hizo. Hali hiyo ni sawa na kutokutengwa fedha kwa ajili ya utafiti japokuwa kwa hesabu wakati wa kupitisha bajeti, fedha ilionekana kutengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa maazimio yanayoendelea kufanyiwa kazi ni pamoja na uwekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba, kulipa ama kupunguza madeni ya Bohari Kuu ya Dawa, Bohari kuu ya Dawa (MSD) kupewa mtaji, udhibiti wa bidhaa bandia, athari na matumizi salama ya tiba asili. Taarifa za utekelezaji zimeonesha kuwa utekelezaji umeanza na unaendelea. Kamati inaendelea kufuatilia na kwamba, wakati wa kuchambua Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ufuatiliaji utaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji ulibainisha Maazimio ambayo hayajatekelezwa kikamilifu. Mfano wa maazimio hayo ni pamoja na maazimio kuhusu udhibiti wa chakula na vipodozi kurejeshwa kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na fedha zilizoidhinishwa na Bunge hususan fedha za miradi ya maendeleo kutolewa kwa wakati. Hili limejidhihirisha katika fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya mwaka wa fedha 2023/2024, ambapo hadi kufika Disemba, 2023 fedha za miradi ya maendeleo zimetolewa kwa kiwango cha asilimia 25.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Taarifa zimeonesha kwamba, sehemu kubwa

ya maazimio imefanyiwa kazi. Hata hivyo baadhi ya maazimio yanaendelea kufanyiwa kazi. Maazimio hayo ni muhimu kutekelezwa na ufuatiliaji unapaswa kuendelea. Mfano wake ni pamoja na azimio kuhusu mkakati wa kupata vyanzo vingine vya ndani vya mapato kwa ajili ya kutekeleza afua za UKIMWI. Taarifa iliyowasilishwa ilionesha kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Kisekta imeandaa andiko linaloainisha mapendekezo ya vyanzo endelevu vya Mapato kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile Taarifa zilifafanua zaidi kwamba, TACAIDS imeendelea kutoa elimu kuhusu unyanyapaa, VVU na UKIMWI kupitia vyombo vya habari kama vile redio za kitaifa na kijamii. Jambo lingine lililoelezwa ni kuendelea kufanyika kwa makongamano, maonesho, midahalo na mijadala kwa vijana kuhusu masuala ya afua za UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulihakikishia Bunge kuwa, Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ambayo yanaendelea kutekelezwa na yale ambayo hayakutekelezwa. Kamati hii ambayo ni nyenzo ya Bunge katika utekelezaji wa madaraka yake, kila itakapopata nafasi ya kutolea taarifa hatua za utekelezaji, itafanya hivyo kwa namna inayoliwezesha Bunge kupata picha halisi na kuchukua hatua za kibunge.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ulifanyika ili kujiridha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa bajeti. Taarifa zilizowasilishwa zilibainisha masuala yafuatayo: -

### (a) Mwelekeo wa Kukusanya Pungufu ya Lengo


**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai, 2023 hadi Disemba 2023), Kamati imebaini kuwa, Makusanyo ya maduhuli ni ya wastani. Hadi mwezi Disemba 2023 jumla ya **Shilingi 328,483,075,222.11** sawa na asilimia 48 ya lengo lililowekwa la kiasi cha **Shilingi 677,621,168,390.95** zilizokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika,** kiwango kilichokusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara ni asilimia 38 kiasi ambacho ni kidogo. Hata

hivyo, Kamati imejulishwa kuwa, makusanyo yanatarajiwa kuongezeka mara baada ya kuanza kutolewa kwa huduma za uchunguzi kwa baadhi ya Taasisi, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali Maalum pamoja na baadhi ya Mabaraza na Bodi za kitaaluma kukusanya ada za usajili wa wanachama wake hasa kwa kipindi cha mwezi Aprili na Juni.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi umeonesha maeneo matatu ya makusanyo kwa Wizara ya Afya. Maeneo hayo ni Hospitali za Rufaa za Mikoa, Taasisi zilizochini ya Wizara ya Afya na Makao Makuu ya Wizara. Taarifa zimeonesha kuwa mchango wa Hosptali za Rufaa za Mikoa katika makusanyo ni wa juu ikilinganishwa na makusanyo kutoka Makao Makuu na kwenye Taasisi za Wizara ya Afya kama inavyoonekana katika Kielelezo Namba 1.

**Kielelezo Na 1: Mchanganuo wa Makusanyo ya Maduhuli kati ya Makao Makuu ya Wizara ya Afya, Taasisi na Hospitali za Rufaa za Mikoa**




***Chanzo; Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba, 2023)***

**(b) Upatikanaji wa kiasi kidogo cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Afya (fungu 52) ilitengewa kiasi cha **Shilingi 1,235,316,516,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufika Disemba 2023, jumla ya **Shilingi 432,149,552,900.68** zilipokelewa, sawa na asilimia 35 ya fedha zilizoidhinishwa kama inavyoonekana katika Kielelezo Namba 2.

**Kielelezo Na 2: Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizotolewa**

| MATUMIZI | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOTOLEWA (JULAI-DISEMBA 2023) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 354,342,486,000.00 | 182,775,315,813.76 | **52%** |
| Matumizi Mengineyo | 148,609,423,000.00 | 62,304,289,622.88 | **42%** |
| Maendeleo Ndani | 430,298,000,000.00 | 116,792,035,527.85 | **27%** |
| Maendeleo Nje | 302, 066, 607,000.00 | 70,277,911,936.19 | **23%** |
| **JUMLA** | **1,235,316,516,000.00** | **432,149,552,900.00** | **35%** |

***Chanzo; Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu Mwaka (Julai - Disemba, 2023)***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi umebaini kuwa, hali ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo si ya kuridhisha. Hadi kufikia Mwezi Disemba 2023 kiasi kilichotolewa ni asilimia 25.5 tu ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hii inaonesha kuwa kiasi cha **Shilingi 187,069,947,464.04** ndicho kimetolewa kutoka katika kiasi cha **Shilingi 732,364,607,000.00** cha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo sio mzuri kwani hali hii inakwamisha utekelezaji wa miradi kwa wakati na kurudisha nyuma maendeleo ya sekta ya Afya. Hivyo, ni muhimu Serikali ikatoa fedha za miradi ya maendeleo ya sekta ya Afya mapema ili miradi itekelezwe na kukamilika ndani ya muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Fungu 92) Taarifa imeonesha kuwa kuna ucheleweshaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Ufafanuzi wa upatikanaji wa fedha unaonesha kuwa bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, fedha zilizoidhinishwa ni **Shilingi 25,862,966,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,670,817,000.00** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 22,192,149,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufika mwezi Disemba 2023, fedha za Matumizi ya Kawaida zimepokelewa **Shilingi 1,702,575,077.64** sawa na **asilimia 46.** Aidha, fedha za Mpango wa Maendeleo zimepokelewa **Shilingi 1,708,798,444.00** sawa na **asilimia 8** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na fedha zilizotolewa umeoneshwa katika kielelezo namba 3.

**Kielelezo Na 3: Ulinganisho wa Kiasi cha Fedha Zilizoidhinishwa na Kiasi cha Fedha Zilizopolelewa na TACAIDS**

| MATUMIZI | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOTOLEWA (JULAI-DISEMBA 2023) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 1,897,434,000.00 | 829,028,766.00 | **44** |
| Matumizi Mengineyo | 1,773,383,000.00 | 873,546,311.64 | **51** |
| Maendeleo Ndani | 1,880,000,000.00 | 500,000,000.00 | **26** |
| Maendeleo Nje | 20,312,149,000.00 | 1,208,798,444.00 | **6** |
| **JUMLA** | **25,862,966,000.00** | **3,411,373,521.64** | **13** |

***Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS (Julai-Disemba, 2023)***

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ni ya wastani kwani fedha za Matumizi ya Kawaida zimepokelewa kwa asilimia 46 na fedha za Miradi ya Maendeleo za Ndani zimepokelewa kwa asilimia 26.

Hata hivyo, Fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo zimepokelewa kwa asilimia 6 tu hali inayodhihirisha kuwa ni lazima Serikali kufikiri na kujipanga kuwa na fedha za ndani kwa wingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya UKIMWI.

**2.3.3 Taarifa za Utendaji za Wizara ya Afya**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za utendaji ulifanyika kwa kuoanisha hali ya utendaji na uendeshaji kwa upande mmoja na matarajio ya wananchi, Ilani ya CCM, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Sera na Sheria kwa upande mwingine. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha masuala yaliyojitokeza kama ifuatavyo: - **Masuala yanayohusu Shughuli za Wizara ya Afya**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa ulijumuisha kuchambua Taarifa zifuatazo: -

(a) **Bohari Kuu ya Dawa**

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya msingi ya Bohari Kuu ya Dawa ni Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Afya kwenda kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za Afya na vile vya binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya. Uchambuzi wa Taarifa ya Utendaji ya Bohari ya Kuu ya Dawa hadi kufikia Mwezi Juni, 2023, umebainisha masuala yafuatayo: -

(i) Mapato yaliyopatikana ni **Shilingi bilioni 373.4** sawa na asilimia 83. Mapato haya ni ongezeko la **Shilingi bilioni 53.5** kutoka **Shilingi bilioni 320.9** Mwaka wa fedha 2021/2022;

(ii) Upatikanaji wa bidhaa za dawa umeimarika kufikia asilimia 80 hadi mwezi Juni, 2023 kutoka asilimia 57 mwezi Julai, 2022. Kwa upande wa bidhaa za Afya 290 ashiria imefikia asilimia 64 hadi mwezi Juni, 2023 kutoka asilimia 52 mwezi Julai, 2022.

(iii) Kumekuwa na mkakati wa ujenzi wa miradi ya viwanda vya uzalishaji wa bidhaa za Afya na Maghala (maghala yamepangwa kujengwa Mikoa ya Dodoma na Mtwara), ambapo viwanda hivyo ni Kiwanda cha Mipira ya Mikono cha Mkoani Njombe na Kiwanda cha bidhaa za pamba cha Mkoani Simiyu. Aidha, Bohari Kuu ya Dawa imeanzisha

Kampuni Tanzu inayoitwa *"MSD Medipharm Manufacturing Company Limited*" ambayo itakuwa na jukumu la usimamizi wa viwanda vyote.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zinazoikabili Bohari Kuu ya Dawa zinazosababisha kutokutekeleza majukumu yake ipasavyo. Changamoto hizo ni pamoja na: -


**(i) Changamoto za Mtaji**

**Mheshimiwa Spika**, Bohari Kuu ya Dawa imebainika kuwa na changamoto ya mtaji, ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23, kupitia Wizara ya Afya iliwasilisha maombi ya mtaji utakaowezesha kufanya shughuli za Uzalishaji, Ununuzi na Utunzaji wa bidhaa za Afya kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Mtaji unaoombwa ni **Shilingi bilioni 561.5** kwa mchanganuo kuwa, **Shilingi bilioni 204** zinahitajika kuwezesha ununuzi wa bidhaa za Afya, **Shilingi bilioni 66.9** kwa ajili ya ujenzi wa Maghala, **Shilingi bilioni 100.46** kwa ajili ya ujenzi wa Viwanda na **Shilingi bilioni 191** kwa ajili ya malipo ya madeni ya washitiri na vituo vya kutolea huduma.

Uwiano wa mahitaji hayo unaonekana katika kilelelezo namba 4

**Kielelezo Na 4: Uwiano wa Mahitaji ya Mtaji kwa ajili ya MSD**




**Chanzo;** ***Taarifa ya Utendaji wa Bohari Kuu ya Dawa Januari, 2024***

**Mheshimiwa Spika,** Ikiwa kiasi hiki cha mtaji kitapatikana kitaiwezesha Bohari Kuu ya Dawa kununua mahitaji yote ya bidhaa za Afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za Afya. Aidha, MSD inadai kiasi cha **Shilingi bilioni 348** kwa ajili ya kufidia sehemu ya huduma iliyotolewa ya utunzaji na usambazaji wa bidhaa za Miradi Msonge.

**(ii) Deni kwa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya**

**Mheshimiwa Spika,** Deni kwa vituo vya kutolea huduma za Afya limefika kiasi cha **Shilingi bilioni 33.6** ikiwa ni ongezeko la **Shilingi bilioni 18.46** sawa na asilimia 122 ya deni la mwezi Juni, 2022 la **Shilingi bilioni 15.14.** Hali hiyo imesababisha deni la Miradi Misonge na Vituo vya kutolea huduma za Afya hadi mwezi Juni, 2023 kufikia kiasi cha **Shilingi bilioni 359**. Aidha, vituo vya kutolea huduma za Afya vilikuwa na madai ya bidhaa za Afya za kiasi cha **Shilingi bilioni 127.5**;

**(iii) Uzalishaji Mdogo wa Bidhaa za Afya Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umebainisha kuwepo kwa Uzalishaji mdogo wa bidhaa za Afya nchini. Hali hii imetokana na uchache wa Viwanda pamoja na kutokufanya kazi kikamilifu kwa baadhi ya viwanda vya bidhaa za Afya. Mfano wa viwanda hivyo ni kiwanda cha Dawa cha Arusha *(Tanzania Pharmaceutical Industries)* na kiwanda cha Dawa cha Keko *(Keko Pharmaceutical Industries)*. Changamoto hiyo husababisha utegemezi wa uagizaji wa bidhaa za Afya kutoka nje ambapo zaidi ya asilimia 80 ya bidhaa hizo huagizwa kutoka nje ya nchi;

(b) **Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba hadi kufikia Mwezi Juni, 2023, umebainisha masuala yafuatayo: -

(i) Katika Mwaka wa fedha 2022/23, Mamlaka ilisajili jumla ya bidhaa 1,263 za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi ikilinganishwa na bidhaa 1,228 ambazo zilisajiliwa Mwaka 2021/22, hili ni ongezeko la bidhaa 35 sawa na asilimia 3 ikilinganishwa na bidhaa zilizo sajiliwa Mwaka 2021/22. Kwa upande wa kusajili maeneo na kutoa vibali vya biashara ya

dawa, vifaa tiba na bidhaa nyongeza, jumla ya maeneo 1,350 yalisajiliwa;

(ii) Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imekuwa kitovu cha umahiri *(Centre of Excellence)* katika tathmini na usajili wa dawa barani Afrika na kuwa na maabara inayotumika kutoa mafunzo kwa mamlaka za udhibiti barani Afrika;

(iii) Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imepata cheti cha umahiri cha kiwango cha ISO 9001: 2015 katika mifumo ya utendaji ya udhibiti wa bidhaa na kuendelea kushikilia cheti hicho Mwaka hadi Mwaka. Vilevile, kupata ithibati ya ISO/IEC 17025: 2017 katika mifumo ya uchunguzi wa kimaabara ya maikrobailojia;

(iv) Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imepanua wigo wa huduma za maabara kwa kujenga maabara ya kisasa ya uchunguzi wa dawa na vitendanishi Kanda ya Ziwa – Mwanza na uchunguzi wa dawa za mitishamba na bidhaa za tumbaku Kanda ya kati Dodoma;

(v) Kuweka mfumo mahiri wa TEHAMA wa kupokea na kuchakata maombi ya usajili wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi (*Regulatory Information Management System – RIMS)*.

**Mheshimiwa Spika,** Imebainika kuna changamoto mbalimbali zinazoikabili Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ambazo huathiri utendaji na kusababisha Mamlaka hiyo kuwa na udhibiti usiotosha wa Dawa na Vifaa Tiba. Changamoto hizo ni: -

(i) Upungufu wa vifaa na rasilimali watu hususan wakaguzi kwa ajili ya udhibiti wa Dawa na Vifaa Tiba mipakani;

(ii) Uchepushaji wa dawa za Serikali kwenye maduka binafsi ya dawa; na

(iii) Kuongezeka kwa maduka mengi ambayo hayajasajiliwa na Baraza la Famasi na hivyo kuleta changamoto kubwa kwenye ukaguzi wa dawa zilizohifadhiwa na kuuzwa.

(c) **Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika,** Chimbuko la kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ni matokeo ya mabadiliko katika Sekta ya Afya ambayo yalianza miaka ya 1990. Katika kufuatilia utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yalibainika yafuatayo: -

(i) Mfuko umesajili wanachama wapya 634,464 sawa na asilimia 89 ya lengo. Idadi hiyo ya wanachama waliosajiliwa, imewezesha Mfuko kuwa na wanachama wachangiaji 1,368,314 na wanufaika 4,978,856 sawa na asilimia 8 ya Watanzania wote;

(ii) Ukusanyaji wa mapato umeimarika kufikia **Shilingi bilioni 706.25** ukilinganisha na **Shilingi bilioni 624.49** zilizokusanywa mwaka 2021/22;

(iii) Mgawanyiko wa mapato unaonesha michango ya wanachama ni asilimia 91 ya mapato yote ya Mfuko, mapato yatokanayo na uwekezaji ni asilimia 8 na Mapato Mengineyo ni asilimia 1. Kwa upande wa michango ya wanachama, lengo ilikuwa kukusanya **Shilingi bilioni 637.02** ambapo jumla ya **shilingi bilioni 643.39** zilikusanywa sawa na asilimia 101 ya lengo;

(iv) Mfuko umesajili vituo vya matibabu 8,482 nchini kote ambapo kati ya vituo hivyo, vituo vya Serikali ni 6,594 (70%), vituo vya Mashirika ya Dini ni 829 (9%), na vituo vya watu binafsi ni 1,763 (21%);

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio ambayo NHIF imeyapata bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiuendeshaji kama ifuatavyo: -

(i) Kukosa uhiari wa kujiunga kwa baadhi ya makundi ya wananchi hususani walioko kwenye sekta isiyo rasmi ambayo wengi wao hujiunga wakiwa wagonjwa;

(ii) Kukosekana kwa mfumo wa kielektroniki unaounganisha taarifa za wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma,

kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali za Rufaa na Taifa *(Medical report portability)*;

(iii) Kukosekana kwa mwongozo wa usimamizi wa kliniki binafsi za Kibingwa (Polyclinics) unaokwamisha usajili wa vituo hivyo katika Mfuko wa Bima ya Afya; na

(iv) Kukosekana kwa kipengele cha Bima ya Afya kwa wanafunzi katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini uwepo wa changamoto nyingine inayokabili uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambapo hivi karibuni kumekuwa na mvutano kati yake na Sekta Binafsi ya Afya jambo lililosababisha Waziri wa Afya kuunda Tume kwa ajili ya kuchunguza na kuja na mapendekezo yatakayosaidia kuondoa mvutano uliopo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee na kwa niaba ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, tunatoa shukrani za dhati kwa kutoa kibali na kuruhusu Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kuitisha vikao ambavyo vilihusisha Wizara ya AfyaMfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) pamoja na wawakilishi wa Sekta binafsi ya Afya ambao ni Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Chama cha Wamiliki wa Vituo vya Afya Binafsi (APHFTA) na Tume ya Huduma za Jamii ya Kikristo (CSSC). Lengo la vikao hivyo ni kupata uelewa kuhusu changamoto iliyopo na hatimae Kamati iweze kuishauri Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao hivyo, Kamati imebaini ushirikiano kati ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Sekta Binafsi ya Afya umekuwa ukisuasua kutokana na mambo yafuatayo: -

(i) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura Namba 395 kutokutambua uwepo wa Sekta binafsi ya Afya kama mnufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;

(ii) Kutoruhusu sekta binafsi za Afya kutumia mfumo wa kuchangia huduma za Afya *(Co-payment)* kwa wanufaika

wa NHIF, wakati mfumo huo unaruhusiwa kwa hospitali za umma tu;

(iii) Kukosekana kwa chombo huru na cha kudumu kinachoratibu na kusimamia bei za huduma za Afya.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia changamoto hizo, Kamati inaona ipo haja ya Serikali kutafuta ufumbuzi wa mvutano huu kwa haraka ili wananchi waweze kuendelea kupata huduma za Afya bora katika vituo vya Afya wanavyopendelea.

(d) **Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC)**

**Mheshimiwa Spika**, Chimbuko la kuanzishwa kwa Taasisi ya Chakula na Lishe lilikuwa ni kuunda chombo mahsusi cha kitaifa cha kuwaunganisha wataalam wa shughuli za ugani na wanasayansi, pamoja na viongozi wa kitaifa katika mapambano dhidi ya utapiamlo nchini. Kwa mujibu wa sheria (Ibara ya 4 ya Sheria ya Chakula na Lishe Sura 109),

**Mheshimiwa Spika**, Wajibu na majukumu ya Taasisi hii ilikuwa ni pamoja na kupanga na kuanzisha programu za chakula na lishe, kutathmini na kufanya marekebisho ya programu za chakula na lishe, kufanya tafiti zinazohusiana na chakula na lishe, kutoa huduma na mafunzo katika masuala yote yanayohusiana na chakula na lishe kwa Taasisi mbalimbali na jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile majukumu mengine ya Taasisi yalikuwa ni kuishauri Serikali, Shule na Wadau mbalimbali kuhusu masuala ya chakula na lishe, kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa chakula bora na athari za utapiamlo, kushawishi umma kutumia mbinu zinazoshauriwa na Taasisi katika kupambana na utapiamlo, kushirikiana na Wizara na Ofisi za Mikoa na Halmashauri zinazoshughulikia mipango ya maendeleo ili kuhakikisha kwamba mipango ya kitaifa ya maendeleo inajumuisha malengo ya chakula na lishe, kushirikiana na wazalishaji, watengenezaji/wasindikaji na wasambazaji wa chakula ili kuhakikisha kwamba chakula kinachouzwa nchini na kusafirishwa nje ya nchi ni bora na salama pamoja na kutoa matokeo na tafsiri ya tafiti zilizofanywa na Taasisi zinazohusu masuala ya chakula na lishe kwa Serikali na wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo mwezi Desemba 2023, Serikali kwa kupitia Msajili wa Hazina ilitangaza kufuta Taasisi hii. Kamati inaona kufutwa kwa Taasisi hii kunaweza kusababisha nchi kukosa chombo mahsusi kilichojikita katika tafiti za lishe na hivyo kusababisha jamii isiyo na lishe bora ikiwa ni pamoja na kuchochea ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

(e) **Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu NIMR**

**Mheshimiwa Spika**, NIMR imeendelea kutekeleza majukumu yake ya utafiti na maendeleo katika sekta ya Afya na kuhamasisha matumizi ya matokeo ya tafiti hizo.

Katika kufuatilia utendaji wa NIMR mambo yaliyobainika ni:-

i) Tafiti mbalimbali zenye mchango mkubwa katika Sera na Miongozo ya kuimarisha mfumo wa Afya zimefanyika. Mfano, utafiti wa kufuatilia hali ya maambukizi ya Malaria nchini kwa kutumia mbinu za vinasaba katika mikoa 13 ya Tanzania Bara. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa tatizo la vimelea vya malaria kubadilika na kuathiri ufanisi wa kipimo cha MRDT halipo nchini. Hivyo basi, vipimo vya MRDT bado vitaendelea kuwa na tija;

ii) Utafiti kuhusu idadi ya dozi ya chanjo ya Saratani ya Shingo ya Kizazi (*Human Papilloma Virus- (HPV*). Matokeo ya utafiti yameonesha ufanisi wa dozi moja ya chanjo dhidi ya HPV ina ufanisi kama dozi mbili au tatu. Matokeo haya yatasaidia kupunguza gharama za chanjo dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi.

**Mheshimiwa Spika**, Ni muhimu kuzingatia na kuwekeza zaidi katika tafiti zenye tija na zenye kuleta ustawi katika jamii.

(f) **Kituo cha Tafiti za Tiba Asili NIMR-Mabibo**

**Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Utafiti wa Tiba Asili Mabibo kilitambulika rasmi tarehe 04 Julai 2022 baada ya kuidhiinishwa kwa Muundo mpya wa Taasisi hivyo kuwa kituo cha saba cha NIMR chenye jukumu la kushughulikia na kusimamia tafiti za tiba asili nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Imebainika kuwa, kituo kina jumla ya dawa za tiba asili nane ambazo zipo katika majaribio kwa binadamu. Dawa hizo ni WARBUGISTAT inayotibu magonjwa nyemelezi, NIMREVIT kinywaji lishe kwa ajili ya kuimarisha Afya, NIMREGENIN kwa ajili ya tezi dume, TANGESHA kwa ajili ya seli mundu, PERSIVIN inayotumika kuondosha uvimbe hasa kwa wagonjwa ya saratani, TMS 2001 kwa ajili ya ugonjwa wa malaria na NIMRCAF iliyosaidia jamii kupambana na UVIKO-19.

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa ni kufanya utafiti wa kubaini na kuhifadhi kumbukumbu ya namna tiba asili ya kitanzania inavyofanywa (*Anthropological study)*. Hii ni miongoni mwa tafiti chache kuwahi kufanyika barani Afrika na kwa mara ya kwanza kufanywa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile, uchunguzi wa usalama na ufanisi wa dawa asili dhidi ya saratani ya matiti, shingo ya kizazi, ubongo na tezi dume katika hospitali ya Saratani Ocean Road na Hospitali ya Taifa Muhimbili unaendelea kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Mabibo kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa watumishi, rasilimali fedha kwa ajili ya kukamilisha kiwanda na uhitaji wa eneo la kuhifadhia malighafi. Changamoto nyingine zinazoikabili NIMR ni pamoja na tafiti nyingi kutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za Wafadhili hali hii inasababisha tafiti hizo kufuata matakwa ya wafadhili wanaotoa fedha bila kujali vipaumbele vya nchi katika kutatua changamoto za Afya.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, pamoja na changamoto hizo, ikiwa nchi yetu itawekeza vya kutosha kwenye tafiti hizi zitaweka misingi ya kumbukumbu ya falsafa ya tiba asili ya Kitanzania.

(g) **Hali ya Magonjwa Yasiyoambukiza**

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za Mwaka 2018 zinaonesha kuwa magonjwa yasiyoambukiza yanachangia asilimia 71 ya vifo vyote duniani. Aidha, zaidi ya asilimia 85 ya vifo vyote duniani vinavyotokana na magonjwa yasiyoambukiza hutokea kwa watu walio kati ya umri wa miaka thelathini hadi sabini katika nchi zinazoendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Kumekuwapo na ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ulimwenguni kote ikiwemo Afrika. Ongezeko hili limechochewa na mabadiliko ya mtindo wa maisha usiobora ambapo tafiti zinaonesha uwepo wa matumizi makubwa ya tumbaku asilimia 15.9, ulaji usiofaa wa vyakula asilimia 97, matumizi ya pombe kupita kiasi asilimia 29.4 pamoja na kutoshughulisha mwili (tabia bwete) asilimia 5.9.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa Serikali imechukuwa hatua mbalimbali katika kukabiliana na magonjwa haya ambapo kwa sasa inatekeleza Mpango Mkakati wa tatu wa kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza (*"The National Strategic Plan for Prevention and Control of NonCommunicable Diseases)* wa Mwaka 2021 – 2026. Kamati inaona ipo haja kubwa kwa Serikali kuongeza juhudi na jitihada katika kudhibiti ongezeko la magonjwa haya sugu yasiyoambukiza kwa kutoa elimu ya namna ya kuepuka au kuzuia magonjwa hayo.

(h) **Vifo vya Mama Wajawazito na Watoto wenye umri chini ya siku Ishirini na Nane**

**Mheshimiwa Spika**, Malengo ya dunia ya Mwaka 2030 ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 70 kwa kila vizazi hai 100,000 na vifo vya watoto wachanga kufikia 12 kwa kila vizazi hai 1000.

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu za utafiti wa demografia na hali ya Afya ya Mwaka 2022 *(Tanzania Demographic Health Survey – TDHS*) inaonesha vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kwa zaidi ya asilimia 80 vikiwa chini ya kiwango cha vifo 150 kwa kila vizazi hai 100,000. Taarifa ya TDHS ya mwaka 2022 na Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaashiria kwamba kama Tanzania itaendelea na kasi ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, basi itaweza kufikia malengo endelevu ya dunia ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 70 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo 2030.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa vifo vya watoto wachanga takwimu zinaonesha kuwa, Mwaka 2022 kulikua na vifo 24 kwa kila vizazi hai 1000, hali inayoashiria kutofanya vizuri katika eneo hili hasa ikizingatiwa kwamba lengo la Malengo ya Maendeleo Endelelevu *(Sustainable Development Goals-SDG's)* kiashiria

*(target)* namba 3.2 inayotaka angalau vifo 12 kwa kila vizazi hai 1000.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa hali ya vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano, takwimu zinaonesha kuendelea kupungua kwa kiasi kikubwa kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1000 Mwaka 2015/16, na kufika vifo 43 kwa kila vizazi 1000 katika Mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zinaonesha sababu ambazo huchangia kwa asilimia 80 vifo vya watoto wachanga ni homa kali, kuharisha, nimonia na kuzaliwa kabla ya wakati. Aidha, sababu ambazo huchangia kwa kiasi cha asilimia zaidi ya 80 ya vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano ni kuzaliwa na uzito pungufu, kushindwa kupumua baada ya kuzaliwa na maambukizi ya bakteria.

**Mheshimiwa Spika**, Ni muhimu Serikali kuendelea na jitihada mbalimbali za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga kwa kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya huduma za uzazi wa mpango, uwepo wa watoa huduma wenye ujuzi, upatikanaji wa huduma za dharura za uzazi na watoto wachanga na mazingira wezeshi kama vile siasa, sera, vifaa na vifaa tiba na motisha pamoja na wataalam wa kutosha.

### 2.3.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za Utendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* zilibainisha mambo mbalimbali kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI. Uchambuzi wa Taarifa hizo umebainisha yafuatayo: -

#### (a) Hali ya VVU na UKIMWI Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 1 Disemba, 2023 ilizinduliwa Taarifa ya Matokeo ya Utafiti wa athari za UKIMWI Tanzania wa Mwaka 2022/2023 *(Tanzania HIV Impact Survey-THIS)* ambapo matokeo ya utafiti yameonesha mafanikio yaliyofikiwa na Taifa katika mwitikio dhidi ya UKIMWI kuwa ni:-

(i) Kuvuka lengo kwenye utekelezaji wa shabaha ya asilimia 95 ya pili inayohusu tiba kwa WAVIU waliotambua hali zao

ambapo tafiti inaonesha imefika asilimia 97 ya WAVIU wapo kwenye tiba. Aidha, shabaha ya tatu inayohusu kufubaza virusi kwa WAVIU wanaoendeleo na tiba, matokeo yameonesha kuwa asilimia 94 ya WIVIU wapo kwenye tiba ya kufubaza. Hata hivyo, Taifa linatakiwa kuongeza nguvu na jitihada zaidi katika kufikia shabaha ya kwanza inayohusu watu wote wanaoishi na maambukizi ya VVU kupima na kujua hali zao za maambukizi ambapo matokeo yanaonesha kufika asilimia 82;

(ii) Kupungua kwa kiwango cha ushamiri wa VVU kutoka asilimia 4.7 Mwaka 2026/17 hadi asilimia 4.4 Mwaka 2022/2023;

(iii) Kupungua kwa maambukizi mapya kutoka watu 87,013 Mwaka 2016/17 hadi watu 60,000 Mwaka 2022/2023;

**(b) Mkakati wa Kutokomeza Unyanyapaa kwa WAVIU**

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya unyanyapaa inahusisha imani na mitazamo ambayo kwa kiwango kikubwa hudhalilisha utu wa mtu au kikundi cha watu. Imebainika kuwa baadhi ya WAVIU wameacha kutafuta au kuhudhuria kwenye huduma za Afya kwasababu tu ya kuhofia kunyanyapaliwa au kubaguliwa. Hivyo, unyanyapaa na ubaguzi vimekuwa ni miongoni mwa vichocheo vya maambukizi ya VVU na kusababisha hofu na usiri miongoni mwa watu juu ya kupima VVU na kuweka wazi hali za Afya.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Taarifa ya Utafiti wa Unyanyapaa kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, Tanzania Bara uliofanyika kati ya Februari 2020 na Septemba 2021, hali ya unyanyapaa na ubaguzi uko juu zaidi Mkoa wa Kilimanjaro asilimia 19.5 ikifuatiwa na Tanga asilimia 10.5. Unyanyapaa upo chini kwa Mkoa wa Iringa asilimia 1.4 na Mkoa wa Mbeya ni asilimia 2.8.

**Mheshimiwa Spika,** Katika juhudi za kushughulikia sababu kuu za unyanyapaa na ubaguzi, umeandaliwa Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Unyanyapaa na Ubaguzi unaohusiana na VVU na UKIMWI wa Mwaka 2022-2026. Hivyo, kwa kutekeleza Mkakati huu kutawezesha kufikia lengo la kuwa na unyanyapaa sifuri ifikapo Mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia utekelezaji wa mikakati ya kutokomeza unyanyapa kwa WAVIU pamoja na Mikakati mingine inayolenga kupunguza maambukizi ya UKIMWI nchini, unyanyapaa umepungua kitaifa kutoka asilimia 28 Mwaka 2013 hadi asilimia 5.5 Mwaka 2021.

**(c) Programu ya Wasichana Balehe na Wanawake Vijana**

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu za viashiria vya Virusi vya UKIMWI Tanzania kwa Mwaka 2016/2017 zinaonesha kuwa asilimia 40 ya maambukizi mapya ya UKIMWI yanatoka kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 na kati yao asilimia 80 ni vijana wa kike (wasichana balehe na wanawake vijana).

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutatua changamoto zinazowakabili wasichana balehe hasa wanaotoka katika kaya masikini, kumeanzishwa programu ya wasichana balehe na wanawake vijana katika Mikoa na Halmashauri ambazo ziliainishwa kwa kuzingatia vigezo vya idadi ya mimba za utotoni, kuacha shule kabla ya kuhitimu, ukatili wa kijinsia, maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI, umasikini na ndoa za utotoni. Kwa kupitia mpango huu, jumla ya Halmashauri 42 zimefikiwa na utekelezaji wa afua jumuishi katika miradi ya *DREAMS (Determined, Resilient, Empowerment, AIDS Free, Mentored and Safe)*.

**Mheshimiwa Spika**, Tangu kuanzishwa kwa mradi huu Mwaka 2016 hadi 2023 wasichana balehe na wanawake vijana wapatao 600,000 wamefikiwa na huduma jumuishi ikiwemo kupatiwa mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya ujasiriamali, vifaa vya kufanyia kazi kama vile cherehani, zana za kilimo, mashine ya kuchakata zao la kokoa na mashine ya kutengeneza sabuni. Aidha, wasichana balehe na wanawake vijana wamepatiwa mafunzo ya kujikinga na VVU, matumizi sahihi na endelevu ya kondomu, kupinga unyanyapaa na ukatili wa kijinsia pamoja malezi na makuzi. Miradi hii yote inatekelezwa kupitia afua jumuishi za kitabibu, mabadiliko ya tabia na kimfumo.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwa na mafanikio na kazi nzuri za vikundi katika Halmashauri za Manispaa ya Shinyanga na Kahama. Kamati ilibaini baadhi ya changamoto zinazowakabili wasichana balehe na wanawake vijana ni vikundi kukosa mitaji

ya kutosha pamoja na kukosa sifa za kusajiliwa kutokana na kutokuwa na vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho vya Taifa.

**(d) Vituo vya Maarifa katika Vituo vya Malori ya Masafa Marefu**

**Mheshimiwa Spika**, Vituo vya maarifa vya kudhibiti UKIMWI ni moja ya programu za kimkakati yenye lengo la kusaidia Halmashauri kuendelea kutekeleza mwitiko wa afua mbalimbali za udhibiti wa VVU na UKIMWI kwa jamii kutokana na kuwepo kwa mwingiliano mkubwa baina ya wananchi wa maeneo hatarishi, wasafiri, madereva, wasaidizi wa madereva, wafanyabiashara na wasafirishaji mizigo kwa kutumia Magari ya masafa marefu. Hivyo vimeanzishwa vituo vya maarifa nchini vikilenga kutoa huduma stahiki za Virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwa madereva wa masafa marefu, wasaidizi wao na jamii zinazozunguka maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufika mwezi Agosti, 2023 vimejengwa vituo kumi na tano (15) katika Mikoa kumi na tatu (13) ambayo ni Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Tanga, Singida, Geita, Shinyanga, Iringa, Mbeya, Songwe, Kigoma na Kagera.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwepo kwa ongezeko kubwa la wananchi waliojitokeza kuhitaji huduma na hivyo kusababisha kituo kuongeza huduma za ziada kama upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza ambayo ni mbali na lengo kuu la kuanzishwa kwa vituo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mafanikio mengine ya vituo hivi ni kuundwa kwa vikundi vya utoaji elimu kwa jamii, kusajiliwa kutoa huduma ya tiba na matunzo (CTC) na kuongezeka kwa idadi ya wateja hasa akina mama katika kliniki ya Huduma za Mama na Mtoto.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya mafanikio hayo, kumekuwepo na changamoto zinazokabili vituo vya maarifa ikiwa ni pamoja na baadhi ya Halmashauri kubadili matumizi ya vituo vya maarifa, uelewa mdogo wa madereva wa masafa marefu na wasaidizi wao kutambua umuhimu wa kutumia huduma zinazotolewa kwenye vituo vya maarifa. Aidha, imebainika katika baadhi ya vituo hususan kituo cha Manyoni-Singida, madereva wa malori wanatozwa gharama wanapoegesha magari katika eneo la kituo

kwa ajili ya kupata huduma jambo ambalo husababisha madereva kutofika eneo la kituo na hivyo kuathiri lengo la programu.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imeeleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati pamoja na kubainisha mafanikio na changamoto kama zilivyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Msingi wa Taarifa hii pamoja na ushauri unaotolewa umezingatia nyenzo muhimu kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi 2020 – 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2021/22 – 2025/26 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (lengo namba 3).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za Afya nchini. Hata hivyo, zipo changamoto mbalimbali zilizobainika ambazo utatuzi wake utasaidia kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za Afya. Kwa sababu hiyo, naomba kutoa mapendekezo ambayo Bunge lako Tukufu litayaazimia kwa ajili ya utekelezaji.

### 3.2 Mapendekezo kuhusu Wizara ya Afya

#### 3.2.1 Kutokutolewa kwa Fedha za Miradi ya Maendeleo

**KWA KUWA**, Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, zimetolewa kwa kiwango kidogo, ambapo hadi mwezi Disemba 2023, imetolewa asilimia 26 tu;

**NA KWA KUWA**, Kiasi hicho kidogo cha fedha pasipokuzingatia wakati kitaathiri utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo iliyokusudiwa;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itenge fedha za kutosha na pia kuhakikisha fedha hizo zinatolewa zote na kwa

wakati ili miradi ya maendeleo itekelezwe katika muda uliokusudiwa.

### 3.2.2 Upungufu wa Watumishi

**KWA KUWA**, Sekta ya Afya inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini kwa kiwango cha **asilimia 64**, jambo ambalo ni kinyume kabisa na tamko la Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inayotaka kuwepo kwa watumishi wa kutosha wenye ujuzi katika taaluma mbalimbali katika ngazi zote za kutolea huduma,

**NA KWA KUWA**, Upungufu huu wa watumishi umekuwa ukiathiri utoaji wa huduma bora za Afya,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazima kwamba,
i. Serikali itoe kipaumbele cha ajira kwenye Sekta hii muhimu kwa ili huduma za Afya katika ngazi mbalimbali ziweze kupatikana kwa wakati na katika ubora unaostahili; na ii. Kipaumbele cha ajira kitolewe kwa wanaojitolea kutoa huduma za Afya katika Hospitali mbalimbali nchini.

### 3.2.3 Ukosefu wa Mtaji Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

**KWA KUWA**, Bohari Kuu ya Dawa imekuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa mtaji kiasi cha **Shilingi bilioni 561.5,**

**NA KWA KUWA**, Kutokupatikana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na pia kushindwa kununua mahitaji yote ya bidhaa za Afya, hivyo kuendelea kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za Afya;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itoe mtaji wa **Shilingi bilioni 561.5** kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa bidhaa za Afya, kusaidia uwekezaji kwenye viwanda na kuongeza uwezo wa kuhifadhi kwa kujenga maghala ya kutosha.

### 3.2.4 Uwekezaji Mdogo wa Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba

**KWA KUWA,** Kumekuwa na uchache wa viwanda vya kuzalisha vifaa tiba pamoja na dawa nchini,

**NA KWA KUWA**, Kutokuwa na viwanda vya kutosha vya uzalishaji wa vifaa tiba na dawa kunasababisha gharama ya bidhaa hizo kuwa ghali na changamoto ya upatikanaji wa dawa muhimu,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye yafuatayo: -

(i) Kuweka mikakati thabiti ya kushirikisha sekta binafsi *(Public Private Partinership-PPP)* na kurahisisha uwekezaji wa viwanda vya dawa pamoja na vifaa tiba nchini ili kukidhi soko la ndani na nje;

(ii) Kufufua Kiwanda cha Dawa cha Arusha *(Tanzania Pharmaceutical Industries)* na kuongeza uzalishaji katika Kiwanda cha Dawa cha Keko (*Keko Pharmaceutical Industries*) ambacho Serikali imewekeza kwa asilimia 70; na

(iii) Bohari Kuu ya Dawa ifanye mchakato wa haraka wa uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na pamba ili kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi kwa kuwa malighafi ya bidhaa hizo (yaani zao la Pamba) inapatikana hapa nchini.

### 3.2.5 Kurejesha Jukumu ya Udhibiti wa Chakula na Vipodozi TMDA

**KWA KUWA**, Mnamo mwaka 2019, Serikali ilipeleka jukumu ya udhibiti wa Chakula na Vipodozi katika Shirika la Viwango Tanzania *(Tanzania Bureau of Standards - TBS)* kupitia marekebisho ya Sheria Sura Namba 219,

**NA KWA KUWA**, Chakula, Dawa na Vipodozi vinauhusiano mkubwa hivyo, kupelekwa kwa jukumu hilo chini ya TBS ambayo ni Taasisi isiyohusiana na masuala ya Afya kunaondoa dhana ya udhibiti unaozingatia athari za kiafya

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali irejeshe TMDA udhibiti wa chakula na vipodozi kutoka Shirika la Viwango

Tanzania (TBS) kwani bidhaa hizo zinahusiana moja kwa moja na Afya ya jamii na endapo udhibiti wake hautazingatia usalama wa Afya ya jamii itasababisha athari mbaya kwa jamii;

### 3.2.6 Changamoto za Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**KWA KUWA**, Imebainika kuwepo kwa upungufu katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,

**NA KWA KUWA**, Upungufu huo unasababisha athari kubwa katika uratibu na usimamizi wa sekta binafsi ya Afya, kwani Sheria ya NHIF ilitungwa mahsusi kwa ajili ya kuhudumia sekta ya umma,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ianze mchakato wa kurekebisha Sheria ya NHIF, Sura ya Namba 395 ili kuitambua Sekta Binafsi ya Afya ambayo ni mdau muhimu wa Afya;

(ii) Serikali ianzishe chombo huru mahsusi na cha kudumu kitakachoratibu na kusimamia bei za huduma za Afya ambacho kitajumuisha wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta binafsi;

(iii) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) iwezeshwe kisheria kwa kuwekewa Kanuni chini ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuipa mamlaka ya kudhibiti utoaji wa huduma za Bima ya Afya nchini;

(iv) Vituo vya Afya binafsi viruhusiwe kuwa na utaratibu wa mgonjwa kuchangia huduma *(co-payment)* ambapo wamiliki wa kadi za NHIF watatakiwa kulipa kwa pesa taslimu gharama zinazozidi kiwango cha kitita kinachochangiwa na NHIF;

(v) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uimarishe mifumo ya TEHAMA ili kukabiliana na changamoto ya ucheleweshaji wa malipo na kudhibiti udanganyifu;

(vi) Kitita cha bei kinachotumika sasa kiendelee kutumika katika kipindi cha mpito, mpaka kitita kipya cha bei

kitakachozingatia maoni ya Wadau wote wa Sekta ya Afya kutoka sekta ya umma na binafsi;

(vii) NHIF ianzishe Kamati ya wataalam ambao watakuwa wanapitia malalamiko ya kitaaluma yanayowasilishwa na vituo vya kutolea huduma au wataalam kuhusu bima ya Afya; na

### 3.2.7 Kukosekana kwa Mwongozo wa Bima ya Afya kwa Watoto Shuleni

**KWA KUWA,** Hakuna mwongozo wa kufanikisha usajili wa watoto katika huduma za bima ya afya shuleni kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya-NHIF,

**NA KWA KUWA**, Kukosekana kwa mwongozo huo kunadhoofisha mwitikio wa usajili wa watoto katika huduma za bima ya Afya,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu iweke mwongozo wa ulazima kwa wanafunzi wote kusajiliwa katika huduma za bima ya Afya kupitia shule; na

(ii) Serikali iweke mfumo na utaratibu wezeshi wa Bima kwa watoto ambao wapo chini ya miaka mitano ambao hawajaanza shule.

### 3.2.8 Nia ya Kufutwa kwa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC)

**KWA KUWA,** Serikali kupitia Msajili wa Hazina ilitangaza nia ya kuifuta Taasisi ya Chakula na Lishe ambayo kimsingi iliundwa kwa lengo la kusaidia Serikali kutatua changamoto ya lishe duni katika jamii na kuwa na mfumo wa kitaifa wa taarifa kuhusu tafiti mbalimbali za lishe,

**NA KWA KUWA**, Endepo kufutwa kwa Taasisi hii, kunasababisha nchi kukosa chombo muhimu mahsusi kinachojikita katika kusimamia tafiti za masuala ya lishe jambo ambalo linaweza kusababisha kuwa na jamii isiyo na lishe bora,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali kuona umuhimu wa kutoifuta Taasisi ya Chakula na Lishe kwani ni chombo mahsusi kinachoshughulikia na kusimamia masuala yote ya lishe nchini; na

(ii) Tafiti zaidi zifanyike kujua sababu za udumavu uliokithiri katika mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula kama Iringa, Njombe na Rukwa.

**3.2.9 Changamoto ya Ugunduzi wa Kifua Kikuu**

**KWA KUWA**, Takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi thelathini (30) zenye maambukizi makubwa ya ugonjwa wa kifua kikuu (TB) na nchi hizi huchangia asilimia 87 ya wagonjwa wote duniani;

**NA KWA KUWA**, Ugonjwa huu huathiri Taifa kwa kupunguza nguvu kazi kwani takwimu za Mwaka 2022 zilizotolewa na Shirika la Afya duniani (WHO) zinaonesha Tanzania ilikadiriwa kuwa na idadi ya vifo 25,800 vilivyosababishwa na ugonjwa kifua kikuu;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iimarishe mfumo wa ugunduzi wa wagonjwa wa kufua kikuu katika jamii kwa kushirikisha wahudumu wa Afya ngazi ya jamii;

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa uhakika wa vitendanishi kwa ajili ya kufanyia uchunguzi sampuli za makohozi kwa wahisiwa wa ugonjwa wa Kifua Kikuu katika Hospitali za Halmashauri kwani imeonekana sampuli zinakaa zaidi ya siku saba bila kufanyiwa uchunguzi kutokana na ukosefu wa vitendanishi; na

(iii) Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusu maambukizi, athari na matibabu ya Kifua Kikuu kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile Redio, Televisheni, Magazeti na mitandao ya kijamii.

### 3.2.10 Kutengwa kwa Kiasi Kidogo cha Fedha za Ndani kwa ajili ya Tafiti

**KWA KUWA**, Kumekuwa na uwekezaji mdogo wa fedha za ndani kwenye masuala ya tafiti,

**NA KWA KUWA,** Kutegemea wafadhili kumekuwa kukiathiri utendaji wa NIMR kwani tafiti nyingi zinazofanywa zinakuwa zikilenga matakwa ya wafadhili wanaotoa fedha hizo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iweke mpango mkakati wa kutenga fedha kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya kufanya tafiti nyingi zaidi kama ilivyoelezwa katika Sera ya Afya 2007 kwamba *''Serikali itaendelea kutenga fedha za kufanya tafiti muhimu za Afya…''*;

(ii) Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kufanya tafiti kuhusu ubora, athari na matumizi salama ya dawa za miti shamba;

(iii) NIMR iweke mfumo wa kuhifadhi tafiti zote zinazofanyika nchini kwa maslahi ya Taifa;

(iv) NIMR iwekeze katika tafiti zinazohusu magonjwa yasiyoambukiza kwa kuwa magonjwa hayo kwa sasa yanachangia asilimia kubwa zaidi ya vifo vya Watanzania.

### 3.2.11 Kukosekana kwa Udhibiti wa Dawa Asili

**KWA KUWA**, Kumekuwa na ongezeko la uvumbuzi na matumizi ya dawa ya asili zinazouzwa maeneo mbalimbali nchini bila kuzingatia utaratibu, ubora, ufanisi na athari hasi zinazoweza kutokana na huduma hiyo;

**NA KWA KUWA**, Kuongezeka kwa matumizi ya tiba hizi pasipokuwa na usimamizi na tafiti za kutosha kunaweza kuwa na athari katika Afya za wananchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali kuimarisha mfumo wa usajili wa dawa asili/mbadala na kuwatambua watoa huduma wa tiba asili/mbadala kwa kuwapa ithibati *(Accreditation)* ili kuwapa wananchi uhakika wakati wa kutumia huduma hizo;

(ii) Kuweka mikakati na juhudi za kuzuia matangazo ya tiba hizi ambayo hayana kibali na namba ya usajili ili kuwapa wananchi uhakika wa watoa huduma wa tiba asili/ mbadala;

(iii) Kufanya marekebisho ya gharama za usajili wa dawa za tiba asili/mbadala ili ziwe gharama stahimilivu ambazo zitasaidia kutoa hamasa kwa wengi kusajili dawa zao; na

(iv) Kuwekeza zaidi kwenye tafiti mbalimbali za dawa za tiba asili/mbadala na kuweka kumbukumbu ya tafiti hizo kwa ajili ya matumizi ya sasa na ya vizazi vijavyo.

**3.2.12 Ongezeko la Magonjwa ya Afya ya Akili**

**KWA KUWA,** Kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa ya Afya ya akili nchini,

**NA KWA KUWA,** Ongezeko hilo linachochea kufanyika kwa vitendo vya ukatili vinavyosababisha ulemavu na vifo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iimarishe upatikanaji wa huduma za Afya ya akili nchini;

(ii) Kuhakikisha madawati ya ushauri nasaha yanaboreshwa na kutoa elimu inayohusu Afya ya akili; na

(iii) Kuongeza watalaam wa Afya ya akili ili kukabiliana na ongezeko kubwa la mogonjwa hayo.

**3.2.13 Kutokutekelezwa Vema kwa Sera ya Matibabu Bure kwa Mama na Mtoto**

**KWA KUWA**, Wananchi wameendelea kulalamikia baadhi ya vituo vya Afya kutoza fedha za huduma za Afya kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, na kwamba utaratibu huo ni jambo ambalo ni kinyume na tamko la Sera ya Afya mwaka 2007 kifungu Na. 5.3.4, kipengele (c) sehemu ya (i*)"Serikali*

*kwa kushirikiana na sekta binafsi inayotoa huduma bila faida, na mashirika ya kimataifa, itaendelea kutoa huduma bila malipo kwa wanawake wajawazito, watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango na watoto wenye umri chini ya miaka mitano*",

**NA KWA KUWA,** Kutozwa fedha ili kupata huduma za Afya ya kwa wajawazito na watoto kunasababisha wasio na uwezo kushindwa kupata huduma stahiki, hivyo kusababisha vifo vya wajawazito na watoto wachanga,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali isimamie kikamilifu Sera ya utoaji wa huduma bila malipo kwa akina Mama wajawazito na Watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

**3.2.14 Ongezeko la Magonjwa yasiyoambukiza**

**KWA KUWA**, Bado wananchi wengi hawana uelewa juu ya namna ya kujikinga na athari kubwa za magonjwa yasiyoambukiza;

**NA KWA KUWA**, Asilimia kubwa ya magonjwa haya yamekuwa ni tishio kwa Afya za watanzania kwani yamekuwa yanachangia takribani **asilimia 33** ya vifo vyote nchini;

**NA KWA KUWA**, Magonjwa haya yanaligharimu Taifa fedha nyingi kutokana na gharama kubwa na ni miongoni mwa sababu kubwa ya kurudisha nyuma uchumi wa mtu mmoja mmoja, familia na Taifa kwa ujumla.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iweke mkazo wa elimu kwa jamii kuhusiana na ulaji na mtindo wa maisha ili jamii ifahamu sababu na madhara yanayotokana na magonjwa haya pamoja na umuhimu wa kujikinga;

(ii) Kuimarisha mfumo wa utoaji huduma kwa magonjwa yasiyoambukiza hadi ngazi ya msingi; na

(iii) Michezo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ikiwemo kukimbia mchakamchaka virudishwe ili kuwajenga kiafya na kiakili.

### 3.3 Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS)

### 3.3.1 Kutengwa kwa Kiasi kidogo cha Fedha za Ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI

**KWA KUWA**, Kiasi kinachotengwa cha fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa afua za UKIMWI ni kidogo, hivyo kufanya utekelezaji wa afua za UKIMWI nchini kutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za wafadhili,

**NA KWA KUWA**, Kutegemea fedha za wafadhili kwa kiasi kikubwa kunaliweka Taifa katika sintofahamu ikiwa wafadhili wataacha kutoa fedha hizo na hivyo Taifa kukosa uhakika wa fedha za mapambano endelevu dhidi ya VVU na ugonjwa wa UKIMWI,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ione umuhimu wa kuwa na mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutenga na kutoa fedha za ndani na kuzitoa kwa wakati; na

(ii) Kuimarisha Mfuko wa Mapambano dhidi ya UKIMWI na kuweka mipango madhubuti ya kupata vyanzo mahsusi vya mapato ya ndani vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya miradi inayolenga kudhibiti VVU na UKIMWI.

### 3.3.2 Kupitwa kwa Wakati kwa Sera ya UKIMWI

**KWA KUWA**, Imebainika kwamba Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 ni ya muda mrefu na imepitwa na wakati,

**NA KWA KUWA**, Sera hii kwasasa haiakisi hali halisi ya mazingira ya sasa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kwa kushirikiana na Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* ifanye mapitio ya Sera hii na kuihuisha iweze kuendana na mazingira yaliyopo sasa.

### 3.3.3 Usimamizi Duni wa Matumizi ya Vituo vya Maarifa kwa ajili ya Madereva wa Malori ya Masafa Marefu *(Roadside Wellness Centres)*

**KWA KUWA**, Kumekuwepo kwa usimamizi duni wa vituo vya maarifa kiasi cha baadhi ya vituo kubadilishwa matumizi yaliyokusudiwa,

**NA KWA KUWA**, Kutokuwa na matumizi sahihi ya vituo hivi hudhoofisha mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI pamoja na kurudisha nyuma jitihada za kutokomeza UKIMWI ifikapo Mwaka 2030 kama ilivyoelezwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (lengo namba 3.3),

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inasimamia matumizi sahihi na yaliyopangwa ya Vituo vya Maarifa vya Malori ya Masafa Marefu ili viweze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wahusika na kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

## 3.4 HITIMISHO

### 3.4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, Nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Mheshimiwa Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. | Stanslaus Haroon Nyongo, Mb | - M-kiti |
| 2. | Mhe. | Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, Mb | - M/M'kiti |
| 3. | Mhe. | Aysharose Ndagholi Matembe, Mb | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. | Bernadeta Kasabango Mushashu, Mb | " |
| 5. | Mhe. | Cecil David Mwambe, Mb | " |
| 6. | Mhe. | Christopher Olenyokie Ole Sendeka, Mb | " |
| 7. | Mhe. | Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb | " |
| 8. | Mhe. | Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mb | " |
| 9. | Mhe. | Elibariki Emmanuel Kingu, Mb | " |
| 10. | Mhe. | George Ranwell Mwenisongole, Mb | " |
| 11. | Mhe. | Kassim Hassan Haji, Mb | " |
| 12. | Mhe. | Hassan Seleman Mtenga, Mb | " |
| 13. | Mhe. | Josephine Johnson Genzabuke, Mb | " |
| 14. | Mhe. | Juliana Daniel Shonza, Mb | " |
| 15. | Mhe. | Khalifa Mohamed Issa, Mb | " |
| 16. | Mhe. | Mohamed Lujuo Monni, Mb | " |
| 17. | Mhe. | Mrisho Mashaka Gambo, Mb | " |
| 18. | Mhe. | Seif Salum Seif, Mb | " |
| 19. | Mhe. | Shamsia Azizi Mtamba, Mb | " |
| 20. | Mhe. | Zubeida Khamis Shaib, Mb | " |
| 21. | Mhe. | Agness Mathew Marwa, Mb | " |
| 22. | Mhe. | Jacquline Andrew Kainja, Mb | " |

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja nae namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, tunawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Hosiana John Mvunta na Ndg. Jairo Joseph Odero pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Gwivaha kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo Taarifa hii.

### 3.4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na

Masuala ya UKIMWI na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Stanslaus Haroon Nyongo, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**

12 Februari, 2024

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Hoja imeungwa mkono na nakushukuru sana.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. *(Makofi)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowekwa mezani asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya jumla; kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa Kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Taarifa hii ni kujulisha Bunge hali ya utekelezaji wa shughuli za umma katika sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Nazo ni Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo pamoja na Uvuvi. Lengo ni kulipa Bunge fursa ya

kuisimamia na kuishauri Serikali kwa Mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati hii ina Muundo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi na orodha za shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi, mafanikio na changamoto, maoni ya ujumla na mapendekezo na hitimisho na kutoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa Wizara;

(ii) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Kuchambua taarifa na utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2023/2024;

(iv) Kufuatilia wa Maazimio ya Bunge katika taarifa ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele (a) kinahusu sekta ya viwanda na biashara; sekta hii ina maazimio nane, kati ya hayo manne yametekelezwa kikamilifu na manne utekelezaji wake unaendelea. Kwa mfano, utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Liganga na Mchuchuma na Mradi wa Maganga Engaruka. Taarifa inaonesha kuwa Serikali inaendelea kutekeleza pendelezo hilo. Kwa hatua hiyo, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa shilingi bilioni 15.4 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi waliopisha mradi wa Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, Kamati inasisitiza kuwa bado kuna umuhimu wa Serikali kuhakikisha kwamba, suala la mwekezaji linafikia muafaka ili mradi huu uanze utekelezaji mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo ilikuwa na maazimio manne ambayo kwa kiasi kikubwa utekelezaji wake unaendelea. Kwa mfano, Azimio lililohusu kuongeza uzalishaji, usafirishaji na mauzo ya mazao ya bustani linaendelea kutekelezwa. Changamoto ya mashamba ya kilimo yakiwemo mashamba ya maua ya Arusha yaliyofungwa, imetatuliwa kwa kiasi kikubwa. Aidha, Serikali imeanzisha Mamlaka ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo itasimamia mazao ya bustani pamoja na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo na uvuvi ina maazimio nane ambayo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa mfano, Azimio linalohusu uimarishaji wa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa miradi linaendelea kutekelezwa. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini na tayari imeanzisha kitengo kipya cha ufuatiliaji wa tathmini ili kuimarisha utekelezaji na usimamizi wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kuanza kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwa kuanzisha muundo mpya wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kitakachosaidia kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 14 mpaka 19 Machi, 2023 Kamati ilitembelea Mikoa ya Lindi, Dar es Salaam na Pwani kukagua miradi katika sekta ya viwanda, biashara, kilimo, mifugo na uvuvi. Katika Ziara hiyo, Kamati ilibaini mafanikio na changamoto ambazo ziliwasilishwa Bungeni kupitia Taarifa ya Kwenye Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge matokeo ya mafanikio na changamoto kwa kila sekta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Viwanda na Biashara Kamati ilibaini mafanikio kama ilivyoelezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020. Kamati ilibaini changamoto katika Sekta ya Viwanda na Biashara mfano, mfumuko wa bei, upungufu wa sukari, upungufu wa malighafi za viwanda hususan

malighafi za uzalishaji wa mafuta ya kula na uwepo tozo nyingi za biashara zinazotozwa na mamlaka mbalimbali za Serikali. Kamati inatoa msisitizo kuwa changamoto hizi zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya kilimo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa Programu ya *BBT* ambayo inalenga kuwezesha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo na biashara ili kuwapa ajira, kuongeza uzalishaji na kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza mchango wa sekta ya kilimo kwenye Pato la Taifa na kuinua hali ya maisha ya jamii ya Watanzania na kukuza mchango wa sekta ya kilimo kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, Kamati ilibaini changamoto katika sekta ya kilimo. Mfano, upungufu wa mbolea inayozalishwa nchini, uhaba wa mbegu na fedha za miradi kutotolewa kwa wakati. Kamati inatoa msisitizo kuwa changamoto hizi zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo na Uvuvi imejikita kuleta mabadiliko makubwa na kisayansi kwa kuhimiza ufugaji wa kisasa wenye kuzingatia kinga, tiba na utafiti wa mifugo ili kuzalisha ajira nyingi hasa kwa vijana, kuinua mchango wa sekta katika Pato la Taifa na kuleta ustawi wa wananchi. Vilevile, kuhakikisha shughuli za uvuvi nchini zinaboreshwa, vitendo vya uvuvi haramu vinadhibitiwa ili kuwezesha upatikanaji wa samaki wenye ukubwa unaokubalika na kuongezeka kwa viwanda vya kuchakata samaki na hivyo kuongeza mauzo ya bidhaa za samaki nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa sekta inakabiliwa na changamoto ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi, kwa mfano Sera ya Mifugo ya mwaka 2006, imepitwa na wakati; pili, ushiriki mdogo wa wadau katika kuthibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi, hali inayosababisha kupungua kwa samaki na uharibifu wa mazalia ya samaki, upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa hususani katika maeneo ya vijiji; na tatu uhaba wa Maafisa Ugani wa Uvuvi pamoja na uhaba wa vifaranga bora na vyakula bora vya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2023 Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama yalivyoelezwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii. Kutokana na matokeo hayo, Kamati ina mtazamo na maoni ya jumla kama ifuatavyo: -

(i) Suala la baadhi ya vituo vya pamoja vya mipakani kukosa mashine za ukaguzi linahitaji kupatiwa ufumbuzi;

(ii) Mfumuko wa bei nchini unaogusa bidhaa muhimu kwa maisha ya watu unahitaji mikakati ya haraka na ya muda mrefu ya Serikali ili kudhibiti madhara yake kwa wananchi na kwa uchumi wa nchi;

(iii) Upungufu wa sukari nchini usipochukuliwa hatua za dharura na madhubuti utaendelea kuathiri maisha ya wananchi kinyume na matarajio yao;

(iv) Upungufu wa malighafi za uzalishaji wa mafuta ya kula unapaswa kushughulikiwa ili kusimamia urari wa fedha za kigeni nchini na kudhibiti ongezezeko la bei ya mafuta ya kula;

(v) Upatikanaji na matumizi ya viuatilifu nchini ni jambo linalostahili hatua madhubuti za Serikali ili kuimarisha usalama wa chakula, afya ya jamii na kukuza Pato la Taifa;

(vi) Changamoto ya uzalishaji wa mbegu nchini inaweza kutatuliwa kwa kuongeza uwezo wa Wakala wa Mbegu za Kilimo;

(vii) Upungufu wa mbolea nchini hauna budi kukabiliwa kwa juhudi za Serikali na kwa ushirikiano na sekta binafsi;

(viii) Tija ndogo katika sekta ya umwagiliaji inayotokana na miundombinu duni na wataalamu wachache ni vyema ikatatuliwa na Serikali ili kuongeza uzalishaji katika Sekta ya Kilimo;

(ix) Tija, ufanisi na manufaa ya ushirika nchini vinaweza kuimarika kwa kufanya maboresho ya sheria na sera zinazosimamia masuala ya Ushirika;

(x) Hasara inayosababishwa na Wakandarasi na Washauri Elekezi wenye uwezo mdogo inapaswa kuepukwa kwa kuzingatia taratibu stahiki za upatikanaji wa wataalamu na Washauri Elekezi;

(xi) Changamoto za kuchelewa kutofika na tofauti ya bei ya mbolea nchini, zinahitaji ufumbuzi wa haraka;

(xii) Malalamiko ya wananchi kuhusu sekta ya uvuvi yanayotokana na hatua za Serikali kudhibiti uvuvi usiozingatia uendelevu yanastahili kufanyiwa kazi ikiwemo kujenga ufahamu kuhusu ufugaji wa samaki na kushughulikia kero na usumbufu wa tozo mbalimbali kwa shughuli za uvuvi;

(xiii) Suala la ukuzaji wa mnyororo wa thamani ya mazao ya mifugo lisipofanyiwa kazi inavyostahili maisha ya wafugaji yataendelea kuwa duni na mchango wa Sekta ya Mifugo utaendelea kuwa mdogo;

(xiv) Sera, Sheria na Kanuni zinazotumika katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, zisipofanyiwa mapitio ya haraka, zitaendelea kuweka misimamo iliyopitwa na wakati, kuweka masharti yasiyoendana na hali halisi na kuweka taratibu zisizikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, zipo changamoto zinazobainika na ambazo utatuzi wake utasaidia kuwezesha huduma bora, kukua kwa uchumi, maisha bora ya wananchi na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, naomba sasa kutoa mapendekezo ya utatuzi wa changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vituo vya pamoja mipakani kukosa mashine za ukaguzi:-

Kwa kuwa, mashine za ukaguzi *(scanner machines)* ni muhimu katika vituo vya pamoja vya mipakani, lakini vituo vingi vinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mashine hizo;

Na kwa kuwa, changamoto hiyo inapunguza tija kutokana na kusababisha: -

(i) Ugumu katika kudhibiti bidhaa zinazoingia nchini; na

(ii) Ongezeko la gharama na muda wa ukaguzi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itenge bajeti ya kununua mashine hizo na kuzisambaza katika vituo vya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumuko wa bei Nchini:-

Kwa kuwa, mfumuko wa bei unaendelea kwa sehemu kubwa unagusa bidhaa muhimu, zikiwemo bidhaa za chakula kama vile sukari, ngano, mchele, mahindi, maharage na vitoweo;

Na kwa kuwa, bidhaa muhimu kwa maisha ya watu zinapoguswa na mfumko wa bei zinagharimu maisha ya mtu mmoja mmoja, jamii, uchumi wa Taifa na ustawi wa watu kwa ujumla;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ifanye tathmini ya hali ya mfumuko wa bei nchini na kuchukua hatua za haraka ili kupunguza madhara yake katika uchumi na maisha ya watu; na

(ii) Serikali iweke mikakati ya muda mrefu ya kuzuia mfumuko wa bei na kudhibiti madhara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa sukari nchini:-

Kwa kuwa, hali ya jumla ya upatikanaji wa sukari inaonesha upungufu mkubwa wa bidhaa hiyo katika baadhi ya maeneo nchini;

Na kwa kuwa, upungufu huo unasababisha kupanda kwa bei ya sukari, jambo ambalo: -

(i) Linaathiri uzalishaji katika viwanda vinavyotumia bidhaa za sukari ikiwa ni sehemu ya malighafi; na

(ii) Linapunguza uwezo wa wananchi walio wengi kumudu ununuzi wa sukari kwa matumizi yao ya kila siku;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua za haraka, madhubuti na za kudumu kuhakikisha upatikanaji wa sukari unakidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa malighafi za uzalishaji wa mafuta ya kula nchini:-

Kwa kuwa, uhaba wa malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya chakula umechangia uzalishaji wa kiasi cha tani 205,000 ambacho ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani 570,000 kwa mwaka;

Na kwa kuwa, upungufu huo wa mafuta unatokana na uhaba wa malighafi, unachangia ongezeko la matumizi ya fedha za kigeni kwa kuagiza mafuta kutoka nje na hivyo kusababisha athari katika Urari wa Fedha za Kigeni;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali: -

(i) Iongeze juhudi za kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu ya *ASA* ili kuongeza upatikanaji wa alizeti ambazo ni malighafi muhimu;

(ii) Iongeze ruzuku ya mbegu bora za alizeti kwa wakulima ili kuhamasisha uzalishaji wa zao hilo; na

(iii) Ihamasishe Sekta Binafsi kuwekeza katika kilimo cha malighafi nchini ili kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungu wa viuatilifu nchini:-

Kwa kuwa, upungufu wa viuatilifu nchini unaathiri uzalishaji wa chakula na Afya ya Jamii;

Na kwa kuwa, juhudi za kukabiliana na upungufu huo zinaathiri uchumi wa nchi kutokana na: -

(i) Ongezeko la matumizi ya fedha za kigeni unaotokana na kuagiza viuatilifu kutoka nje ya nchi kwa lengo la kupunguza uhaba; na

(ii) Kuvurugika kwa uwiano wa biashara ya kigeni *(Balance of trade)* na uwiano wa malipo ya fedha za kigeni *(Balance of Payment)* kwa sababu ya kupungua kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi ikilinganishwa na ununuzi wa viuatilifu kutoka nje ya nchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Ijenge viwanda vya kutengeneza viuatilifu nchini ili kupunguza utegemezi wa viuatilifu toka nje ya nchi;

(ii) Iweke utaratibu mzuri wa kudhibiti matumizi ya dawa katika uzalishaji wa mazao ya vyakula ili kusimamia usalama wa chakula inavyostahili;

(iii) Iongeze na kuimarisha mafunzo ya mara kwa mara kwa Maafisa Kilimo ili kuboresha ufanisi wa huduma wanazozitoa;

(iv) Iendelea kuwatumia Maafisa Kilimo kwa ajili ya kuwaelimisha wakulima juu ya umuhimu wa kutumia viuatilifu; na

(v) Itumie ndege zisizo na rubani ili kumwaga dawa za kuua wadudu waharibifu na magugu vamizi inapobidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu athari za changamoto za Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA)* katika uzalishaji wa mbegu:-

Kwa kuwa, Wakala wa Mbegu za Kilimo inakabiliwa na changamoto za kiuendeshaji kama vile maeneo yake kuvamiwa, mtaji mdogo, kutopata fedha kwa wakati; na upungufu wa vitendea kazi;

Na kwa kuwa, changamoto hizo zinaathiri uwezo wa wakala kuzalisha mbegu bora, na upatikanaji wa mbegu bora kwa wakati;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali: -

(i) Iweke mikakati kushirikiana na Sekta Binafsi katika uzalishaji wa mbegu;

(ii) Iwezeshe Wakala kuzalisha mbegu ipasavyo na kuzifikisha kwa wakulima kwa wakati; na

(iii) Iwapatie Wakala wa Mbegu vitendea kazi vya kutosha na kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora ya mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa mbolea nchini:-

Kwa kuwa, mbolea inayozalishwa nchini haikidhi mahitaji halisi ya tani 1,000,000 za mbolea kwa mwaka;

Na kwa kuwa, hali hiyo inachangia utegemezi wa mbolea inayonunuliwa kutoka nje ya nchi jambo ambalo: -

(i) Linaongeza matumizi ya fedha za kigeni na kuathiri uwezo wa uchumi wa nchi; na

(ii) Linaongeza gharama kutokana na kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iweke mikakati ya kuanzisha viwanda vya mbolea nchini pamoja na kuboresha uzalishaji kwenye viwanda vilivyopo ili kukidhi mahitaji; na

(ii) Ihamasishe na kuhimiza Sekta Binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchango mdogo wa Tasnia ya Umwagiliaji katika Sekta ya Kilimo:-

Kwa kuwa, Tasnia ya Umwagiliaji imebainika kuwa na mchango mdogo katika Sekta ya Kilimo kutokana na: -

(i) Ufinyu wa Bajeti na ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

(ii) Idadi ndogo ya wataalamu wa umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya; na

(iii) Upungufu wa mitambo na magari ya umwagiliaji;

Na kwa kuwa, changamoto hizo zinakwamisha tija iliyokusudiwa na kusababisha uzalishaji mdogo wa Sekta ya Kilimo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iongeze fedha za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji. Aidha, fedha zilizotengwa zitolewe kwa wakati;

(ii) Serikali iajiri Wataalam wa umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya ili kuimarisha usimamizi wa miradi ya umwagiliaji; na

(iii) Serikali inunue mitambo na magari kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu katika mfumo wa kisheria na masuala ya ushirika nchini:-

Kwa kuwa, mfumo wa kisheria wa masuala ya ushirika nchini unategemea Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 na Kanuni zake na kwamba Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2008 na Kanuni zake zimeonekana kuwa na upungufu;

Na kwa kuwa, upungufu wa Sheria na Kanuni hizo umedhoofisha utaratibu na usimamizi wa dhana ya ushirika nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Ikamilishe mchakato wa mapitio ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 ili kupendekeza maboresho katika mfumo wa Sheria; na

(ii) Ihakikishe mchakato wa kuboresha Sera ya Ushirika ya Mwaka 2002 ili kubainisha masuala ya kisera *(policy issues)* yanayohitaji matamko ya kisera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya Wakandarasi na Wataalam Elekezi:-

Kwa kuwa, utaratibu wa kuwatumia Wakandarasi na Wataalam Elekezi katika utekelezaji wa miradi unalenga kufanikisha miradi hiyo kwa namna ilivyokusudiwa;

Na kwa kuwa, Wakandarasi na Wataalamu Elekezi wasiokidhi vigezo ikiwemo uwezo mdogo wa kifedha wanachelewesha miradi na kuathiri ubora kutokana na kutokuwa na fedha jambo ambalo: -

(i) Linasababisha ongezeko la gharama kutokana na kuchukua muda mrefu; na

(ii) Linachelewesha upatikanaji wa tija tofauti na malengo yaliyowekwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali: -

(i) Isimamie utaratibu wa kujiridhisha *(due diligence)* kabla ya kukabidhi mradi kwa Wakandarasi ili kuepuka uwezekano wa Wakandarasi wasio na uwezo kupewa kazi na kusababisha hasara na usumbufu usio wa lazima; na

(ii) Iweke Wataalam Elekezi wenye uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha na kwa wakati ili kupata tija iliyokusudiwa na kufikia ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tija ndogo na ufanisi usiokidhi wa Kampuni ya Mbolea *(TFC)*:-

Kwa kuwa, Kampuni ya Mbolea Tanzania ilianzishwa kwa ajili ya usambazaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea na viuatilifu ili kuleta utulivu wa bei za pembejeo nchini, lakini azma hiyo inakwama kutokana na: -

(i) Changamoto za kiuendeshaji zinazotokana na mfumo wa ununuzi katika Sekta ya Umma ikilinganishwa na urahisi wa ununuzi katika Sekta Binafsi; na

(ii) Ukosefu wa vitendea kazi kwa ajili ya usambazaji wa pembejeo;

Na kwa kuwa, changamoto hizo zinakwamisha ufanisi katika Sekta ya Kilimo kwa sababu ya kutofika, na tofauti ya bei ya mbolea katika maeneo mbalimbali nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali: -

(i) Ifanye mapitio ya taratibu za ununuzi wa umma ili kuona namna ya kuiruhusu kampuni ya mbolea kumudu mazingira ya ushindani katika soko la mbolea;

(ii) Ipatie *TFC* zana na vitendea kazi kwa ajili ya uendeshaji ikiwemo usambazaji wa mbolea; na

(iii) Iendelee kuzingatia ushauri wa kuwa na vifungashio vya ujazo tofauti tofauti vya mbolea kwa lengo la kuwafikia wakulima wa ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto za uvuvi na ufugaji wa samaki:-

Kwa kuwa, Sekta ya Uvuvi inalalamikiwa kwa: -

(i) Kuhimiza matumizi ya vizimba vya samaki ambayo yana tija ndogo kutokana na ufahamu duni wa wananchi;

(ii) Kuwa na tozo za aina mbalimbali ambazo ni kero kwa wavuvi; na

(iii) Kuzuia shughuli za uvuvi baadhi ya wakati kwa lengo la kukabiliana na athari za uvuvi haramu;

Na kwa kuwa, mambo yanayohusishwa na kupungua kwa upatikanaji wa samaki ambao pia unasababishwa na: -

(i) Kukosekana kwa nyenzo madhubuti za uvuvi katika bahari, mito, mabwawa na maziwa nchini; na

(ii) Ufugaji wa samaki kushindwa kuongeza katika soko kwa sababu ya uelewa mdogo wa wananchi walio wengi kuhusu ufugaji wa samaki kibiashara;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ihimize uvuvi wa kutumia vizimba na itoe elimu kuhusu umuhimu wa uvuvi bora; na

(ii) Serikali ifanye mapitio na kuunganisha au kuondoa baadhi ya tozo katika Sekta ya Uvuvi ili kupunguza usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi hafifu wa utekelezaji wa miradi ya uvuvi:-

Kwa kuwa, Miradi mingi ya uvuvi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inaanzishwa ili kuongeza tija katika Sekta ya ndogo ya uvuvi, lakini haifanikiwi kutokana na kutokamilishwa;

Na kwa kuwa, kutokamilika kwa miradi hiyo kunakosesha manufaa ya miradi kwa shughuli za uvuvi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ikamilishe uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi Shughuli za Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchango mdogo wa sekta ya mifugo:-

Kwa kuwa, idadi kubwa ya mifugo nchini haichangii ipasavyo katika Pato la Taifa kutokana na kukosekana kwa uongezaji wa thamani katika mnyororo wa mazao ya mifugo nchini;

Na kwa kuwa, hali hiyo inatokana na kutokuwa na chombo mahsusi cha kusimamia sekta ya mifugo nchini jambo linalosababisha maisha ya wafugaji kuendelea kuwa duni na mchango hafifu wa Sekta katika uchumi wa nchi licha ya idadi ya jumla ya mifugo nchini kuwa kubwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iweke mkakati madhubuti ili kuiwezesha Sekta hii kuchangia ipasavyo katika Pato la Taifa na kuwawezesha wafugaji kunufaika na rasilimali hizi; na

(ii) Ikamilishe uanzishwaji wa Mamlaka mahsusi ya kusimamia sekta ya Mifugo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi:-

Kwa kuwa, Sera hutoa msimamo na mwongozo, Sheria huweka masharti ya utekelezaji na Kanuni hubainisha taratibu za kufuatwa. Hata hivyo, Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo, Mfugo na Uvuvi zimepitwa na wakati na zinakinzana hivyo kutofautiana na misimamo inayotakiwa, masharti yanayostahili na taratibu zinazopaswa kufuatwa;

Na kwa kuwa, hali hiyo haisaidii uchumi wa nchi wala maisha ya wananchi wanaojishughulikisha katika Sekta hizo na haiendani na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya sasa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ikamilishe mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni ili kuendana na wakati; na

(ii) Serikali iwianishe Sera, Sheria na Kanuni za Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili kuongeza manufaa ya kiuchumi yatokanayo na Sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Mafanikio ya Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Januari, 2024 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii, unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wabunge na kuwapa msaada wa kitaalam na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mbunge), Naibu wake Mheshimiwa Exaud Silaoneka

Kigahe (Mbunge), Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe (Mbunge), Naibu wake Mheshimiwa David Silinde (Mbunge), Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Ulega (Mbunge) na Naibu wake Mheshimiwa Alexander Mnyeti (Mbunge), Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote katika Wizara kwa ushirikiano waliouonyesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika kuratibu usimamizi wa shughuli za kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa baada ya kueleza shughuli zilizotelekezwa na Kamati uchambuzi wa matokeo na utekelezaji wa shughuli hizo na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KWA MWAKA, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa Kipindi cha Kuanzia

Februari, 2023 hadi Januari, 2024. Taarifa hii inahusu shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha mwaka mmoja.

**1.2 Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imeundwa na sehemu nne kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi na maelezo ya shughuli za Kamati, Muundo wa Taarifa msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati, na mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

(ii) Sehemu ya pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;

(iii) Sehemu ya tatu inatoa maoni ya jumla na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi; na

(iv) Sehemu ya nne inatoa hitimisho na kutoa hoja ili Bunge liweze kujadili na kufanya maamuzi.

**1.3 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati unatokana na Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inaeleza kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi wake. Aidha, Ibara ya 63(2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ina wajibu wa kufanya masuala mbalimbali yaliyoainishwa katika Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo ni: -

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
(iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na

(iv) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Februari, 2024 Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo: -
(i) Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Wizara hizo pamoja na taasisi zake.

(ii) Kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara inazozisimamia;

(iii) Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2023/2024 za Wizara inazozisimamia;

(iv) Kujadili taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Desemba, 2023);

(v) Kufuatilia Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya Mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Mwezi Februari, 2023.

**1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 142 ambayo pamoja na mambo mengine inataka kubainisha njia au mbinu zilizotumika. Naomba kulijulisha Bunge kuwa Kamati ilitumia njia na mbinu zifuatazo: -

(i) Kufanya vikao na Wizara inazozisimamia kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo na Taasisi zake;

(ii) Kufanya ziara kwa lengo la kuona hali halisi ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara na Taasisi zake;

(iii) Kupokea, kujadili na kufanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali, ikiwemo taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iv) Kushiriki mafunzo na semina mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taasisi Binafsi na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii; na

(v) Kufanya majumuisho ya masuala yaliyobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano ili kuorodhesha mambo makuu ya kutolewa maoni na ushauri.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kutumia mbinu hizi tofauti ni kuwawezesha wajumbe wa Kamati kupata ufahamu wa kutosha katika maeneo wanayoyasimamia na kuishauri Serikali. Naliomba Bunge lako tukufu lipokee na kuijadili Taarifa hii kwa kuzingatia ufanisi wa njia na mbinu zilizotumika.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Maelezo ya Shughuli

**Mheshimiwa Spika**, Kama inavyofahamika, Kamati hii ni miongoni mwa Kamati kumi na moja za kisekta na inasimamia shughuli za umma kwenye sekta tatu: Sekta ya Viwanda na Biashara, Sekta Kilimo na Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kwa mpangilio wa Wizara, Sekta hizo zipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha masharti ya Kifungu cha 7(1) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanazingatiwa, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

**2.1.1 Bajeti za Wizara zilizo chini ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia Bajeti za Wizara zilizo chini yake. Kwa msingi huo, tarehe 21 - 30 Machi, 2023, Kamati ilichambua bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mujibu wa kifungu cha 7(1)(a) hadi (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Matokeo ya uchambuzi huo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 2 - 9 Mei, 2023, wakati wa vikao vya Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Bajeti ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 bado ipo katika hatua za utekelezaji wake, Naomba kulijulisha Bunge kuwa ufuatiliaji wa bajeti hizo unaendelea, na kwamba maoni na ushauri kuhusu utekelezaji utatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (5) ya Kanuni za Bunge.

**2.1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 14 - 19 Machi, 2023 Kamati ilitembelea na kukagua miradi sita (6) iliyotekelezwa na Wizara hizi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Miradi hiyo ni:-

(i) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Matekwe;

(ii) Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa;

(iii) Mradi wa Jengo la TIRDO;

(iv) Mradi wa Uimarishaji wa Idara ya Uhandisi kwa kununua vifaa vya upimaji ubora bila kuharibu (Non-Destructive Testing);

(v) Mradi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (Tanzania Biotech Products Ltd. – TBPL), Kibaha; na

(vi) Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa, miradi hiyo ikitekelezwa kwa ufanisi, itasaidia kuboresha maisha ya watanzania na kuongeza ustawi wa wananchi. Ikiwa hivyo, lengo kuu la Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakuwa limefanikishwa. Aidha, ahadi waliyopewa wananchi katika aya za 37, 40, 47 na 49 za Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 zitakuwa zimetimizwa.

**Mheshimiwa Spika**, Masharti ya kifungu cha 7(1) (d) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 6(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, nayo yalizingatiwa. Kamati ilitembelea mikoa nane (8) ya Dodoma, Dar Es Salaam, Tabora, Arusha, Iringa, Mbeya, Kagera na Mwanza. Ziara hizo ziliwezesha Kamati kufuatilia masuala yafuatayo: -

(i) Kukagua utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji ili kujiridhisha na juhudi za Serikali za kuachana na kilimo cha kutegemea mvua;

(ii) Utendaji wa Shirika la Viwango (TBS) ili kuona namna linavyotekeleza majukumu yake katika kuhakikisha linadhibiti ubora;

(iii) Kujionea utekelezaji wa shughuli za Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Mwanza; na

(iv) Kutembelea Kituo cha pamoja cha Mpakani - Mutukula (*Mutukula One Stop Center*) - Kagera ili kuona utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa Vipimo (WMA) hasa upatikanaji wa huduma katika dirisha moja.

**2.1.3 Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Ili kulisaidia Bunge kufuatilia maazimio yake, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka 2023 ya Shughuli za Kamati hii. Naomba kulijulisha Bunge kuwa, uchambuzi huo ulionesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio hayo. Hatua hizo zinajumuisha baadhi ya maazimio kuwa yametekelezwa kikamilifu, mengine yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake. Mchanganuo wa hatua za utekelezaji ni kama ifuatavyo: -

**(a) Sekta ya Viwanda na Biashara**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lilitoa Maazimio nane (8) kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kutokana na Taarifa ya iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Taarifa ya utekelezaji imeonesha kuwa Maazimio manne (4) kati ya nane (8) yametekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na manne (4) utekelezaji wake bado unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa azimio ambalo utekelezaji wake bado unaendelea linahusu Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Liganga, Mchuchuma na Mradi wa Magadi Soda Engaruka. Taarifa ilionesha kuwa Serikali inaendelea kutekeleza azimio hilo. Kwa hatua hiyo, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa **shilingi bilioni 15.4** kwa ajili ya kulipa fidia na riba Wananchi waliopisha Mradi wa Liganga na Mchuchuma.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na pongezi hizo, Kamati inasisitiza kuwa bado kuna umuhimu wa Serikali kuhakikisha kwamba, suala la mwekezaji linafikia muafaka ili mradi huu uanze utekelezaji mapema iwezekanavyo.

**(b) Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta hii ilikuwa na maazimio manne (4) ambayo kwa kiasi kikubwa utekelezaji wake unaendelea. Kwa mfano, Azimio lililohusu kuongeza uzalishaji, usafirishaji na mauzo ya mazao ya bustani linaendelea kutekelezwa. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kuwa, changamoto ya mashamba ya kilimo yakiwemo mashamba ya maua ya Arusha yaliyofungwa imetatuliwa kwa kiasi kikubwa. Aidha, Serikali imeanzisha Mamlaka ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*Cereal and Other Produce Authority*) ambayo itasimamia mazao ya Bustani pamoja na mazao mengine.

**(c) Sekta ya Mifugo na Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta hii ina maazimio nane (8) ambayo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Kwa mfano, Azimio linalohusu uimarishaji wa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa Mradi linaendelea kutekelezwa. Jambo hilo kwa kawaida ni endelevu katika miradi. Aidha, Kamati

ilijulishwa kuwa Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini na tayari imeanzisha kitengo kipya cha ufuatiliaji wa tathmini ili kuimarisha utekelezaji na usimamizi wa miradi;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikiwa ya kuanza kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwa kuanzisha muundo mpya wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kitakachosaidia kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa Miradi. Hata hivyo, bado kuna umuhimu kwa Serikali kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ili itekelezwe kikamilifu.

**2.1.4 Kushughulikia Mikataba ya Kimataifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa **Kanuni ya 108 (1)** ikisomwa pamoja na **kifungu cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati ilishughulikia **Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika ya Mwaka 2012 (*SADC Protocol on Trade in Services,* 2012)**. Matokeo ya shughuli hiyo ni Maoni na Ushauri wa Kamati yaliwasilishwa Bungeni tarehe 31 Agosti, 2023 wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge.

**2.1.5 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za taasisi ishirini na moja zilizo chini ya Wizara inazozisimamia. Lengo lilikuwa ni kufuatilia shughuli za umma chini ya taasisi hizo na kujiridhisha iwapo zinasaidia katika lengo la kuwezesha maisha bora kwa kila mtanzania na ustawi wa watu kwa ujumla. Uchambuzi wa taarifa hizo, ulifanyika kwa kuoanisha maudhui, hali halisi na matarajio ya wananchi katika Sekta hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, utaratibu wa kupokea na kujadili taarifa kutoka Serikalini uliiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, bado kuna umuhimu wa kuzisisitiza Wizara ziendelee kutoa taarifa za kina zinazohitajika kwenye Kamati za Bunge kwa wakati ili kutimiza dhana ya uwazi na uwajibikaji Bungeni. Iwapo Taarifa

zitawasilishwa kwa kuchelewa zitawanyima Wajumbe fursa ya kufanya uchambuzi wa kina na kuathiri tija ya uchambuzi.

### 2.2 Uchambuzi wa Matokeo ya Shughuli zilizotekelezwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kuelezea shughuli hizo, sehemu hii ya Taarifa inaonesha uchambuzi wa kina wa yaliyojitokeza na kubainisha ubora na dosari. Lengo ni kuhakiki shughuli za umma zilizotekelezwa katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii kwa kuzingatia matarajio ya wananchi. Naomba kulijulisha Bunge matokeo ya uhakiki yanayoonesha mafanikio na changamoto kwa kila Sekta kama ifuatavyo: -

#### 2.2.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Viwanda na Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Viwanda na Biashara ni chimbuko la maendeleo ya haraka ya nchi mbalimbali. Sekta hii imekuwa mhimili mkuu wa kutegemewa kwa ajili ya kuongeza thamani ya malighafi, kutoa ajira kwa wananchi, kuongeza mapato ya Serikali pamoja na fedha za kigeni na kuongeza na kuboresha sayansi na teknolojia ambayo yote kwa pamoja yanasababisha ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa taarifa umeonesha mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Viwanda na Biashara kwenye Miradi na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

#### (a) Hali ya Sekta Ndogo ya Biashara Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ndogo ya Biashara nchini imeendelea kuwa nguzo muhimu inayochangia kuinua kipato kwa wazalishaji, wafanyabiashara, kukuza uchumi na kuongeza mapato ya Serikali. Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonesha kuwa kwa kipindi cha mwaka 2022, mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa ulikuwa **asilimia 7.9** upungufu wa **asilimia 0.8** ikilinganishwa na mwaka 2021. Aidha, kasi ya ukuaji wa Sekta ya Biashara ilikuwa **asilimia 3.6** mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia **3.8** mwaka 2021 sawa na upungufu wa **asilimia 0.2.**

**Mheshimiwa Spika**, Udadisi wa Kamati ulifanikisha upatikanaji wa majibu kwamba, upungufu huo wa mchango katika pato la taifa

na ukuaji kupungua, unatokana na migogoro mingi inayoendelea duniani ikiwemo vita ya Urusi na Ukreini. Athari hiyo imeukumba uchumi mkubwa duniani na ni tatizo kutoka nje ya uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zimeonesha kuwa Sekta ya Biashara imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Kuboresha mazingira ya biashara, kuvutia uwekezaji na kusaidia kukuza Sekta mbalimbali za uchumi;

(ii) Kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji, Serikali imefanya juhudi za kuboresha taratibu za kufungua biashara nchini.

(iii) Kufupisha na kusimamia vizuri taratibu za kupata leseni za biashara kupitia Mfumo wa Leseni za Biashara (Business License Registration System) ambapo sasa leseni za biashara zinapatikana kwa njia rahisi na kwa muda mfupi kutoka wastani wa siku 7 hadi 9 hapo awali na kufikia wastani wa kati ya siku 1 hadi 2.

(iv) Kuimarisha mifumo ya uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo ikiwemo Soko la Bidhaa, Stakabadhi za Ghala, Minada na Kilimo cha Mkataba. Katika kipindi hicho, mazao ya kahawa na kakao yaliuzwa kupitia mifumo ya minada na Soko la Bidhaa na mazao ya korosho na mbaazi yaliuzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

(v) Mazao ya mahindi na mchele yaliuzwa kupitia mfumo wa soko huria na mfumo wa kilimo cha mkataba ulitumika kwenye mazao ya chai, tumbaku, alizeti, pamba na kahawa.

(vi) Kuimarika kwa bei ya baadhi ya mazao ya kilimo katika soko la ndani.

(vii) Kufungua soko la zao la parachichi katika nchi ya China na soko la korosho zilizobanguliwa katika nchi ya Marekani.

(viii) Kusaini na kuridhia Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) kwa lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi na biashara baina ya nchi wanachama (Intra-African Trade);

(ix) Kuongezeka kwa mauzo katika Soko la AGOA kwa mwaka 2021 kutoka kwa Dola za Marekani milioni 39.1 mpaka Dola za Marekani milioni 74.6 kwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 90.8;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi za kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kibiashara ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Biashara nchini kama ifuatavyo:-

(i) Uwepo wa Sera na Sheria zilizopitwa na wakati. Hali hii inapelekea kupunguza ufanisi kwa kutokidhi mahitaji ya sasa. Mfano wa Sera na Sheria hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996), Sera ya Taifa ya Biashara (2003), Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003) na Sera ya Masoko na Bidhaa za Kilimo (2008), Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania Sura ya 159, Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Sheria Na. 4 ya mwaka 2009), Sheria ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Sura ya 112, Sheria ya Vipimo Sura ya 340, na Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 208.

(ii) Uhaba wa fedha za kigeni ambao unaathiri moja kwa moja Sekta ya Biashara nchini;

(iii) Uwepo wa wafanyabiashara wengi wadogo wasio rasmi kwenye Sekta ya biashara nchini;

(iv) Uzalishaji bidhaa hususani za kilimo ambazo hazizingatii ubora na mahitaji ya soko la kimataifa;

(v) Ugumu wa upatikanaji wa mitaji kutokana na riba kubwa na masharti magumu toka taasisi za kifedha;

(vi) Kukosekana kwa miundombinu ya kuhifadhia bidhaa zinazoharibika (Cold rooms) kwenye maeneo ya masoko, viwanja vya ndege na bandarini;

(vii) Uwepo wa tozo nyingi za biashara zinazotozwa na Mamlaka mbalimbali za Serikali kama vile tozo ya service levy, OSHA, Zimamoto, tozo ya afya n.k.;

(viii) Miundombinu isiyo rafiki kwenye masoko hususan kwenye Halmashauri;

(ix) Kukosa masoko ya uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa; na

(x) Ukosefu wa dhamana kwa ajili ya kuomba mkopo toka taasisi za kifedha na gharama za mkopo zisizo rafiki hasa kwa wafanyabiashara wadogo;

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa, Serikali iendelee na kukamilisha zoezi la kufanya mapitio ya Sera na Sheria zake za kisekta ili ziendane na mabadiliko ya kimaendeleo yaliyofikiwa tangu kutungwa kwake.

**(b) Hali ya Viwanda Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Viwanda na Biashara ina jukumu kuu la kusimamia, kuendeleza na kuweka mazingira bora ya ukuaji endelevu wa Sekta ya Viwanda nchini. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Serikali imefanikiwa kuanzisha Kongani ya Viwanda Kwala Mkoani Pwani;

(ii) Serikali imefanikiwa kuanzisha Kongani ya kisasa ya Viwanda Chalinze Mkoani Pwani;

(iii) Serikali imeviwezesha viwanda vya Kilimanjaro Machine Tools (KMTC) cha kutengeneza vipuri vya mashine mbalimbali na Tanzania Biotech Products Limited (TBPL) cha kuzalisha dawa za viuadudu na viuatilifu ambapo uzalishaji unaendelea;

(iv) Serikali imefanikiwa uandaaji wa michoro ya majengo ya kiwanda cha kisasa cha vifaa tiba;

(v) Serikali imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu na tafiti mbalimbali viwandani;

(vi) Serikali imefanikiwa kuendeleza tafiti na teknolojia mbalimbali za kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kuwa, mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa ulikuwa **asilimia 7.1** mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 7.2** mwaka 2021. Vilevile, Hali halisi ya kiwango cha ukuaji wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa **asilimia 4.2** mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 4.8** mwaka 2021.

Kamati ilielezwa sababu za kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji wa bidhaa, kulikosababishwa na kuongezeka kwa bei za malighafi kutoka nje ya nchi hususani bidhaa za petroli kulikochangiwa kwa kiasi kikubwa na athari za vita inayoendelea baina ya Urusi na Ukraine. Aidha, uchambuzi ulionesha kuwa, mapato yaliyotokana na uzalishaji bidhaa viwandani yalifikia **Shilingi bilioni 25,034.5** mwaka 2022 ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 22,758.7** mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi zaidi ulionesha kwamba, yapo mafanikio katika uzalishaji viwandani. Pamoja na hayo, ilibainika kuwepo kwa changamoto kwa kila bidhaa. Kwa mfano, katika uzalishaji wa sukari nchini viwanda vilitarajiwa kuzalisha si chini ya tani 630,000 ambazo ni mahitaji kwa mwaka. Hali halisi ilionesha kuwa, uwezo wa viwanda kuzalishaji sukari nchini kwa msimu wa mwaka 2022/2023 ulikuwa tani 456,019.73 ikiwa ni upungufu kwa tani 173,980.27 sawa na upungufu wa asilimia 27.62%.

**Mheshimiwa Spika**, Udadisi ulidhihirisha kwamba, upungufu huo wa sukari unatokana na uchache wa viwanda vya kuzalisha sukari pamoja na baadhi ya viwanda kufungwa kikimwemo kiwanda cha TPC. Aidha, sababu nyingine ni mvua nyingi ambazo zinasababisha mambo yafuatayo: -

(i) Kasi ndogo ya kuvuna miwa inayotokana na uwepo wa mvua kubwa inayoendelea kunyesha nchini; na

(ii) Ubora wa sukari kwenye miwa kuathiriwa na mvua inayoendelea kunyesha.

**Mheshimiwa Spika**, Maelezo ya Serikali yameonesha kuwa serikali imejipanga kukabiliana na changamoto ya upungufu wa sukari nchini kwa mambo yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vipya;

(ii) Kuchochea na kuongeza uwezo wa viwanda vilivyopo; na

(iii) Kuhimiza ongezeko la mashamba ya uzalishaji wa sukari.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mikakati ya Serikali ya kutatua changamoto hizi, Kamati ina maoni kuwa, Serikali inapaswa kuboresha mikakati ya kuwapatia wakulima ruzuku ya mbegu. Kwa kufanya hivyo, wakulima wengi wataweza kuzalisha zaidi na kwa tija kubwa kuliko ilivyo kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zilizopo kuhusu uzalishaji wa mafuta ya kula nchini zinaonesha mahitaji halisi ya mafuta kuwa tani 570,000. Ulinganisho na uzalishaji wa mafuta nchini unaonesha kwamba, kiasi kinachozalishwa ni tani 205,000, ambazo ni pungufu ya mahitaji. Udadisi umebainisha kwamba, hali hii ya uzalishaji pungufu ya mahitaji imetokana na uzalishaji mdogo wa mbegu za mafuta unaosababishwa na matumizi ya nyenzo za kizamani zisizokuwa na tija na uduni wa kilimo cha mbegu hizo kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umeonesha kuwa, mikakati ya Serikali kutatua changamoto hiyo ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kupitia ASA; kuongeza na kuimarisha vituo vya uzalishaji; na kuimarisha miundombinu na teknolojia.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa mchango wa uzalishaji wa bidhaa za ndani katika pato la Taifa, Taarifa za Serikali zilionesha kwamba, mchango wa shughuli za **uzalishaji** wa bidhaa viwandani ulikuwa **asilimia 7.1** kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 7.2** mwaka 2021. Aidha, hali halisi ya kiwango cha ukuaji wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani ilikuwa **asilimia 4.2** mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 4.8** mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebainisha sababu za kupungua kwa kasi ya ukuaji. Miongoni mwa sababu hizo ni kuongezeka kwa gharama za uzalishaji wa bidhaa kutokana na kuongezeka kwa bei za malighafi kutoka nje ya nchi. Ongezeko hilo limegusa bidhaa za petroli na linatokana na athari za vita inayoendelea baina ya Urusi na Ukraine.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa pia zinaonesha kwamba mapato yaliyotokana na uzalishaji wa bidhaa viwandani yalifikia **Shilingi bilioni 25,034.5** mwaka 2022 ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 22,758.7** mwaka 2021. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini, mafanikio katika uzalishaji viwandani kwa baadhi ya bidhaa, changamoto zilizopo kwa kila bidhaa na mikakati iliyowekwa ya kukabiliana na changamoto hizo. Kwa ujumla changamoto katika Sekta ya Viwanda nchini zinatofautiana kulingana na aina ya kiwanda au aina ya bidhaa.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto za jumla za uzalishaji wa bidhaa viwandani ni pamoja na: -

(i) Uchakavu wa miundombinu ya uzalishaji pamoja na uchakavu wa barabara zinazotumika kupeleka malighafi viwandani na kupeleka bidhaa sokoni;

(ii) Gharama kubwa wanazotozwa wenye viwanda kutoka Mamlaka za udhibiti ambapo Kamati ilifahamishwa kuwa kumekuwa na malalamiko kuwa wenye viwanda wanatozwa gharama kubwa na taasisi za udhibiti hususani OSHA, ambao kila mwaka wanatoza shilingi 75,000 kwa mfanyakazi mmoja na baadhi ya viwanda vina wafanyakazi zaidi ya 3,000;

(iii) Kukosekana kwa soko la uhakika la umeme wa ziada unaozalishwa na baadhi ya viwanda kwa kuwa TANESCO hailazimiki kununua umeme huo;

(iv) Kukosekana kwa umeme wa kutosha na wa uhakika kwenye viwanda;

(v) Kukosekana kwa malighafi stahiki/sahihi ya viwanda vya samaki kumepelekea viwanda vingi vya kuchakata samaki kufungwa nchini;

(vi) Uzalishaji mdogo wa Mbegu za Mafuta ya kula Nchini unasababisha viwanda kufanya kazi kwa muda mfupi (kati ya miezi miwili au mitatu tu kwa mwaka);

(vii) Ukosefu wa mitaji kwa wenye viwanda kuwawezesha kununua malighafi ya kutosheleza uzalishaji kwa mwaka mzima;

(viii) Matumizi ya teknolojia duni za uchakataji na usindikaji wa bidhaa za wajasiriamali wadogo;

(ix) Ukosefu wa elimu ya usimamizi wa biashara na ujasiriamali;

(x) Ukosefu wa masoko ya uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa viwandani; na

(xi) Uhaba wa fedha za kigeni za kuagiza vitu muhimu kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na juhudi za Serikali za kuendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazokabili Sekta ya Viwanda na Biashara, Kamati ina maoni kwamba, kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kuongeza kasi ya utatuzi wa changamoto zinazoikabili Sekta hii.

**(c) Utendaji wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE)**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) iliyopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge, Na. 4 ya mwaka 2009 na kupewa jukumu la kukuza na kuendeleza biashara ya ndani na nje ya nchi ili kuimarisha biashara yenye tija katika maendeleo ya kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonesha kuwa Mamlaka hiyo imefanikiwa kutafuta masoko, kuratibu matukio mbalimbali ikiwemo programu za utafiti, kongamano, misafara ya kibiashara, maonesho na mikutano ya

kuunganisha wazalishaji na wanunuzi kwa lengo la kupata masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini. Kufuatia uratibu huo, Mamlaka ilifanikiwa kuratibu masoko katika nchi 9 za Kenya, Uturuki, Komoro, Saudi Arabia, Oman, DRC, Sudani Kusini, Afrika Kusini na Malawi kwa kushirikisha kampuni takribani 920.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zilionesha kuwa, katika muda wa miaka mitano 2018/2019 - 2022/2023 Mamlaka imefanikiwa kufanya yafuatayo: -

(i) Kuuza Tani 37 za korosho zenye thamani ya Dola za Marekani 202,700 kupitia maonesho yaliyofanyika nchini Afrika Kusini;

(ii) Kampuni za Tanzania zilifanikiwa kufanya mauzo ya papo kwa papo yenye thamani ya Dola za Marekani 100,000 kwa bidhaa mbalimbali za kilimo na pembejeo pamoja na kupata miadi ya mauzo yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 20.3 kupitia msafara wa Malawi.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado kuna changamoto mbalimbali zinazoikabili Mamlaka hii. Changamoto hizo zinazohitaji kufanyiwa kazi ni kama ifuatavyo: -

(i) Sheria ya Biashara ya Mwaka 2009 kutoendana na mahitaji ya kisheria kwa wakati huu kwa kuwa imepitwa na wakati. Hali hii inakwamisha shughuli za biashara nchini.

(ii) Mamlaka ina changamoto ya kushughulikia mazao mengi na kupunguza ufanisi;

(iii) Mifumo mingi ya biashara mtandao inachangia kudumaza ufanyaji biashara nchini pamoja na kuibuka kwa misafara ya kibiashara isiyofuata taratibu; na

(iv) Uchakavu wa miundombinu katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. J. K. Nyerere uliopo barabara ya Kilwa Jijini Dar Es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na changamoto ya uhaba wa fedha za kigeni (USD) nchini, Kamati inaona kuwa, bado kuna uhitaji wa

kufanya tafiti za masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuongeza uwezo wa kupeleka bidhaa nje ya nchi. Aidha, Serikali isimamie na kuweka mkazo katika kujiimarisha kuuza bidhaa nje ya nchi zaidi kuliko kuingiza bidhaa kutoka nje.

**(d) Utekelezaji wa Mikakati Madhubuti ya Kuimarisha Biashara Mtandao (e-commerce)**

**Mheshimiwa Spika**, Biashara mtandao ni utaratibu wa ununuzi au uuzaji wa bidhaa au huduma kwa njia ya kielektroniki. Utaratibu huo unahusisha miamala pasipo kuonana au kuwa katika sehemu moja na unapunguza gharama za ufanyaji biashara. Taarifa zilionesha kuwa kwa kuzingatia manufaa ya biashara mtandao, mwezi Julai, 2022 Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) iliandaa na kupitisha mkakati wake wa Biashara Mtandao (*EAC e-Commerce Strategy*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa, Tanzania imeandaa Mkakati wa Biashara Mtandao ambao pamoja na masuala mengine utawezesha wadau wengi nchini kufanya biashara hiyo. Lengo la Mkakati huu ni kuboresha mazingira ya biashara mtandao na kuwezesha ukuaji wake. Maboresho hayo, yataiwezesha Tanzania kama nchi zingine duniani kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi zitokanazo na biashara mtandao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa, biashara mtandao duniani ni kichocheo cha uchumi kutokana na mfumo wake wa ufanyaji kazi. Katika biashara hii, huduma za mtandao (*internet*) na simu (*telephone services*) hutumika na kurahisisha shughuli za kufanya biashara. Aidha, biashara hii huwezesha ulipaji wa kodi kwa namna ya moja kwa moja kupitia mfumo mara baada ya miamala kufanyika. Hali hii inafanikisha madhumuni ya kodi katika uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea zimefanikiwa kiuchumi kutokana na mchango wa biashara mtandao. Nchi hizo ni pamoja na China, ambayo imeuza bidhaa zenye thamani ya Dola za **Marekani bilioni 2,780.** Mauzo hayo ni asilimia 52 ya jumla ya mauzo ya bidhaa zote katika sekta ya biashara. Nchi nyingine ni Marekani iliyouza bidhaa zenye thamani ya **Dola za Marekani bilioni 843.** Mauzo

hayo ni asilimia 19 ya mauzo ya sekta ya biashara. Mfano mwingine ni Uingereza yenye mauzo ya **Dola za Marekani bilioni 169**; Japan yenye mauzo ya Dola za Marekani bilioni 144 na Hispania **Dola za Marekani bilioni 37.**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi umeonesha kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoikabili biashara mtandao. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Hakuna mfumo wa kisera na kisheria wa aina moja unaobeba utatuzi wa biashara mtandao;

(ii) Biashara mtandao kushindwa kutatua changamoto ya malipo kwa biashara ya bidhaa na huduma kutoka nchi nyingine hususan nchi jirani *(cross border payment);*

(iii) Kuwepo kwa changamoto ya utapeli kwenye biashara mtandao inayowasababishia wananchi kupata hasara;

(iv) Ukosefu wa vifaa sahihi kwa ajili ya biashara mtandao *(Gadgets);* na

(v) Changamoto ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili kuendeleza Sekta ya Biashara Mtandao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba Serikali iendelee kuchukua hatua ili kuimarisha Biashara mtandao ikiwemo kuandaa sheria husika na kuhuisha Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003, pamoja na Kuhamasisha uwekezaji wa vifaa sahihi vya kielektroniki vinavyohitajika kwenye biashara mtandao.

**(e) Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala – WRRB**

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala *(WRRB)* ni Taasisi iliyoundwa kwa Sheria Namba 10 ya mwaka 2005 na Marekebisho Kifungu 4 Sura 339 R.E. 2016. Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ulianzishwa kwa dhumuni la kukuza juhudi za Serikali kurasimisha mifumo ya masoko iliyopo kwa lengo la kupunguza vipingamizi mbalimbali vinavyokwaza uzalishaji wenye tija na utafutaji masoko kwa bidhaa mbalimbali hususan mazao ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, Bodi katika utekelezaji wa majukumu yake imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Ongezeko la bei za mazao, mapato ya mkulima na mapato ya Serikali kwa wastani wa asilimia 200 kutokana na urasimishaji;

(ii) Ongezeko la uzalishaji wa mazao kwa wastani wa asilimia 12 kwa mwaka;

(iii) Kichocheo cha ubora wa mazao yanayofikishwa sokoni;

(iv) Upatikanaji wa takwimu sahihi za mazao yanayopita kwenye Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

(v) Ongezeko la mapato ya uhakika kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; na

(vi) Kukuza huduma za fedha vijijini, kufanikisha uanzishaji wa Soko la Bidhaa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana Bodi inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Upinzani mkubwa toka kwa wafanyabiashara na wadau wengine wanaonufaika na mifumo isiyo rasmi ambapo hununua kwa bei ndogo na vipimo visivyo rasmi kutoka kwa wakulima;

(ii) Wakulima kuwa na uelewa mdogo wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

(iii) Maagizo kinzani na Sheria ya Stakabadhi za Ghala wakati wa utekelezaji wa Mfumo;

(iv) Wadau saidizi kama vile Vyama Vikuu vya Ushirika kuchelewesha malipo kwa wakulima licha ya fedha kulipwa kwa wakati katika akaunti zao;

(v) Uhaba wa maghala bora na ya kisasa;

(vi) Kutoanza kutumika kwa Soko la Bidhaa katika baadhi ya mazao kama vile kokoa na kusuasua kwa soko la korosho; na

(vii) Ufinyu wa bajeti ya Bodi na kusababisha uhaba wa vitendea kazi kama magari na vifaa vya mifumo ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kwamba, Mfumo huu wa Stakabadhi za Ghala ni mzuri kwa kuwa unaweka utaratibu unaowawezesha wazalisha bidhaa kukusanya nafaka katika Ghala Kuu kwa malengo mbalimbali. Miongoni mwa malengo hayo ni kuuza kwa pamoja kupitia minada ya upili kwa lengo la kupata bei nzuri; kupata huduma za kifedha kama vile mikopo; na kuhifadhi ghalani ili kurahisisha usindikaji.

**Mheshimiwa Spika,** Mtazamo wa Kamati ni kuwa, ili malengo mazuri ya uanzishwaji wa mfumo yafikiwe, Serikali haina budi iongeze nguvu katika kukabiliana na changamoto zilizopo, hasa kwa kuwekeza kwenye utoaji wa elimu kwa wakulima na wananchi kwa ujumla kuhusu uwepo wa Stakabadhi za Ghala na faida zake. Kwa msingi huo, kuna umuhimu wa Serikali kuiongezea bajeti Bodi hii ili kuweza kufikia malengo ya kuwa na maghala bora na vitendea kazi vingine ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Bodi.

**(f) Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Chuo cha Elimu ya Biashara yapo kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 31 ya Mwaka 1965 pamoja na Kanuni zake. Majukumu hayo ni pamoja na Kutoa mafunzo ya elimu katika fani ya biashara, Kufanya tafiti katika fani za biashara na Kutoa ushauri wa kitaalam katika fani za biashara. Katika utekelezaji wa majukumu hayo, Chuo kimepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Maktaba katika Kampasi ya Dar es Salaam ambapo jengo hilo lina uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2000 kwa wakati mmoja, ofisi za wafanyakazi 45 na kumbi kubwa 5 za kufundishia;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa uzio na ukarabati mkubwa wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika Kampasi ya Dodoma;

(iii) Kuanza hatua za awali za kuyaendeleza maeneo yake ya Nzuguni na Medeli yaliyopo Dodoma. Hatua hii inatokana na Chuo kuwa na eneo dogo la Kampasi ya Dodoma,

(iv) Kununua eneo la kujenga Chuo Kampusi ya Mwanza; na

(v) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya awali na kuhamia kwenye eneo lake la Iganzo - Mbeya. Aidha, Kampasi ya Mbeya imeanza ujenzi wa mgahawa wa chuo ili kuweza kuboresha huduma bora za chakula kwa watumishi na wanafunzi.

**Mheshimiwa Spika,** Mbali na mafanikio hayo, Taarifa zimeonesha kuwa Chuo cha Elimu ya Biashara kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Upungufu wa rasilimali fedha unaokwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(ii) Kuchelewa kwa mapato yatokanayo na ada kwa wakati ukizingatia kuwa ada ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya chuo;

(iii) Ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kama vile kompyuta na vifaa kwa ajili ya maabara ya vipimo na mizani;

(iv) Barabara inayoenda chuoni (Kamapasi ya Mwanza) haina lami na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa;

(v) Kukosekana umeme wa kutosha na wa uhakika;

(vi) Kampasi ya Mwanza haina uzio (fence) hali inayohatarisha usalama wa mali za chuo na afya za wanachuo;

(vii) Uhaba wa hosteli za wanafunzi katika Kampasi ya Mwanza; na

(viii) Ukosefu wa bwalo/ukumbi katika Kampasi ya Mwanza unaoweza kutumika kwa sherehe mbalimbali ikiwemo mahafali hasa nyakati za mvua na kutumia gharama kubwa ya fedha kukodi ukumbi kutoka maeneo mengine.

**(g) Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)**

**Mheshimiwa Spika**, BRELA ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Sura ya 245 na kuzinduliwa rasmi tarehe 3 Desemba, 1999 chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Majukumu ya BRELA ni kama yalivyoainishwa katika Hati ya Kuanzisha Taasisi Na. 38 ya Tangazo la Serikali Na. 294A la tarehe 8 Oktoba, 1999. Katika kutekeleza majukumu yake, BRELA imepata mafanikio yafuatayo:-

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2023, BRELA imefanikiwa kusajili Makampuni 37,038, Majina ya Biashara 71,505, Alama za Biashara na Huduma 9,879, Hataza 136, kutoa Leseni za Viwanda 542 na Leseni za Biashara Kundi "A" 40,757.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miaka mitatu (3) mfululizo BRELA imejiendesha na kutoa Gawio Serikalini. Gawio hilo limekuwa likiongezeka kutokana na kukua kwa makusanyo. Katika kipindi hiki BRELA imechangia fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi bilioni 43.11.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio yaliyoainishwa, BRELA inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo: -

(i) Kutokuwepo kwa Sera ya Taifa ya Miliki, hali inayosababisha kutokuwa na miongozo madhubuti ya kusimamia masuala ya Miliki Ubunifu kwa maendeleo ya Taifa;

(ii) Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoendelea kutoa Leseni za Biashara kwa kutumia Mfumo wa Tanzania National Business Portal (TNBP);

(iii) Baadhi ya wateja kutokuwa na uelewa unaohitajika wa matumizi ya TEHAMA hasa maeneo ya vijijini na Wilayani, pia uelewa mdogo wa Sheria zinazosimamiwa na Taasisi na kusababisha wananchi kutumia watu wa kati (vishoka);

(iv) Ucheleweshaji wa Uhuishaji wa Taarifa za Kampuni na Majina ya Biashara kutokana na tatizo la wateja kutowasilisha nyaraka mbalimbali kwa mujibu wa sheria, hali inayosababisha ongezeko kubwa la madeni; na

(v) Kukosekana kwa Matawi ya BRELA mikoani jambo ambalo linasababisha ugumu kwa Wananchi kupata Huduma za BRELA kwa wakati hasa ukizingatia ukosefu wa elimu ya kutosha ya masuala ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kuendelea kusimamia Utendaji wa BRELA hali iliyopelekea kuongeza gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Kamati inashauri kuwa Sheria ya BRELA ifanyiwe mapitio ili kurahisisha utendaji wa shughuli zake, kuongeza tija ikiwa ni pamoja na kuanzisha matawi mikoani.

**(h) Wakala wa Vipimo (WMA)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Vipimo ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Taasisi hiyo ambayo ilianzishwa tarehe 13 Mei, 2002 kwa Tangazo la Serikali Namba 194 la tarehe 17 Mei, 2002. Wakala wa Vipimo inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, Sura Na 340 na mapitio yake ya mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika**, Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakiki pampu za kuuzia mafuta ya nishati 42,894 dira za maji 248,352 pamoja na kuhakiki mizani 823,557 zitumikazo kuuzia bidhaa mbalimbali kama vile nyama n.k.;

(ii) Vipimo 44,494 vinavyotumika kuuzia vifaa vya ujenzi ikiwa ni pamoja na misumari (uzito), malori yabebayo kokoto na mchanga (kiasi) na Gauge za mabati vimehakikiwa;

(iii) Vipimo 27,194 vinavyotumika katika ununuzi wa mazao vimehakikiwa;

(iv) Tenki kubwa (Bulk fuel storage tanks) 1,293 zinazotumika kuhifadhia mafuta mara yanapotoka melini zimehakikiwa ujazo wake;

(v) Mita za Mafuta (Flowmeters) 3,843 zitumikazo kujaza mafuta kwenye tenki za Magari yatumikayo kusafirisha mafuta zimehakikiwa;

(vi) Matanki ya Magari yabebayo mafuta 23,153 yamehakikiwa ujazo wake, (Dip sticks) na chati (Verification Charts) zinazotumika wakati wa kushusha mafuta kwenye visima vituoni ziliandaliwa;

(vii) Visima (Fixed storage tanks) 5,742 vinavyopokea mafuta toka kwenye matanki ya magari yabebayo mafuta kwenye Depo za kupokea mafuta pamoja na vituo vya kuuzia mafuata (Fuel Filling Stations) vimehakikiwa';

(viii) Mizani 3,217 zinazotumika kupima magari ya mizigo na mabasi zimehakikiwa; na

(ix) Mizani 10,252 zinazotumika katika Sekta ya Afya zimehakikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Kamati ilijulishwa changamoto zinazoikabili WMA kama ifuatavyo:-

(i) Uhaba wa watumishi wenye ajira ya kudumu hususani wa Kada ya Vipimo na madereva;

(ii) Ukosefu wa vifaa vya kitaalamu (*Technical Working* Standards), kwani vifaa vyote vinapatikana nje ya nchi, ni ghali na michakato yake huchukua muda mrefu; na

(iii) Utungaji na matumizi mabaya ya Sheria Ndogo za Halmashauri zisizozingatia mahitaji. Halmashauri nyingi

hazikutunga Sheria Ndogo za Ada na Ushuru wa Mazao kwa kuzingatia hitaji la mazao kuuzwa kwa Sheria ya Vipimo, SURA 340 na kanuni zake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya kukosekana kwa mashine za ukaguzi (scanner) katika vituo vya mipakani na kusabisha zoezi la ukaguzi wa mizigo kuwa gumu hata wakati mwingine kushindwa kudhibiti mizigo inayoingia nchini. Mfano, kituo cha mpaka wa Mutukula (OSBP) hakina mashine ya kukagulia mizigo hali inayosababisha wafanyabiashara kutumia muda mrefu kukaguliwa mizigo yao na wanatumia gharama kubwa kuwalipa makuli kupakua na kupakia mizigo wakati wa ukaguzi. Vilevile, muda mwingi unapotea katika zoezi hili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina rai kwamba, Serikali inunue mashine hizo katika vituo vyote vya mipakani ili kurahisha zoezi la ukaguzi, udhibiti na kuokoa muda wa ukaguzi.

**2.2.2 Mafanikio na Changamoto Katika Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Maendeleo katika Sekta ya Kilimo ni muhimu hasa katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa sekta ya viwanda. Ukuaji wa sekta hii una umuhimu mkubwa katika kuzalisha chakula cha kutosha ili kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula na lishe kwa wananchi wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kujadili na kuchambua taarifa mbalimbali za Wizara ya Kilimo kuhusu utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zinazoikabili Sekta ya Kilimo nchini kama ifuatavyo: -

a) **Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania *(Tanzania Plant Health and Pestcides Authority - TPHPA*)**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania *(*Tanzania Plant Health and Pestcides Authority - TPHPA) imeundwa kwa Sheria Namba 4 ya 2020 *(Plant Health Act. No. 4)*.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka hii imepewa majukumu yafuatayo kwa mujibu wa sheria ya uanzishwaji wake:-

(i) Kuwezesha masoko ya mimea na mazao ya mimea hapa nchini na kimataifa kwa kufanya *Pest Risk Analysis (*PRA*);*

(ii) Kufanya ufuatiliaji wa usafi wa mimea na mazao mashambani, ghalani na mipakani ili kuzuia kuenea kwa visumbufu;

(iii) Kudhibiti uagizaji, usafirishaji, utengenezaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya viuatilifu na vifaa vya unyunyiziaji wa viuatilifu ili kuleta tija katika kilimo;

(iv) Kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa usimamizi endelevu na bora wa viuatilifu na afya ya mimea; na

(v) Kutoa huduma ya utambuzi na uhifadhi wa bioanuai za mimea na vinasaba vya mazao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka. Baadhi ya mafanikio ni haya yafuatayo:-

(i) Mamlaka imefanikiwa kupata ithibati kwenye maabara ya uchambuzi wa viuatilifu (ISO 17025:2017);

(ii) Jumla ya kampuni kubwa 16 zilikaguliwa na mamlaka;

(iii) Jumla ya sampuli 102 zilichunguzwa na mazao yote yalikidhi matakwa ya masoko ya kimataifa;

(iv) Chunguzi za sampuli 103 za shehena za mimea zilifanyika katika maabara na vitalu nyumba, sampuli zote zilikidhi viwango vya ubora;

(v) Jumla ya maombi 762 ya vibali vya kuingiza vipando nchini Tanzania yalipokelewa, jumla ya vibali 756 sawa na asilimia 99.2 vilitolewa;

(vi) Kaguzi 7 zilifanyika katika karantini za wazi kwa mazao ya miwa na viazi mviringo na matunda ya sapodilla ambapo

vipando vyote kwenye Karantini hizo vilikidhi matakwa ya afya ya mimea ya Tanzania;

(vii) Katika kuwezesha biashara ya mazao ya Kilimo nje ya nchi, Mamlaka imekagua na kuruhusu tani 5,343,380.59 za nafaka, mazao ya bustani, mizizi na mbegu za mafuta kusafirishwa nje ya Nchi;

(viii) Jumla ya vyeti 29,033 vya usafi wa mimea kwa ajili ya kuruhusu mazao kusafirishwa nje ya nchi na vyeti 3,359 vya kuruhusu mazao kuingia nchini vimetolewa; na

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka hii ambapo utekelezaji wake umeisaidia Sekta ya Kilimo katika kupata ufumbuzi wa changamoto nyingi zinazokabili mimea nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Mamlaka hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Uwepo wa wafanyabiashara wa viuatilifu wasiotii sheria;

(ii) Upungufu wa rasilimali watu, vifaaa vya maabara za afya ya mimea na viuatilifu;

(iii) Uchakavu wa miundombinu ya vituo vya mipakani; na

(iv) Upungufu wa miundombinu ya Kilimo Anga.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuna haja ya Serikali kuhakikisha changamoto hizi zote zinapatiwa ufumbuzi ili kufikia lengo lililokusudiwa la uanzishwaji wa Mamlaka hii.

b) **Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC). Mradi huu ulianza mwaka 2019 na utadumu kwa miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la Mradi ni kuimarisha usalama wa chakula, afya ya jamii na kukuza Pato la Taifa kupitia ongezeko la

mauzo ya mazao ya chakula nje ya nchi, kwa kudhibiti uchafuzi wa Sumukuvu kwenye mnyororo wa uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi na karanga.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mradi huu, taarifa ilieleza kuwa, TANIPAC imefanikiwa katika: -

(i) Kuanza ujenzi wa maghala 14 yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 21,500;

(ii) Ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Magonjwa ya Kibiolojia ya Mimea uliogharimu **shilingi 3.82**; na

(iii) Ujenzi wa Kituo Mahiri cha Mazao baada ya Kuvuna ambacho kina sehemu kuu tatu (3) ambazo ni sehemu ya soko la mazao, sehemu ya usindikaji na sehemu ya uhawilishaji wa teknolojia juu ya elimu ya sumukuvu.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine ni mafunzo juu ya udhibiti wa Sumukuvu yaliyotolewa kwa Maafisa Kilimo na Mameneja wa Mashamba 70 kutoka makambi 11 ya Jeshi la Kujenga Taifa. Mafunzo hayo yatasaidia kuhakikisha ubora wa nafaka zinazozalishwa nchini. Kwa upande wa Zanzibar, Kamati ilifahamishwa kuwa, jumla ya maafisa ugani 900 watapatiwa mafunzo haya katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Kamati ilielezwa uwepo wa changamoto zinazoukabili Mradi huu kama ifuatavyo: -

(i) Uwezo mdogo wa wataalamu elekezi uliosababisha kutokamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Kibaiolojia Kibaha na Maghala 14 kutokana na usimamizi usioridhisha wa mtaalam elekezi;
Jambo hili limeendelea kusababisha usumbufu na hasara kwa Serikali kwani utekelezaji wa baadhi ya Miradi unaathirika na kukosa tija iliyokusudiwa. Kamati inaamini kuwajengea uwezo wataalam elekezi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha na kwa wakati ni jambo la kutiliwa mkazo.

(ii) Uwezo mdogo wa kifedha kwa baadhi ya wakandarasi umepelekea kutokamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Kibiolojia katika eneo la Kibaha na Maghala, kinyume na walivyyoonesha katika makabrasha yao wakati wa mchakato wa zabuni;
Kamati inatoa rai kuwa, Serikali ihakikishe wakandarasi wanaopewa kazi wanakidhi vigezo vinavyotakiwa ili kutoendelea kuleta hasara na usumbufu usio wa lazima; na

(iii) Mlipuko wa vita vya Urusi na Ukraine umesababisha ongezeko la ghafla la bei za vifaa vya ujenzi na kuathiri Mradi. Kamati ilielezwa kuwa, Mkandarasi alikataa kusaini mkataba wa ujenzi wa Maabara Kuu ya Kilimo kwa madai ya kufanya mapitio ya bei kinyume na matakwa ya kisheria, Mradi ulilazimika kufuta zabuni na kuitangaza upya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaona kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kuwapatia Maafisa ugani mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha utendaji kazi wao. Aidha, Serikali kuendelea kuwatumia Maafisa Ugani kutoa elimu kwa wakulima kuhusu sumukuvu na namna ya kudhibiti.

c) **Tume ya Maendeleo ya Ushirika Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Tume hii ni Udhibiti na Usimamizi wa Vyama pamoja na Uhamasishaji wa Maendeleo ya Ushirika nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Utendaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika umejielekeza katika maeneo saba (7) yanayolenga kuufanya ushirika kuwa imara na shindani ambayo ni:-

(i) Uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidijitali ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji katika Vyama vya Ushirika pamoja na Mamlaka za Usimamizi;

(ii) Kuharakisha taratibu za uanzishaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika;

(iii) Kuhamasisha mfumo wa Ushirika kujiendesha kibiashara wenye kuaminika na shindani;

(iv) Kuboresha Sera, Sheria, Mfumo wa Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika ili kuchochea ukuaji na maendeleo ya Ushirika;

(v) Kuhamasisha Ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika na Ushirika;

(vi) Kuimarisha uwekezaji wa mali za ushirika katika uzalishaji; na

(vii) Kushirikiana na wadau mbalimbali kutatua changamoto za ushirika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa, katika kutekeleza jukumu la Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika, Tume imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Imesajili katika Daftari la Usajili wa Vyama vya Ushirika jumla ya **Vyama 7,349,** ikilinganishwa na **Vyama vya Ushirika 9,741** katika kipindi cha mwaka 2021;

(ii) Idadi ya Wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka **Wanachama 6,965,272** mwezi Desemba, 2021 hadi **Wanachama 8,358,326** kuishia mwezi Machi, 2023.

(iii) Imefanya ukaguzi kwa kuvitembelea Vyama vya Ushirika 4,712 kati ya 7,349. Aidha, ukaguzi kupitia Mfumo *(Off-Site Supervision)* ulifanyika wa SACCOS 531 sawa na asilimia 69 ya SACCOS ziliwasilisha taarifa za utendaji; na

(iv) Tume ilifanya Ukaguzi wa sifa za uongozi kwa Watendaji wa Vyama vya Ushirika vya upili 77 katika mikoa 26 *ambapo* sifa za viongozi 116 zilifanyiwa ukaguzi na kubaini viongozi 41 pekee ndio wenye sifa stahiki katika nafasi zao.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, katika utendaji wake, Kamati ilifahamishwa kuwa, Tume inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo zifuatazo:-

(i) Upungufu wa watumishi ambapo kwa sasa wapo **watumishi 481** badala ya **watumishi 856** hali inayopelekea kutotekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(ii) Ina upungufu wa magari 16, pikipiki 71, kompyuta 129 na samani (meza, viti na cabinet 325);

(iii) Upungufu wa majengo kwa ajili ya matumizi ya Ofisi za Makao Makuu, Ofisi za Warajis Wasaidizi wa Mikoa na Maafisa Ushirika wa Wilaya; na

(iv) Uhaba wa fedha na mitaji unaokwamisha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla changamoto zinazoikabili Tume zinahusu bajeti. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea Tume bajeti ili iweze kukidhi mahitaji yake na kutekeleza majukumu yake katika kuhakikisha ustawi wa wananchi unapatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imeona kuna changamoto kubwa ya kiutendaji inayotokana na namna shughuli za ushirika zinavyotelekezwa kutokana na mgawanyo wa majukumu. Kwa mfano, Maafisa Ushirika waliopo chini ya Halmashauri, usimamizi na uwajibikaji wao unakuwa mgumu kwa kuwa wapo chini ya Mamlaka tofauti na Tume ya Ushirika. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mapitio ya Sheria ya Ushirika ili kutatua changamoto zinazotokana na usimamizi na uwajibikaji wa Maafisa Ushirika. Vilevile, Kamati inaitaka Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha Benki ya Ushirika kwani suala hili limechukua muda mrefu.

d) **Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge, Namba 15 ya 1982,

iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Kwa ujumla, Shirika lina majukumu yafuatayo kwa mujibu wa sheria:-

(i) Kutoa huduma ya ukaguzi kwa Vyama vya Ushirika, Makampuni ya Kibinafsi, Umma na Taasisi nyinginezo;

(ii) Kutoa huduma ya usimamizi kwa vikundi tarajali vya Ushirika na Vyama vya Ushirika;

(iii) Kufanya utafiti na kutoa huduma za ushauri; na

(iv) Kusimamia makampuni mengine ya ukaguzi yatakayotoa huduma ya ukaguzi kwa Vyama vya Ushirika.

**Mheshimiwa Spika**, COASCO katika utekelezaji wa majukumu yake, imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kukagua Vyama 3,878 ambapo Vyama 478 (12.33%) vimepata hati inayoridhisha; Vyama 2,453 (63.25%) vimepata hati yenye shaka; Vyama 825 (21.27%) vimepata hati mbaya; na Vyama 123 (3.15%) vimepata hati isiyokuwa na maoni; na

(ii) Kamati pia ilielezwa kuwa, hadi kufikia Juni, 2023, Shirika lilikagua jumla ya vyama 3,878 sawa na asilimia 78 ya lengo la kukagua vyama 5000 kutokana na ufinyu wa bajeti, changamoto ambayo inahitaji kupatiwa ufumbuzi na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuipatia COASCO watumishi wa kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwa jambo hili limekuwa la muda mrefu na hivyo kuendelea kuzorotesha utendaji wa shirika.

Aidha, Serikali iongeze bajeti ya Shirika ili liweze kujiendesha na kutatua changamoto zake ikiwemo uhaba wa vitendea kazi na majengo yanayohitajika ili kufikia lengo lililokusudiwa.

e) **Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**
**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Sura 245. Wakala ina jukumu la kutekeleza shughuli kuu zifuatazo: -

(i) Kununua na kuhifadhi chakula;

(ii) Kutoa chakula kukabiliana na upungufu na majanga;

(iii) Kuzungusha akiba ya chakula;

(iv) Kupunguza mfumuko wa bei za nafaka na kuchochea soko; na

(v) Kufanya biashara ya nafaka ili kupata fedha za kuboresha uhifadhi.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, Kamati ilielezwa mafanikio ambayo wakala imepata ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa uwezo wa kuhifadhi;

(ii) Kupata hati za umiliki wa viwanja;

(iii) Kuhudumia maeneo yenye upungufu wa chakula na kasi kubwa ya kupanda kwa bei za nafaka;

(iv) Kuhamisha jumla ya tani 70,525.419 za mahindi;

(v) Kutekeleza mradi wa ujenzi wa vihenge na maghala kwa asilimia 83.5 ambapo Babati, Sumbawanga na Mpanda zimekamilika na kuanza kutumika;

(vi) Kuongeza fursa za kiuchumi;

(vii) Kuchangia mapato ya Halmashauri ya Wilaya;

(viii) Kutoa elimu kwa wadau;

(ix) Kuboresha mifumo ya ndani ya utendaji kazi na kutumia mifumo ya kielektroniki; na

(x) Kuchangia maendeleo ya Ushirika nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana Kamati imebaini uwepo wa changamoto zifuatazo: -

(i) Mabadiliko ya tabianchi kuathiri upatikanaji wa nafaka
Kamati inatoa rai kuwa, Serikali ibainishe mahitaji halisi ya chakula nchini na kuchukua tahadhari kwa kuhifadhi chakula cha kutosha ili kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Kuchelewa kupatikana kwa suluhu ya Mkandarasi M/S Feerum S.A.
Kamati inashauri Wakala kupata suluhisho la Mkandarasi huyu ili kukamilisha miradi ambayo imesimama na kuokoa gharama zitokanazo na mradi kutokamilika kwa wakati.

(iii) Baadhi ya wakulima kuleta nafaka zisizokidhi vigezo vya ubora vilivyowekwa na Wakala wakati wa ununuzi
Suala hili linahitaji elimu zaidi kwa wananchi ili kuepuka hasara wanazopata kwa kutokidhi vigezo. Serikali ihakikishe wakulima wanapata elimu ili kuondoa changamoto hii; na

(iv) Uwepo wa baadhi ya miundombinu chakavu ya uhifadhi
Kamati inatoa rai kwa Serikali kuendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kukarabati miundombinu chakavu ya kuhifadhia chakula nchini kote. Aidha, Wakala utekeleze miradi ya ujenzi wa maghala katika maeneo ambayo yana uhitaji ili kusogeza huduma kwa wananchi.

f) **Tume ya Umwagiliaji – NIRC**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ni Taasisi ya Serikali inayojitegemea iliyoanzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 04 ya mwaka 2013 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali (GN) Na. 402 la tarehe 11 Septemba, 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Tume imepewa jukumu la kuratibu, kuendeleza na kusimamia Maendeleo ya Sekta ya Umwagiliaji nchini. Aidha, Sheria imeipa Tume majukumu mahsusi yafuatayo:-

(i) Kuishauri Serikali katika utekelezaji na kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, Mkakati wa Maendeleo ya Umwagiliaji, Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji na Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji;

(ii) Kuiwakilisha Serikali kwenye mikutano ya kitaifa na kimataifa katika masuala yote yanayohusu uendelezaji na usimamizi wa kilimo cha umwagiliaji;

(iii) Kuratibu shughuli zote za umwagiliaji katika sekta ya umwagiliaji zinazotekelezwa na washirika au wadau wengine wa maendeleo;

(iv) Kuhamasisha na kudumisha ushirikiano na taasisi za kimataifa zenye kutekeleza majukumu yanayofanana na Tume katika masuala ya umwagiliaji;

(v) Kupanga, kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kujenga na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

(vi) Kuanzisha na kuendesha vituo vya ukodishaji wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kuisaidia sekta binafsi kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji;

(vii) Kusajili na kutunza orodha ya wamwagiliaji; na

(viii) Kuhamasisha na kudumisha mahusiano na taasisi zinazotoa programu za mafunzo na kusaidia upatikanaji wa rasilimali watu kwa madhumuni ya kupata wataalamu katika sekta ya umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu tajwa, Tume iliripoti mbele ya Kamati kupata mafanikio kadhaa yakiwemo yafuatayo: -

(i) Hadi tarehe 30 Septemba, 2023, eneo la umwagiliaji limefikia hekta 783,748 sawa na asilimia 65 ya lengo la kufikia hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025;

(ii) Kupitia Mfuko wa maendeleo ya umwagiliaji, Tume imefanikiwa kukusanya maduhuli ya Shilingi 1,101,587,805 kutoka Julai hadi Septemba, 2023/24 ukilinganisha na makusanyo ya mwaka 2022/2023 ya jumla ya Shilingi 907,033,880.52;

(iii) Tume imefanikiwa kusajili vyama vya umwagiliaji 115 na hivyo kufikia jumla ya vyama 586 kufikia Septemba, 2023;

(iv) Tume imefanikiwa kuongeza idadi ya watumishi kutoka 208 kwa mwaka 2020 hadi watumishi 532 mwaka 2023;

(v) Kununua magari 53 na mitambo 32 kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya umwagiliaji;

(vi) Kufungua Ofisi za Umwagiliaji ngazi ya Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kusogeza huduma karibu na wakulima;

(vii) Tija ya uzalishaji wa mazao katika skimu za umwagiliaji imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 - 2.0 kwa hekta hadi tani 4.0 - 8.0 kwa hekta kwa zao la mpunga; zao la mahindi kutoka tani 1.5 hadi tani 3.7-5.0; vitunguu kutoka tani 23 hadi 26 kwa hekta; nyanya kutoka tani 5 hadi 18 kwa hekta; na

(viii) Tume inaendelea kuainisha, kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali yanayotoa fursa kwa wakulima na wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuona umuhimu wa Sekta ya Umwagiliaji na kutenga fedha ambazo zimeanza kuleta mapinduzi katika kilimo cha umwagiliaji nchini ikiwa ni mpango wa kupunguza utegemezi wa kilimo cha kutegemea mvua.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio haya makubwa, Kamati imebaini kuwa Tume inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaweza kupunguza kasi ya utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni hizi zifuatazo:-

(i) Uhaba wa fedha kwa ajili ya shughuli za Umwagiliaji unaotokana na ukomo mdogo wa bajeti. Ukomo wa bajeti unaotolewa kwa Tume hii umekuwa kidogo ikilinganishwa na uzito wa majukumu yake na miradi inayostahili kutekelezwa na Tume. Aidha, mtiririko wa kupokea fedha hauridhishi kwa kuwa hazitoki kwa wakati na hazikidhi mahitaji.

(ii) Ucheleweshaji wa malipo ya hati za madai ya wakandarasi zinazowasilishwa Wizara ya Fedha. Hali hii imeendelea kuathiri kasi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umwagiliaji.

(iii) Mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa vyanzo vya maji. Mafuriko yanayotokana na tabianchi yanasababisha kuharibika kwa miundombinu katika vyanzo vya maji na sehemu nyingine. Kwa upande mwingine, ukame huathiri uzalishaji na upatikanaji wa chakula.

(iv) Uchakavu wa baadhi ya miundombinu ya Umwagiliaji iliyojengwa miaka ya nyuma kabla ya kuanzishwa kwa Tume. Mfano, kwa sasa asilimia kubwa ya mifereji ni ya asili.

(v) Ushiriki Mdogo wa Sekta Binafsi katika Uwekezaji wa Sekta ya Umwagiliaji licha ya kuwepo kwa fursa za ardhi inayofaa kwa Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto hizi ni za muda mrefu, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuzipatia ufumbuzi kwa kutenga fedha za kutosha za kutekeleza kilimo cha umwagiliaji ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

g) **Programu ya Jenga Kesho Bora (*Builiding a Better Tomorrow* - BBT)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inatekeleza Programu ya kuwezesha ushiriki wa Vijana na Wanawake katika

kilimo biashara (*Building a Better Tomorrow Youth Initiative for Agribusiness* (BBT-YIA). Programu hii inalenga kuwezesha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo biashara ili kuwapatia ajira, kuongeza uzalishaji na kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza mchango wa sekta ya kilimo kwenye Pato la Taifa na kuinua hali ya maisha ya jamii ya Watanzania na kukuza sekta ya kilimo kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 (Ajenda 10/30).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kuwa, utekelezaji wa BBT unaenda sambamba na mipango na miongozo mingine ya Serikali ambayo ni Dira ya Taifa (2025), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (III) (2021/22 - 2025/26, Sera ya Kilimo (2013), Ilani ya Chama cha Mapinduzi, (2020 - 2025), Mkakati wa Vijana (NYSIA) 2016-2021 na ASDP II 2017 – 2028.

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina malengo ya Kimkakati yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha vijana na wanawake kwa kubadili mtazamo kuhusu kilimo biashara;

(ii) Kujengea uwezo vijana na wanawake kupitia mafunzo ya vitendo ya Kilimo Biashara;

(iii) Kushirikisha vijana na wanawake katika usimamizi wa biashara za kilimo chenye tija na faida endelevu;

(iv) Kuwezesha vijana na wanawake kibiashara kwa kuboresha mazingira ya kufanya biashara; na

(v) Kuratibu kwa ufanisi mipango mbalimbali inayotekelezwa na wadau ili kuwezesha kilimo biashara kwa vijana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kuwa, Programu ya BBT itatekelezwa kwa kipindi cha miaka minane. Lengo ni kuwezesha angalau biashara moja ya kilimo yenye faida na endelevu inayoongozwa na Vijana katika vijiji 12,000. Programu hii inatarajiwa kutengeneza ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata taarifa kuhusu mfumo wa utekelezaji wa programu ambapo vijana wanapatiwa mafunzo kwa muda wa miezi isiyopungua minne (4) kuhusu kilimo biashara. Baada ya mafunzo, wahitimu wanakabidhiwa mashamba yenye ukubwa kuanzia ekari 5 -10 kulingana na aina ya zao kwa ajili ya kuanza shughuli za uzalishaji kupitia mashamba makubwa ya pamoja (*Block Farms*).

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile, utoaji wa Mitaji kwa Vijana kupitia Programu unatolewa na Wizara kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF). Mfuko huu unatoa mikopo yenye riba nafuu (*soft loan*) yenye riba ya asilimia 4.5, kwa ajili ya kuwawezesha Vijana na Wanawake kushiriki katika Sekta ya Kilimo, kwa kutatua changamoto ya upatikanaji wa mitaji. Vijana wanaofanya shughuli za kilimo katika mnyororo wa thamani wa mazao wanahimizwa kutumia fursa hiyo muhimu ili waweze kukuza biashara zao.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zilionesha kuwa jumla ya maombi yaliyopokelewa ni 20,227. Kati ya maombi hayo, Maombi 4,722 sawa na asilimia 23.4 ya maombaji yote, yalikuwa ni ya wanawake. Aidha, maombi 15,493 sawa na asilimia 76.6 ya maombi yote yalikuwa ni ya wanaume. Baada ya uchambuzi na udahili wa maombi, jumla ya vijana 812 walichaguliwa. Kati yao, Wanawake ni 282 sawa na asilimia 34.73 na wanaume ni 530 sawa na asilimia 65.27 ya waliochaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Programu hii inahusisha vijana wenye umri wa **miaka 18 - 40** na elimu ya kuanzia darasa la saba hadi shahada ya uzamili (*Masters*). Hadi sasa mafanikio ya program hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuwezesha mafunzo ya kilimo biashara katika mnyororo wa thamani wa mazao kwa vijana 763 wa BBT kwa awamu ya kwanza;

(ii) Kuandaa mashamba kwa ajili ya uzalishaji wa mazao kwa vijana yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 4,400, kuandaa miundombinu ya umwagiliaji na kuanza ujenzi wa nyumba

100 katika Shamba la Ndogowe na nyumba 46 katika Shamba la Chinangali II; na

(iii) Kuwezesha Vijana kupata mikopo zaidi ya **shilingi milioni 100** wanaojishughulisha na kilimo biashara katika mnyororo wa thamani ya mazao.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hayo, ipo changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa programu kwa wakati. Athari ya changamoto hiyo ni kuchelewa kwa baadhi ya shughuli.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uchambuzi wa kina, Kamati ina mtazamo kwamba, program hii inaweza kuleta tija zaidi ikiwa itawekewa mikakati madhubuti ya usimamizi katika hatua zote za utekelezaji. Hatua hiyo itafanikisha mpango wa Serikali kuwawezesha Vijana kujikwamua kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Idadi ya wanawake wanaoshiriki kwenye programu bado ni ndogo, ikizingatiwa kwamba, wao ndio wanaoshiriki kwa wingi katika shughuli za kilimo nchini. Aidha, ili kuepuka migogoro ya ardhi pale programu inapochukua ardhi, kuna umuhimu kwa Serikali kuwashirikisha wananchi kupitia viongozi wao. Jambo hili linawezekana kwa kuwapa elimu kuhusu miradi ya BBT inayoanzishwa kwenye maeneo yao.

h) **Kampuni ya Mbolea Tanzania - TFC**

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Mbolea ilianzishwa tarehe 6 Julai, 1968 chini ya Sheria ya Makampuni (Companies Ordinance CAP 212) ambayo kwa sasa inafahamika kama Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 (Companies Act 2002 CAP 212). Kamati ilifahamishwa kuwa, Kampuni hii ipo chini ya Wizara ya Kilimo na inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 ambapo uendeshaji wake unazingatia Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya mbolea inatekeleza majukumu yafuatayo kisheria:-

(i) Kuagiza, kusambaza na kuuza aina zote za mbolea za kilimo zitumikazo hapa nchini;

(ii) Kusaidia kutoa taarifa za kitaalam zinazohusiana na uzalishaji, ubora na viwango vya mbolea ndani na nje ya nchi;

(iii) Kushirikiana na taasisi za utafiti katika kufanya utafiti juu ya masuala ya mbolea na pembejeo nyingine za kilimo hapa nchini; na

(iv) Kuanzisha viwanda vya kuzalisha na kuchanganya mbolea.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongezea Kampuni ya Mbolea Tanzania mtaji wa kutoka **shilingi Bilioni 6** hadi kufikia **shilingi bilioni 40** kwa ajili ya kuiwezesha kufanya biashara ya mbolea.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Mbolea Tanzania inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Upungufu wa vyombo vya usafiri katika kuwezesha uratibu na usimamizi wa biashara. TFC ina magari madogo mawili (2) ambayo yanatumika Makao Makuu kwa ajili ya Ofisi;

(ii) Kampuni haina magari makubwa ya kusambaza mbolea kwenye vituo vya mauzo na hivyo kulazimika kukodi magari binafsi;

(iii) Uchakavu wa miundombinu ya kuhifadhi mbolea, majengo ya Ofisi na makazi ya wafanyakazi;

(iv) Taratibu za manunuzi zilizowekwa na Serikali zimeendelea kuwa kikwazo na kuzinyima Kampuni/Taasisi za Serikali zinazofanya biashara kushindwa kuonesha ushindani katika biashara;

(v) Ufinyu wa nafasi katika Ofisi za Makao Makuu yaliyopo Masaki Chole Road, Dar es Salaam kulingana na idadi ya wafanyakazi waliopo; na

(vi) Uhaba wa vitendea kazi zikiwemo kompyuta na samani.


**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Changamoto zote zilizotajwa zitaendelea kupatiwa ufumbuzi ili kuiwezesha Kampuni kufanya biashara kiushindani.

i) **Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo Tanzania (Tanzania Agricultural Inputs Support Project - TAISP)**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Kilimo inatekeleza Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo Tanzania (*Tanzania Agricultural Inputs Support Project - TAISP*). Utekelezaji huo unafanyika kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank-AfDB*) na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (*Japan International Cooperation Agency-JICA*). Lengo la Mradi huu ni kuongeza uzalishaji na tija katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele ya Alizeti, Ngano na Mpunga.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zilibainisha kuwa, Mradi huu unatekelezwa katika kipindi cha miaka sita (6) (2022/23-2027/28) na utagharimu jumla ya **Dola za Marekani Milioni 154.06.** Fedha hizi zinachangiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **(Dola za Marekani Milioni 10.61)** kupitia Bajeti ya Wizara ya Kilimo, misamaha ya kodi na mishahara ya watumishi; AfDB (**Dola za Marekani Milioni 73.45)** ikiwa ni mkopo na msaada na JICA (**Dola za Marekani Milioni 70.00)** ikiwa ni mkopo**.**

**Mheshimiwa Spika,** takwimu hizo zinaonesha kuwa sehemu kubwa ya gharama za mradi huo inategemewa kutoka kwa wahisani. Bajeti inayotengwa na Serikali kwa ajili ya programu hiyo, kiasi cha misamaha ya kodi kinachochangia kwenye mradi na mishahara ya watumishi kwa pamoja ni asilimia 7 tu kama inavyoonekana katika grafu.




**Mheshimiwa Spika**, Taarifa pia zilionesha maeneo makuu matatu (*components*) yatakayotekelezwa na Mradi huu. Maeneo hayo ni:-

(i) Uzalishaji wa Chakula kuongezwa kwa kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora zinazohimili mabadiliko ya Tabianchi;

(ii) Ugharamiaji wa upatikanaji na uwezo wa kumudu gharama za mbolea;

(iii) Mazingira wezeshi ya kisera na uimarishaji wa Taasisi; na

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla wake, Mradi huu unatarajiwa kuwa na matokeo makuu matatu ambayo ni:-

(i) Ongezeko la upatikanaji na uwezo wa kumudu gharama ya mbegu za Alizeti, Ngano na Mpunga ambazo ni stahimilivu kwa mabadiliko ya tabia nchi;

(ii) Ongezeko la upatikanaji na uwezo wa kumudu gharama za mbolea kwa wakulima; na

(iii) Ongezeko la uwekezaji wa sekta binafsi katika upatikanaji wa mbolea na mbegu bora kwa wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla Mradi wa TAISP unalenga kutoa ruzuku ya mbolea na mbegu bora za mazao ya ngano, alizeti na mpunga ili kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji na kuongeza tija na faida. Mradi pia unatarajia kunufaisha kaya 1,200,000 za wakulima wadogo (wenye wastani wa hekta 2) zenye jumla ya wakulima 4,800,000 wakiwemo asilimia 40 ya vijana na wanawake.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umeonesha kuwa mradi huu unaweza kuwanufaisha Watanzania 1,000 wakiwemo wazalishaji wadogo na wa kati wa mbegu, na wauzaji wa pembejeo za kilimo. Vilevile, mradi huu unaweza kuwasaidia vijana 10,000 wa kike na kiume wasio na ajira kupitia mnyororo wa thamani wa mazao husika.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zilionesha kwamba, Mradi wa TAISP umefanikiwa kupitia kazi mbalimbali. Kwa mfano, katika Ukaguzi wa Maduka ya Mbegu kwa mwaka 2022/2023, maduka 454 ya mawakala wanaouza na kusambaza mbegu bora nchini katika Halmashauri za Wilaya 23 yalifanyiwa ukaguzi na uhakiki.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio yaliyoanza kupatikana katika utekelezaji wa Mradi wa TAISP, Kamati imebaini kuwa Mradi unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Kutosajiliwa kwa baadhi ya wakulima kwenye mfumo ni miongoni mwa changamoto inayowakosesha wakulima uwezekano wa kupata mbolea za ruzuku. Hali hii inawapunguzia uwezekano wa kuongeza mavuno kwenye mazao.

(ii) Mbolea kutokufika kwenye baadhi ya maeneo hususan vijijini. Kamati inaona changamoto hii inaweza kutatuliwa kwa Serikali kuweka mikakati ya kufikisha mbolea kwenye maeneo mengi zaidi hususan vijijini ili wakulima wengi waweze kunufaika na mbolea hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na umuhimu wa Mradi huu wa Kuwezesha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo Tanzania (*Tanzania Agricultural Inputs Support Project – TAISP*) ambao kwa

sasa unahudumia mikoa 14 na Halmashauri 56 pekee nchini, ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione namna ya kupanua wigo wa utekelezaji wa Mradi huu mikoa mingi zaidi nchini kulingana na aina ya mazao yanayostawi ili kuongeza tija na kuwasaidia wakulima kunufaika na Mradi kiuchumi.

j) **Wakala wa Mbegu za Kilimo (Agriculture Seed Agency- ASA)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) ulianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Namba 30 ya mwaka 1997 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2009, na kuzinduliwa rasmi tarehe 23 Juni, 2006 ikiwa ni Taasisi ya Serikali inayoshirikiana na Sekta ya Umma na binafsi katika mfumo wa uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora hapa nchini. Lengo kuu la kuanzishwa kwa ASA ni kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima kwa bei nafuu.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Mbegu za Kilimo una majukumu makuu manne (4) ambayo ni kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora; kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora; kuhamasisha wakulima kutumia mbegu bora; na kushirikiana na vituo vya utafiti ili kuhakikisha mbegu mpya zinazalishwa na kusambazwa kwa wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala katika utekelezaji wa majukumu yake, umepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Kuongeza idadi ya mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora. Katika mwaka 2020/21 Wakala uliongeza mashamba manne yenye jumla ya hekta 5,586.8 ya Msungura (hekta 100), Mazizi (hekta 4.8), Namtumbo (hekta 3,580) Kilimi (hekta 1,102) na Luhafwe (hekta 800);

(ii) Uzalishaji wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 3,033 mwaka 2020/21 hadi tani 3,502 mwaka 2022/23;

(iii) Wakala umeongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 400 kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia hekta 1,400.5 mwaka 2022/23;

(iv) Wakala umeweza kuongeza usimamizi wa mbegu, kuongeza usafi na ubora wa mbegu kwa kiasi kikubwa. Mwaka 20219/20 Wakala umeweza kujenga maabara ya upimaji wa mbegu (ASA Seed Quality Control Lab) ili kuimarisha zaidi ubora wa mbegu ndani ya Taasisi;

(v) Wakala umeweza kuongeza mitambo ya uchakataji kutoka mitambo mitatu (3) kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia mitambo saba (7) ya usafishaji na uchakataji wa mbegu kwa mwaka 2021/22;

(vi) Wakala umeweza kuongeza zana na vifaa mbalimbali ambavyo ni muhimu katika uzalishaji wa mbegu ikiwemo magari na matrekta;

(vii) Wakala umeweza kuongeza ushirikiano na sekta binafsi katika nyanja mbalimbali ikiwemo, kutumia mashamba ya Wakala katika uzalishaji wa mbegu hasusan Kampuni zinazomilikiwa na wazawa, kutumia mitambo ya Wakala katika uchakataji wa mbegu na kubadilishana uzoefu katika uzalishaji wa mbegu;

(viii) Wakala umeongeza kiasi cha mbegu zinazozalishwa na kusambazwa kutoka tani 1,680 mwaka 2020/21 hadi tani 2,667 mwaka 2022/23. Aidha, Wakala umeongeza vituo vya mauzo ya mbegu kutoka vitano (5) mwaka 2020/21 hadi kufikia vituo 11 mwaka 2022/23;

(ix) Idadi ya mawakala imeongezeka kutoka mawakala 10 mwaka 2020/21 hadi kufikia mawakala 55 mwaka 2022/23;

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umebainisha kuwa pamoja na mfanikio yaliyopatikana, wakala unakabiliwa na changamoto ambazo kimsingi zinachelewesha kufikia malengo yaliyokusudiwa. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

(i) Mabadiliko ya tabianchi ambayo yameleta changamoto kwenye uzalishaji wa mbegu kama vile kubadilika kwa misimu ya mvua, mtawanyiko usio sawa wa mvua, milipuko ya visumbufu vya mazao, uharibifu wa miundombinu ya

shamba pale mvua zinapozidi pamoja na kupotea kwa virutubisho ardhini;

(ii) Upungufu wa watumishi ikilinganishwa na ongezeko la maeneo ya uzalishaji chini ya Wakala;

(iii) Uhaba wa vitendea kama vile, magari na pikipiki kwa ajili ya kusimamia na kusambaza mbegu; na

(iv) Uelewa mdogo wa matumizi ya mbegu hali inayochangia wakulima kutozalisha kwa tija.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, ukosefu wa bajeti ya kutosha ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo pamoja na mtiririko wa utolewaji wa fedha usioridhisha toka Hazina umeathiri utendaji kazi wa Wakala. Aidha, utegemezi wa maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji wa mashamba ya mbegu umesababisha uzalishaji kushuka kwa kiasi kikubwa. Vilevile, mashamba ya mbegu yanakabiliwa na uvamizi wa wananchi wanaoyazunguka kutokana na kukosekana kwa uzio na kuhatarisha usalama wa mbegu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua nia njema ya Serikali kuanzisha Wakala hii. Ni matarajio ya Kamati kwamba, Serikali itazingatia ushauri wa Kamati wa kuiwezesha Wakala hii kibajeti na fedha kupatikana kwa wakati ili kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, Serikali iiongezee uwezo TARI ifanye utafiti wa mbegu za msingi ambazo ASA itazalisha na kusambaza kwa wakulima.

**2.2.3 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi**

(a) **Hali ya Sekta ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Uvuvi inajumuisha shughuli za uvuvi katika maji ya asili na ukuzaji viumbe maji. Uvuvi wa maji asili hufanyika katika eneo la maji baridi, bahari na maeneo mengine ya maji yanayojumuisha maziwa madogo, mito na mabwawa. Eneo la bahari limegawanyika katika eneo la Maji ya Kitaifa *(Territorial Sea)* na lina ukubwa wa takribani kilometa za mraba 64,000, pamoja na eneo la Bahari Kuu *(Exclusive Economic Zone)* lenye ukubwa wa takribani kilometa za mraba 223,000.

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Sheria za Uvuvi na Notisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Majukumu kwa Mawaziri ya mwezi Mei, 2021 kwa pamoja zinaielekeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) kutekeleza majukumu mengi ikiwemo yafuatayo: -

(i) Kutayarisha, kufanya mapitio na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango na Mikakati ya kuendeleza Sekta ya Uvuvi;

(ii) Kuimarisha usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi na utunzaji wa mazingira;

(iii) Kuboresha uthibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi;

(iv) kuendeleza na kuimarisha utafiti katika maeneo ya uvuvi, ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za mafunzo na ugani;

(v) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi, uhifadhi na usambazaji wa takwimu za uvuvi;

(vi) Kuendeleza na kusimamia miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji;

(vii) Kuendeleza, kusimamia na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na miundombinu yake;

(viii) Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii za wavuvi na wadau wengine katika kulinda, kusimamia na kuendeleza Sekta ya Uvuvi;

(ix) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi na Kusimamia uendelezaji wa mazao yatokanayo na uvuvi; na

(x) Kuimarisha ushirikiano na Taasisi za Kikanda na Kimataifa zinazosimamia Sekta ya Uvuvi hususan kwenye maeneo ya maji yanayomilikiwa kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na udadisi wa Kamati, ilibainika kuwa Sekta ya uvuvi inakabiliwa na changamoto, ikiwemo zifuatavo:-

(i) Ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi. Hali hii imesababisha kupungua kwa samaki katika bahari, maziwa na mito, uharibifu wa mazalia ya samaki na mazingira kwa ujumla;

(ii) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa (Post - Harvest Losses) unaokadiriwa kufikia asilimia 30 – 40 hususan katika maeneo ya vijijini;

(iii) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa Bahari Kuu na usindikaji wa mazao ya uvuvi unaathiri mchango wa sekta katika Pato la Taifa;

(iv) Uhaba wa maafisa ugani wa uvuvi ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam hao katika Halmashauri; na

(v) Uhaba wa vifaranga bora na vyakula vya samaki vyenye ubora.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto hizi katika Sekta ya Uvuvi zimekuwepo kwa muda mrefu sasa na zinaendelea kuzorotesha sekta na hivyo kuinyima fursa ya kuchangia kwa ukubwa katika Pato la Taifa. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ikamilishe uanzishwaji wa Mamlaka mpya za usimamizi wa utekelezaji wa Miradi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambapo kwa upande wa Sekta ya Mifugo pamoja na mambo mengine, wahusike na kusimamia mabwawa ya mifugo, majosho, minada, malambo, visima n.k.; na kwa upande wa Sekta ya Uvuvi ianzishe Mamlaka itakayoratibu shughuli zote za uvuvi baharini, kwenye maziwa, mito na mabwawa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa upo umuhimu kwa Serikali kufanya mapitio ya tozo katika Sekta ya Uvuvi na kuona namna ya kuzipunguza au kuunganisha baadhi ya tozo. Msingi wa maoni hayo ni kuwa, tozo hizo zimekuwa kero kubwa kwa

wavuvi hali inayochangia utoroshaji wa mazao ya uvuvi (samaki) nje ya nchi na kuikosesha nchi fedha za kigeni.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa uvuvi wa dagaa ni biashara inayotegemewa na wavuvi wengi na pia inachangia fedha za kigeni nchini, bado inasababisha uharibifu wa mazalia ya samaki hasa sangara na dagaa. Kwa jambo hili, Serikali inahitaji kuangalia namna bora ya kuvua dagaa bila kuathiri mazalia ya samaki.

(b) **Hali ya Sekta ya Mifugo Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi ya pili kwa idadi ya ng'ombe Barani Afrika ikiwa na ng'ombe takribani milioni 36.6. Mifugo mingine iliyopo ni mbuzi milioni 26.6, kondoo milioni 9.1, kuku milioni 97.9, nguruwe milioni 3.7 na punda milioni 0.66.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zilionesha kuwa, Sekta inachangia asilimia 7 katika Pato la Taifa na asilimia 27 ya Pato la Sekta ya Kilimo hasa kutokana na nyama ya ng'ombe (40%), maziwa (30%) na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku (30%). Asilimia 33 ya kaya 9,109,150 nchini zinajihusisha na kilimo na mifugo na 2% zinajihusisha na shughuli za ufugaji tu *(National Panel Survey Data 2020/21)*.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kukuza Sekta ya Mifugo nchini Wizara imefanikiwa kufanya yafuatayo: -

(i) Ujenzi wa majosho 246 umekamilika kati ya majosho 257 katika Halmashauri;

(ii) Ujenzi na ukarabati wa mabwawa 14 yaliyopangwa upo katika hatua mbalimbali za ujenzi;

(iii) Ujenzi wa visima virefu 7 kwa ajili ya mifugo nao unaendelea na upo katika hatua mbalimbali za kukamilika, vikiwemo visima 6 vya NARCO kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho kwenye Ranchi ya Kongwa;

(iv) Kununua ng'ombe wazazi 2,160 kwa ajili ya NARCO (1,000) na LMUs (1,160) na madume 366 yaliyosambazwa kwa vikundi vya wafugaji;

(v) Kuanzisha mashamba darasa 100 ya malisho katika Halmashauri;

(vi) Vituo 10 vya kukusanya maziwa vilivyopangwa kujengwa vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi;

(vii) Vituo atamizi 8 vya BBT Mifugo vimeendelea na programu ya kuwafundisha vijana unenepeshaji wa ng'ombe;

(viii) Vifaa shamba pamoja na mifugo vimenunuliwa ili kuimarisha NARCO, kuimarisha tafiti za mifugo kupitia TALIRI, pamoja na tafiti za chanjo kupitia TVLA; na

(ix) Kuboresha Vyuo vya LITA na kuongeza idadi ya wataalam.

**Mheshimiwa Spika**, ili mafanikio halisi katika Sekta yaonekane, Kamati inaona kuna umuhimu wa kukamilisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006 ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa hasa yahusuyo mabadiliko ya teknolojia na mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Udadisi ulibainisha kuwa, katika kipindi cha miaka mitano (2018/2019 - 2022/2023) kazi ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo imefanyika kama ifuatavyo:-

(i) Magonjwa ya milipuko yamepungua kutoka matukio 5,203 hadi kufikia matukio 2,341. Uzalishaji wa chanjo umeongezeka kutoka dozi 55,555,750 hadi dozi 64,434,600;

(ii) Milipuko ya magonjwa yatokayo kwa wanyama kwenda kwa binadamu yamepungua kutoka milipuko 5 mwaka 2018 hadi milipuko 2 mwaka 2023. Aidha, Serikali imeandaa na inatekeleza Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD). Uchanjaji wa kuku wa kisasa umefikia asilimia 100 na uchanjaji kwa kuku wa kienyeji ni asilimia 40;

(iii) Serikali imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Kutokomeza Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa nchini kuanzia mwaka 2010 - 2030 ambapo takribani mbwa 827,238 wanachanjwa dhidi ya ugonjwa huo kila mwaka; na

(iv) Kiwango cha vifo vya mifugo kimeshuka kutoka asilimia 72 ya vifo vyote vya mifugo mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 52 mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, uboreshaji wa mbari za Mifugo umetekelezwa kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Nchi yetu ina mifugo mingi ambayo uzalishaji wake hauna tija ukilinganisha na mifugo iliyoboreshwa. Wizara inaendelea kukiimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kuzalisha mbegu za mifugo;

(ii) Wizara inaendelea kununua madume ya ng'ombe na kuyagawa kwenye vikundi vya wafugaji kuboresha mifugo. Pia, Wizara inaendelea kuhamasisha wafugaji kufanya uhimilishaji ili kuboresha tija ya mifugo na

(iii) Wizara inaendelea kuimarisha mashamba matano (5) ya mifugo ili kuzalisha mitamba kwa ajili ya kuwauzia wafugaji kwa ruzuku.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na Utekelezaji wa Programu ya BBT - Life & LGH kama ifuatavyo:-

(i) Inalenga kuongeza fursa za ajira kwa vijana na wanawake na kuongeza malighafi kwa viwanda vya nyama nchini, mafunzo yanatolewa kwa vijana na wanawake 240 katika unenepeshaji wa mifugo. Vilevile, **shilingi 4,640,000,000.00** zimetumika kujenga miundombinu na kuwezesha kila mnufaika kununua ng'ombe 10;

(ii) Mwaka 2023/2024 vinaanzishwa vituo vipya 8 vya BBT-Mifugo kwa ajili ya vijana 932 kunenepesha ng'ombe, mbuzi na

kondoo; kuzalisha malisho na ufugaji bora wa mbuzi na kondoo;

(iii) Hekta 7,800 zimetengwa katika ranchi za Kagoma, Kitengule, Usangu na Mkata zitakazotumika watakapomaliza muda wa mafunzo kwa vitendo; na

(iv) Kwa kushirikiana na Digital Media Africa (DMA) na Master Card, BBT inaingia masoko ya kimtandao pia katika ranchi hizo inaanzishwa Livestock Guest Housing. Mfumo huu unapangisha mifugo kwa muda maalum na baada ya muda huo huondolewa kwa ajili ya uvunaji.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi ulionesha kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika Mradi wa BBT. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Uwepo wa soko la uhakika la ng'ombe wanaonenepeshwa;

(ii) Uwepo wa malisho ya kutosha kutokana na uvamizi wa mara kwa mara wafugaji jirani na vituo atamizi kutokana na kutokuwepo kwa ulinzi wa uhakika pamoja na makazi ya vijana karibu na maeneo ya miradi;

(iii) Baadhi ya vijana kuonesha weledi na ari ndogo ya kutekeleza mafunzo kwa vitendo. Hii imetokana na vijana kuchaguliwa kwa kuzingatia sifa za elimu bila kuhusisha nia ya vijana hao kushiriki katika programu hii;

(iv) Nakisi ya fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa vituo. Ni asilimia 74 ya bajeti iliyotengwa kuendeshea vituo ndiyo iliyopokelewa kutoka Hazina; na

(v) Ongezeko la vijana wengi zaidi wanaoomba kujiunga na Programu ya BBT - LIFE kuliko uwezo wa vituo vilivyopo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na nchi yetu kuwa na mifugo mingi bado Kamati haijaona tija na mchango mkubwa wa sekta hii katika pato la Taifa. Pamoja na mafanikio yaliyoelezwa, kuna haja ya kuanzisha viwanda vinavyotokana na mazao ya mifugo.

Viwanda hivyo ni kama vile, viwanda vya Ngozi, nyama na maziwa ili kuongeza thamani ya mifugo hapa nchini.
Kamati pia ina maoni kuwa, Serikali inapaswa kuimarisha mfumo wa kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo na kufanikisha uuzaji wa mazo hayo nje ya nchi. Kwa kufanya hivyo, thamani ya mazo hayo itaongezeka na nchi itapata fedha za kigeni kupitia rasilimali hizo.

(c) **Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO**

**Mheshimiwa Spika**, TAFICO ilianzishwa kupitia Amri ya Rais (*Establishment Order*) ya mwaka 1974 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969 na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 58 la tarehe 01 Machi, 1974, Toleo la II. Lengo kuu la kuanzishwa kwa TAFICO lilikuwa ni kuendeleza uvuvi wa kibiashara na Sekta ya Uvuvi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika hili linatekeleza majukumu muhimu katika kutoa huduma jumuishi za usaidizi wa maendeleo ya Sekta ya Uvuvi nchini kama ifuatavyo: -

(i) Kukuza maendeleo ya Sekta ya Uvuvi nchini;

(ii) Kufanya uvuvi, ufugaji wa samaki, kununua, kutafuta masoko, kuuza aina zote za samaki na mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi;

(iii) Kushiriki katika kuhamasisha uanzishwaji na uendelezwaji wa maendeleo ya uvuvi wa kitaifa na kimataifa unaolenga kuendeleza Sekta ya Uvuvi na mazao yake;

(iv) Kushiriki na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya uchakataji wa samaki, chakula cha samaki, vifaa vya uvuvi na kuongezwa thamani ya mazao ya uvuvi;

(v) Kushiriki au kuanzisha ubunifu wowote wa kibiashara unaohusiana na Sekta ya Uvuvi; na

(vi) Kuhamasisha au kuchangia katika utafiti wa masuala yanayohusiana na Sekta ya Uvuvi ikilenga kuongeza thamani ya soko la samaki na mazao ya uvuvi.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa majukumu yake, TAFICO imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Mtambo wa kuzalisha barafu umenunuliwa, wenye uwezo wa kuzalisha tani 5 kwa siku pamoja na kengevuke ya kuendesha mtambo huo ikiwa ni nishati mbadala wakati wa uhaba;

(ii) Taratibu za kumpata mkandarasi/mzabuni wa kukarabati miundombinu ya uzalishaji ya Shirika iliyopo Ras Mkwavi, Kigamboni, Dar es Salaam, zimekamilika na ukarabati ulitarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2023;

(iii) Kufikisha Mkongo wa Taifa wa mtandao katika Ofisi za TAFICO ambao umefanikisha kuwepo na mawasiliano bora na kuliwezesha Shirika kujiunga na mifumo ya mtandao Serikalini;

(iv) Tovuti ya Shirika https://www.tafico.co.tz/ imeanzishwa ambapo wadau mbalimbali wamekuwa wakipata taarifa na pia kuwawezesha wadau wa sekta binafsi kuona fursa mbalimbali za uwekezaji; na

(v) Shirika limefanya tathmini ya mali zake zilizopo katika Mkoa wa Dar Es Salaam zenye thamani ya Tshs. 108 Bilioni. Aidha, zoezi la uthamini wa mali za TAFICO zilizopo katika mikoa mingine ya Tanzania Bara bado linaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio yaliyopatikana TAFICO inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo: -

(i) Vitendea kazi na miundombinu wezeshi ya uzalishaji ya TAFICO kutotosheleza mahitaji yaliyopo;

(ii) Utegemezi wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kunachelewesha utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa kuwa bado halijaanza uzalishaji; na

(iii) Uwepo wa mabaki ya Meli ya MV Tawariq 1 kwenye eneo la TAFICO la RAS Mkwavi ambao unakwamisha kuanza kwa ukarabati wa Gati. Kutokuondolewa kwa mabaki ya Meli hii kunakwamisha TAFICO kufanya shughuli zake kwa ufanisi za kuongeza mapato ya Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi unaonesha kuwa, Serikali inahitaji kukamilisha zoezi la kuhamisha mabaki ya meli ya MV Tawariq 1 kwenye eneo la TAFICO la RAS Mkwavi. Kutokamilika kwa zoezi hilo kunachelewesha ukarabati wa Gati na kukwamisha manufaa ya gati hilo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Mtazamo na Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na Shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2023 Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama yalivyoelezwa Sehemu ya Pili katika taarifa hii. Kutokana na matokeo hayo Kamati ina mtazamo na maoni ya Jumla kama ifuatavyo:-

(i) Suala la baadhi ya Vituo vya Pamoja vya Mipakani kukosa mashine za Ukaguzi linahitaji kupatiwa ufumbuzi;

(ii) Mfumuko wa bei nchini unaogusa bidhaa muhimu kwa maisha ya watu unahitaji mikakati madhubuti na ya muda mrefu ya Serikali ili kudhibiti madhara yake kwa wananchi na kwa uchumi wa nchi;

(iii) Upungufu wa sukari nchini usipochukuliwa hatua madhubuti utaendelea kuathiri maisha ya wananchi kinyume na matarajio yao;

(iv) Upungufu wa malighafi za uzalishaji wa mafuta ya kula unapaswa kushughulikiwa ili kusimamia Urari wa fedha za kigeni nchini na kudhibiti ongezezeko la bei ya mafuta ya kula;

(v) Upatikanaji na Matumizi ya viuatilifu nchini ni jambo linalostahili hatua madhubuti za Serikali ili kuimarisha usalama wa chakula, afya ya jamii na kukuza Pato la Taifa

(vi) Changamoto ya uzalishaji wa mbegu nchini inaweza kutatuliwa kwa kuongeza uwezo wa Wakala wa Mbegu za Kilimo;

(vii) Upungufu wa mbolea nchini hauna budi kukabiliwa kwa juhudi za Serikali na kwa ushirikiano na Sekta binafsi;

(viii) Tija ndogo ya Sekta ndogo ya umwagiliaji inayotokana na miundombinu duni na wataalamu wachache ni vyema ikatatuliwa na serikali ili kuongeza uzalishaji katika Sekta ya Kilimo;

(ix) Tija, Ufanisi na Manufaa ya Ushirika nchini vinaweza kuimarika kwa kufanya maboresho ya Sheria na Sera zinazosimamia masuala ya Ushirika;

(x) Hasara inayosababishwa na Wakandarasi na Washauri Elekezi wenye uwezo mdogo inapaswa kuepukwa kwa kuzingatia taratibu stahiki za upatikanaji wa wataalamu na Washauri Elekezi;

(xi) Changamoto ya kuchelewa kwa mbolea katika baadhi ya maeneo nchini au kutokufika kabisa kwa mbolea kwa maeneo mengine ya nchi na tofauti ya bei ya mbolea kwa wakulima wa nchi moja katika maeneo tofauti si jambo jema na linahitaji ufumbuzi;

(xii) Malalamiko ya wananchi kuhusu Sekta ya Uvuvi yanayotokana na hatua za Serikali kudhibiti uvuvi usiozingatia uendelevu yanastahili kufanyiwa kazi ikiwemo kujenga ufahamu kuhusu ufugaji wa samaki na kushughulikia kero na usumbufu wa tozo mbalimbali kwa shughuli za uvuvi;

(xiii) Suala la ukuzaji wa mnyororo wa thamani ya mazao ya mifugo lisipofanyiwa kazi inavyostahili maisha ya wafugaji

yataendelea kuwa duni, mchango wa Sekta ya mifugo utaendelea kuwa mdogo.

(xiv) Sera, Sheria na Kanuni zinazotumika katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, zisipofanyiwa mapitio zitaendelea kuweka misimamo iliyopitwa na wakati, kuweka masharti yasiyoendana na hali halisi na kuweka taratibu zisizikidhi mahitaji. Aidha, Sera, Sheria na Kanuni hizo za kila Sekta zisipofungamanishwa na miongozo, mashati na taratibu za Sekta nyingine kati ya hizo zitakosesha manufaa ya kiuchumi ya Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo na Uvuvi.

**3.2 Mapendekezo**

**3.2.1 Vituo vya Pamoja vya Mipakani (*OSBP*) Kukosa mashine za Ukaguzi**

**KWA KUWA,** Mashine za ukaguzi (**scanner machines**) ni muhimu katika vituo vya pamoja vya mipakani, lakini vituo vingi ninakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mashine hizo,

**NA KWA KUWA,** Changamoto hiyo inapunguza tija kutokana na kusababisha,

(i) Ugumu katika kudhibiti bidhaa zinazoingia nchini;

(ii) Ongezeko la gharama na muda wa ukaguzi.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ianze kutenga bajeti ya kununua mashine hizo na kuzisambaza katika vituo vya mipakani.

**3.2.2 Mfumuko wa Bei Nchini**

**KWA KUWA,** Mfumko wa bei unaoendelea kwa sehemu kubwa unagusa bidhaa muhimu, zikiwemo bidhaa za chakula kama vile sukari, ngano, mchele, mahindi, maharage na vitoweo (nyama, Samaki),

**NA KWA KUWA,** Bidhaa muhimu kwa maisha ya watu zinapoguswa na mfumko wa bei zinagharimu maisha ya mtu mmoja mmoja, jamii, uchumi wa taifa na ustawi wa watu kwa ujumla,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ifanye tathmini ya hali ya mfumko wa bei nchini na kuchukua hatua za haraka ili kupunguza madhara yake katika uchumi na maisha ya watu; na

(ii) Serikali iweke mikakati ya muda mrefu ya kuzuia Mfumko wa bei na kudhibiti madhara yake.

**3.2.3 Upungufu wa Sukari nchini**

**KWA KUWA**, Hali ya Jumla ya upatikanaji wa sukari inaonesha upungufu mkubwa wa bidhaa hiyo katika baadhi ya maeneo nchini,

**NA KWA KUWA**, Upungufu huo unasababisha kupanda kwa bei ya sukari, jambo ambalo: -

(i) Linaathiri uzalishaji katika viwanda vinavyotumia bidhaa za sukari ikiwa ni sehemu ya malighafi; na

(ii) Linapunguza uwezo wa wananchi walio wengi kumudu ununuzi wa sukari kwa matumizi yao ya kila siku,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua haraka, madhubuti na za kudumu kuhakikisha upatikanaji wa sukari ili kukidhi mahitaji.

**3.2.4 Upungufu wa Malighafi za Uzalishaji wa Mafuta ya Kula Nchini**

**KWA KUWA**, Uhaba wa malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya chakula umechangia uzalishaji wa kiasi cha tani 205,000 ambacho ni kidogo ikilighanishwa na mahitaji halisi ya tani 570,000 kwa mwaka,

**NA KWA KUWA**, Upungufu huo wa mafuta unaotokana na uhaba wa malighafi, unachangia ongezeko la matumizi ya fedha za kigeni kwa kuagiza mafuta kutoka nje na hivyo kusababisha athari katika Urari wa Fedha za Kigeni

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali -

(i) Iongeze juhudi za kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu ya ASA ili kuongeza upatikanaji wa alizeti ambazo ni malighafi muhimu;

(ii) Iongeze ruzuku ya mbegu bora za alizeti kwa wakulima wengi zaidi ili kuhamasisha uzalishaji wa zao hilo; na

(iii) Ihamasishe Sekta Binafsi kuwekeza katika kilimo cha malighafi nchini ili kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje ya nchi.

**3.2.5 Upungufu wa Viuatilifu Nchini**

**KWA KUWA,** Upungufu wa viuatilifu nchini unaathiri uzalishaji wa chakula na Afya ya Jamii,

**NA KWA KUWA**, Juhudi za kukabiliana na upungufu huo zinaathiri uchumi wa nchi kutokana na: -

(i) ongezeko la matumizi ya fedha za kigeni unaotokana na kuagiza viuatilifu kutoka nje ya nchi kwa lengo la kupunguza uhaba,

(ii) kuvurugika kwa uwiano wa biashara ya kigeni (*Balance of trade*) na uwiano wa malipo ya fedha za kigeni (*Balance of Payment*) kwa sababu ya kupungua kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi ikilinganishwa na ununuzi wa viuatilifu kutoka nje ya nchi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Ijenge viwanda vya kutengeneza viuatilifu nchini ili kupunguza utegemezi wa viuatilifu toka nje ya nchi;

(ii) Iweke utaratibu mzuri wa kudhibiti matumizi ya dawa katika uzalishaji wa mazao ya vyakula ili kusimamia usalama wa chakula inavyostahili;

(iii) Iongeze na kuimarisha mafunzo ya mara kwa mara kwa Maafisa Kilimo ili kuboresha ufanisi wa huduma wanazozitoa;

(iv) Iendelea kuwatumia Maafisa Kilimo kwa ajili ya kuwaelimisha wakulima juu ya umuhimu wa kutumia viuatilifu; na

(v) Itumie ndege zisizo na rubani ili kumwaga dawa za kuua wadudu waharibifu na magugu vamizi inapobidi.

### 3.2.6 Athari za Changamoto ya Wakala wa Mbegu za Kilimo – ASA katika Uzalishaji wa Mbegu

**KWA KUWA**, Wakala wa Mbegu za Kilimo inakabiliwa na changamoto za kiuendeshaji kama vile -

(i) Maeneo yake kuvamiwa;
(ii) Mtaji mdogo wa uzalishaji;
(iii) Kutopata fedha kwa wakati; na
(iv) Upungufu wa vitendea kazi na nyingine,

**NA KWA KUWA**, Changamoto hizo zinaathiri -

(i) Uwezo wa Wakala kuzalisha mbegu bora; na
(ii) Upatikanaji wa mbegu bora kwa wakati,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali: -

(i) Iweke mikakati ya kujenga uzio katika mashamba ya mbegu yanayomilikiwa na ASA ili kuzuia uharibufu unaoweza kutokea;

(ii) Iwezeshe Wakala wa Mbegu kununua ardhi na kuimiliki kisheria ili kuepuka migogoro ya ardhi na wananchi wanaozunguka mashamba hayo;

(iii) Iweke mikakati ya kushirikiana na Sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu, ili kuongeza uzalishaji na kuimarisha upatikanaji wa mbegu zinazozalishwa nchini;

(iv) Iiwezeshe Wakala kuzalisha mbegu ipasavyo na kuzifikisha kwa wakulima kwa wakati;

(v) Iipatie Wakala wa Mbegu vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari na pikipiki kwa ajili ya kusimamia na kusambaza mbegu ili kupunguza gharama za kukodi malori kwa ajili ya usambazaji wa mbegu; na

(vi) Iiwezeshe na kusimamia utoaji wa elimu kuhusu matumizi ya mbegu bora ili kuwasaidia wakulima wenye uelewa mdogo wa matumizi ya mbegu bora.

### 3.2.7 Upungufu wa Mbolea Kutokana na kuwepo kwa kiwanda Kimoja Nchini

**KWA KUWA, mbolea inayozalishwa nchini haikidhi mahitaji halisi** ya tani 1,000,000 za mbolea kwa mwaka;

**NA KWA KUWA,** Hali hiyo inachangia utegemezi wa mbolea inayonunuliwa kutoka nje ya nchi jambo ambalo: -

(i) Linaongeza matumizi ya fedha za kigeni na kuathiri uwezo wa uchumi wa nchi; na katika fedha za kigeni; na

(ii) Linaongeza gharama kutokana na kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iweke mikakati ya kuanzisha viwanda vya mbolea nchini pamoja na kuboresha uzalishaji kwenye viwanda vilivyopo ili kukidhi mahitaji ya mbolea nchini; na

(ii) Ihamasishe na kuhimiza sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vyambolea nchini.

### 3.2.8 Mchango mdogo wa tasnia ya umwagiliaji katika sekta ya Kilimo

**KWA KUWA**, Tasnia ya umwagiliaji imebainika kuwa na mchango mdogo katika sekta ya Kilimo kutokana na:-

(i) Ufinyu wa Bajeti na ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

(ii) Idadi ndogo ya wataalamu wa umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya; na

(iii) Upungufu wa mitambo na magari ya umwagiliaji,

**NA KWA KUWA**, Changamoto hizo zinakwamisha tija iliyokusudiwa na kusababisha uzalishaji mdogo wa sekta ya kilimo,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iongeze fedha za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji. Aidha, fedha zilizotengwa zitolewe kwa wakati;

(ii) Serikali iajiri Wataalam wa umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya ili kuimarisha usimamizi wa miradi ya umwagiliaji;

(iii) Serikali inunue mitambo na magari kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji.

### 3.2.9 Upungufu katika Mfumo wa Kisheria wa Masuala ya Ushirika Nchini

**KWA KUWA**, Mfumo wa Kisheria wa uendeshaji wa masuala ya ushirika nchini unategemea Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 na Kanuni zake na kwamba Sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2008 na Kanuni zake zimeonekana kuwa na upungufu,

**NA KWA KUWA**, upungufu wa Sheria na Kanuni hizo umedhoofisha utaratibu na usimamizi wa dhana ya ushirika nchini,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Ikamilishe mchakato wa mapitio ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 ili kupendekeza maboresho katika mfumo wa Sheria; na

(ii) Iharakishe mchakato wa kuboresha Sera ya Ushirika ya mwaka 2002 ili kubainisha masuala ya kisera (*policy issues*) yanayohitaji matamko ya kisera (*Policy statement*).

### 3.2.10 Changamoto za Wakandarasi na Wataalamu Elekezi

**KWA KUWA**, utaratibu wa kuwatumia wakandarasi na Wataalamu Elekezi katika utekelezaji wa miradi unalenga kufanikisha miradi hiyo kwa namna ilivyokusudiwa,

**NA KWA KUWA**, Wakandarasi na Wataalamu Elekezi wasiokidhi vigezo ikiwemo uwezo mdogo wa kifedha wanachelewesha miradi na kuathiri ubora kutokana na kutokuwa na fedha jambo ambalo: -

(i) Linasababisha ongezeko la gharama kutokana na kuchukua muda mrefu;

(ii) Linachelewesha upatikanaji wa tija ya mradi tofauti na malengo yaliyowekwa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali: -

(i) Isimamie utaratibu wa kujiridhisha kabla ya kukabidhi mradi kwa Wakandarasi ili kuepuka uwezekano wa Wakandarasi wasio na uwezo kupewa kazi na kusababisha hasara na usumbufu usio wa lazima; na

(ii) Iweke Wataalam Elekezi wenye uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha na kwa wakati ili kupata tija iliyokusudiwa na kufikia ustawi wa wananchi.

**3.2.11 Tija ndogo na Ufanisi Usiokidhi wa Kampuni ya Mbolea – TFC**

**KWA KUWA**, Kampuni ya Mbolea Tanzania ilianzishwa kwa ajili ya usambazaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea na viuatilifu ili kuleta utulivu wa bei za pembejeo nchini lakini azma hiyo inakwama kutokana na:-

(i) Changamoto za kiuendeshaji zinazotokana na mfumo wa ununuzi katika Sekta ya Umma ikilinganishwa na urahisi wa ununuzi katika Sekta Binafsi; na

(ii) Ukosefu wa vitendea kazi kwa ajili ya usambazaji wa pembejeo;

**NA KWA KUWA**, Changamoto hizo zinakwamisha ufanisi katika Sekta ya Kilimo kwa sababu ya kuchelewa kwa mbolea kuwafikia wakulima katika baadhi ya maeneo;

(i) Kutokufika kabisa kwa mbolea na pembejeo katika baadhi ya maeneo ya nchi; na

(ii) Tofauti ya bei za pembejeo katika maeneo mbalimbali nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali -

(i) Ifanye mapitio ya taratibu za ununuzi wa umma (Public Procurement) ili kuona namna ya kuiruhusu TFC kumudu mazingira ya ushindani katika soko la mbolea;

(ii) Iipatie TFC zana na vitendea kazi kwa ajili ya uendeshaji ikiwemo usambazaji wa mbolea;

(iii) Ihakikishe mbolea inayosambazwa inaendana na jiografia na hali halisi ya udongo wa maeneo yanayohusika;

(iv) Iendelee kuzingatia ushauri wa kuwa na vifungashio vya ujazo tofauti tofauti vya mbolea kwa lengo la kuwafikia wakulima wa ngazi zote;

**3.2.11 Changamoto za Uvuvi na Ufugaji wa Samaki**

**KWA KUWA**, Sekta ya Uvuvi inalalamikiwa kwa –

(i) Kuhimiza matumizi ya vizimba vya samaki ambayo yana tija ndogo kutokana na ufahamu duni wa wananchi;

(ii) Kuwa na tozo za aina mbalimbali ambazo ni kero kwa wavuvi inayochangiwa na mfumo utozaji wake; na

(iii) Kuzuia shughuli za uvuvi baadhi ya wakati kwa lengo la kukabiliana na athari za uvuvi haramu na uvuvi usiozingatia uendelevu wa mazalia ya samaki,

**NA KWA KUWA**, Mambo hayo yanahusishwa na kupungua kwa upatikanaji wa Samaki ambao pia unasababishwa na: –

(i) Kukosekana kwa nyenzo madhubuti za uvuvi katika bahari, mito, mabwawa na maziwa nchini,

(ii) ufugaji wa samaki kushindwa kuongeza samaki katika soko kwa sababu ya uelewa mdogo wa wananchi walio wengi kuhusu ufugaji wa samaki kibiashara,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali itoe elimu kwa wavuvi kuhusu dhana na umuhimu wa uvuvi bora na jinsi ya kukabiliana na madhara ya uvuvi unaoathiri mazalia ya Samaki;

(ii) Shughuli za ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba zihimizwe na kuhamasishwa sambamba na kuboresha huduma za ughani katika ufugaji wa samaki;

(iii) Udhibiti wa uvuvi haramu uendelee kufanyika kwa namna inayozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu sambamba na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudhibiti shughuli za uvuvi;

(iv) Tafiti zinazohusu ufugaji wa samaki ziendelee kufanyika na matokeo yake yatumike kutatua changamoto za ufugaji wa samaki; na

(v) Serikali ifanye mapitio na kuunganisha au kuondoa baadhi ya tozo katika sekta ya uvuvi ili kupunguza usumbufu kwa wavuvi.

**3.2.13 Usimamizi Hafifu wa Utekelezaji wa Miradi ya Uvuvi**

**KWA KUWA,** Miradi mingi ya uvuvi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inaanzishwa ili kuongeza tija katika Sekta ya ndogo ya uvuvi, lakini haifanikiwi kutokana na kutokamilishwa,

**NA KWA KUWA,** Kutokamilika kwa miradi hiyo kunakosesha manufaa ya miradi kwa shughuli za uvuvi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ikamilishe uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi Shughuli za Uvuvi.

**3.2.14 Mchango Mdogo wa Sekta ya Mifugo**

**KWA KUWA**, Idadi kubwa ya mifugo nchini haichangii ipasavyo katika pato la Taifa kutokana na kukosekana kwa uongezaji wa thamani katika mnyororo wa mazao ya mifugo nchini,

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inatokana na kutokuwa na chombo mahsusi cha kusimamia sekta ya mifugo nchini jambo linalosababisha maisha ya wafugaji kuendelea kuwa duni na mchango hafifu wa Sekta katika uchumi wa nchi licha ya idadi ya jumla ya mifugo nchini kuwa kubwa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali-

i) Iweke mkakati madhubuti ili kuiwezesha Sekta hii kuchangia ipasavyo katika pato la taifa na kuwawezesha wafugaji kunufaika na rasilimali hizi; na

ii) Ikamilishe uanzishwaji wa Mamlaka mahsusi ya kusimamia sekta ya Mifugo nchini;

### 3.2.15 Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**KWA KUWA**, Sera hutoa msimamo na mwongozo, Sheria huweka masharti ya utekelezaji na Kanuni hubainisha taratibu za kufuatwa. Hata hivyo, Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo, Mfugo na Uvuvi: -

(i) Zimepitwa na wakati na zinakinzana hivyo kutofautiana na misimamo inayotakiwa, masharti yanayostahili na taratibu zinazopaswa kufuatwa; na
(ii) Zimekosa mfungamano (*alignment*) na kusababisha shughuli za sekta hizi kutosaidiana na wakati mwingine masharti ya sekta moja kukinzana na stahili za shughuli ya sekta nyingine.

**NA KWA KUWA,** hali hiyo haisaidii uchumi wa nchi wala maisha ya wananchi wanaojishughulikisha katika Sekta hizo na haiendani na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya sasa;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ikamilishe mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni ili kuendana na wakati;

(ii) Serikali iwianishe Sera, Sheria na Kanuni za Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili kuongeza manufaa ya kiuchumi yatokanayo na Sekta hizo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA

### 4.1 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako. Mafanikio ya Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Januari, 2024 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali. Ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii, unatokana zaidi na

Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Deodatus Mwanyika, Mb, - Mwenyekiti
2. Mhe. Mariam Mzuzuri, Mb, Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb,
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb
5. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb
6. Mhe Dkt. Christine Ishengoma, Mb
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb
10. Mhe. Dr. Medad Kalemani, Mb
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
14. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb
17. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb
18. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb
19. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb
20. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
21. Mhe. Toufiq Salim Turky, Mb
22. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Mb
23. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb), na Naibu wake Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe, (Mb), Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb) na Naibu wake Mhe. David Ernest Silinde, (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Hamis Ulega na Naibu Waziri wake Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano

waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge – Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, ndc, kwa kuwaongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.1 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo, na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja: ***Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii***.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Deodatus Philip Mwanyika, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**
9 Februari, 2024

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara, Kilimo na Ufugaji Mheshimiwa Deodatus Mwanyika hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge sasa tutaanza na uchangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa niaba ya ndugu zangu wa Musima Vijijini wameniomba nitoe salamu za rambirambi na mimi nadhani hapa ndiyo sehemu yake kwa kuondokewa na aliyekuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mbunge wa miaka mingi wa Monduli. Poleni familia, poleni Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona sisikiki vizuri. Nasikika vizuri?

**MWENYEKITI:** Unasikika Mheshimiwa.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mchango wangu, kwanza hizi Kamati mbili Afya, Kilimo binadamu wote duniani hizo ndio Kamati zinawahusu kwelikweli, mambo ya afya na mambo ya chakula. Kwa kuwa muda ni mfupi na nikitaka tufaidike zaidi nimechukua kitu kimoja tu chakula. *Food security*, usalama wa chakula na *food business,* biashara ya chakula. Kwa sababu niko kwenye chakula inamaanisha kuhudumia wananchi, kuhudumia binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka nioneshe jinsi ambavyo sisi wenyewe tunaweza kujihudumia na jinsi ambavyo tunaweza kufanya biashara duniani, ni huduma kwa wananchi binadamu. Tanzania leo hii ukiacha sensa takwimu za sensa zimeshapitwa na wakati sasa hivi tuko milioni 67. Nimechukua mpaka mwaka 2030 ambapo ndiyo programu zetu za kilimo zinatupeleka huko, mwaka 2030 tutakuwa watu milioni 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo Waafrika kwa sasa ni bilioni 1.5230 Afrika watakuwa bilioni 1.7 biashara hiyo. Duniani sasa hivi tuko bilioni 8.230 mambo yetu ya *BBT* yakiwa yameiva tutakuwa bilioni 8.6 biashara hiyo. Nimeenda kwenye Shirika la Chakula la Dunia kuangalia ni chakula kipi ni mazao yapi ambayo yanatumika sana duniani ni matano cha kwanza ni mchele, cha pili ni ngano, cha tatu ni mahindi, cha nne ni viazi, cha tano ni sukari, *sugar cane*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hivi vitano tukichukua mchele, mahindi, ngano ni chakula kikuu kwa 80% ya watu duniani kote. Kwa hiyo, kama tuko watu bilioni 8.1 sasa hivi na 80%

hiki ndiyo chakula chao kama Tanzania tunasema kilimo ni biashara basi tuwekeze kwenye *rice, wheat* na *maize*. Wakati huo huo kwenye mchango wangu nitaonyesha madhara ya tabianchi ambapo ripoti zilizotolewa hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunategemea kufika 2030 ndiyo tufike 1.5-*degree Celsius* lakini tumeshavuka hapo. Halafu ntaongelea umwagiliaji kidogo, sasa mifano ambayo napenda kuitumia mara kwa mara ni ya China na India kwa sababu mbili; kwanza miaka ya 50/60 umaskini wa India na umaskini wa China ulifanana sana na umaskini wa Tanzania. Vilevile, napenda kutumia hizi nchi mbili kwa sababu Mwalimu anapata uhuru alitupeleka sana India na China labda alikuwa na maono kwamba yatakuja kuwa Mataifa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho kinanifanya nachukua India mwaka 1961 wakati tunapata uhuru ukichukua matrekta yaliyokuwa India yani ilikuwa 0.19 trekta kwa kila hekta 1000 zinazolimwa, ulikuwa umaskini mkubwa sana. Mwaka 2000 hiyo trekta *density* wingi wa matrekta India walifika tisa kwa kila hekta 1000 zinazolimwa. Kwa hiyo, ni mfano mzuri, sasa hivi kuna majimbo yana matrekta 96 kwa kila hekta 1000 zinazolimwa kwa hiyo ni mifano mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye kwenye mahindi. Watu wanaotumia mahindi kama chakula kikuu duniani tuko bilioni 1.2 na wengi ni Afrika na Amerika Kusini; na Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara karibu 50% mahindi ni chakula kikuu. Duniani uzalisha wa mahindi duniani kwa msimu wa mwaka 2021/2022 zilikuwa *metric* tani bilioni 1.4, Afrika ikazalisha *metric* tani milioni 90.8 unaona jinsi ambavyo uzalishaji wa Afrika uko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji Afrika ni kwamba 64% zinazolimwa 24% zinazolimwa Afrika uzalishaji wa mahindi ni kati ya tani moja mpaka tani mbili kwa hekta lakini wastani huo duniani ni tani 5.5 kwa hekta moja. Nchi zinazofanya vizuri Afrika hapa ya kwanza ni Ethiopia wao kwa hekta moja wanapata tani tisa mpaka 12 wakati sisi Tanzania tuko tani 1.7 kwa hekta moja. Kwa hiyo, hapa tunahitaji kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha kutumia mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi duniani mbolea ambayo wanaipendelea kwenye mahindi ni *NPK* yaani inaongeza *nitrogen*, inaongeza *phosphorus*, inaongeza na *potassium* na uwiano wamechukua *ratio 120 to 60 to 40kg per hector* kwa hiyo, tuwekeze kwenye mahindi yanatumiwa na watu wengi lakini lazima tumwagilie na tutumie mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pili ni mchele, *rice*, sasa mchele, *rice* ni 50% ya wakazi wa dunia hii wanatumia mchele kama chakula kikuu. Kwa kuwa tupo watu zaidi ya bilioni 8 na 50% ndiyo chakula chao kikuu sasa kilicho tulichoamua kiwe cha biashara hebu tukalime huo mpunga huo kwa sababau walaji ni wengi. Sasa duniani kwa msimu uliopita walizalisha tani milioni 520, mzalishaji wa kwanza kabisa duniani ni China, yeye alizalisha karibu tani milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa pili ni India tani karibu 189. Kwa hiyo duniani bado ni wale wale ambao tulikuwa tuna umaskini sawa sawa miaka ya 1960 sasa wanaongoza kwenye upande wa kilimo kwa nini na sisi tusijifunze kwao tuweze na sisi kuingia kwenye masoko ya dunia. Sasa huo mpunga kwa hekta China wanatoa hekta tani karibu 150 kwa hekta moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vietnam iliyokuwa kwenye vita ya miaka mingi wanatoa karibu tani 27 kwa hekta moja wenzetu wapo mbali sana. Ukichukua India jimbo moja tu kama *West* Bengaluru wanazalisha tani karibu milioni 16 kwa mwaka. Kwa hiyo, Tanzania twende tukalime mpunga kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa tatu ni ngano; ngano 40% ya watu duniani wanatumia ngano kama chakula kikuu. Ngano msimu uliopita duniani zilizalishwa tani milioni 770. Wa kwanza kwenye uzalishaji huo bado ni China tani milioni 137, wa pili ni India lakini wazalishaji sita bora wa ngano wa kwanza ni China, wa pili India, wa tatu Russia, wanne Marekani, wa tano Ufaransa, wa sita Canada. Nimemuweka Canada wa sita nilitaka nimwache niishie wa tano lakini nikakumbuka alivyotusaidia sisi kwenye mambo ya ngano miaka ya 60/70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndugu zangu bado turudi huko huko Canada wanaweza bado kutusaidia. Uzalishaji kwa hekta China anatoa tani tano za ngano kwa hekta moja na mbolea anayoitumia ni *Urea* ndiyo maana Mwenyekiti wetu wa Kamati nashukuru sana alivyosisitiza na mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo kwamba tujenge kile kiwanda chetu cha mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzalishaji wa pili wa ngano bado ni India, yeye anatoa karibu tani tano kwa hekta moja na yeye mbolea anayoitumia *NPK*. Sasa ngano kwa Afrika, namalizia; mfano mzuri ni Ethiopia. Ethiopia mwaka huu watazalisha tani milioni 6.7 na wana uzalishaji wa aina mbili wa kumwagilia na wa mvua za kudra ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, nije nimalizie namna tunavyopaswa kufanya umwagiliaji Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumie maji yaliyopo juu ya ardhi *surface water* na tutumie maji yaliyopo chini ya ardhi. Sasa kwenye *surface water* nimechukua mfano wa Ziwa Victoria na niwape tahadhari Ziwa Victoria ambalo lina miaka zaidi ya laki nne umri wake watu wengine wanadhani Ziwa Victoria halijawahi kukauka, limewahi kukauka mara kadhaa na mara ya mwisho ziwa Victoria lilikauka ni miaka 17,000 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha Tanzania kukwepa kukauka kauka kwa maziwa haya ni lazima twende kwenye maji yaliyopo chini ya ardhi ambayo *statement* ya mwisho *ground water* duniani kote ndiyo inatumika sana kwenye umwagiliaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sospeter Mwijarubi Muhongo.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwakumbushe Kanuni ya 175(2) ambapo Mheshimiwa Spika akishatoa pongezi ama pole Waheshimiwa Wabunge hawaruhusiwi tena kutoa pole au pongezi. Kwa hiyo, na pia kwa kulinda muda naomba Waheshimiwa tuendelee na michango moja kwa moja.

Sasa namtaja Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, mheshimiwa Charles Mwijage, ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nianze kwa kukushukuru sana wewe pamoja na ofisi yako kwa kutupa nafasi hii. Niendelee kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya na kutambulika Taasisi za Kimataifa za *academic* na za aina nyingine kwa uweza wake, lakini nataka nimhakikishie kule Vunjo sisi tunasema ni mwanamapinduzi, mbeba maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuzipongeza Kamati zote na mimi naunga mkono mapendekezo yote na ya Kamati ambazo zimefanya kazi, kusema kweli inafurahisha kuona kwamba mambo muhimu yote ambayo binadamu anaweza akafikiria Kamati hizi zimeenda kuchanganua na kuleta mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema hivi kauli mbiu ya mipango yetu ya muda mfupi na wakati, kauli mbiu inayoongoza ni kwamba tunataka tujenge uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya wananchi. Sasa naomba nijikite zaidi kwenye upande wa viwanda kwa sababu inasema ndiyo *the building*. Tuna *transformation* inatokana kwa nchi kama yetu ambayo imekuwa ni ya kilimo kila mtu anaijua lakini hakina tija basi kwetu sisi *the building* tulifikiri kwamba ni viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme hivi, katika kujenga uchumi shindani kuna sera za aina mbili, sera ya kwanza ni *structural policies* ambazo zinashughulika na masuala ya kuongeza tija ya uzalishaji, kuweka mifumo ambayo itatumika na wale wazalishaji kufikisha mazao yao sokoni kwa gharama ambazo zinastahili na aweze kupata faida hivyo ni mojawapo ya *finding* ya sera ambazo zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili sera nyingine ambayo huwezi kukwepa kwenye uchumi shindani ni Sera ya *Exchange Rate Management* na mimi nilisema nimebobea kwenye mambo hayo ya *exchange rate management* na mambo ya fedha, kwa hiyo hakuna mtu anaweza kunipinga. Kusema kweli tulichokuwa tunakifanya sasa hivi ni kwamba tumechanganya sana na hatuwezi kuona mwelekeo ambao

tunakwenda katika ku-*rebuild* uchumi wetu uwe *resilient* na hiyo ni '*R*' yetu ya pili na tuelewe kwamba hauta yumbayumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea sasa hivi ni kwamba kila soko hasa soko huria, natumia soko huria kidogo ambalo lina-*allow regulation* lakini kama kila soko huria linapokupa kiashiria fulani kuhusiana na wapi wawekezaji wakimbizane ili waweze kupata faida, kwa sababu uwekezaji unafuata faida. Ina maana kufuata soko huria ni kwamba unataka vile viashiria vikwambie mahali ambapo kuna faida ni hapa, wawe ni wawekezaji wa ndani au wa nje wataona pale kuna faida wanakimbizana, lakini kinachotokea sasa hivi ni *every time* linapotokea tatizo, mfumuko wa bei unapotaka kupanda kidogo tu kunakuwa na *administrative interventions* za ajabu ambazo zinaweza kuvuruga hata vile viashiria, vile vigezo ambavyo vinatokana na *profitability* na *return* ya *investment* kwenye maeneo mbalimbali. Hivyo, tunaziba kwa kuingiza *administrative interventions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *administrative interventions* zinaweza zikawa za aina mbili, kwa mfano bei elekezi ni *administrative intervention* tu, inaingilia soko yaani ni kwamba hatutafika mbali, ni kwamba tutakuja kuishia tu kusema tunakimbizana na hizi za kuongeza tija za akina Mheshimiwa Bashe wanazofanya kwenye Wizara ya Kilimo, wanatengeneza mifumo ya umwagiliaji lakini *at the end of it* ni uchumi wa namna gani uta-*revolve*? hautaweza kuwa shindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ni hivi, ukiangalia hiyo unayosema *productivity* ya viwanda vyetu, labda tuseme ya sukari, sisemi kwamba haviko vizuri, lakini vya sukari, kwamba haviwezi kushindana na sukari inayotoka nje, kitu kinachosababisha ni nini? Je, ni *productivity per se* au ni ile *exchange rate*, ile bei unayopata ya dola ukileta dola ndani hapa kwetu haina thamani? Ni rahisi sana kwa sababu bei unayopata wewe unaipeleka nje ukaleta zile dola, ile bei uliyopata unazidisha kwa *exchange rate,* sasa kama ile *exchange rate* imekandamizwa kama unavyosema, hutapata viashiria vile ambavyo vinafanya wawekezaji wa-*move*. Kwa mfano waongeze viwanda vya sukari na kadhalika, lakini ukweli ni kwamba kama uchumi utakuwa umekaa, umetulia tu, ni kama

vile tumevurugika, tumekaa tu hivi hatujui tunakokwenda, yaani hakuna kitu kinachotupeleka kwamba twende kule mbele na kitu kitakachotupeleka ni kukubaliana na viashiria vya soko, kama hatukubaliani navyo basi hatutaenda mbali, hakuna mambo ya ushindani hata kidogo hapo, tutakuwa tunajichanganya tu kwamba tu-*import* sukari, tufanye nini, kumbe siyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba katika upande wa *central policy* wa viwanda kwa mfano, wanasema kwamba kuna huduma duni za kiuchumi, umeme unakatika, maji yanakatika na ukizipata hizi huduma za kiuchumi zinazohitajika kwenye viwanda gharama zake zinakuwa ni kubwa, kwa hiyo ushindani unakuwa umekandamizwa, kwa hiyo *central policy* ni *important* kwa masuala ya umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapokuja *issue* ya riba za mikopo ziko juu na kadhalika, kingine ni kwamba ushindani kutoka bidhaa za nje, sasa hivi huwezi ku-*import* maziwa kutoka nje na ukayauza hapa kwa faida, ukabadilisha zile shilingi unazopata ukapata dola nyingi ukapeleka nje ukaleta tena, kwa hiyo ikawa, *we are just importing country*, kwa sababu ni *very cheap* ku-*import*. Hakuna mtu ambae amevaa kitenge cha hapa nyumbani hata mmoja, hata mimi hii siyo ya ndani kwa sababu ni *cheaper, if I buy this from Turkey*, *from China is much cheaper*. Wanakuja ku-*damp* hapa na sisi tunawa-*accommodate* kwa sababu hatujaangalia sera zetu za *exchange rate* zikoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ambayo inachangia hapa deni la Taifa linakuwa ni himilivu kwa sababu umekandamiza bei*, it is not true!* Kwa sababu hiyo *equation* ina pande moja wa *import* na kulipa madeni na upande mwingine wa *export* ambayo ndiyo ina-*drive* uwezekano wa nchi kuendelea zaidi bila kutegemea haya mambo ambayo tunasema nafuu ipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukinga nchi yetu na *damping*, kuleta maziwa hapo ya Zambia yanajaa kwetu huku, afadhali tuangalie upya ni namna gani tunasimamia huu uchumi. Aidha, tuusimamie kwa kusema tuna-*administer* kama tulivyokuwa tunafanya *planning* zamani au soko ndiyo litupe viashiria vya yale mageuzi yanayotakiwa na *reforms* ambazo zinatakiwa na

*rebuilding* ambayo tungetaka kufanya katika nchi yetu hii, lakini ukweli ni kwamba hapa tumekwama kidogo na matatizo haya yataendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vingine lazima niseme, unajua *profitability* ndiyo ina-*drive* uchumi na uchumi lazima uwe na moto fulani na kama hauna moto maana yake umepooza, lakini ukweli ni kwamba ukiangalia *producer price index* ya Tanzania ambayo Mtakwimu Mkuu wa Serikali ana-*publish* na *consumer price index, b*ei ya mzalishaji inapanda sambamba na *the same rate* kama bei ya mlaji, kwa hiyo yule mtu anayezalisha *virtually* anakuwa *eroded* kabisa, yaani anabaki anabahatisha tu aweze kukopa hapa na pale aweze ku-*survive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji unakuwa hauna faida na ndiyo sababu watu tunakimbizana kupata wawekezaji lakini hatuwapati, licha ya hivyo *private* sekta bado haijapewa heshima kabisa katika nchi hii, kwa sababu watu kama akina Mo Dewji, watu kama akina Bakhresa ambao tunajua wanatakiwa kuendesha viwanda hivi, kwa nini Serikali haijamteua mmoja akamwambia atuendeshee Kiwanda cha Mkulazi, kwa nini? Tunajua wanaweza kuendesha vile viwanda, mwambie endesha, wewe kuwa Mwenyekiti wa Bodi ile sijui ya sukari au wapi, tuendeshee kiwanda au mpangishe kiwanda kiwe kina *operate profitable,* kwa nini hatufanyi hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujawahi kuona mfanyabiashara mzuri ameteuliwa kule akaambiwa basi sasa wewe uwe Mwenyekiti wa Bodi ya *Parastatal* hapa au vile! Kwa hiyo, hatujaona umuhimu wa kutumia nyenzo za kisekta binafsi au uongozi ulioko kwenye sekta binafsi kuwezesha kuendesha mashirika yetu ya umma ya biashara kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie masuala haya ambayo yanaweza yakatusaidia kuibadilisha nchi hii hapo tuendapo. Naambiwa *time* imeenda, nina dakika ngapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, bado dakika moja.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niseme katika masuala haya ya kuendesha uchumi au kutafuta uchumi ambao utakuwa shindani kama nilivyosema, tujaribu ku-*review* yale matatizo ambayo Serikali inafanya vizuri kwa ku-*incorporate either infrastructure* inakwenda vizuri lakini pamoja na hiyo tuweke mazingira ambayo yanawezesha bei za vitu kupanda, maana *price stability* siyo kwamba eti ukae *the same three percent*, hata nchi zilizoendelea hazikai *three percent* zinapanda na kushuka, lakini una-*stabilize* ile *price* kwenye *a certain mean* na ile *mean* ina-*move* inakuwa ina *overshoot* kidogo kila baada ya muda kuonesha kwamba hali ya mazingira ya uzalishaji inabadilika na ndivyo hivyo utaweza kuhakikisha kwamba wawekezaji wanapata hamasa ya kuwekeza kwa sababu wanajua kwamba faida yao itakuwa inaongezeka lakini sasa hivi hakuna faida inayoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *3.5 percent producer price index* ime-*grow for the last year, the same* ime-*grow* ile ya *consumer price index,* kwa hiyo, *I think* tuko mahali ambapo hatujaweza kutafakari vema ni wapi tuende ili tuweze kujenga uchumi ambao ni shindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, nilimtaja Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Godwin Kunambi na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Kamati hizi, nitachagua kidogo kwa sababu hii Kamati ni kubwa sana. Mimi nitachangia sekta ya samaki lakini kabla sijachangia sekta ya samaki, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa maamuzi na maelekezo aliyotoa kuhusu mgogoro wa Mwisa na Rutoro, katika Wilaya yangu ya Muleba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu uliodumu kwa miaka 18, Mheshimiwa Rais aliutatua kwa masaa sita, tunakwenda vizuri, ombi langu na Waziri wa Ardhi, nimekuandia barua na Mheshimiwa Kikoyo na wakubwa wote nimewaandikia. Msitutupe

tuende tufanye *transition* mpaka *point* ya mwisho amani ipatikane. Kwetu mtoto huwa halii ujombani, tarehe 22, Januari Mjomba Ulega alikuja akatoa maelekezo. Niwaase wadau wote mfuate maelekezo ya Waziri wa Mifugo. Baada ya hapo nichangie sekta ya samaki, nitajaribu kwenda sambamba na Maprofesa waliotangulia tuone kama tutaelewana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya samaki inaajiri watu milioni 4.5, lakini sekta ya samaki inaondoa umaskini, sekta ya samaki inajenga uchumi jumuishi, kwa hiyo ni sekta muhimu. Nimeisikia Kamati mlivyosema, ninatofautiana nanyi. Hoja siyo kuanzisha mamlaka, tumeshachelewa mkokoteni umeshatangulia farasi, hoja ni kuanzisha chombo kitupeleke pale tunapotaka kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze kwa nini mimi ninataka haraka, mauzo ya Taifa letu nje ya nchi *export* ni bilioni 12.258, mchango wa samaki haupo, lakini Tanzania tuna *body water*, maji ya kuweza kufuga *square kilometer* 145, ukiwauliza wataalam wa samaki, *the potential* tunaweza kupata samaki tani milioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Muhongo aliniambia Mwijage usiwe una-*compare* watu hapa, nina-*compare* na Vietnam, Vietnam wanapata samaki tani milioni saba kwa hiyo ukifanya *exploration,* sisi tungeweza kupata kati ya *dollar* bilioni tatu mpaka tano kwenye samaki. Nataka kuwaeleza kwa nini tuwekeze kwenye samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yetu ni bilioni 12.58, samaki inaweza kuleta siyo kwa miujiza ni hesabu tu, inaweza kuleta bilioni tatu mpaka tano, kwa hiyo tunao mgodi tumeukalia! Ndiyo maana nasema taasisi ianze haraka na hiyo mamlaka ije baadae, kwa nini? Moja, hatutunzi maji yetu. Tarehe 30 Mheshimiwa Rais akiwa Mwanza alizungumzia namna ya kutunza ziwa ikiwemo uvuvi haramu, akawaambia Wakuu wa Mikoa, akawaambia Wakuu wa Wilaya kwamba hiyo haiwezi kusaidia, hawa watu wanapaswa kuratibiwa na chombo maalum wawe na uelewa maalum, tunakwenda namna gani kudhibiti hiyo? lakini katika kudhibiti uvuvi haramu ambapo mimi sikubaliani nacho, kwa mfano ili kudhibiti uvuvi haramu Ziwa Victoria inabidi

tuwe na nguvu ya pamoja *equal thrust,* Kagera wakizuia, Mara wazuie, Mwanza wazuie na watu wote walioko ziwani, maana yake nini tuwe na watu wa kuhakikisha kwamba hakuna watakapovua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani kwangu kuna vituko, kuna mtawala mmoja alikwenda kudhibiti mambo ya uvuvi haramu, hajawahi kwenda anawafuata wananchi, kwanza anakwambia utakuwa *informer* halafu pili anakupiga makofi, sasa *informer* anapewa *incentive* na makofi siyo *incentive*. Wakuu wa Wilaya ile ukiwaambia wanasema huyu achana naye. Hapana! Huwezi kumpiga *informer,* unavunja nyumba ya mtu unachukua *engine* zake na unavunja mitumbwi yake, hizo ni zilipendwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Ulega kama *Scania* ikibeba mkaa wa magendo dawa siyo kuichoma *Scania* dawa ni kumkamata yule aliyehusika, kwa hiyo mnapaswa kulitunza ziwa, kuhakikisha kwamba ziwa linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapi tunakwama kwenye vizimba? Mheshimiwa Mwenyekiti wa sekta, vizimba ni lazima mchochee watu kuwekeza katika *food production*. Tunahitaji mashine au mitambo ya kuzalisha chakula cha samaki kwa sababu ukifuga bila chakula yule anayetengeneza chakula kutoka *abroad* ndiye anachukua pato lote, lakini tunazo *ingredients* zote, mazao, mahindi ya njano, soya na vingine vinapatikana hapa. Kwa hiyo tutengeneze *chain* ya kilimo na uvuvi ili tuzalishe chakula hapa, lakini Wananchi wa Tanzania kwamba hawana elimu hiyo hakuna, elimu ni kufanya faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais ametuma vizimba 222 akavigawa Mwanza bado Kagera, Kagera tuna *square kilometer* 10,200 za maji na tunasubiri tuletewe vizimba vyetu, watu waliokuja kupima vizimba kwetu, watu wa *TARI* hamjaleta *certificate* za Kemondo, Kamgaza hamjaleta, Mgasa hamjaleta. Mtuletee *certificate* kwa sababu kuna faida kubwa katika ufugaji wa samaki. Wale wa kwanza watakaoanza watawavuta wenzao ili kusudi waende kufuga, nimewaambia faida iko kwenye samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo kwenye tija ya mifugo. Ili upate tija achana na sera ni kuwaambia Watanzania waache kuchunga waende kwenye kufuga, wabadilishe tabia, waache kuchunga waende kufuga. Sisi Kagera Mamlaka ya Mkoa imeomba Ranchi za *NARCO* zenye hekta karibu laki mbili zilizoko kule, mia mbili tisini na tisa elfu, tunaomba Kagera tutumie kama *modal,* ufugaji uanzie Kagera, sehemu zingine za nchi muendelee kuchunga kusudi mje mjifunze Kagera muangalie tija inayopatikana, muweze kupata nyama, mweze kupata maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani ukasafiri na ng'ombe kilometa zaidi ya 6,000 ukategemea ng'ombe aweze kuwa na tija. Ng'ombe ni mbale, ng'ombe ni malisho, ng'ombe ni menejimenti na mazao yanayotokana ni soko. Sasa hawa ng'ombe wanaotembea mwaka mzima hawawezi kupata soko kwa sababu nyama yao haina ubora wala maziwa yao hayana ubora au yako mbali na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema leo tunahitaji chombo haraka kisimamie haya maziwa yetu kwenye mazingira na kuweza uhakikisha wavuvi wako vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nimalizie kwa kuwaomba wanaowapiga ma-*informer* makofi waache. Kazi ya Seremala hawezi kuingia *theater* anayeingia *theater* ni Daktari, wekeni watu wenye uwezo wa kudhibiti ziwa na hao wako Wizara ya Mifugo, siyo Polisi au siyo mahali popote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage. Nilimtaja Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi niendelee moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali ambayo tunaweza kujiuliza kama Watanzania, katika nchi ambayo Mungu alitupendelea, katika nchi ambayo Mungu alitupa madini,

akatujalia mito, ardhi kubwa, sekta ya utalii kila kitu kipo. Kama Watanzania tujiulize maswali ni wapi tunakwama? Wapi tunakwama? Kwenye hitimisho langu nitaeleza wapi tunakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na sekta ya kilimo hasa kwenye eneo la umwagiliaji. Taifa letu limejaliwa ardhi inayofaa kwa kilimo hekta milioni 44 na katika hekta milioni 44 eneo linalolimwa mpaka sasa ni hekta 16 tu, eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 29.4 na hadi sasa tumefanikiwa kupeleka miundombinu ya umwagailiaji kwenye hekta takribani 729,000 tu. Sasa utaona tuna kazi kubwa ya kufanya kuwekeza kwenye eneo hili la umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema kwenye hotuba yangu wakati wa bajeti, Wizara ikiwasilisha bajeti yake nilisema hivi, nchi hii ina mito ya kutosha, ninasikitika sana kuona Wizara inaendelea kujikita kutumia fedha nyingi sana kwenye umwagiliaji kwa kuchimba mabwawa. Sasa najiuliza kama ukienda Mkoa wa Morogoro ule Mlima Udzungwa maji yanamwagika tu, unajiuliza hivi hawa watu huwa hawaoni hata haya maji ya mito? *Anyway,* najaribu kusisitiza tu kwamba ninaishauri Wizara ya Kilimo iwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji hasa kwenye mito, kwa sababu uwekezaji ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia pale samahani kuna sehemu mmepeleka bilioni 24 mnachimba mabwawa, aah! Sijui lakini najaribu tu kusema na ninasisitiza kwamba tuwekeze kwenye kilimo chetu cha umwagiliaji kwa kutumia mito yetu ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, sisi Morogoro tuna eneo pale la Bonde la Mto Kilombero linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, takribani heka 888,516. Sasa, hilo eneo tukiwekeza kule; nitaeleza baadaye kwenye mchele ambayo ameeleza pale Mheshimiwa Profesa Muhongo, baadaye kidogo nitaeleza umuhimu wa zao la mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najaribu kujiuliza, kama tutawekeza kwenye umwagiliaji kwenye hizi hekta 888 tunawezaje kunufaika kama Taifa kupitia umwagiliaji ndani ya Bonde la Mto

Kilombero? Unapolitaja Bonde la Mto Kilombero unaitaja Mlimba na kata zake zote, sisi tuko ndani ya Bonde la Mto Kilombero na eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 888,516.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye eneo hili muhimu. Profesa ameeleza kwenye habari ya mpunga, ni kweli zao la kwanza au bidhaa ya kwanza au chakula kinachopendwa sana na watu wote duniani ni mchele. Naomba niseme kidogo, kwa Taifa letu hapa Tanzania, kwa takwimu ya kwamba kila Mtanzania, watu takribani milioni 61, kila Mtanzania akila walau kilo 30 za mchele kwa mwaka, mahitaji ni tani milioni 2.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mtanzania akala kilo 30 tu, maana wengine wanakula mchele siku za sikukuu. Eeh, familia nyingi karibu asilimia 50 wanakula mchele siku za sikukuu, kwa sababu ya upatikanaji wake ni mgumu. Sasa, kila Mtanzania akiweza ku-*afford* kilo 30 kwa mwaka, mahitaji yetu kwa nchi nzima ni tani milioni 2.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa umuhimu wa Mkoa wa Morogoro kwenye kuzalisha mchele, Mkoa wa Morogoro pekee unazalisha tani 966,745 katika mahitaji ya tani milioni 2.7. Sasa, ndiyo Mkoa unaoongoza kwa kuzalisha mchele. Sasa angalia kichekesho, ndio mkoa wa mwisho kwenye miradi ya umwagiliaji, lakini ndiyo mkoa unaolisha zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania. Sasa, sijui wenzetu wa Wizara ya Kilimo mnatuangaliaje Mkoa wa Morogoro? Mngeutazama Mkoa wa Morogoro kama mkoa muhimu kulisha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze kwa kusema kwenye hiyo hiyo bidhaa ya mchele kwamba, duniani takribani watu bilioni 3.5 wanakula mchele. Niliwahi kupata fursa kidogo ya kwenda Japan pale Tokyo kwenye *training* ya *Quality Infrastructure System,* nilikutana na *Vice President* wa *JICA* alinielea kwamba wao wanaagiza chakula cha mwaka mzima Japan kwa sababu wana eneo dogo sana la kilimo. Akaendeleza nchi ambazo wanaagiza Afrika, akaitaja Zimbabwe na Zambia. *Why not* Tanzania? *Why not* Tanzania? Wakati mwingine *maybe we might be speaking in tongue,* hatueleweki kama tunanena kwa lugha hapa, lakini

tunatamani kuona walau wenzetu mnasikia na mnachukua hizi hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa nijikite kwenye kuchangia ni eneo la kilimo biashara. Taifa letu linahitaji wakulima wa aina mbili tu; wakulima wakubwa na wakulima wadogo wadogo. Tena wakulima wakubwa hawahitajiki wengi sana. Ukipata wakulima wakubwa walau 100 kwenye Taifa letu, nchi hii tunaweza kufanya *export* na kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania ukitaja wakulima wakubwa kwenye Taifa letu, labda Shamba la Kapunga, labda na mwenzetu Sumry kule Sumbawanga, sidhani kama kuna mwingine. Sasa, tukipata wakulima wenye uwezo wa kulima walau mkulima mmoja akalima hekta 10,000, hekta 20,000; labda nikumbushie nyuma. Wakati wa Hayati Baba wa Taifa, alianzisha mashamba ya Serikali. Kwa bahati mbaya, hatukufanikiwa sana kwa sababu Serikali ilikuwa inataka iwekeze yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri Wizara ya Kilimo, tafuteni maeneo, nimeeleza hapa eneo la linalofaa kwa kilimo lina hekta takribani milioni 44. Tutafute maeneo tukaweke mashamba makubwa, tukawekeze kule miundombinu ya umwagiliaji, tukawekeze na barabara zipitike, twende tukatafute wawekezaji wakubwa wawekeze kwenye kilimo. Tuta-*export* tu. Ni jambo dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuwa na *peasant*. Ni kweli kuna umuhimu wa kuwa na wakulima wadogo, nao tuwawezeshe kwa sehemu yao. Niliona niliseme hilo eneo angalau kidogo wenzetu wa Wizara ya Kilimo waone namna nzuri ya kukaa na kubadilisha kilimo kiwe kilimo biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Kilimo, wakati anawasilisha bajeti atueleze tu namna gani *BBT* hasa wale vijana, ni wangapi wamenufaika na *BBT* mpaka sasa? Waliosajiliwa na walioondoka, tupate ukweli. Niliwahi kusema hapa, kilimo ni *tiresome work,* sikueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kilimo hakihitaji *motivational,* yaani kuzungumza. Hakihitaji maneno. Kilimo kinahitaji uhalisia. Kilimo ni *passion.* Niliwahi kusema kilimo ni *passion,* siyo kila mtu atalima jamani. Sijui kama huwa naeleweka! Kilimo ni *tiresome work,* nikasema nendeni kule ambako vijana wanajishughulisha na kilimo. Sijui kama walinisikia! Sasa mmewachukua watu wengine pale, mtu anakwambia yuko Katavi ana-*apply* kwenye mfumo kumbe yuko Dar es Salaam. Samahani, *and I stand to be corrected,* baadhi wameanza kukimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamchukua *graduate,* amemaliza *UDOM* ukamleta pale Chamwino pale, miaka minne anasubiri zabibu. Niliomba kazi benki, benki wameniita nikafanye kazi, nitabaki pale Chamwino, katika hali ya kawaida nilime? Nani anabaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, najaribu tu kushauri jamani, wakati mwingine tutazame tu katika hali ya kawaida, twende kwa watu wanaoshughulika na kilimo *(field)*. Nendeni kule Mlimba, nendeni kule Morogoro, nendeni Katavi. Sasa sijui kama naeleweka! Sasa unachukua vijana! Halafu nikawa najiuliza maswali. Samahani, niseme tu, hivi pale Chamwino kile ni chuo au shamba? Samahani, naomba niulize, kile ni chuo au shamba? *I stand to be corrected.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaambiwa kuna *investment* ya *40 billion*, sidhani kama nina uhakika na ninambiwa kuna ekari kama 200, *something like that.* Sasa najiuliza maswali, pale ni chuo au shamba? Shamba linawekwa *fence*? Tunataka ku-*achieve* nini? Kijana wa miaka 30 unamweka pale, anakaa kwenye *double decker*, ana mke, anasubiri zabibu *four years*! *Are we serious? Really, are we serious?* Fedha yenyewe bado Taifa letu halina hela nyingi. Pesa yetu ni ndogo. Sasa, pesa hii hii ndogo…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani naomba unilinde. Nimalizie kwa kusema, naomba kile kiwe chuo, siyo shamba. Haliwezi kuwa shamba unaweka *fence*.

*Investment* ambayo ni ya *more than 20 billion* unalima heka 200. Mimi nalima heka 300 kwa shilingi milioni 150. *Are we serious? As a nation, what do we need to achieve?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema, tulianza na Kilimo ni Uti wa Mgongo, biashara ikapita; Kilimo cha Kufa na Kupona, biashara ikapita; tukaja na Kilimo Kwanza, tukaishia kununua *V8*; leo tuna *BBT*. Maneno yote ya Kiswahili yameisha, tumekuja ya Kiingereza. *I am sorry*, yaani mimi napata shida kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu ni wapi tunakwama? Naomba nihitimishe. Watanzania tunakwama kuendelea kwa sababu tuna-*deal* na *personalities and not substances, and not issues.* Tume-*graduate* kwenye majungu. Yaani watu wote wenye uwezo kwenye sekta zote hawapati nafasi. Watu fulani hivi ndiyo wanapata nafasi. *We have people who are best* kwenye hii nchi yetu, lakini hawapati nafasi. Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mtu amefaulu kuwa karibu na kiongozi, anapeleka majungu juu ya huyo mtu, *personality* tu. Unajua yule mrefu, mwembamba, mfupi, lakini hawaangalii *credibility, why don't we test credibility?* Hatuwezi kutoka tukiendelea na majungu kama Taifa. Nawaambia kwa ukweli. Tukiacha majungu, Taifa letu litaondokana na umasikini… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Godwin Kunambi. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wake mzuri wa kazi zilizofanywa kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuelezea kuhusu changamoto zilizopo kwenye maeneo ya mipaka ya Tanzania na nchi jirani. Kuna baadhi ya vituo kwenye mipaka yetu hakuna

vitendea kazi vya kutosha kwa mfano, *Scanner* za kupimia mizigo. Jambo hili linachangia mizigo kukaa kwa muda mrefu pale ili kuifanyia uchunguzi, linakosesha mapato makubwa ya Serikali na kuwapa usumbufu mkubwa wafanyabiashara wanaotoka na kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Serikali ilione ili twende sambamba na ukuaji wa uchumi na kuhimiza kupata mapato ya kigeni ndani ya nchi. Tuwekeze na sisi kwenye maeneo yetu ya mipakani ili tuwe na vifaa vya kisasa vya kupimia na kuchunguza mizigo inayoingia ndani ya nchi. Hili litasaidia kuongeza mapato na pia katika kujua vifaa au biashara hatarishi zinazoingizwa ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta za uzalishaji na biashara; kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda, kuna baadhi ya sheria zake ni za muda mrefu sana ambazo zinakwamisha harakati za ukuaji wa uchumi na kuwarejesha nyuma wazalishaji na wafanyabiashara. Naiomba Serikali, sheria hizi na Kanuni hizo zifanyiwe marekebisho ya haraka kwa sababu nyingine ni za tangu mwaka 2000 na 2002. Kuendana na kasi ya uchumi na teknolojia ya sasa hivi, sheria nyingi zimepitwa na wakati na zinatakiwa zifanyiwe marekebisho ya haraka ili kuleta maendeleo na tija kwa nchi na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuwekeza fedha nyingi katika sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na katika sekta ya umwagiliaji. Hata hivyo, fedha zile hazitoki kwa wakati. Tunaomba Serikali zile zitoke kwa wakati ili zikafanye kazi iliyokusudiwa, kwa sababu, fedha kutokutolewa kwa wakati kunarudisha nyuma maendeleo na azma ya Serikali ya kukomboa nchi hii kiuchumi na kimaendeleo ikiwemo kuendelea kuongeza fedha katika sekta hizi za umwagiliaji na sekta nyingine za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye umwagiliaji kuna uhaba mkubwa wa vitendea kazi, wataalamu na miundombinu ya umwagiliaji. Jambo hili linatakiwa lifanyiwe marekebisho ili kuweza kujikita zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji na hasa kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili nchi

yetu mara kwa mara ikiwemo mafuriko, ukame na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye umwagiliaji ndiyo kilimo ambacho kitatukomboa sisi wananchi wa Tanzania kwa usalama wa chakula, lakini pia kilimo biashara. Bila kujikita kwenye umwagiliaji, usalama wetu wa chakula unaweza ukawa hatarini lakini pia kilimo biashara kinaweza kisifanikiwe kwa uzuri zaidi. Changamoto hii ni ya kuitatua kwa haraka ili tuweze kuendana na soko la dunia ambalo linahitaji chakula kwa wingi sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya viuatilifu ni muhimu kwa wakulima. Wakulima wanapata hasara kubwa kwa kutumia aidha viuatilifu *fake*, au kutumia viuatilifu kinyume na utaratibu kwa sababu hawaelewi. Kwa hiyo, inatakiwa tuwape elimu watu wetu wanaohusika na kilimo (Maafisa Ugani) ili kuweza kutoa taaluma kwa wakulima wetu wasipate hasara. Hasara imekuwa kubwa kwa kutumia viuatilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililotaka kuchangia, tuwekeze zaidi kwenye utafiti. Utafiti utatusaidia kupata mbegu bora na mbegu bora ndizo zitamsaidia mkulima kujikwamua kiuchumi na nchi kupata mafao ya kiuchumi pamoja na malighafi za viwandani, mbegu bora ni muhimu. Hivyo tuimarishe taasisi yetu ya *ASA* kwa kupatiwa vitendea kazi bora, yakiwemo maghala ya kuhifadhia mbegu kwa sababu kuna uhaba wa kuhifadhia mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna uhaba wa magari ya kusambazia mbegu, kiasi kwamba inabidi wakakodi kwa watu binafsi. Hivyo, ikimfikia mkulima, tayari inakuwa na bei kubwa kutokana na gharama za hapa katikati mpaka inapomfikia mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema kwamba, Serikali iwekeze zaidi kwenye viwanda vya mbolea ambavyo vitamilikiwa na wananchi wa Tanzania hapa nchini, ambavyo vitaendana na hali ya wakulima wetu na kujua mbolea yetu itakuwa ya aina gani kulingana na udongo wetu. Tuzalishe mbolea itakayomfaa Mtanzania humu nchini, kulingana na

vipimo vya afya ya udongo. Tukipima afya ya udongo, tutajua tutumie Mbolea ya aina gani na hivyo viwanda vijengwe kwa kutengeneza mbolea ya aina gani ambayo malighafi zinapatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuwekeza kwenye bandari ya uvuvi kule Kilwa. Juhudi tunaziona, bandari inaendelea vizuri. Tunaomba juhudi hizo za Serikali ziendelee ili tuweze kuingia kwenye uvuvi wa Bahari Kuu na kupata fedha nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza zaidi kwamba Serikali iendelee na kununua meli za uvuvi. Tunahitaji bandari ya uvuvi na meli za uvuvi ili tuingie kwenye sekta ya uvuvi wa Bahari Kuu. Kuna fedha nyingi kwenye uvuvi wa bahari kuu. Samaki sisi hatuwafugi, hatuwapelekei mbolea wala hatuwapelekei chochote. Samaki wapo baharini, tusipowavua sisi wanatembea nchi za jirani, wanavuliwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza Serikali iweke chombo kitakachosimamia uvuvi. Ni mamlaka ya uvuvi ndiyo itarahisisha utekelezaji wa sekta hii ya uvuvi ili uvuvi wetu uwe endelevu na utoe tija kwa nchi, na wananchi wenyewe na kuinua kipato cha wavuvi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu ni duni, maslahi yao ni madogo lakini kazi inayofanyika baharini na kwenye maziwa ni kubwa, kazi inayohitaji uvumilivu na ustahimilivu, kwa sababu unapokwenda hujui dhoruba gani itakukuta? Utakwenda au utarudi, mvuvi hajui. Mvuvi anachojiua ni kwenda, kurudi hajui, kwa sababu kitakachomkuta baharini au kwenye ziwa kubwa hajui ni kitu gani? Tuimarishe uvuvi na kuwasaidia wavuvi kwa zana bora za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali imeanza kugawa boti, wavuvi wetu wataanza kuvua kisasa na kitaalam, lakini tuendelee kuwekeza katika sekta hii ya uvuvi kwa vifaa bora na wavuvi wetu waachane na vifaa duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza Serikali kwa kuwekeza kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji. Isichoke na iendelee kuwekeza kwa sababu tunahitaji mafanikio katika nchi yetu. Mwisho kabisa, natoa pole kwa wazalishaji wa sukari nchini kwa hasara kubwa waliyoipata, mashamba ya miwa yote yameharibika, yameingia maji na ikatusababishia changamoto kubwa ya sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naipongeza Serikali kwa hatua inayochukua katika kukabiliana na janga hili la Taifa kwa ajili ya sukari ili sukari iweze kufika kwa wananchi. Serikali imejitahidi, imeingiza fedha nyingi kule Mkulazi ili tuondokane na kadhia hii ya uagizaji wa sukari, lakini Mwenyezi Mungu anasema, ukisema lako na Mungu naye anapanga lake. Tumeingiza fedha nyingi, lakini ndiyo mwaka tuliopata hasara kubwa, fedha zote zile zimepotea. Naipa pole sana Serikali kwa sababu tumepata janga kubwa. Ile miwa yote haifai na haiwezi kuzalisha kwa kweli inatia uchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wa Wizara zetu tunazozishughulikia zote kwa kazi kubwa na ushirikiano wetu wa pamoja uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Nilimtaja Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hizi mbili na nianze kwa kumpongeza Spika kwa kuunganisha na kuunda Kamati moja inayosimamia viwanda, biashara, kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo, kwa sababu wakulima wakizalisha, wafugaji wakizalisha, wavuvi wakizalisha, sasa tunaangalia biashara ya hivi vitu inakwendaje; na viwanda vinaanzishwaje kutokana na utendaji wa hizi Wizara ambazo nimezitaja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadui wetu watatu tokea tupate uhuru ni ujinga, maradhi na umaskini, mimi niipongeze sana Serikali yetu kwa sababu kwenye upande wa ujinga tumejenga shule nyingi na ujinga tunaufuta tumejitahidi, hata kwenye Elimu ya Watu Wazima Tanzania tunafanya vizuri. Kwa upande wa afya pia tunafanya vizuri ijapokuwa hatujafikia pale ambapo tulitaka tuwe lakini tuna vituo vya afya vya kutosha, zahanati na hospitali lakini umaskini hicho cha tatu, bado ni kikwazo kikubwa na tuna mlima mkubwa wa kupanda kama Watanzania ili kukabiliana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita hii ya kupambana na umaskini tukubaliane Waheshimiwa Wabunge, kwamba ni sisi Wabunge tutaishauri Serikali ili wananchi wetu, baba zetu, mama zetu ambao ni wakulima, wavuvi na wafugaji wataondokana na umaskini kama tutaishauri Serikali vizuri sisi Wabunge ili tuwaondoe baba zetu na mama zetu kwenye huu umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ukweli kwa miaka mitatu iliyopita Serikali imejitahidi kupambana na umaskini, tunaona nia thabiti ya Serikali yetu ya kupambana na umaskini. Serikali imewekeza, inajitahidi ukilinganisha katika historia, ikilinganishwa na huko nyuma tulikotoka Serikali imejitahidi kuwekeza, nitatoa mfano kwenye Sekta ya Kilimo na mifugo bajeti zimeongezeka kidogo kutoka karibia shilingi milioni 294 kwenye kilimo mpaka zaidi ya shilingi bilioni 900 kwenye kilimo lakini ukizichanganya zote mbili tunapata karibia trilioni moja na zaidi kwenye hizi sekta za kilimo na mifugo, kwa hiyo *somehow* Serikali inapambana na umaskini kwa kutoa fedha za kutosha ili hizi Sekta ambazo nimezitaja ziweze kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingi ambayo kama Mwenyekiti wetu wa Kamati alivyosema imetekelezwa. Kuna miradi ya umwagiliaji inatekelezwa nchi nzima, mradi wa mbegu unatekelezwa, ruzuku ya mbolea tunaona nia nzuri ya Serikali pikipiki kwa Wagani wetu pande zote mifugo na kilimo zimetolewa utafiti, kwenye viwanda *TIRDO* wamepata pesa ya kutosha, *TAFIR* wamepata pesa angalau kidogo, *TARIRI,* wamepata pesa na *TARI* wamepata na kwenye ushirika vilevile tunaona Serikali ina nia njema ya kuongeza fedha za ushirika.

Tumeanzisha *BBT life* kwa mifugo na kilimo na bandari ya uvuvi imejengwa. Hii ni nia njema ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaondoa umaskini na tunawasaidia wananchi wetu kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye swali la msingi, katika ripoti zote tulizopokea kutoka kwenye Wizara zetu tatu tunazozisimamia Viwanda na Biashara, Kilimo na Mifugo, hata Mwenyekiti amesema pale kuna changamoto ya kuwa na fedha za kutosha pamoja na kwamba Serikali inaonyesha nia ya kutoa fedha lakini bado fedha hizi ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kuondokana na umaskini lazima Waheshimiwa Wabunge tuwe na uamuzi mkubwa wa kuhakikisha kwamba tunawekeza kikamilifu katika Sekta hizi, katika Wizara hizi ambazo tunazisimamia ili ile kitu tunayoiita umaskini kule kwa watu wetu tuondokane nao, tusipofanya hivyo bado historia itajirudia ni uamskini, umaskini na tusikubali kabisa, tuwekeze kwenye hizi Wizara tatu ili angalau kinachofanyika kionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano kidogo tu wa nchi yetu na Nchi ya Netherlands, Uholanzi ni nchi namba mbili Duniani kwa kupeleka bidhaa za *net exporter* wa *product* za kilimo mifugo hapa duniani lakini nchi hii ya Uholanzi ni ndogo ukilinganisha na Tanzania. Eneo la Uholanzi ni $km^2$ 41,850 eneo letu sisi Tanzania ni $km^2$ 904,587 sasa eneo la kilimo la Uholanzi ambalo wamewekeza ni hekta milioni mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama tulivyoona hapa tuna eneo ambalo linafaa kwa kilimo ni hekta milioni 44 kama alivyosema Mheshimiwa Kunambi lakini hekta ambazo tumewekeza kwenye umwagiliaji ni hekta 727,000 tu. Sasa nchi yetu ni kubwa sana ina eneo kubwa maji mengi kuna kanda nyingi za kilimo lakini hatuendi mbele ni kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuige Uholanzi walifanya nini? Uholanzi wamefanikiwa na ni *net exporter* wa mazao ya bustani mbogamboga nyama mayai na maziwa, tuna-*import*

hivyo vitu kutoka Uholanzi ni kwa nini wamefanikiwa wakafika hapo, wamewekeza kwenye masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wamefanya uwekezaji mkubwa kwenye Sekta ya Kilimo, hawajaidharau na mnajua mpaka *South Africa,* Uholanzi wanakwenda wanalima kule na hata hapa Tanzania tuna makampuni yako kule Arusha na Kilimanjaro ya Waholanzi wanakuja kulima hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wamewekeza katika mbinu bora, utafiti, wamewekeza kwa kiasi kikubwa wanasaidia watafiti wao wanazalisha mbinu bora za kuzalisha mbegu bora na kadhalika pia matumizi ya maji wameyamiliki *(irrigation)* kule kwao maji hayapotei wanayapeleka mashambani na wanafanya kilimo cha biashara na vilevile kuna *greenhouse technology* ambayo imewasaidia sana kufika hapo walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini sisi Tanzania pamoja na kuwa na eneo kubwa maji mengi, kanda nyingi za kilimo kwa nini tusiwekeze ili tuwasaidie wafugaji wetu waweze kuzalisha nyama za kutosha? Wakulima wetu wavuvi wetu na viwanda tuwasaidie waweze kuchakata na kuanzisha viwanda ambavyo vitakuwa vinachakata mazao ya mifugo na ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri naomba Wabunge wote kwenye haya maazimio kwamba tuongezee hizi Wizara fedha kama tunataka tuondokane na umaskini ambao uko kule kwetu kila mmoja hapa ana kundi kubwa la watu maskini, tuwasaidie wenye hizi Wizara Tatu wapate pesa ya kutosha ili waondoe watu wetu kwenye umaskini, tusipofanya hivyo kuna kitu kitakuwa kinatu-*harm behind* kwamba hatujatekeleza wajibu wetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipendekeze tukiwatengea fedha waende wakaanzishe viwanda vidogovidogo vya kuchakata mazao ya kilimo, mazao ya mifugo, mazao ya uvuvi, viwanda vianzishwe, tukianzisha viwanda vidogovidogo kule wananchi watakuwa hawapati hasara watakuwa wanapata faida

wakizalisha kiwanda kiko karibu pale anapeleka mazao yake anauza anapata pesa ya kutosha, hicho ni kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwasaidie Wizara ya Mifugo, niwe mkweli hapa hawa watu wanahitaji msaada wa hali ya juu ili Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi iweze kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa bado pesa tunayowapa ni ndogo na wameomba hata sisi kwenye Kamati tumeona kwamba wanahitaji msaada mkubwa ili waweze kufanikisha azma yao ya kuchangia kwenye Pato la Taifa na la mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine Sekta ya Kilimo vilevile pamoja na kwamba tumeshawapa pesa ni vyema tuwape pesa ya kutosha ili wazipeleke kwenye mbegu, tuendelee kuwapa watu ruzuku ya mbolea na kutengeneza mbolea yetu wenyewe, tuanzishe viwanda kama wenzangu walivyosema na tuwekeze sana kwenye umwagiliaji kwani eneo la umwagiliaji, eneo la kulima hapa nchini ni kubwa na tukiwekeza kwenye umwagiliaji najua tutachomoa vizuri sana. Vilevile, utafiti usaidiwe ili tukishapata watafiti wanaotuzalishia mbegu bora, watafiti wanaotuzalishia mbinu bora za uzalishaji tija itakuwepo umaskini utaondoka na Mungu atatubariki kwa kuwatetea hao watu ambao walitutuma tuje hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi. Nilimtaja Mheshimiwa Francis Isack Mtinga

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Kamati hasa ya Viwanda Kilimo Mifugo na Uvuvi. Nimshukuru Mwenyekiti wangu kwa kuwasilisha vizuri hoja ya Kamati, lakini pia nishukuru sana Mawaziri wote watatu na Manaibu wao ambao wanahusika na Kamati hii kwa utendaji mzuri wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita katika kuchangia suala la sukari lakini vilevile suala la uanzishwaji wa Mamlaka mbili muhimu, Mamlaka ya Mifugo na Mamlaka ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari ni zao ambalo ni siasa kwa nchi yetu, siasa ya Tanzania huwezi kuikwepesha na sukari kwa sababu ndio zao ambalo linatumika kuanzia na mtu wa hali ya chini kabisa mpaka mtu wa hali ya juu, hakuna mahali unaweza ukakwepa matumizi ya sukari kwa Watanzania. Mazao mengine yanaweza yakawa hayamgusi moja kwa moja mwananchi wa kila eneo, linagusa baadhi ya meneo lakini sukari ina mgusa kila Mwananchi wa Tanzania. Sukari katika nchi yetu ndio sehemu pekee ambako tumekuwa na mpaka Sheria zinalinda viwanda vya sukari. Sheria kabisa kulinda viwanda vya sukari, kuonyesha umuhimu wa zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kinasikitisha pamoja na kulinda, pamoja na yote haya sukari ya Tanzania haijawahi kutosha na tangu ianze kupanda bei mimi nikiwa mdogo kabisa mpaka nimekuwa hivi haijawahi rudi nyuma ikashuka, hiyo bei iliyofika hapo kabla ya hii habari ya mvua za mwaka huu ya 2,700 mpaka 3,000 imeenda haijawahi rudi chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uhalisia sidhani kama zao hili linahitaji kufika bei hiyo kwa sababu malighafi ya zao la sukari inapatikana nchini ni mabonde ambayo tunayo ya kulima miwa na miwa yenyewe inalimwa na inakubali popote pale mradi kuwe na maji, hatuagizi chochote kikubwa zaidi ya kiwanda tu chenyewe na kiwanda ukishakiagiza mara moja ni kitu cha miaka mingi lakini ile malighafi ya kila siku ambayo ni miwa inapatikana hapa nchini. Kwa hiyo, kiasi kwamba hakukuwa na sababu sana ya sukari kuendelea kupanda lakini hakukuwa na sababu pia ya sukari kutokutosha nadhani kuna mahali tu kuna tatizo ndio maana hii sukari haijawahi kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha pengine viwanda vyetu wanafanya makusudi kwamba wanajijua ni wao wachache kwa hiyo wanatengeneza kiwango ambacho kinawapa wao faida lakini tunaendelea kutengeneza nakisi ya soko kule kwa walaji ili wao wanendelee kuwa na uhakika wa kuuza. Nadhani kitu kama

hicho kinaweza kikawepo, nishukuru kwamba sasa angalau kuna viwanda kama Kiwanda cha Mkulanzi kinataka kuanza kazi nishukuru pia Bakhresa kiwanda chake kimeongezeka pale lakini bado sukari haijawahi kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani sasa tunabidi tufanye jambo la ziada kwenye sukari, kwa kuangalia zaidi nini hasa kinatufelisha. Miwa ipo, mabonde yapo na sasa nchi yetu Mama yetu ametuongezea bajeti kubwa kwenye umwagiliaji kiasi kwamba tunaweza kulima miwa ya kutosha mpaka tukapata sukari ya kutosha ili Watanzania hii *product* yao muhimu sana ambayo wanaitegemea kwa kila kitu iweze kupatikana kwa wingi lakini kwa bei ya chini, kwa sababu sukari bado inatusababishia fedha zetu chache za kigeni tunazitumia kuagiza sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri wa sasa wa Kilimo angalau mwaka huu alikuwa anaenda kumaliza ilibaki asilimia 30 tu kabla ya mvua hizi za *El Nino* kuingilia kati, wananchi wetu wengi wanashindwa kuelewa inakuwaje mvua inafanya upungufu wa sukari wakati miwa inahitaji mvua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba hapa ningeomba Serikali sasa itazame vizuri, kule kwenye mashamba ya miwa kuna miundombinu ambayo inahitaji kutoa miwa pale inakolimwa kuifikisha kwenye kiwanda ambacho kiko hapohapo shambani. Sasa kuna barabara nyingine ni za muhimu sana ambazo zimevamiwa na mvua na zimekatika. Kwa mfano Kiwanda cha Mtibwa kilisimamisha uzalishaji kwa sababu tu daraja linalounganisha shamba lao kubwa la Dakawa na pale kiwandani limezidiwa na maji na barabara haipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali kwenye maeneo kama haya barabara muhimu kama hizi iweke jicho lake na nguvu yake kwa sababu zao hili ni siasa ya nchi yetu, kwamba kiwanda kisije kikasimama tena eti kwa sababu tu daraja limezuia na hiyo barabara ni ya Serikali, shamba lao kubwa liko Dakawa kiwanda kiko huku Tuliani. Kwa hiyo sasa pale katikati wameshindwa kupeleka malighafi uzalishaji mkubwa umesimama. Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika hili suala la umeme na suala la barabara ndio kitu ambacho Serikali inaweza ikaongeza nguvu

kule kwenye mashamba ili kuweza kujua kwamba zao hili linazalishwa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niishauri Serikali, kama tunaweza kununua mahindi tunatunza, tunanunua mazao mengine ya chakula tunatunza. Ifike mahali sasa nadhani *NFRA* tuwaongezee na hili jukumu la kununu sukari na kuiweka ghalani, kwa sababu kila mwaka mwezi wa pili lazima sukari iadimike wakati viwanda vinasafishwa. Sasa wakati huu ndio wakati ambao ungefaa *NFRA* sasa ipeleke sukari ile ambayo ilitunza wakati viwanda vinasafishwa, kwa sababu inaelekea ni utaratibu wa viwanda kwamba kila mwezi wa pili lazima vifungwe visafishwe na ukifunga tu siku moja tayari kwa sababu ni zao muhimu sana, ni bidhaa muhimu sana kwa wananchi, tayari *effect* inafika mpaka mpaka kwa mwananchi wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa wizara yangu, Waziri wangu Mheshimiwa Bashe na timu yako yote mfikirie kuwaongeza *NFRA* jukumu la kununua sukari kwenye viwanda wakati huu ambako hakuna upungufu itunzwe ili ikifika mwezi wa pili *flow* ya sukari isiyumbe iendelee na ikibidi bei itashuka zaidi. Niombe viwanda vyetu sasa kwa sababu tumetunga mpaka sheria ya kuwalinda, waongeze uzalishaji na hii Serikali itupie jicho kabisa kwenda kuwauliza kwa nini hauongezi viwanda? Mashamba yapo, kama mashamba hayatoshi nimuombe pia Waziri wangu hii *BBT* japo kuna mjumbe hapa alikuwa anaiponda. *BBT* ni nzuri na yeye mwenyewe anasema kilimo siyo kila mtu atalima halafu hapohapo tena anaponda tena kwamba *BBT* haifai, yaani hilo jibu lake la kilimo siyo kila mtu analima ndio Waziri amepata jibu kwamba sasa anachukua wachache anawawezesha, amawapa miundombinu ili wazalishe zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni jambo zuri na linafaa, nimuombe sasa katika hii *BBT* ilenge tu sasa mazao mengine ambayo ni ya muhimu, kwa mfano tukiweka shamba kubwa la *BBT* la Miwa, kwa mfano katika Mkoa huu wa Morogoro ambao huyu bwana alikuwa anausema kwa sababu ardhi bado ipo shamba lenye ekari nyingi vijana wakalima miwa wenye viwanda watafuata ile miwa, tutamwambia mtu lete kiwanda

chako hapa tayari kuna miwa ya kutosha na sukari itafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiweka shamba kubwa la *BBT* la Chikichi la kudumu unajua pale mwenye kiwanda atapeleka mafuta yatakuwa *processed* hela za kigeni zitaokolewa na nchi yetu itafika vizuri. Kwa hiyo, mimi niombe katika suluhisho la sukari pia suala la mashamba kadhaa ya *BBT* yaongezeke ya miwa na viwanda viongezeke kwa sababu sukari bado haijatosha na inatakiwa ishuke bei, bei ya 3000 kwa sukari bado ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari yetu inatakiwa yaani isifike huko iishie 1,000, 1,200 ili kila mwananchi aendelee kunywa chai, vitumbua tunatumia sukari, wanaouza mandazi tunatumia sukari, kila kitu, wengine wanauza togwa wanatumia sukari, kila kitu ni sukari. Kwa hiyo inatakiwa isifike hata zaidi ya 1,000 na inawezekana kwa sababu malighafi ni hapahapa nchini tuendelee kulima mashamba makubwa na Serikali iweke mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kidogo kuhusu Mamlaka ya Mifugo na Mamlaka ya Uvuvi, jambo hili ni la msingi sana. Kila siku tunaimba wimbo tumekuwa nchi ya pili duniani, Afrika, tuna mifugo mingi wimbo ambao hautusaidii mfugaji bado anaendelea kuishi maisha ya kimaskini. Pato letu bado halichangiwi kwa kiasi kikubwa kutokana na mifugo, hii yote inaonyesha kwamba mifugo hatujaipa jicho la kutosha hatujampa msimamizi, Wizara haina Wagani, Wagani wako TAMISEMI, Wizara inaishia mahali fulani yaani tunakuwa tupo tu tunaelea elea kwa sababu ya kukosa msimamizi. Kwa hiyo, sisi kama Kamati tumeona kabisa Wizara ikiwa na Mamlaka ya Mifugo tutakuwa tuna mtu wa kumuuliza mifugo hii itakula wapi majani yake, mifugo hii imechanjwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana hata nyama hatuuzi, nchi yetu hatujawahi kuchanja mifugo yaani kuwe na *program* maalum kubwa ya kuchanja mifugo ya nchi hii. Kuna baadhi ya masoko ya nyama tunayakosa kwa sababu hatuchanji mifugo

yetu. Sasa tukiwa na Mamlaka tutakuwa tuna mtu wa kuuliza wewe *program* ya kuchanja mifugo nchi hii inaendaje, *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano hai, tumeanzisha Mamlaka za *TARURA* tumeona mafanikio, tumeanzisha *RUWASA* tumeona mafanikio, mimi wakati sijaingia Bungeni hapa malalamiko ya Wabunge ilikuwa ni maji, maji, barabara, barabara, tangu tuanzishe hizi Mamlaka mnaona mambo yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, tukianzisha Mamlaka ya Mifugo na hakika kabisa tutakuwa tuna mtu wa kumuuliza ngozi zetu kwa nini hatuuzi, tutamuuliza nyama kwa nini hatuuzi, tutamuuliza maziwa kwa nini tuna *import* wakati tuna ng'ombe wengi, angalau tutakuwa tuna Chombo ambacho kitatuambia nipeni hiki, nipeni hiki na mambo yataenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali huu mpango ambao tumeanza wa kuanzisha Mamlaka ya Mifugo mifugo uende kwa spidi na niombe Waheshimiwa Wabunge mtakaonyanyuka kuchangia hebu kila mtu aguse hili jambo ili Serikali isikie na ili jambo liende haraka tuone faida ya mifugo na tukomboe wananchi wetu wengi ambao wanafuga na bado wanaishi umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili Mamlaka ya Uvuvi tuna Bahari kutoka Tanga mpaka Mtwara Mwambao wote ule tunajivunia tuna hiyo *beach* haitusaidii chochote, tuna Maziwa makubwa ukienda Victoria asilimia kubwa kwetu, ukienda Nyasa, nenda Rukwa achana na haya maziwa ya kutengeneza ambayo sasa hivi tunazuia mito ili tumwagilie, tena namshangaa tena tene huyu bwana anasema tusijenge mabwawa, sijui leo ameamkaje mabwawa tukiwa na chanzo cha maji cha uhakika tutalia zaidi ya mara mbili. Kwa hiyo, sasa hivi tutakapokuwa na haya mabwawa tunayoanzisha tutafuga huko kwenye mabwawa, tutamwagilia lakini bado tuna maziwa yetu ya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe namshukuru Rais wetu ameendelea kuongeza hela za vizimba na nini, hebu Wabunge wote tunyanyuke tuseme Wizara ya Mifugo iongezwe pesa kama ilivyoongezwa ya kilimo. Mtaona jinsi ambavyo uchumi wetu huu

utabadilika, maziwa yetu haya tutayatumia vizuri hii hata habari ya kufunga maziwa hatutakuwa hatufungi kwa sababu yatakuwa yamejaa vizimba. Kwa hiyo, niombe sana tumuombe Mama yetu aendelee kufungua pochi kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi halafu na hizi Mamlaka zianzishwe mtaona jinsi ambavyo nchi yetu itakimbia kwa sababu hii ndio Sekta inayogusa wananchi wa kawaida, wa chini ambao ndio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzee wangu Mwijage anasema tuanzishe chombo kwanza Mamlaka ije moja kwa moja itakuwa na sheria zake inailinda kama zilivyo Mamlaka za *EWURA* mmeona zimefanikiwa, Mamlaka zingine nyingi zimefanikiwa, tukianzisha hizi hakika, nchi yetu itakimbia, kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge leo mtakao changia kila anayeamka aguse hizi Mamlaka ziende haraka fedha iongezwe ili muone nchi yetu ambayo itakimbia na hivi ndio vitu vinavyogusa wananchi wa chini kabisa na ndio wanaotulisha tunakula samaki, tunakula ugali, tunakula mchele kwa sababu ya hivi vitu ambavyo tukiviwekea mkazo vitatusaidia sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja, niwaombe sana Wabunge wenzangu tuchangamkie hili jambo liweze kwenda mbele, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge huyo ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu. Naomba niwataje wale ambao wataanza kuchangia jioni, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mheshimiwa Yustina Rahhi na Mheshimiwa Iddi Kassim.

Baada ya kuwatangaza hao kuna matangazo mawili, tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye hayupo yuko nje ya Mkoa wa Dodoma kwa shughuli za kikazi kuanzia leo tarehe 12 Februari, 2024 kwa hiyo, wakati yeye hayupo Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko atakuwa

anakaimu nafasi ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaporejea. *(Makofi)*

Pia, kuna wageni ambao wapo Bungeni mchana huu, ni Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 150 wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally viongozi wa UWT kutoka Wilaya ya Urambo na Wilaya ya Kaliua, Mkoa wa Tabora, wako wapi wageni? Hao hapo, karibuni sana viongozi wetu wa UWT kutoka Wilaya ya Urambo na Wilaya ya Kaliua Mkoa wa Tabora karibuni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo niwatakie mchana mwema na ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023**
**na**
**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala, tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Christine

Ishengoma, Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae na Mheshimiwa Janejelly James atafuata.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hizi ambazo tunachangia leo. Kwanza kabisa nimpe pongezi Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana anazozifanya kwa kuendeleza nchi yetu. Pili, nawapa pongezi sana Mawaziri husika ambao tunajadili Kamati zao na Wizara zao. Tatu, nawapa pongezi Kamati zote mbili ambazo zimeleta mapendekezo yao na taarifa yao na naunga mkono mapendekezo yao na hasa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitaweza kuchangia kwenye sekta za uzalishaji na sekta za uzalishaji nitachangia sana sana kuhusu kilimo. Katika kwenye kilimo nitaanza kwa kuchangia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ina majukumu mbalimbali ambayo imepewa hasa unakuta kuna jukumu la kuendeleza, kusimamia pamoja na kulinda hasa hii sekta ya umwagiliaji. Sekta ya umwagiliaji kwenye kilimo ni muhimu sana na ninyi watu ambao mnajua mambo ya kilimo na watu wote, mnajua kuwa Tanzania watu wengi asilimia zaidi ya 65 tunategemea kilimo na hasa kwa upande chakula asilimia 70 kinazalishwa na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Umwagiliaji ina matatizo baadhi, baadhi ya matatizo unakuta bajeti haitoshi na hela zilizotengwa pamoja na kupitishwa na Bunge, mtiriko wake si mzuri. Kwa hiyo, naishauri na naungana na Kamati kuwa fedha zinazotengwa ziweze kutolewa kwa wakati, pia na bajeti iweze kuongezwa. Hata hivyo nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutenga fedha kwenye sekta hii ya umwagiliaji lakini tunasema kuwa kufuatana na hitaji la kilimo cha umwagiliaji kwa Mikoa mingi na kutokana pamoja na tatizo ambalo lipo la tabianchi tunashauri kuwa fedha zaidi ziweze kutengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutonana hilo kuna Wakala wa Mbegu, Wakala wa Mbegu nawapongeza kwa sababu na wenyewe wameanza kilimo cha umwagiliaji. Unakuta kwenye mashamba yao ambayo wanalima mbegu na hasa mashamba manne, tayari wameongeza eneo la uzalishaji wa mbegu, ikiwepo shamba moja tulilolitembelea ambalo lipo Tabora linaitwa Kilimi ambalo linatumia miundombinu bora sana. Pia na Shamba la Msimba ambalo na lenyewe limeanza kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, Serikali tulikuwa tunaishauri na kuiomba kuwa iongeze fedha kusudi mashamba yote ya umwagiliaji ya *ASA* yaweze kutumia kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua bado tuna tatizo la mbegu, mbegu nyingi asilimia 60 inatoka nje. Kwa hiyo, tulikuwa tunashauri hivi, mbegu ziweze kuzalishwa hapa nchini kwa kushirikiana *ASA* pamoja na *TOSCI* ambayo inaleta *quality* pamoja na taasisi nyingine ambayo inazalisha, ambayo yenyewe inaangalia utafiti. Kwa hiyo, naomba sana kuwa hizi ziweze kuungana kwa pamoja kuweza kuzalisha mbegu ambazo zinasambazwa kwenda kwa wakulima ili iweze kushirikiana pamoja na sekta binafsi ambayo inaweza kuzalisha mbegu ikiwepo JKT, ikiwepo Magereza, waweze kuzalisha mbegu pamoja na wananchi ambao tayari wameshaanza kuzalisha mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wakandarasi ambao zipo hati za madai za hawa ambao wako kwenye upande wa umwagiliaji, nashauri kwamba, unakuta kuwa wanapomaliza hati zao za malipo zinachelewa kulipwa na mimi nauliza kuna nini huko Wizara ya Fedha? Nashauri kuwa, Wizara ya Fedha iweze kuangalia na Serikali waweze kutoa fedha kuwalipa hawa Makandarasi mara wanapomaliza kazi zao ili waweze kuendelea na *stage* ambayo inafuata, kwa sababu wakifanya hivi unakuta kuwa miradi haiendelei na haiwezi kukamilika kwa wakati. Hii naiunganisha pamoja nikiwa kwenye Sekta ya Kilimo naiunganisha pamoja na Sekta ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Maji, unakuta kuwa Wakandarasi wanamaliza kazi zao lakini wanachukua muda mrefu sana kuja kulipwa fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta wafanyakazi siyo wengi wataalam kwenye upande wa umwagiliaji ili tuweze kuwa na kilimo cha biashara na chenye tija lazima tutumie kilimo cha umwagiliaji na lazima tuwe na wataalam na sana sana ma-*engineer* ambao wamebobea kwenye mambo haya ya kupima na kuchimba visima pamoja na malambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbegu za mafuta ya kula, unakuta mpaka sasa hivi bado tuna tatizo la mafuta ya kula, mafuta ya kula hayatoshi bado tunayaagiza kutoka nje tatizo ni nini? Nchi yetu imejaliwa, ina ardhi ya kutosha ina watu ambao ni nguvu kazi, ina muda wa kufanya. Kwa hiyo, nashauri kuwa mbegu ziweze kuzalishwa za kutosha zikiwa ni malighafi za viwanda na kuwepo utaratibu na mkakati wa Serikali wa kuweza kuanzisha viwanda vya kusindika mafuta ili kusudi tuweze kula mafuta yanayosindikwa hapa nchini badala ya kula mafuta na kutumia hela zetu kuweza kuagiza kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mikoa ambayo ilitengwa, Mkoa wa Singida, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Simiyu kwa kulima alizeti lakini mpaka sasa hivi haitoshi. Kigoma wanalima michikichi na Mikoa mingi sasa hivi inalima naiomba Serikali iweze kuona jinsi ya kupunguza hili tatizo la kuagiza mafuta kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu mbolea. Siwezi kuacha kuongelea mbolea, huwezi kupata kilimo chenye tija bila kuongelea mbolea. Mpaka sasa hivi tuna viwanda viwili hapa nchini, kiwanda cha hapa Dodoma na Kiwanda cha Minjingu cha Arusha, kwa nini? Naiomba Serikali iweze kusema ni lini kiwanda cha Kilwa, kiwanda cha Kibaha kitajengwa kusudi tuweze kupata viwanda vyetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mazingira mazuri ambayo yanaweza kuleta tija.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kuwa uvuvi haramu, wakala

wa mifugo pamoja na uvuvi ambao utaratibu mambo haya yaende vizuri. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mheshimiwa Yustina Rahhi ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia nafasi nami niungane na Kamati mbili zilizowasilisha taarifa zake leo, Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya UKIMWI lakini Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, leo wakati natajwa hapa nilivyotoka nje nikapokea simu mwananchi wangu wa miaka 15 aitwaje Kuwedo Kanusi Siwale, Kata ya Kabwe amekamatwa na mamba mchana wa leo akiwa ametoka shambani na mama yake akaona angalau afute yale matope lakini saa tisa kasoro wananchi wamefanikiwa kuupata mwili akiwa tayari ameshafariki. Ni aibu Taifa letu mpaka leo ni mwezi uliopita nimesema amepata shida mtu kwa ajili ya tembo, leo amekufa kijana wa miaka 15, mamba kumng'ata ni aibu kwenye Taifa letu, haileti picha nzuri hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuchangia, nitagusa kidogo kwenye Wizara inayohusika na afya, naomba nitoe ushauri kwa sababu ya muda, suala la kadi za watoto wadogo za kliniki na wanawake wajawazito nashauri zirudi Wizarani, ziratibiwe na Wizara kwenye Kitengo cha Mama na Mtoto, kuiachia Halmashauri hakutaleta takwimu sahihi kwenye Wizara lakini pia uratibu wake utakuwa hauna ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kushauri eneo hilo kwa sababu ya muda na ninaomba niende sasa kwenye Wizara ambayo inahusika na Mifugo pamoja na Kilimo. Naomba nianze

na suala la kusitisha au kufunga Ziwa Tanganyika. Ninawapongeza Kamati wamelizungumzia vizuri sana hili jambo, tumefika hapa kwenye kuhakikisha kwamba Ziwa linafungwa ni kwa sababu ya changamoto ya upungufu wa samaki. Nini kimepelekea upungufu wa samaki? Ni uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja, mimi Mbunge nakubaliana kwamba samaki wamepungua lakini nilisema mwaka jana na mwaka huu narudia ni vizuri wanaohusika na tafiti watuambie ni aina gani ya samaki imepungua Ziwa Tanganyika, kwa sababu samaki waliopo Ziwa Tanganyika ni zaidi ya aina 400. Waje watueleze kwenye tafiti zao ni aina gani ya samaki imepungua, lakini swali lingine ni kwamba kufunga Ziwa au kupumzisha Ziwa miezi mitatu ni suluhisho la kumaliza uvuvi haramu? Jibu si suluhisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kufunga ziwa, mwaka jana nimeshauri na leo narudia huwezi kufunga Ziwa bila kuwa na mbadala kwanza, mbadala wake ni vizimba. Leo ni mwezi Februari na tunataka kufunga Ziwa mwezi wa Tano, je, hivyo vizimba vitafanikiwa? Wakati tunaendelea kufikiri kusitisha hilo ziwa kwa miezi mitatu, elimu imetolewa kiasi gani kwa wavuvi wetu? Ushauri wangu kwa Serikali, yawezekana nia ni njema lakini dhamira itapimwa kwa ushirikishwaji kwa wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wananchi au wavuvi wamekata leseni, tunapoenda kufunga Ziwa tumeandaa kiasi gani kwa ajili ya kuwapa kwa hicho kipindi ambacho hawataweza kuvua. Kama elimu itatolewa kwa kuwashirikisha, natambua kazi ambayo inafanyika na Wizara na tayari wameshafika mpaka Mkoa wa Rukwa lakini walifika Sumbawanga Mjini, niwaombe Wizara, Ziwa Tanganyika haliko Sumbawanga Mjini. Ziwa Tanganyika liko Mwambao kwa maana ya Kata ya Kabwe, Kilando maeneo yote mpaka Nkasi Kusini. Kwa hiyo, twende tukazungumze na wavuvi si kikao cha kuchukua watu wawili kufanya *sampling*, hapana! Tukakutane na wavuvi tuzungumze nao, changamoto zao ni zipi ili sisi kama Serikali tujue tunafanya nini kwenye hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaenda hapo Serikali ije na majibu, mkakati wa muda mrefu wa kwenda kuepukana na uvuvi haramu, miezi mitatu si suluhisho kwa sababu tutakapofunga miezi mitatu tukija kufungua wale ambao hawana hata leseni na ambao ndiyo wavuvi haramu ndiyo watakwenda kunufaika zaidi kuliko wale ambao wanalipa leseni. Kwa hiyo, tuje na mkakati wa kudumu kwenye hili jambo, najua kutakuwa na mkakati wa muda mfupi na mkakati wa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kama Taifa tujiridhishe zile nchi ambazo tuna-*share* kwenye Ziwa Tanganyika kwa maana ya Congo, Burundi, Zambia na maeneo mengine, je na wao wanafunga wakati huo? Ni kweli wanasimamia tuliyokubaliana? Kwa sababu hawa samaki na dagaa hawana akili kama binadamu, usipomvua Tanzania ataenda Congo atavuliwa. Kwa hiyo mwisho wa siku tutawapa umaskini wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vizuri tunapofikiri kuhusu uvuvi haramu tujue kabisa ni lazima tuwape vitu ambavyo vitaendana na teknolojia hawa wavuvi. Tusichukue ile mikopo tunawapa wavuvi wa Ziwa Victoria, kwa sababu leo mkienda kwamba mnataka mkawakopeshe zaidi ya milioni 100 hakuna mvuvi ataingia hapo, kitakachotokea watu watashindwa. Kwa hiyo, ni vizuri mkakopesha kulingana na mahitaji yanahusika. Mwingine anahitaji mashine, mwingine anahitaji nyavu hahitaji vitu vyote. Kwa hiyo, twende na huo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vizimba ni muhimu sana na mje mtuambie kama tutafanikiwa kabla ya kufunga ziwa, hivyo vizimba kama vitakuwa vimefika Ziwa Tanganyika. Tumeona sijajua kwamba kama na Ziwa Victoria na wao wanafunga Mwezi wa Tano, kama sivyo kupeleka vizimba kwanza Ziwa Victoria kabla ya Ziwa Tanganyika na ndio linaloanzwa kufungwa ni kumchonganisha Rais na wananchi wa Ziwa Tanganyika. Lazima tuanze eneo ambalo tunaanza kufunga ili tuone kwamba jitihada zetu ni zipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa sababu ya muda, naomba nizungumzie utitiri wa tozo. Hapa kuna changamoto ya sheria yenyewe ya uvuvi pamoja na kanuni zake.

Ukija kwenye leseni huyu Mtanzania ambaye anaenda kufungiwa Ziwa Tanganyika wakati ana changamoto ya shughuli yake ya uvuvi, kwanza, anapotaka kutoa samaki nje ya nchi, nimesema Ziwa Tanganyika kuna aina ya samaki zaidi ya 400. Aina moja ya samaki ili akapime ile *sample* lazima atoke Tanganyika kwa maana ya Kabwe au Kilando aende Mwanza kwenye maabara iliko kwa ajili ya kupima, lakini kwa mwezi mmoja kwenye aina moja ya samaki anatakiwa alipe 150,000 kwa hiyo, kwa mwaka ni 1,800,000 huyo mvuvi. Nani anaweza? Tumezungumzia aina moja, kwa hiyo akiwa na aina 400 atalipa shilingi ngapi kwa mwaka? Haiwezekani! Tukae tuzipitie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze hapa kwenye aina ya uvuvi, hizi tozo ni lazima Serikali ikae ifikirie namna ya kuziondoa ambazo ni kero kwa wavuvi wetu. Kuna uvuvi wa *ring net*, huu uvuvi wa *ring net* Waziri wanajua na wengine wanajua tena hiyo kanuni imeandikwa inasema mvuvi mwenyewe kwa maana ya mmiliki, mvuvi atalipa dola kumi, mmiliki wa kile chombo kinachotumika dola 55, wakati mtumbwi atalipa dola 50, kwenye hicho hicho kitu kimoja, yaani mmiliki analipia chombo na yeye mwenyewe analipa na anayeenda kuvua naye alipe, haiwezekani! Haya mambo hayapo, unafanya hivi kwa kumkomoa nani? Ni mvuvi kweli unataka tumsaidie awe tajiri au tunataka aendelee kufikiri kuvua samaki wa kula chakula nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo nyingine ya ajabu, kuna uvuvi wa ndoano, huu uvuvi wa ndoano yaani kale kamtumbwi wanaweza wakaingia watu wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dakika zangu ziliondoka naomba uniongezee …

**MWENYEKITI:** Malizia mchango Mheshimiwa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hilo huyo mvuvi wanaweza wakaingia wawili wakijitahidi yule anaenda kuvua kwa ndoano na yeye anaambiwa ule ule mtumbwi wake ambao unaingiza watu wawili alipe dola kumi na yeye alipe dola 10. Tena kanuni zinazema dola 10, nchi ya

Tanzania ambayo inatumia Kiswahili tunasema dola kumi, mbona mnatumia lugha za watu? Haikubaliki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janejelly James Ntate atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Rahhi, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai na sasa hivi nimesimama hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi alioonesha kwenye hizi Wizara za kisekta hasa kwenye Kilimo, Uvuvi na Mifugo na Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanza na *BBT.* Naipongeza sana Wizara ya Kilimo kwa uthubutu mliofanya kwa *BBT.* Sawa, unapoanza, kwetu sisi kuna msemo kwamba "*natabasagaya.*" Yaani hata yule ambaye hawezi kufanya, atadharau ukifanya. Ni lazima tuipongeze Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuanzisha *BBT,* inaenda kumaliza shida ya vijana kutokuwa na ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda Chinangali pale, vijana ambao wameenda Jeshini wakafunzwa, wamerudi pale. Nawashukuru Wizara ya Kilimo na Wizara ya Kazi kupitia Idara ya Vijana. Idara ya Vijana inatoa posho ya kujikimu kwa vijana wale mpaka watakapofikia kuvuna. Hilo ni dogo kwa Serikali! Siyo dogo. Vile vile wamepewa hati, wanamiliki yale mashamba, wamejengewa nyumba za kukaa mpaka watakapokuwa wamefikia hatua ya kujenga nyumba zao wenyewe. Nawapongeza, msikate tamaa, Wizara ya Kilimo endelea kutekeleza maono ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye *NFRA*. Hii ni taasisi inayokusanya mazao yetu, lakini ukiangalia wao wanasema wanakusanya mchele, wanakusanya mahindi na mtama, lakini tuna mazao mengi ambayo tunatakiwa tukusanye. Nawashauri hasa kwa tabianchi hii inayobadilika kila wakati, inabidi hii taasisi *agency* yetu ijitahidi iwe na mwelekeo wa kujua kwamba yanapotokea majanga, tunaweza tukahitaji tani ngapi za chakula ndani ya Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni Hanang, wakulima waliokuwa wamelima, vyote vimechukuliwa na mafuriko. Ni lazima tuwe na tahadhari, lakini wajiandae na kwenye utunzaji wa zile nafaka wanazonunua, kwa sababu wakati mwingine ni nafaka ambazo zimenyeshewa na mvua, wanazifanyaje ili ziwe salama kwa matumizi ya Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende Wizara ya Viwanda. Naipongeza sana jinsi ilivyoboresha taasisi zake, na haya ni maono ya Mheshimiwa Rais, na wale aliowapa majukumu wametekeleza ipasavyo. Miaka ya 1990 mpaka 1980 mpaka 2000, ukienda *BRELA* ilikuwa imejaa vishoka wa shirika. Kusajili kampuni ilikuwa ni shida. Ukienda wanakugombania, lakini leo hii *BRELA* wamefikia mahali kwa siku mbili wanasajili kampuni, na ni kwenye mtandano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niwashauri. *BRELA* wanasomana na *TRA,* siku ukisajili unapata na *TIN number*. Naomba waongeze, kwani mfanyabiashara anaposajili kampuni, siyo siku hiyo hiyo anapopata kazi ya kufanya. Anakuwa na kipindi cha kuomba kazi. Anaweza akaomba, na asipate, lakini shida iliyopo *TRA* wakishaona mtu amesajili kampuni, siku hiyo hiyo wanaanza kumhesabia kodi. Sasa watafute namna ya kusomana zaidi wawe na taarifa mfanyabiashara huyu ameanza lini kufanya biashara ndiyo wahesabu kodi kwa kulinda Watanzania na vijana wetu wanaoingia kwenye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *FCC* ambayo ni Bodi ya Ushindani, hawa nao tuangalie, kuna kazi ambazo wanaingiliana. Aidha, sasa Serikali iamue madaraka inampa nani? Hawa kuna kipengele wanaangalia ubora, lakini

tunachojua *TBS* naye anaangalia ubora, na Bodi ya Chakula wanaangalia ubora. Sasa hapa nani ni nani? Serikali wajipange vizuri ni nani apewe mamlaka ya kutosha kuangalia vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye uvuvi. Nawapongeza sana kwa mlivyokabidhi boti, na vizimba vya kufugia samaki Mwanza lakini nawaomba isiwe Mwanza tu. Leo hii mwenzangu aliyemaliza kuchangia amesema Ziwa Tanganyika tunaenda kufunga, na tunafunga kwa nia nzuri, basi hiyo miradi iende na Ziwa Tanganyika. Kipindi ambacho tunafunga samaki wakue, hao wavuvi wetu tuwafungulie sasa hivyo vizimba waanze kufuga samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende mpaka baharini, tuna Bahari ya Hindi. Vijana walioko kule nao wapewe hivyo vifaa waendelee nao kwenye uvuvi wa samaki, na hiyo nayo iwe *BBT*. Tukienda hivyo kwa vijana wa Tanzania na akinamama wa Tanzania tutakuwa tumewasaidia kwa kujiajiri wao wenyewe, na Ilani ya Chama cha Mapinduzi itakuwa imetekelezwa ipasavyo, kuwatafutia vijana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanayofanyika yote, nimeongelea *BRELA*, *FCC* na *NFRA*, lakini bila watumishi wa kutosha hatuwezi kufika. Serikali ijitahidi, hizi taasisi zake ambazo imeamua kuwapa mamlaka ya kufanya kazi ihakikishe inawapa rasilimali watu ya kutosha. Ajira zitoke za kutosha, lakini tuache ile ya *head hunting,* inatuletea matatizo, wakati mwingine tuna-*hunt* vitu ambavyo haviko sawa sawa. Ajira zitangazwe, vijana wako mtaani wengi, waombe wapewe hizo ajira ili wakasaidie hizi taasisi zetu kuweza kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kuwapongeza, hongera Waziri wa Kilimo, hongera Waziri wa Viwanda, hongera Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mnafanya kazi, ziba masikio msisikilize maneno, msisikilize kubezwa, tembea fanya kazi, tutawaunga mkono Kamati yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja yote Kamati yetu iliyoyaleta na Kamati zote mbili kwa sababu ni za Bunge, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly. Nilimtaja Mheshimiwa Yustina Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia hoja hizi za Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekeze mchango wa kwanza kwenye Wizara ya Kilimo. Ukisema kilimo, lengo la msingi kabisa la kilimo ni kujitosheleza kwa chakula na la pili ndiyo kupata kipato. Usalama wa nchi ni kuwa na chakula na ndiyo maana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa katika kipindi chake cha miaka mitatu amekuwa akiongeza bajeti ya kilimo mara tatu katika miaka mitatu. Bajeti ya Kilimo imetoka shilingi bilioni 254 mpaka shilingi bilioni 970 na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza wakulima wadogo wadogo ambao kwa 90% ndiyo wanaofanya shughuli za kilimo katika nchi yetu. Hao wameleta usalama wa chakula katika nchi kwa mazao makuu ya chakula. Tuna usalama wa chakula kwa zaidi ya 103%, lakini bado tuna upungufu wa mazao muhimu kama sukari, mafuta na ngano. Mazao haya ndiyo tunaagiza kutoka nje na tunatumia fedha za kigeni takribani shilingi trilioni karibu 1.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujue kwamba huwa tunaomba "Mungu Ibariki Tanzania," nchi yetu imebarikiwa, wamesema wenzetu. Kuna *potential* nyingi ya kuachana na upungufu wa vyakula. Tumesema kwamba ardhi inayofaa kwa kilimo na ndiyo inatumika kwa kilimo iko zaidi ya hekta milioni 44 na tumeweza kutumia 38% mpaka 40%. Tuna *potential* za *irrigation* hekta milioni 29 na *point* lakini bado sisi tunazalishiwa chakula tunaingiza. Hili jambo naomba tuweze kusaidia Wizara ya Kilimo ipate fedha za kutosha tuondokane nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sukari tukiacha *stress* ya juzi ya mvua kubwa kwamba wameshindwa kuvuna miwa na tukapata changamoto kubwa ya sukari, lakini tulikuwa tunaenda vizuri. Ile *sugar gap* imetoka tani 120,000, mwaka 2023 tulikuwa na *gap* ya tani 30,000 na hizi zingeisha kwa sababu ya kuongeza viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika kuachana na changamoto ya sukari, Wizara ikawekeze kwenye kuzalisha miwa na kusaidia viwanda vidogo vidogo ambavyo vingeweza kufunguliwa *locally*. Kwa mfano, kule kwangu Manyara, kuna *Manyara Sugar* ambayo ilikuwa inazalisha sukari guru lakini kwa sasa sukari nyeupe. Kwa hiyo, *locally* ingeweza ku-*solve* upatikanaji wa sukari. Kuna Kiwanda cha Mkulazi, hii na yenyewe iko *special* kwa ajili ya kuzalisha sukari ya viwandani ambapo tulikuwa hatuzalishi sukari ya viwandani, kwa asilimia tulikuwa tunaitoa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ikasaidie kuweka miundombinu, ikasaidie kufanya utafiti ili hawa wapate mbegu nzuri na waweze kuzalisha. Pamoja na kuwasaidia *out growers,* ikawekeze kwa *out growers* wapate mbegu na vile vile wanunue mazao ya *out growers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mafuta, tuna *gap* karibu ya tani 300,000 kwa sababu *demand* iko kwenye 570,000 na sisi tunazalisha 200,000. Wizara ilikuwa imeweka utaratibu mzuri wa kutafuta mashamba makubwa Kigoma, Katavi na sehemu nyingine iweze kupanda michikichi ya zaidi ya miche 2,000. Sasa wanahitaji fedha ya kupata mbegu bora, wanahitaji utafiti ili tuweze kupata mbegu bora. Naomba Serikali ikatoe hela hii azma iweze kuwepo tumalize hii *gap* ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ngano hivyo hivyo, tunatumia zaidi ya tani milioni moja na sisi tunazalisha kwenye tani 200,000, zaidi ya 90% ya ngano tunaingiza kutoka nje. Tunajua umaarufu wa Tanzania kuzalisha ngano, sasa Wizara ika-*acquire* yale mashamba yote yaliyokuwa yanazalisha ngano pamoja na kupata mengine na kupata wawekezaji na wajenge mazingira rafiki ili wawekezaji waendelee kutuzalishia ngano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na changamoto pia ya mbegu hasa ya ngano na alizeti. Naishukuru *ASA* inazalisha mbegu *OPV* lakini ukienda kwenye *famer's choice* wanataka mbegu pengine kwa mfano za alizeti wanahitaji mbegu za *hybrid*. Kwa mfano, mbegu ya *Hysun* kilo moja inauzwa kwenye shilingi 50,000, ni wakulima wangapi wenye mashamba makubwa wanaweza wakamudu? Kwa hiyo, aidha Serikali iweke ruzuku au waweke nguvu zaidi kwenye uzalishaji wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nisiache uzalishaji wa mazao ya bustani. Haya mazao yanaitwa *high value crops* ambayo *return* yake ni kubwa sana. Moja kwa moja niende kwenye shamba la maua lililoko Arusha. Lile shamba limekufa, limekuwa pori. Tulikuwa tunapata dola milioni 20 kwa mwaka hazipo, kulikuwa na wafanyakazi zaidi ya 4,000 tena wanawake na vijana hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miundombinu kule ikiwepo *green house* (kitalu nyumba) ambapo kujenga moja gharama yake inaenda kwenye shilingi milioni 20, zote hizo zinakufa. Tunaomba Serikali ikatoe hela kwa Wizara ya Kilimo ikafufue mashamba ya maua yaliyoko Arusha. Tulikuwa mpaka tuna-*import*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua *demand* ya maua *roses* siku hizi kwenye *functions* nyingi tunazitumia lakini hatuna, hatuzizalishi. Pamoja na kuwapongeza tu kwamba wameanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko pamoja na Mazao ya Mboga Mboga, ikasimamie ili katika bandari na viwanja vya ndege watengeneze *code chain*. Haya mazao ambayo ni *perishable* yaweze kutunzwa vizuri yasiharibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kwenye Wizara ya Mifugo. Tunasema tuna *potential* kubwa kwenye mifugo, sisi sijui ni wa pili Afrika kuwa na mifugo mingi, lakini hii mifugo iko kwa nani? Ni ya nani? Tulikuwa na zoezi la kutambua mifugo ambayo Serikali Novemba, 2022 ilisitisha ikawapa Wizara kwenda kufanya tathmini ya namna gani bora kuweza kufanya utambuzi wa mifugo, sijui mpaka leo hawajapata majibu! Ni muhimu sana kuitambua hii mifugo. Ni muhimu ili

kupunguza migogoro kati ya wafugaji na wakulima, kudhibiti wizi na Serikali pia kuwa na mipango mizuri kwamba inapeleka wapi majosho, inapeleka wapi *vaccine*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri hili zoezi sasa kama changamoto ni fedha, naomba Serikali itoe fedha, ni muhimu sana. Kuna mwingiliano wa mifugo wa nchi za jirani huku kwetu hatuwezi kuitambua. Kama changamoto ilikuwa ni gharama pengine ya ununuzi wa hereni za kielektroniki ambapo ng'ombe mmoja ilikuwa gharama yake ni shilingi 1,750/=, mbuzi na kondoo 1,000 na kwa kweli zilikuwa kubwa. Sasa Wizara waje na majibu. Kwa umuhimu wa kufanya zoezi la kutambua mifugo wetu wa-*review* tuone sasa utaratibu mzuri. Kama siyo hereni za kielektroniki, basi watuambie kitu kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kwenye Wizara ya Viwanda. Kwenye Wizara ya Viwanda niende moja kwa moja kwenye *WMA* (Wakala wa Vipimo Tanzania). Mimi nawapongeza sana, kwa mara ya kwanza nimeona wakulima wanauza mazao yao kwa kutumia vipimo vya mizani tofauti na kule nyuma wanatumia ndoo, sijui wanatumia lumbesa na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia wanafanya kazi nzuri sana ya kupima *pump* za mafuta ya nishati, tanki, mpaka mita za maji, lakini hizi mita bado zina changamoto na vile vile mizani hizi za barabarani. *Concern* yangu ni kwenye hizi mizani za barabarani ambapo wafanyabiashara wengi wenye malori na magari makubwa imekuwa ni changamoto kubwa sana kwao. Sijui kwa nini kuna tofauti ukitoka mzani huu unaenda mzani mwingine unakuta vipimo hivi ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Serikali za Mitaa, Manispaa wana mizani zao. Wafanyabiashara hawa wanaweza wakapima gari wakawa na risiti ya Manispaa lakini wakitoka wakaenda tena kwenye hizi mizani za barabarani wanapata vipimo tofauti. Ukisogea ukaenda mzani mwingine unapata vipimo tofauti. Sasa inakuwa mbaya zaidi kama hizi lori zimebeba *perishable crops.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa mfano lori ichukue vitunguu kutoka Mang'ola, ikipita Makuyuni vipimo viko sawa, ikienda mbele pengine mpaka mzani wa Njiapanda wa Himo imezidi, anazuiwa pale *yard,* mpaka awasiliane pengine na tajiri yake na kadhalika, kama ni vitunguu vile vimeharibika vimeoza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho ni vipimo vya mipakani, lazima vipate *scanner.*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla na Mheshimiwa Jacqueline Kainja ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia leo. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, bila kumsahau Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambazo wanaendelea kuzifanya za kumsaidia Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitajikita kwenye kuchangia kwenye maeneo matatu tu, lakini yote haya nita-*refer* Wizara ya Viwanda na Biashara. Wizara ya Viwanda na Biashara na kaka yangu yuko hapo rafiki yangu sana, natamani sana atakapokuja kupata nafasi ya kuchangia aweze kutueleza kwamba hii Wizara ya Viwanda na Biashara inafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia kilimo huwezi kuwaacha watu wa viwanda na biashara, unapozungumzia Wizara ya Afya huwezi kuwaacha Viwanda na Biashara, kila unapogusa ni viwanda na biashara. Leo hii tunazungumzia habari ya sukari na niende moja kwa moja kuzungumza kwenye habari ya kilimo na kaka yangu Mheshimiwa Silinde yuko hapo ananisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ku-*refer* juzi. Juzi nilienda sehemu moja kununua sukari. Nilipofika kwenye duka lile la kununua sukari, yule muuzaji aliniangalia kuanzia chini mpaka juu na baadaye akaniambia sukari haipo wakati nilikuwa naiona iko pale, lakini nilipoingia duka la pili yake kwenda kununua vifaa vingine, nikaulizia hitaji la sukari, yule mwenye duka akaniambia ngoja nikakuchukulie sukari. Akaenda kwenye duka lile lile ambalo mimi nimeenda nikaambiwa sukari hakuna na matokeo yake akaja na sukari naye akaniangalia chini mpaka juu halafu akaniambia unatoa shilingi 94,000?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii sukari imekuwa kama unataka kuuziwa bangi. Sasa inasikitisha sana kaka yangu Mheshimiwa Silinde uko hapo, mnafanya kazi nzuri sana na Waziri wako Mheshimiwa Bashe, lakini kwa nini mpaka sasa sukari inakuwa adimu? Naomba sana utakapokuja kusimama hapa utueleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri jambo moja. Ni wakati sasa umefika wa Wizara ya Kilimo kuwa na mikakati madhubuti ya kutenga maeneo *specific* kwa ajili ya kuweza kuanzisha kilimo hiki cha miwa kwenye maeneo husika ya nchi yetu hii. Mimi huwa najiuliza, Wizara ya Viwanda na Biashara ukiwa unapita, ukifika Magu kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kiswaga ukiwa unaenda Mkoa wa Mara, pale darajani utakuta vijana wanauza miwa 24/7 wako pale. Sasa ni namna gani hii Wizara ya Viwanda na Biashara mmekaa na kubuni na kufikiria namna ya kuwahamasisha vijana wetu waanzishe viwanda mbalimbali vidogo vidogo vya kuchakata sukari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata Wizara ya Kilimo na yenyewe ni namna gani mmetenga maeneo ya kimkakati

kuhakikisha kwamba mazao haya ya miwa yanalimwa kwa wingi ili kuhakikisha kwamba *availability* ya *material* inapatikana kwenye maeneo hayo? Utaona Wizara ya Viwanda na Biashara wamesinzia, lakini pia hata Wizara ya Kilimo na yenyewe bado imekaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nishauri, ukichukua Mkoa wa Kagera, ukachukua Mkoa wa Mara ambako watu wote tunafahamu hali ya hewa ya Mkoa wa Mara huwa wanalima mara mbili kwa msimu; pia ukianzia pale Magu mpakani ukaambaa ambaa pembeni ya Ziwa Victoria, ukaenda ukavuka Mkoa wa Simiyu, ukaenda mpaka Musoma, eneo lote lile pale kama Wizara ya Kilimo itaamua kuwekeza kwa wingi fedha za kutosha maana yake ni nini? Tunaweza tukapata malighafi ya kutosha ya miwa na Wizara ya Viwanda na Biashara wakaenda kuwasaidia vijana wetu hasa wajasiriamali wadogo wadogo kuanzisha viwanda vya kuchakata sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyoisha tulifanya ziara, tulienda India na tulienda Pakistan. Tuliona namna gani hawa wajasiriamali wadogo wadogo wanachakata sukari. Sukari inatengenezwa mpaka na mjasiriamali mdogo. Leo hii kaka yangu Mheshimiwa Silinde uko hapo nataka uje utwambie ni mkakati upi? Tunaenda kwenye bajeti kama ni suala la bajeti leteni. Tengeni maeneo ya kimkakati kuonesha kwamba zao la miwa kwenye nchi hii ukitafuta maana yake twende Mkoa wa Morogoro, twende Mkoa wa Kagera na twende Mkoa wa Mara kwa sababu ni maeneo ambayo kwa zao hili tunaweza kuwekeza fedha na kuhakikisha kwamba malighafi ikapatikana bila kuleta kisingizio cha mvua nyingi zimezidi na bwawa limekatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Wizara ya Viwanda na Biashara ni muda sasa wa ninyi umefika kujitafakari na kuona namna gani mnataka muwasaidie wajasiriamali kwenye nchi hii ili waweze kufanya biashara kwenye maeneo haya. Bado mwamko wa uanzishwaji viwanda kwenye nchi hii uko chini sana, nani mwenye jukumu hili? Jukumu hili liko kwa watu wa viwanda na biashara. Ninyi ni *coordinator* wa wizara zote ni *coordinator* wa sisi. Leo hii ninyi mnatakiwa kuhakikisha ya

kwamba wafanya biashara kwenye nchi hii wanafanya biashara vizuri bila kuwa na vikwazo vya aina yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hapa Bunge lililopita, nikasema leo hii tunakabiliwa na changamoto kubwa ya wajasiriamali wetu kwenda kufanya *competition,* kwenda kufanya ushindani na wageni wanaokuja kwenye nchi hii. Tukasema ni lazima Wizara hii ya Viwanda na Biashara mje na mkakati hapa mtueleze kwamba tujue watu wa uwekezaji na ninyi wa viwanda na biashara ni masharti yapi mnayaweka kwa wawekezaji wa nje wanaokuja hapa ili kulinda wafanyabiashara wetu na viwanda nchini hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikatolea mfano nikasema leo hii kuna wakinamama wajasiriamali tunawapa fedha kule za halmashauri wanatengeneza batiki, lakini wakati huohuo kuna Wachina nao ambao wanaleta batiki hapa. Sasa tunawalinda vipi hawa wajasiriamali? Leo hii mchina anauza pazia, anauza kiatu lakini na dada yangu pale nae anatengeneza viatu, tunamlindaje mjasiriamali wa ndani? Wakati hawa hatuna kiwango na hatuna masharti ya wao kuja kuwekeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii huwezi ukatoka hapa ukaenda China ukasema unataka kuanza kuuza mapazia. Huwezi ukatoka hapa ukaenda nchi nyingine yoyote ile ukasema unataka kuwekeza. Kuna viwango vya uwekezaji kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe sana Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwenye bajeti inayokuja msipokuja na mkakati wa kutuonyesha kwamba mmejipanga vipi kuonesha kwamba mnawatetea na mna mkakati gani kuonesha uanzishwaji wa viwanda kwenye nchi hii unaenda kuwa ni chachu ya maendeleo. Mimi nitakamata shilingi kwa sababu ninyi ndiyo ma-*coordinator* wa wizara zote za kibiashara hapa nchini. Kwa hiyo, hilo kaka yangu naomba ulichukue kwamba wafanyabiashara wetu Kariakoo na kwenye maeneo mbalimbali hawapati fursa ya kuuza bidhaa zao kwa sababu wanatengeneza bidhaa zao kwa gharama lakini bado wageni wanakuja kuwekeza hapa na bidhaa zile zinauzwa kwa bei ya

chini na kuua viwanda vya wajasiriamali wetu wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kumekuwa na changamoto ya wafanyabiashara wetu kwenye maeneo mbalimbali wakikabiliwa na changamoto mbalimbali…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Cherehani.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji. Sasa hivi kwenye sekta ya tumbaku hatuna *duty twine* lakini tunategemea kutoka nje ya Wizara ya Viwanda na Biashara ipo, lakini mpaka sasa hivi hakuna mkakati wowote ambao unafanyika kuokoa hii changamoto ambaypo iko nchini kwa wakulima wa tumbaku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi muda naona umeisha malizia mchango wako.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubali taarifa ya Ndugu yangu Mheshimiwa Cherehani hapo lakini pia nimalizie kwa kuchangia kwenye sekta ya afya kidogo. Kwanza kabisa nimpongeze Dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu anafanya kazi kubwa sana na Naibu Waziri wake wa Afya. Nitoe wito na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais. Dada yangu Mheshimiwa Ummy mmetupatia vituo vya afya vingi sana tunawashukuru sana, mmetupatia zahanati nyingi sana lakini bado kumekuwa na changamoto ya upungufu wa watumishi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana Mheshimiwa Waziri muone namna gani mnaweza mkatupa kipaumbele kwenye Jimbo la Msalala ili tuweze kupata watumishi

wengi. Kumekuwa kuna changamoto ya bima, kulikuwa kuna mjadala unaendelea…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umekwisha.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma ajiandae.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuchangaia kwenye taarifa hizi za Kamati tatu zilizowekwa mezani leo asubuhi na Wenyeviti wa Kamati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwapongeze Wenyeviti pamoja na Kamati zote kwa kazi nzuri ya kuishauri na kuisimamia Serikali ambayo wameendelea kuifanya kwa kipindi chote. Pia, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kuletwa Bungeni kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea ya kiafya katika nchi yetu ililazimika kutafuta suluhu ya namna nzuri zaidi ya ku-*finance* mfumo wa afya hapa nchini hususan ikizingatiwa kwamba kwa miaka mingi toka tumepata uhuru mpaka hapa tulipofikia *financing* kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya ilitegemea sana msaada wa wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa afya ulikuwa *heavily funded* na *donors*. Hivyo, kuleta changamoto nyingi za kiutendaji lakini pia za kuweka vipaumbele vyetu hapa ndani sisi wenyewe. *Political will* ama utashi wa kisisasa wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan utatuwezesha kufikia malengo tuliyojiwekea ya kutoa usawa katika upatikanaji wa huduma za afya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili si jambo dogo maana afya katika vigezo kumi vya *happiness index* (Kipimo cha Furaha) kwenye nchi vigezo vinne vinahusiana na Sekta ya Afya. Hivyo, kuwekeza kwenye Sekta ya Afya kama ambavyo *World Development Report* ya mwaka 1994 ilivyosema, ile ripoti maarufu sana ya *Investing in Health,* inaelezwa ni kwa kiasi gani kuwekeza kwenye afya ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa lolote lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia msingi wa Sera ya Afya katika nchi yetu kuanzia ile Sera ya mwaka 1990. Hata ile Sera ya Afya ya mwaka 2007 unatokana na sera za kutoa usawa za kuleta utu lakini pia za kuleta heshima ya mwanadamu ambazo ziliasisiwa na wazee wetu kupitia Azimio la Arusha mwaka 1967. Pamoja na matamko mbalimnbali ya kisera ikiwemo Mwongozo wa Sera za Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 1981.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema msingi huu ili ijulikane kwamba kupatikana kwa afya kwa wote, usawa wa afya kwa wote ni jambo linalotuhusu sana sisi wana CCM katika Taifa letu. Nalisema hili kufuatia mabadiliko ya Kisera na kiuelekeo yaliyoanza Mwaka 1984 kupitia *Structural Adjustment Programme (SAP1)*. Pia *ERP1* na *ERP2* ya mwaka 1986 lakini pia kufuatia *Structural Adjustment Programme* ya mwaka 1993 ambapo Tanzania kufuatia *pressure* za mashirika ya *Bretton Woods (IMF & World Bank)* mwaka 1986 walianza kutulazimisha tuingie kwenye Mfumo wa Soko Huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huo ulitusababisha Mwaka 1993 kuanza kufikia ku-*introduce cost sharing* (Uchangiaji kwenye Huduma). Hivyo, kuanza kuweka *user charges* katika huduma mbalimbali za kijamii ikiwemo afya ambayo nakusudia kuizungumzia leo. Sasa *introduction* ya gharama, uchangiaji kwenye Sekta ya Afya ulianza ku-*introduce* pia mgawanyiko kati ya walionacho na wasionacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo kama sisi wana CCM ambao wazazi wetu, waasisi wa chama chetu kupitia Azimio la Arusha mwaka 1967 tusipokuwa macho kuangalia namna ya kutoa usawa kwa watu wote, namna ya kuondoa uwezekano wa uwepo wa ubaguzi na ukandamizaji wa watu

wasionacho, tusiposimama imara tukawasemea, tukaijenga Tanzania ya miaka 50 huko mbele ambayo itatoa usawa kwa watu wote, tuhakikishe kabisa kwamba tutakuwa tunatoka kwenye misingi ya wasisi wetu. Hivyo, tutakuwa tumekiangusha chama chetu na tumewaangusha Watanzania lakini pia tumewasaliti waasisi wa chama chetu ambao pia ni waasisi wa Taifa hili kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu tulipopitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa wote mwaka jana tuliazimia kuanzisha Mfuko wa Usawa ili wale watu wasiojiweza waweze kuchangiwa. Kuna upungufu mkubwa wa kimuundo na kimfumo ambayo yanapatikana kwenye sheria ambayo tuliipisha hapa. Sasa ni mapema sana kusema tunaweza kuzungumzia kubadilisha sheria lakini kwa sababu kwenye sheria hiyo kuna fursa ya kutungwa kwa kanuni tunaishauri Serikali iende ikatunge kanuni na kwenye hizo kanuni izingatie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuanzishwe chombo katika muundo wa Bima ya Afya hapa nchini ambacho kitatengeneza bei. Bei za kwenye huduma za afya kwamba kwenye Sekta Binafsi bei zitakuwa hizi na kwenye Sekta ya Umma bei zitakuwa hizi. Hiki chombo ni lazima kiwe huru. Hiki chombo ni lazima kiwe jumuishi. Kichukue wadau wote wa *Private Sector* wa *Voluntary Sector* na *Public Sector* ili kitoe bei ambazo zinakubalika katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye kanuni hizo ni lazima kuwekwe mfumo wa *means testing*. Mfumo wa kuwatambua watu wasio na uwezo. Kwenye maelezo waliyotuletea wenzetu wa Serikali kwenye Kamati ya Afya wanasema watatumia vigezo vya kuwatambua wasio na uwezo kwa kutumia *formula* inayotumiwa na watu wa *TASAF*. Sasa mfumo huo una changamoto ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa *TASAF* unahusisha watu asilimia nane tu. Wakati watu wasio na uwezo kwa mujibu wa Takwimu za *NBS (National Bureau of Statistics)*, watu wasio na uwezo wanakadiriwa kufikia 26.4%. Sasa mfumo unaoenda kuwatambua watu asilimia nane wale wa chini kabisa hauwezi

kuwa-*capture* watu 26.4% ambao wote wanapaswa kuwa wanufaika katika Mfumo mpya wa Bima ya Afya kwa Wote ambao tuliupitisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishauri Serikali iende ikatengeneze mfumo mpya mzuri zaidi ambao utawatambua watu wasio na uwezo kwa haki bila kubagua wala kumuacha nje ya mfumo mtu yeyote yule. *No one shall be left behind. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika muundo wa Bima ya Afya kwenye kanuni zitakazotengenezwa ni lazima Serikali itengeneze chombo ndani ya hizo kanuni ambacho kitaenda kutambua teknolojia ambazo zinapaswa kutumika kwenye sekta ya afya na gharama zake ili siyo kila taasisi ijiingizie teknolojia yake na ianze kuwa-*charge* wananchi na kuu-*charge* Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jacqueline Kainja atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ajiandae.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Niipongeze sana Kamati kwa kazi nzuri iliyofanya, kwa hoja walizotoa na kuchambua kwa ufasaha na wanakamati wote kwa ujumla. Vilevile, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya kuhakikisha Wizara hii ya Afya na sekta inafanya kazi kwa ufasaha kwa maslahi mapana ya wananchi wa Tanzania. Hususan ikiwa ni wananchi wa maeneo ya pembezoni na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati imeonesha kwamba kuna changamoto ya fedha za bajeti zilizotengwa kwa

mwaka 2023/2024 ikiwa sasa hivi ni mwezi wa saba wa Mwaka wa Serikali. Fedha zilizokuwa zimetengwa ni shilingi 732,364,000,000. Kiasi ambacho kimekwenda mpaka sasa hivi katika Wizara ya Afya ni shilingi 187,089,000,000 sawa na 26%. Napata wasiwasi na ukakasi sana nikifikiria ndoto alizonazo Mheshimiwa Rais mawazo yake juu ya Sekta hii ya Afya ambayo afya ni kiini na kitovu kwa kila mwananchi na binadamu yeyote yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tuna miezi saba fedha hizi zimetolewa ni 26% je, 74% zitakamilika kwa muda gani? Je malengo ya Mheshimiwa Rais tutaweza kuyakamilisha kwa wakati? Kiu ya Mheshimiwa Rais ya kuona wananchi wake wanapata huduma bora, je, tunaweza tukafikia malengo? Hivyo, niiombe sana Serikali fedha ambazo tumepitisha kwenye Bunge hili Tukufu ziwe zinatoka kwa wakati ili ile mipango ambayo wametusomea hapa na tukaweza kuipitisha kwamba tumetenga fedha hizi na tumekubaliana kwamba ziende basi ziwe zinatolewa kwa wakati. Vinginevyo basi hatuna sababu ya kusema tuna mipango moja, mbili na tatu itakayogharimu shilingi bilioni kadhaa na sisi tunapitisha hapa shilingi bilioni 732 kumbe labda uwezo huo hatuna, kwa nini inachelewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali ijitahidi sana kutusaidia wananchi wana changamoto. Tumekuwa na majengo mazuri, zahanati nzuri na vituo vya afya vimejengwa kwa wingi lakini bado tuna changamoto sana upande wa huduma za afya bado zina changamoto lakini changamoto kubwa ni mapungufu ambayo fedha haziendi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie suala la *MSD* ambayo ni kitovu na kiini cha Wizara ya Afya na Sekta ya Afya kwa ujumla. Bado wana changamoto, uwezo wao ni mdogo sana kuweza kukidhi haja ya huduma ya afya hususan kwa Serikali na mashirika binafsi kama hospitali za wenzetu wakatoliki na mbalimbali kama hizo wanazoenda kuchukua mzigo *MSD*. Bado wana changamoto kwa sababu ya bajeti yao bado ni ndogo, fedha zao ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *MSD* wao wanasema wakiwa na shilingi bilioni 561 wanauwezo wa kujiendesha vizuri. Hapo hapo *MSD* tumeipa jukumu la kuweza kuzalisha viwanda vya vifaa tiba. Sasa ili iweze kufanya vizuri ku-*supply* dawa na vifaa tiba kwenye hospitali zetu zote kuanzia zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoani na hospitali Kitaifa tunahitaji tui-*support,* Serikali iweke nguvu zaidi kwenye *MSD. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo ni changamoto kubwa inayowakumba wananchi na hususan wa maeneo ya mbali sana ya vijijini, kwa mfano mwanakijiji au mwananchi anashida ya tezi dume, hii hawezi kutibiwa zahanati, hawezi kwenda kituo cha afya ataenda moja kwa moja hospitali ya wilaya lakini anafika pale ataandikiwa dawa hospitali inakuwa ina *essential drugs* ambazo wameziweka pale. Bado *essential drugs* zile hazipatikani mgonjwa anaambiwa ni *OS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara ikaja na utaratibua wa kuzuia *form 2C* ambayo inatoka kwenye Bima ya Afya. Sasa unazuia *form 2C* mgonjwa asiwe nayo kuweza kujitafutia dawa wakati huo *MSD* hujaiwezesha. Wataalamu na watendaji wetu tunawapa wakati mgumu sana hasa katika ku-*dispense* na ku-*prescribe medicine* kwa sababu inabidi waende *store* waangalie ni kitu gani kilichopo kwamba tuna dawa hizi. Kwa hiyo, mwananchi anajikuta analishwa kilichopo na siyo kinachohitajika kwa sababu tu, tumezuia *form 2C.* Anafika hospitali anaambiwa dawa hii haipo ila utakuja baada ya siku tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi ambao kwa Mkoa wangu wa Tabora jiografia yake ni ngumu sana, mtu ametoka Kahamanhalanga huko Bukene kwenda Nzega hospitali ya Wilaya, unamwambia arudi baada ya siku tatu na hujampa hata jina la dawa labda atanunua mkononi kwa pesa zake, kwa hiyo inabidi arudi siku ya tatu. Gharama zile, anafika tena anaambiwa dawa hakuna! hivi Wizara sijui mmewaza nini? Nashindwa kuelewa lakini mmewaza nini mpaka mkaona kwamba mzuie kwanza kabla hamjatatua tatizo la kuhakikisha *MSD* inakuwa na fedha za kutosha kuweza ku-*supply* kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Serikali, Wizara, Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy, mtusaidie hii changamoto wananchi wetu wanateseka, mnaweza mkaona ni kwa sababu labda ni wafamasia tunachangia na mambo mengine lakini huo ndiyo uhalisia. Mimi kama Mbunge ninapokea simu nyingi kwa wananchi, wanaenda hospitali, wanafika kwanza anakatwa Bima lakini ile huduma hapati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe kama tunataka kupata *quality service* basi tuhakikishe tunajikita kweli kwenye hiyo *quality service* ili mtu aipate, siyo mtu anafika pale anakosa hiyo huduma. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kutusaidia *MSD* kuwekewa fedha za kutosha, itengewe hii shilingi bilioni 561 waliyosema tukipewa hii pesa itatutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline. Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mheshimiwa Luhaga Mpina ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye taarifa zetu mbili, taarifa ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo na Afya na Masula ya UKIMWI. Nafasi ikitosha nitachangia kwenye masuala ya kilimo lakini nikipata nafasi pia nitagusia kidogo masuala ya udhibiti wa bidhaa hasa chakula na vipodozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wachangiaji waliotangulia na mtazamo wa Serikali kwamba kilimo sasa ni biashara na kwamba mabilionea wa siku zijazo watatokana na kilimo, ufugaji na uvuvi. Kwa sababu idadi ya watu inaongezeka na mahitaji yanaongezeka. Naipongeza sana Serikali chini ya usimamizi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona hilo, imeanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Bodi ambayo imepewa kazi ya kuhakikisha kwamba inaratibu jinsi soko linavyoenda ili hatimaye wale wafanyabiashara binafsi wasi-*collude* na hatimaye watu wetu na wakulima wakakosa ile bei

shindani kwenye mazao ambayo wanayalima, hasa nafaka na mazao mchanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria Namba 19 ya mwaka 2009 na iliunganisha mashirika yetu mawili ambayo moja ni Shirika la Uuzaji wa Mazao ya Kilimo Nje ya Nchi *(GAPEX)* na Shirika la Usindikaji la Taifa *(NMC)*. Kati ya majukumu makubwa ambayo Bodi hii imepewa ni kununua na kuuza nafaka, pia pale ambapo tunakuwa na uhaba wa chakula nchini yenyewe imepewa jukumu la kuagiza nafaka na mazao mengine nje ya nchi ili iweze kusaidia ule upungufu ambao utajitokeza. Lingine ni wajibu wa kusindika mazao ya wakulima hasa nafaka na mazao mchanganyiko. Bodi hii pia inafanya kazi ya kuhifadhi nafaka na kutafuta taarifa ya masoko ili hatimaye mazao ya wafanyabiashara, mazao ambayo yamelimwa na wakulima wetu wadogo yaweze kupata masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi inatoa ushauri wa teknolojia mbalimbali ambazo zinaweza kuleta tija kwenye kilimo chetu, pia inashirikiana na taasisi zingine kuhakikisha kwamba vyama vyetu vya ushirika vinafanya kazi sawa sawa. Nimesema haya ili hatimaye tuone namna ambavyo Serikali yetu imejipanga na namna ambavyo inaweza kuwagusa wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za karibuni kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi hasa kwenye suala la Stakabadhi Ghalani. Mfumo huu ni mzuri ambao Serikali umeuanzisha kwa nia ile ile ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata soko la uhakika, pia inaondoa vizingiti vya uzalishaji wa tija kwa wakulima wa Tanzania. Ukiangalia mfumo wake unavyofanya kazi, mkulima anawajibika kukusanya mazao yake kwenye Chama cha Ushirika, Chama cha Ushirika baadaye kitachukua yale mazao na kuyasafirisha kwenye ghala kuu ambako ndiko mnada unafanyika, mazao yaliyokusanywa kwenye ghala kuu, taarifa zitatolewa halafu yatatangazwa na kuuzwa kielekroniki kupitia *TMX*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku za karibuni kumekuwa na kukimbizana sana kati ya watu wa Stakabadhi Ghalani, Serikali na

wananchi ambao wanataka kuuza mazao yao, ambayo wamelima wenyewe mashambani, wamehangaika wao lakini baadaye tumeanza kuweka mageti mengi. Ukiangalia Sheria ambayo imeanzisha Stakabadhi Ghalani na sheria ambayo imeanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko *(CPB)* hakuna mahali popote ambako kuna katazo la wafanyabiashara binasfsi kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazao, kwa mfano kwa Mkoa wetu wa Manyara, mazao kama mbaazi, dengu, ni mazao ambayo yamependekezwa kuingia kwenye stakabadhi ya ghala ni utaratibu mzuri, ninachoomba kwenye eneo hili; moja, watu wasilazimishwe kwenye mfumo, mfumo uvutie watu. Ninachoomba *CPB* iwezeshwe ili iweze kutafuta taarifa za masoko, hatimaye ijaribu kushirikiana na wadau wengine ikiwepo Tume ya Maendeleo ya Ushirika ili kuhakikisha kwamba ushirika unaimarika, yale yanayofanyika kwenye ushirika yanawavutia Watanzania, kwa sababu historia ya nyuma ya ushirika ndiyo inayowafanya Watanzania wengi wasivutiwe na jinsi ushirika unavyoenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo likishakaa sawa Watanzania wenyewe wataenda kwenye mfumo wa Stakabadhi Ghalani bila ya kulazimishwa. Kwa sababu ni mfumo mzuri ambao Serikali imeutengeneza lakini usianze kutenga watu, sheria ya nchi hii na biashara zetu ni huria. Ninachoshauri hapa biashara za mazao hata yale ambayo yamekuwa *earmarked* kwa ajili ya Stakabadhi Ghalani biashara zifanyike kwa uhuru. Kuna sehemu muhimu ambako ukitumia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani inakuwa rahisi kukusanya mapato ya Serikali Kuu na mapato ya Serikali za Mitaa. Tukisema kwamba hiyo ndiyo hoja pekee na ndiyo hoja kuu maana yake ni kwamba Serikali haitekelezi wajibu wake wa kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mfumo wa uongozi kuanzia ngazi ya kitongoji. Tuna uongozi ngazi ya Kijiji, tuna uongozi ngazi ya Kata, Tarafa mpaka Wilaya, *instrument* hizo zikitumika bado kodi inaweza kukusanywa bila shida yoyote, hakuna sababu ya kuweka mageti na kukamata wafanyabiashara. Mtu ambaye ameenda shambani, analima, hakulazimishwa, kwa hiari yake

mazao yake akiyapata awe na uhuru wa kufanya biashara popote anapotaka kwa sababu sheria inaruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hili, naomba kuchangia kidogo kwenye eneo la udhibiti wa bidhaa za chakula na vipodozi. Bunge letu Mwaka 2019 lilitoa shughuli ya usimamizi wa chakula na vipodozi kutoka iliyokuwa *TFDA* kwenda *TBS*. Sisemi kwamba kulikuwa na makosa kwenye eneo hilo ila matokeo ya uamuzi huo kwa sasa unatupa changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa, vipodozi na chakula zipo bidhaa ambazo ni vipodozi lakini pia ni dawa kwa sababu zinatumika kwenye upande wa tiba. Ili kuweza kusimamia vizuri, kwa kiingereza zinaitwa *border line products,* lazima uwe na taaluma ya dawa, ugusie kidogo upande wa vipodozi ndiyo unaweza kusimamia hilo vizuri. Chakula pia, kuna chakula lishe ambacho kinatengenezwa kwa *formula* mahsusi kwa ajili ya matibabu. Ukiweka pamoja usimamizi wake unakuwa rahisi kuhakikisha kwamba ubora, ufanisi na usalama wa Wananchi wetu unasimamiwa vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa malizia.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya hususan katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wenyeviti wa Kamati hususan Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Mifugo ambayo leo

hii nitaenda kuchangia, kwa taarifa yao ambayo wamewasilisha leo ambayo imetupa nafasi ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na sekta ya kilimo. Wenzangu wamechangia upande wa sekta ya kilimo, hili nimekuwa nikilichangia sana kama kweli tunataka kuleta mapinduzi ya kilimo, kilimo cha Tanzania lazima tutilie mkazo sekta ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *trend* ya *financing* ya sekta ya umwagiliaji, kimsingi imeweza kukua ndani ya miaka hii miwili. Tulitoka shilingi bilioni 42 tukaenda mpaka shilingi bilioni 100, tupo *almost* shilingi zaidi ya bilioni 200. Tafiti zinaonyesha kwamba ili hawa ndugu zetu wa Tume ya Umwagiliaji waweze kuwa na *confidence* kwamba sasa wanaendana na kilimo cha umwagiliaji wenye tija wanahitaji *at least* shilingi bilioni 500 kwa mwaka ili waweze kufikia malengo yao, bado tunasuasua kwenye suala la kutoa fedha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Manyoni Mashariki nina skimu nyingi, nina skimu moja ambayo ipo kwenye sera mbalimbali vilevile inakuwepo kila mwaka na kila tunapokuwa na uchaguzi inawekwa ambayo ni *Scheme* ya Mbwasa, bahati nzuri Waziri anaifahamu, pia tuna Skimu ya Udimaa, tuna Skimu ya Msemembo, Ngaiti hata Skimu ya Uharaka. Hizi ni skimu ambazo ni muhimu sana kwa Bonde la Ufa na kwa Jimbo langu la Manyoni Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hatuzitendei haki hizi skimu, ukiacha kwamba Serikali imeongeza bajeti, kama nilivyotangulia kusema, kutoka shilingi bilioni 42 imeenda zaidi ya shilingi bilioni 200 lakini bado tunakumbushwa kwamba ili angalau hizi skimu ziweze kuwa na tija Serikali lazima iwekeze angalau kuanzia shilingi bilioni 500. Ushauri wangu kwa Serikali na kwa Kamati, tunahitaji kuibana Serikali, tunahitaji kuisimamia Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinapelekwa lakini fedha zinatengwa ili watu wa Tume ya Umwagiliaji waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Waziri, sasa hivi katika kila Mkoa wamepeleka magari na kuajiri

mameneja wa Mkoa wamwagiliaji. Mimi kule Singida Meneja wetu wa Umwagiliaji kwa kweli anafanya kazi kubwa sana, kila wakati unamuona anazunguka kwenye hizo skimu anakutana na wakulima, bado tunahitaji kuhakikisha zile *scheme* tunaenda kuzitengeneza ili ziwe na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Waziri Bashe hayupo hapa lakini Naibu Waziri yupo, kwa kweli zile *Scheme* za Manyoni nilizozisema naomba tuwasaidie wakulima wangu. Mwaka huu hawajaweza kulima kabisa. Kwa mfano *Scheme* ya Msemembo mwaka huu imechukuliwa na maji hawajalima. *Scheme* ya Chikuyu hawajalima, *Scheme* ya Udimaa hawajalima na wale watu wanategemea zaidi umwagiliaji ili waweze kulima kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo napenda kuchangia ni kuhusu mifugo. Kwanza naishukuru Kamati kwenye upande wa mifugo wamekuja na *proposal* kwamba wanataka kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Maendeleo ya Mifugo Tanzania, *(Tanzania Livestock Development Authority)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwakumbushe mwaka 1974 Hayati Julius Kambarage Nyerere alianzisha mamlaka, ilikuwa Julai 30, ali-*assent* mamlaka ambayo ilikuwa inajulikana kama *Tanzania Livestock Development Authority.* Sasa nilitaka kujifunza kutoka kwa Kamati na Serikali, watuambie ni Sheria ipi iliyofuta hii mamlaka. Kwa sababu hii mamlaka ilianzishwa mwaka 1974 na Sheria yake ipo kwenye Tovuti ya Bunge. Sasa ni Sheria ipi iliifuta hii mamlaka na kwanini hii mamlaka ilifutwa na sasa hivi tunahitaji kuanzisha hii mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya kuanzisha hii mamlaka. Nina sababu nyingi za msingi, kwanza, sekta ya mifugo kwa Tanzania ni mojawapo ya sekta ambazo ni muhimu sana. Mimi natoka kwenye eneo la wafugaji, upande wa minada, kwanza naishukuru sana Serikali katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki pale Kintiku wamejenga mnada wa shilingi milioni 276 ingawa bado kuna vitu vya kumalizia, kuna vyoo, ofisi na vitu vingine lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na

Watendaji wa Wizara ya Mifugo wamejenga mnada mkubwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu vinahitaji kuwa na mamlaka ambayo ingeweza kusimamia kama tulivyo na Mamlaka zingine kama *TARURA* na *TANROADS*. Lingine, upande wa mabwawa na malambo, wenzangu wameongelea hapa, wakati wa kiangazi mifugo yetu inapata shida sana. Pale kwangu mimi kwa mfano katika Jimbo la Manyoni Mashariki, nina Kijiji cha Heka na Kata ya Heka, ina mifugo mingi sana lakini mwaka huu walikuwa na bwawa lao limechukuliwa lote na maji ya mafuriko, sasa hivi mifugo inapata shida sana, maeneo kama haya ndiyo sasa tunahitaji hii mamlaka ianzishwe ili iweze kuisaidia vizuri Serikali katika kukuhakikisha kwamba mabwawa na malambo yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu minada yetu. Hivi bado tunapeleka ng'ombe minadani? Watu wanauza kwa kukisia ukubwa wa mfugo? Kweli ndiyo aina ya ufugaji ambao bado tunaenda nao Tanzania? Kwa nini tusije sasa na teknolojia, tubadilike kutoka kukisia mfugo kwamba huyu ng'ombe anaweza kuuzwa labda shilingi laki tano au laki sita kwanini tusianzishe mfumo wa mizani, mimi nadhani ni muda muafaka sasa tunapofikiria kuja na hii mamlaka tufikirie vilevile mamlaka lazima ihakikishe inabadilisha aina ya minada yetu. Tunawanyonya wafugaji, mfugaji ametunza mfugo miaka nane anaenda kupewa shilingi laki mbili kwa sababu mtu anakisia tu. Anamwambia huyu ng'ombe wako huyu hana afya, nitakupa shilingi laki tatu, huyu nitakupa shilingi laki nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili ni eneo mojawapo ambalo nadhani linaweza ku-*justify* vizuri kwanini tunahitaji kuja na hii mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la vituo vya kukusanyia maziwa. Mimi huwa najiuliza sasa hivi kwa mfano masika ukienda kwa Wasukuma kule watani zangu au Wamaasai hata sisi kule Wagogo na Wanyaturu maziwa mengi sana…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa malizia.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maziwa mengi sana lakini hatuna mfumo wa kukusanya maziwa na kuyauza, tunawasaidiaje wafugaji, naomba hilo nalo Serikali ilichukue.?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya Kamati, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejadili sekta nyingi na ukweli ni kwamba kila sekta tunayoifikia kunakuwepo na mambo mazuri ya kupongeza na kunakuwepo na changamoto zinazostahili nguvu ya pamoja kuweza kuzitatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye changamoto wakati mwingine inaleta changamoto, mtu akitoa changamoto baadhi ya watu wanatafsiri vibaya, aah huyo anaichafua CCM au huyo anamchafua Rais, lakini hakuna mahali popote katika Chama cha Mapinduzi ambako imeruhusu uzembe, dhuluma, wizi, ufisadi hakuna! Ninaweza ku-*quote* vitabu vya CCM kwenye utangulizi tu kabla hujaanza na Ibara, imeyakataa mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu Katiba ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 1977, Toleo la mwaka 2022 kipengele cha (3), ukurasa wa (vi); "Chama tutakachokiunda tunataka kiwe chombo madhubuti katika muundo wake na hasa katika fikra zake na vitendo vyake vya kimapinduzi vya kufutilia mbali aina zote za unyonyaji nchini na kupambana na jaribio lolote lile la mtu kumuonea mtu au shirika au chombo cha nchi kuonea au kumdhalilisha mwananchi, kuudhoofisha uchumi au kuzorotesha maendeleo ya Taifa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hakuna mahali popote CCM imeruhusu uzembe wa aina yoyote wala wizi wa aina yoyote. Kwa hiyo, mtu akijificha kwenye CCM hakuna pango hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Katibu wetu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Ndugu Paul Christian Makonda, kwa maabara anayoifanya katika maeneo mbalimbali anayopita, kwanza nampongeza kwa kazi nzuri sana anayoifanya ya Chama cha Mapinduzi. Pili, anathibitisha baadhi ya mambo muhimu sana tuliyoyaibua hapa Bungeni, tukayapigania, tukayakataa na Mawaziri wetu hakutusikiliza, ndiyo hayo hayo ambayo leo wananchi baada ya sauti za Wawakilishi wao kutokusikilizwa, leo wanapaza sauti wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, anathibitisha baadhi ya mambo muhimu sana tuliyoyaibua hapa Bungeni, tukayapigania, tukayakataa na Mawaziri wetu hawakutusikiliza, ndiyo hayo hayo ambayo leo wananchi baada ya sauti za wawakilishi wao kutokusikilizwa, leo wanapaza sauti wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina changamoto ya muda, lakini naseme tu kwamba, baada ya kupokea Taarifa hii ya Kamati zote mbili, Kamati ya Afya na Masuala ya Ukimwi na Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, nimekuja na mapendekezo mapya saba na nitawatumia Wenyeviti. Mawili ya Kamati ya Afya na Masuala ya Ukimwi na matano kwa ajili ya Kamati ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa changamoto hiyo ya muda, naingia kwenye uchangiaji eneo la Sekta ya Afya. Natambua Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inasisitiza uchangiaji ili kuleta nguvu zaidi na kupata uwezo wa kifedha kugharamia matibabu, lakini kumekuwa na changamoto nyingi sana za wananchi wetu kumudu baadhi ya gharama za matibabu haya na wengi wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na aidha uwezo mdogo wa kulipia hizo gharama na wakati mwingine matatizo hayo yanawakuta kwenye mazingira gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hapa na leo nasema, kwa mfano, gharama ya kusafisha figo *(dialysis)* wastani kwa wiki

moja, kwa mwananchi ambaye anasafisha mara tatu ni shilingi 540,000/=. Kwa hiyo, kwa mwezi atahitaji kuwa na shilingi milioni 2,160,000/= na kwa mwaka atahitaji awe na shilingi milioni 25,920,000. Wananchi wetu hawa wanauza mali zote, zinaisha, bado hawajaweza kumtibu ndugu yao. Wengine wamefiwa na ndugu zao mikononi, hawana uwezo, wameshauza mali zote na mwisho wa siku wamepoteza ndugu na mali hana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja hapa kama Taifa tukafanya maamuzi. Tulishasamehe mambo mengi, tumesamehe mpaka wafanyabiashara wanaokuja kuwekeza hapa wawekezaji mahiri tukawasamehe, leo tutashindwa nini kusamehe gharama za matibabu wananchi hawa wanaopata mateso makubwa haya? Lipo suala la gharama za kuhifadhi mwili wa marehemu, lakini kuna gharama za matibabu za marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi gharama zote tunaweza kuzifuta zikawa bure tu. Hakuna sababu, hawa Watanzania wenzetu, kwanza wamepoteza maisha wakiwa wanalipigania Taifa hili katika nyanja mbalimbali, leo wametangulia mbele ya haki, gharama za kuhifadhiwa tu kwenye jokofu lazima alipie! Leo tu ameondoka duniani, gharama za matibabu. Mwingine amefariki tu kwenye ajali, ndugu zake hata *access* ya kupata fedha ya kuweza kulipia hizo gharama nyingine wanashindwa. Natambua ule Waraka Na. 1 wa Mwaka 2021, lakini sioni sababu, nimependekeza gharama za maeneo haya tuzifute, tuwasamehe wananchi wetu na wapewe bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali za Serikali kuongeza makalio na matiti. Nimesoma Taarifa ya Kamati, nimesikiliza viongozi, nimesoma Taarifa ya Viongozi Wakuu wa Nchi. Taarifa ya Kamati haijazungumza jambo hili, lakini Daktari Erick Muhumba kupitia tangazo la Tarehe 10 Oktoba, 2023, alitangaza kuanzia Tarehe 27 – 28 Oktoba, 2023, huduma ya kuongeza makalio na matiti itaanza kutolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Mlonganzila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia kuona je, hili jambo linaruhusiwa na Sera yetu. Nimesoma, Sera ya Afya ninayo hapa, hakuna mahali Sera ya Afya ya Mwaka 2007 imeruhusu jambo hili.

Operesheni ya matibabu, operesheni kwa ajili ya kuongeza makalio na matiti ni operesheni ya kimapambo *(cosmetic surgeries)* siyo ya mtu ambaye ana changamoo yeyote ile ya afya. Kwa hiyo, kwenye sera yetu, jambo hili halipo. Kwa nini Hospitali ya Mloganzila iliruhusu jambo hili kufanyika? Pia sheria zote na kanuni… *(Makofi)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Shabiby.

**TAARIFA**

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mchangiaji kwamba hata kiuno kikikaa vibaya, hiyo ni changamoto ya kimatibabu. Kwa hiyo, kuweka kiuno vizuri ni kusababisha binadamu atembee vizuri na awe na umbo zuri. Ahsante. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa siipokei, naendelea. Serikali imeanzisha huduma hizi bila kibali cha Bunge, hakuna sheria, hakuna kanuni, hakuna mwongozo na hivyo wananchi wetu leo hii wakienda kupata matatizo makubwa pale kwenye huo upasuaji hakuna sheria inayowaongoza kuhusu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha, malizia.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika mbili nimalizie.

**MWENYEKITI:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sheria, hakuna kanuni, hakuna mwongozo, na hivyo leo hii wananchi wetu wakipata matatizo, hawawezi ku…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina shida na mchango wa Mheshimiwa Mbunge, ila tu nilitaka kumwelewesha kwamba kwenye tiba na kwenye tiba za kawaida; kwanza maana ya afya ni nini? Kuwa na afya siyo tu kutokuwepo magonjwa, unaweza ukawa una afya, huna ugonjwa lakini una shida ya afya kwa sababu kisaikolojia hauko vizuri, wala kisosholojia hauko vizuri. Kwa hiyo, sisi kiafya, hatukuangalii wewe kwa umaana ya ugonjwa, binadamu siyo *disease entity* ni *totality* ya kimawazo, kiakili, kimwili na kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza niendelee kumfundisha hilo. Pili, sisi hapa Tanzania, hapa Tanzania…

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni moja, ananipotezea muda huyu. Ananipotezea muda, Taarifa ni moja tu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu, *plastic surgery* ina…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, inatosha, ameshaelewa. Malizia mchango wako, muda umeisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matibabu kokote duniani yanaongozwa na sera ya nchi. Sera yetu ya nchi haijazi-*accommodate* huduma zote, huduma za kimapambo hazipo. Sasa huyu Mheshimiwa Waziri anaongea nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana, muda wako umeisha. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Eric Shigongo, ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia muda wa kuchangia kidogo, nami nitajikita kwenye Sekta ya Uvuvi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nawapongeza Mawaziri wote pamoja na Wenyeviti wa Kamati. Nitajikita kwenye Sekta ya Uvuvi leo. Yamesemwa mengi yanayohusiana na uboreshaji wa sekta yetu ya uvuvi. Nilikuwa napitia hapa taarifa moja, Sekta ya Uvuvi kwa Taifa letu, pamoja na kuwa na maji mengi, lakini hatuyatumii ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea suala la vikwazo ambavyo vinakabili Sekta ya Uvuvi. Moja ya kikwazo kikubwa hasa sisi tunaotoka kwenye Kanda ya Ziwa, ni uvuvi haramu. Serikali yetu imekuwa ikifanya kazi kubwa kukabiliana na changamoto ya uvuvi haramu, lakini ukiangalia nyenzo tunazozitumia kupambana na uvuvi haramu, inatia wasiwasi kama tumedhamiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeachia suala la uvuvi haramu kwenye utashi wa kila wilaya na kila mkoa. Utakuta baadhi ya wilaya zinapambana na uvuvi haramu, sehemu nyingine wametulia na wame-*relax* kweli kweli. Changamoto hii ni kubwa na tusipokuja na mkakati madhubuti, Ziwa Victoria na maziwa mengine yatabaki mapambo, yatabaki kuwa ni maji kwa ajili ya shughuli za kuogelea na shughuli nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipambana na uvuvi haramu, lakini ukiangalia mfumo tunaoutumia siyo jumuishi. Nimesema, kwa mfano sisi Muleba tunapambana na uvuvi haramu, lakini hatuna hakika mfumo tunaoutumia kama ndio huo huo unaotumiwa na Wilaya nyingine kama Ukerewe na nyinginezo. Walioachiwa kupambana na uvuvi haramu, wanafanya kama kazi ya kujitolea. Wengine wanafanya kwa sababu wana maslahi binafsi na ndiyo maana imekuwa iki-

*victimize* watu wengi wakati mwingine hata ambao hawana hatia. Hiki kimekuwa ni kichaka cha rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwenye hili, mengi yameongelewa lakini kama tunataka kupambana na uvuvi haramu, kama waliotangulia kupendekeza, tuje na mamlaka mahsusi inayohusiana na mazao ya uvuvi. Hii Mamlaka itatengeneza kanuni, itakuja na utaalamu na zaidi itatupa *modality* mahususi ambayo itakuwa jumuishi kwa maziwa yote na hata bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye hili, sisi tunaoishi kwenye maziwa ni mashuhuda. Ukiangalia Ziwa Victoria kwa mfano, hasa Wilaya ya Muleba na Wilaya zinazozunguka Ziwa Victoria, kwa kukosekana kwa mamlaka hii au chombo hiki, unakuta kila halmashauri ina mfumo wake, ina tozo zake, inaendesha mambo yake kadri inavyotaka yenyewe. Kama tungekuwa na chombo mahususi, kingeweza kuja na tozo ambazo zina-*cut across* wilaya zote, mikoa yote na hii ingesaidia kuboresha hii Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna manung'uniko mengi na kwenye Taarifa ya Kamati imesomwa, tozo lukuki. Kwa mfano, ukija kwangu pale Muleba utakuta wale wavuvi wanatozwa tozo. Kuna shilingi 300 ambayo inakuja kwenye mamlaka yangu ya Halmashauri, lakini kuna tozo nyingine shilingi 100. Kwa hiyo, utakuta Mvuvi wa Muleba anatozwa tozo ya shilingi 400 wakati Mvuvi wa Chato anatozwa shilingi 100, Mvuvi wa Bukoba Mjini anatozwa shilingi 200. Sasa ukiangalia ziwa ni moja, lakini tozo ni tofauti. Hapa kuna jambo la kujiuliza kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo dhana ya kuwa na chombo mahsusi na kuona Wakala kinapata msukumo kwamba tunakuwa na chombo ambacho kitakuja kupanga hata hizi tozo kumpunguzia adha mvuvi na hao wote wanaohusika na suala la uvuvi. Miaka kama mitatu iliyopita, kulikuwepo operesheni zilizoendeshwa hasa za uvuvi haramu, mali za wavuvi zikachukuliwa. Hapa naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, juzi alikuwa Kagera, alikuwa pale Katembe Magarini, akatoa tamko kwamba mitumbwi inayokamatwa ikifanya uvuvi

haramu, kuivunja na kuiharibu ni kosa. Nakubaliana naye na ninaomba kumpongeza kwa niaba ya wavuvi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nchi kavu, tunapokamata pikipiki inafanya makosa au inafanya magendo, hatuichomi wala hatuiharibu, lakini ikiwa kwenye uvuvi, mtumbwi unaharibiwa na hapa tunateketeza mali ambayo ingewasaidia hawa wavuvi wetu kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kidogo kwenye mifugo. Kwenye Taarifa imeonesha bayana *NARCO* wanafanya kazi nzuri, lakini ukiangalia Mfumo wa *NARCO* wanaoutumia, uwezo wao kifedha, kwa kweli Serikali inabidi iangalie. Pamoja na changamoto nyingi walizonazo, hata kwetu huko Kagera kuna *ranch* nyingi sana, lakini kuna migogoro mikubwa sana baina ya wafugaji na wakulima. Ukiangalia kwa nini tuna migogoro hiyo? Ni kwamba, *NARCO* hawana uwezo wa kuendesha shughuli za ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hawana bajeti ya kutosha, wanaendeleza uchungaji badala ya ufugaji. Ndiyo matokeo yake tunakuwa na migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Huku kwetu imekuwa changamoto kubwa, lakini naishukuru Wizara, matatizo tuliyokuwanayo Rutoro, Mwisa II, tunaendelea kukabiliana nayo. Natumaini kwa nia njema Wizara iliyonayo, tunakwenda kuyamaliza, lakini kuyamaliza siyo suluhu ya kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie *NARCO,* kama tunataka iendelee kuwepo, tuwapatie bajeti ya kutosha ili wanapopangisha vile vitalu vyao, wahakikishe wanaweka miundombinu yote kama ambavyo tunapangisha nyumba zetu. Huwezi kumpangisha mtu nyumba haina madirisha, haina milango wala bati, huo siyo upangishaji. Kwa hiyo, tuwasaidie hawa *NARCO* wapate pesa za kutosha ili wajenge miundombinu kwenye vitalu vyao. Badala ya kuwa wapangishaji, nao wajaribu kufanya kazi kama wenzetu wanavyofanya, mfano Zimbabwe, badala ya kuendekeza uchungaji, tuje kwenye ufugaji ambao utatusaidia kuleta tija lakini utatupunguzia migogoro ambayo *NARCO* wamekuwa wakipambana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taarifa nyingi, *NARCO* wanapoteza muda mwingi kwenye kutatua migogoro badala ya kuendeleza ufugaji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Serikali iangalie *NARCO* ili iweze kutupatia tija katika Sekta ya Ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kikoyo. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric Shigongo na Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Waziri wa Afya, ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mjadala ulioko mbele yako hasa hasa hizi hoja za Kamati mbili. Nitakuwa na mambo machache na nitakuwa nimejikita zaidi kwenye Sekta ya Kilimo na Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, napongeza Kamati zote mbili kwa mchanganuo mzuri ambao wameusoma na kwa kweli unaeleweka na unatupa mwongozo vizuri kama Bunge kwa jinsi ambavyo Serikali inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa kazi nzuri anayoifanya hasa ku-*control* mfumuko wa bei ya mafuta kupanda nchini. Kwa muda mrefu sasa bei zimekuwa zikishuka, zikishuka, zikishuka, nasi kama Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tukilalamika hapa ndani kwamba bei zinapanda, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu amefanya kazi nzuri sana, tunaona ame-*balance* mambo sasa bei zinazidi kushuka kila siku. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi, natumia nafasi hii kuipongeza Ofisi yake na pia kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ombi pia kwa Wizara ya Kilimo, sisi watu wa Makete tuna changamoto, tumepata wadudu wanaitwa *cat worms* ambao wameathiri zaidi ya hekta 994, zimevamiwa na hao wadudu. Kwa hiyo, kwenye viazi kumekuwa

na changamoto kubwa. Tunaomba kama ni *emergency*, Serikali ilichukue hili jambo, iende ikalifanyie kazi haraka ili kuepusha njaa na kuondoa changamoto ya wakulima kuharibikiwa na mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni la dharura, limejitokeza na sisi hatukupanga lijitokeze. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Kilimo ichukue hatua kwa haraka ili Wananchi wa Matamba, Makete, Kituro na wananchi wa maeneo mengine Wilayani Makete waweze kutatuliwa kwa haraka kwenye changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kwenye sekta ya ngano. Kwanza, sisi watu wa Makete, Wizara ya Kilimo wakati wanasoma Bajeti, walitu-*term* kama sisi ndiyo *locked land* kwa ajili ya kuzalisha ngano kwenye Taifa letu. Nasema wazi kwamba, uzalishaji wa ngano Makete unaendelea vizuri na Mheshimiwa Rais ametupatia tani 1,000 bure za mbegu kwa ajili ya wakulima wetu. Kwa hiyo, wakulima wa Makete wamepokea hizo mbegu na tayari zimeshasambazwa kwa wakulima na uzalishaji wa ngano unaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana-Makete wananisikiliza na wanaiomba Serikali ku-*control* soko. Tulikubaliana hapa ndani kwamba wazalishaji wa ngano mlikaa nao, mkaenda hadi maabara, waka-*certify* kwamba hiyo ndiyo ngano inayostahili kuzalishwa kwa Eneo la Makete. Katika angalizo ambalo tulilitoa, mnunuzi wa ndani anunue kwanza ngano ya ndani ndipo aruhusiwe ku-*import* ngano kutoka nje, lakini kumekuwa na changamoto ya soko kwenye ngano yetu. Wakulima wetu wamevuna, sasa hivi ngano ipo ndani hainunuliki, wanunuzi wamekuwa wanasuasua kuja kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hii ina-*demoralize efforts* za mkulima lakini wanaona kabisa kwamba sisi sasa tunafanya siasa badala ya kufanya uhalisia kwenye Sekta ya Kilimo hususani kwenye ngano. Naomba sana Serikali ilichukue katika uzito. Wakulima wako tayari na wamekuwa wakionesha utayari kwenye kulima ngano Wilayani Makete ili kuisaidia Serikali, badala ya ku-*import* ngano nyingi kuingia nchini, tuzalishe nyingi kutokea ndani

ili wakulima wetu waweze kunufaika. Kwa hiyo, ninaomba sana suala la soko liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye viwanda. Tumepata tetesi kwamba Serikali ina mkakati wa kujenga viwanda kwa ajili ya mazao mchanganyiko. Moja kati ya zao mnalokwenda kujenga kiwanda ni zao la ngano. Tunawaomba, kiwanda kiweze kujengwa kwenye eneo ambalo ngano inazalishwa ambako ni Wilayani Makete. Hatutategemea kuona kwamba kiwanda kinaenda kujengwa mkoa mwingine ambako ngano haizalishwi, itakuwa siyo tija, kwa sababu tunahitaji mnyororo wa thamani kwa mkulima wetu uweze kuongezeka. Kwa hiyo, ni vyema kiwanda kikajengwa pale kwa ajili ya kuleta tija kwa ajili ya wananchi wa Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niseme wazi, sisi ni Wabunge ni vema tukawaelimisha wananchi nje kwenye suala la sukari. Suala la sukari ni kweli kwamba, sekta ya kilimo kwenye sukari kumepata changamoto lakini tumetoka wapi na wapi tupo Serikali kuna kazi kubwa ambayo imeifanya kwenye sekta ya sukari. Mwaka 2020/2021 Watanzania wanafahamu *gap sugar* ya nchi yetu ilikuwa ni zaidi ya tani 120,000 lakini Mheshimiwa Rais, Mama Dkt. Samia Suluhu kwa sababu ana utayari wa kisiasa *(political will)* akaipigania kwa kuruhusu uwekezaji kwenye sekta ya viwanda, viwanda vikaongezeka na uzalishaji ukaongezeka tukaenda kupunguza *gap sugar* kutoka tani 120,000 hadi tani 30,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutoe pongezi kwanza kwa Mheshimiwa Rais misimu karibia miwili, ndugu zetu Waislam wako hapa karibia misimu miwili ambapo kuna wakati mwingine tunasikia kilio cha kukosekana kwa sukari kipindi cha Ramadhan lakini Ramadhan karibia zote mbili zimepita, Waislam hawajakuta changamoto hiyo wakati wa Ramadhan na mfungo ambao Watanzania wengi huwa tunashiriki. Niseme wazi Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa, hili lililotokea la mvua kunyesha ndio changamoto kubwa iliyojitokeza na nadhani *effort* za Serikali imeshaagiza tani 100,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe angalizo kwa Serikali, *TMA* kwa maana ya Mamlaka ya Hali ya Hewa siyo wote waliojificha, walitangaza hii hali toka siku nyingi kwamba kutakuwepo na mvua nyingi. Kwa hiyo, ni vema Serikali muda mwingine iweze kuamini vyombo vyake na ikajipanga inapotokea majanga kama haya ili kuweza kuleta utatuzi na wananchi wetu waweze kuona kabisa jitihada za Serikali. Niseme wazi kwamba, sukari ni changamoto na hizo tani 100,000 zilizoko safarini na zingine zimeshaanza kuingia Serikali ifanye uharaka ili ziingie kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ni ku-*control* mnaweza mkaingiza sukari lakini watu wasioitakia mema nchi wakawa wameificha sukari bado tukaendelea kuona *gap sugar* mtaani. Kwa hiyo, ni vyema pia Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na vyombo vyote vya usalama viweze kufanya kazi ili sukari inayoingia tuanze kuona kwamba kuna tija kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la viwanda, nilitoa angalizo kwenye uwekezaji wa viwanda lazima tuende na *strategic plans* za Serikali za muda mrefu na muda mfupi. Kuna wakati nilisema Serikali ya Mheshimiwa Rais imewekeza kwenye kujenga madarasa lakini pili na kuweka *furniture* kwa maana ya miundombinu kwenye mashule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapoenda kujenga madarasa na inaitafuta *furniture* ni muda muafaka kwa Serikali kwa maana ya Wizara ya Viwanda kutafuta wawekezaji ambao wanaweza wakawekeza kwenye sekta ya viwanda. Nikasema mathalani Serikali ndio inamiliki Msitu wa *Sao Hill* ambao unazalisha miti ambayo unaweza ukatengenezea madawati kwa ajili ya kujenga, kwa ajili ya kusambaza madawati nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. FESTO R. SANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu neno moja tu. Serikali kuna haja gani ya kuendelea kukaa badala ya kuwekeza kwenye sekta hiyo ya viwanda vya kutengeneza *furniture* na tukasambaza madawati nchi nzima kwa sababu mapori tunayo, magari ya jeshi tunayo ya kusambaza ni utayari tu

wa Wizara kutafuta wawekezaji ili iweze kuleta tija kwa ajili ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana lakini niipongeze Serikali sana sana kwa jinsi ambavyo inapambana kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zilizoko mezani, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Eric Shigongo atafatiwa na Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kumshukuru Mungu *Jehovah Jireh* kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge hili. Nikushukuru sana wewe kunipa nafasi ya kuzungumza na huruma yako imetumika maana yake sikua kwenye ile orodha ya waliopangwa kuzungumza jioni ya leo na kwa sababu mimi ni kitinda mimba kwa siku ya leo ikikupendeza unaweza ukaniongezea dakika chache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nizungumze jambo moja tu, hali ngumu ya maisha mtaani. Watanzania hawana pesa mfukoni, hawana pesa ya kununua *(purchasing power)* imeshuka, watu hawawezi ku-*afford* maisha. Wachumi watakuwa wananielewa, mimi sio mchumi lakini nasoma kidogo. Nimesoma mahali juu ya neno linaitwa *economic hostility,* hali ambayo wananchi wanakuwa na mahitaji lakini hawana pesa, hilo ndio nitaongelea jioni ya leo na naliongelea kwa sababu ni Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ambayo inaratibu biashara katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe kwanza taswira ya hali yetu ya sasa kama Taifa; Pato la Taifa linaongezeka, pato la kila mwananchi mmoja mmoja *(per capital income)* inaongezeka, *balance of trade* kati ya Tanzania na Kenya, Tanzania imeuza zaidi Kenya kuliko Kenya inavyouza Tanzania, Shilingi ya Tanzania

inaimarika kuliko Shilingi ya Kenya. Ni kweli zamani tulikuwa tunabadilisha Shilingi ya Kenya kwa shilingi 21,000 leo hii ni shilingi 15, ina maana shilingi yetu inaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dalili ya kwamba uchumi wetu unaimarika pamoja na changamoto zote za dunia *COVID-19,* Vita ya Ukraine, Palestina na Israel bado Tanzania imeweza kustahimili na kupiga hatua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ipo kwenye vitabu, nikiwaeleza Wananchi wa Buchosa kwamba *per capital income* imeongezeka, nikiwaeleza Wananchi wa Buchosa kwamba, *GDP* imeongezeka wananiambia *GDP* ndio nini wakati mimi sina pesa mfukoni. Sina pesa mfukoni *GDP* ni kitu gani, kwa hiyo, uchumi wetu unakua *macroeconomics* lakini *microeconomics* haikui. Tumeshindwa kushusha uchumi kutoka juu kwenda kwenye meza ya mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuko hapo? Kwa nini Taifa langu? Nitasema kwa nini na namna ya kutoka tulipo. Mawazo mimi kama Shigongo Mbunge wa Buchosa sasa naweza nikasahihishwa na wataalam waliopo hapa lakini naongea kama mwananchi wa kawaida ambaye sijasoma uchumi natumia tu akili yangu, *logic* kufikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuko hapo? Tuko hapo kwa sababu ya vita nilizozitaja, tuko hapo kwa ajili ya mambo ambayo Awamu ya Tano iliyafanya. Awamu ya tano ilikuwa ni awamu ya *risk takers* awamu ya kudhubutu, iliingia kwenye miradi mikubwa mikubwa, sana ambayo si jambo baya, ni jambo ambalo tuliingia kwenye reli, tukaingia kwenye bwawa, Daraja la Busisi, miradi mikubwa mikubwa sana, si jambo baya, tukichomoka tutakuwa tumekua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tony Robbins alisema ukitaka ku-*grow put yourself in trouble* ili kusudi ukitoka kwenye *trouble* utakuwa umeshakua. Rais wangu Dkt. Magufuli Hayati apumzike na Mama Samia Suluhu makamu wake waliamua kuingiza nchi kwenye *discomfort* ili kesho ikue, jambo jema lakini matokeo yake ni nini? Watu wa mahesabu mnajua kuna kitu kinaitwa *balance*

*sheet* kwenye *financial economy* kuna kitu kinaitwa *balance sheet* na hili ni jambo la kawaida tu, mimi nina chombo changu ninajua. Mapato yakazidiwa na matumizi, *certificate* ya bwawa ikiiva, *certificate* ya reli ikiiva lazima Mheshimiwa Dkt. Mwigulu achanganyikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta pesa zote zinalipa *certificate* zile kwa sababu hiyo tumetengeneza *hostility,* uhaba wa fedha kwenye mifuko ya watu wetu, watu hawana fedha ya kununua, ndio hayo tuliyonayo huko nje zunguka na ninyi wote ni mashahidi watu wanalalamika hali ya maisha ni ngumu hawana pesa ya kununua. *suicide rate* imeongezeka, watu wanasitisha maisha yao kwa sababu maisha ni magumu sana huko mtaani lakini bado magonjwa ya akili yameongezeka hali ya uchumi ni ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye nini kama Taifa? Nina mambo matano muda hautanitosha. Mimi nataka niseme jambo moja tu, sekta za uchumi za nchi hii lazima zichangie Pato la Taifa, hazichangii, *agriculture* 27%, *tourism* imepanda kidogo 25% *mining 10%, fishing 1.8%.* Taifa letu ni tajiri mno, sekta hazichangii, nataka sekta za uchumi za nchi hii zichangie Pato la Taifa ili mwisho wa siku kapu likijaa tupunguze hata kodi zetu. Hakuna ubaya kapu likijaa kutoka kwenye sekta tukasema *VAT* iwe 4% kwani shida ni nini? Tukisema hivyo wafanyabiashara wataenda *voluntarily* kulipa kodi *compliance* itaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawalipi kodi, *tax base* yetu haifiki milioni 6 kwenye Taifa hili, nataka sekta zichangie, la kwanza kwenye *agriculture* ichangie, *mining* ichangie, *fishing* ichangie; la pili, *we must cut down unnecessary spending* kama Taifa, lazima tupunguze matumizi yetu. Lazima matumizi yanapozidi mapato unajipanga kupunguza matumizi, fedha zetu zielekezwe kwenye mambo ya msingi. Kuna shida gani mdogo wangu Mnyeti kwa mfano, natoa tu mfano ni mdogo wangu hatakasirika, akienda kwenye semina kuna shida gani gari lake likizimwa, kwa nini linanguruma mpaka semina iishe? Hiyo pesa haiwezi kununua *laptop* ya mtoto wa shule ya msingi? Natamani *cut down unnecessary spending*. Marekani ilipotoka kwenye

*Covid*-19 ilichukua trilioni 2 ikagawia wananchi wake, hatuna uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema jambo moja tu, tulikabidhiwa nchi hii na wazee wetu tukapata *political freedom* sasa tunachokihitaji sisi kama Bunge hili tuwatengeneze, watoto wetu *economic freedom* kwa maamuzi tutakayoyafanya kama Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eric Shigongo tunakushukuru sana, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu atafatiwa na Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mheshimiwa David Ernest Silinde ajiandae.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na masuala na UKIMWI kwa taarifa yao nzuri ya Kamati. Katika hatua hii nasema sisi kama Serikali tunakubali mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati. Hata hivyo, ningependa kutoa ufafanuzi katika masuala machache, nimeambiwa nina dakika saba kwa hiyo, nitakwenda harakaharaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ambalo kamati imeazimia ni kwamba, Serikali itoe kipaumbele cha ajira kwa ajili ya watumishi wa afya. Suala la kuajiri watumishi wa afya ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais wetu Daktari Samia Suluhu Hassan, Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi hata kama huo mwaka hakuna ajira lakini ajira za watumishi wa afya zitatolewa. Kwa hiyo, sisemi kwamba wanatosha lakini muione dhamira ya dhati ya Serikali ya kutoa vibali vya ajira kila mwaka kwa kuajiri watumishi wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali, tunatumia fedha za wadau kuajiri wataalamu wa mikataba pia wiki iliyopita tulizindua wahudumu wa afya ngazi ya jamii. Hawa watakwenda kupunguza mzigo wa watumishi wa afya katika vituo vya kutoa

huduma za afya kwa sababu wata-*attend* kesi nyingi katika ngazi ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la mtaji kwa *MSD* tumelipokea pia dhamira ya Serikali mtaiona katika hotuba kuu ya bajeti kuu ya Serikali ambapo Wizara ya Fedha wameahidi kuipatia mtaji *MSD* kwa hiyo, tunaamini fedha hizi zitatoka kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la Taasisi ya Chakula na Lishe, kamati inashauri kwamba iendelee kuwepo. Naomba nitoe ufafanuzi kwamba, nia ya Serikali kufanyia marekebisho Taasisi ya Chakula na Lishe haina maana kwamba suala la lishe siyo suala la kipaumbele, lishe bado imeendelea kuwa kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Sita. Kilichotokea ni kubadilisha *legal status* ya Taasisi ya Chakula na Lishe kwa sababu lile ni shirika la umma halizalishi hata shilingi moja. Kwa hiyo, kinachofanyika sasa hivi tumechukua wataalam wanatufanyia tathmini ni jinsi gani tutaweza kuendeleza kazi nzuri ya *TFNC* bila kuwa na shirika la umma. Tunaamini ndani ya wiki mbili tutaweza kupata taarifa lakini Waheshimiwa Wabunge niwatoe wasiwasi bado sasa hivi *TFNC* ipo na tumeielekeza iendelee kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni gumu kidogo lakini kwa sababu ya muda nitalieleza kwa ufupi ni suala la Bima ya Afya ikiwemo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Tunakubali maoni na ushauri wa Kamati lakini angalizo hatutafanya maamuzi bila kuzingatia tathmini ya uhai na uendelevu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata kamati inaposhauri kitita kilichopo kiendelee, tumeunda timu ya wataalam kutoka ndani ya Serikali na nje ya Serikali, watatuletea na wameshatuletea maoni tutawaita *private sector* tutajadiliana nao mwisho wa siku Bima ya Afya ni namba hakuna kitu kingine, kama namba zitakubali tutakwenda jinsi namba zinavyotaka tuende, kama namba zitatuambia twende upande huu tutakwenda upande huo lakini maazimio mengine yote tumeyapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni sera ya matibabu bure kwa mama na mtoto, Sera ya Afya ya mwaka 2007 haijabadilika inatutaka tutoe huduma bila malipo kwa kina mama wajawazito, watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 na wazee wasio na uwezo; lakini hali yetu ya kiuchumi tunakwenda hatua kwa hatua na ndio maana sasa hivi hakuna mtoto anadaiwa fedha ya chanjo za kuwakinga na magonjwa. Tunatumia zaidi ya bilioni 40 kwa ajili ya chanjo za akina mama wajawazito, chanjo za watoto wachanga, chanjo za watoto wa chini ya miaka mitano kwa kadiri uchumi wetu utakavyoruhusu ndivyo tutakwenda kutekeleza sera hii kwa asilimia 100.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunasema hivi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ummy kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Daktari Hamisi Kigwangalla.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba, suala la akinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutibiwa bure, siyo tu ni suala la kisera kwa mujibu wa Sera ya Afya mwaka 2007 pia kwa wana-CCM ni suala la usawa kutokana na Mwongozo wa Sera za CCM mwaka 1981, kutokana na Azimio la Arusha na kutokana na Imani zetu, siyo suala la kusema uchumi wetu ukikua tutaangalia hivi na vile, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa sababu akinamama wajawazito na watoto imekuwa kama kawaida kuchajiwa gharama hawatibiwi bure na hii ni kinyume cha Sera za CCM, ni kinyume cha mwongozo wa sera zetu sisi CCM pia ni kinyume cha Sera ya Afya ya 2007 na sera zote zilizotangulia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ummy Mwalimu unaipokea taarifa hiyo.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Afya haijabadilika na ndio maana nimesema, tunakwenda tunaitekeleza hatua kwa hatua kutokana na uwezo wetu wa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mahesabu hapa, bilioni 250 na kitu kwa mwaka kwa ajili ya wajawazito tu. Bajeti ya dawa ya Wizara ya Afya ni bilioni 200, tuseme ukweli lakini Bunge hili limepitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa wote hii ndio mwarobaini wa kutoa huduma za matibabu kwa watu wasio na uwezo asilimia 26 ya watanzania siyo asilimia nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tulichokibajeti tutatoa matibabu bure au Bima ya Afya kwa wasio na uwezo asilimia 26 ya watanzania. Tutakuja hapa; lakini juzi nimewaandikia wenzetu Wizara ya Fedha tukaambia hii ndio hali halisi ya gharama za matibabu kwa wajawazito, kwa hiyo, wenzetu wanalitafakari wanatafuta chanzo kingine cha fedha kuwagharamia wajawazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa sababu ya muda ni suala la Mheshimiwa Mpina kwamba je, ni kipaumbele sasa hivi kutoa huduma za kuongeza makalio? Tunaongozwa na tafsiri au na miongozo ya Shirika la Afya Duniani. Afya ni ukamilifu wa binadamu kimwili, kiakili na kijamii na kutokuwepo kwa magonjwa lakini sera hii pia inatutaka tutoe huduma kwa kuzingatia mahitaji ya kila mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakwenda kutafuta huduma India, Uturuki wanaenda kulipa dola kwa nini hizi dola wataalamu wetu wana uwezo wamesoma, kwa nini wasitoe huduma hizo ndani ya nchi? Fedha hizi ndio tunatibia hawa wagonjwa wa msamaha, fedha hizi ndio tunatibia akina mama wajawazito, fedha hizi ndio tunatibia watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano. Kwa hiyo, ni suala la vipaumbele, watanzania wakaanze kupambana na ndege wataalam wamesoma, lakini usitegemee Muhimbili akaenda kutibu Malaria ile ni Hospitali ya

Ubingwa na Ubingwa bobezi, kwa hiyo wame-*focus* kwenye *reconstructive and cosmetics surgery…*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na maazimio yote tumeyapokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kwenye taarifa za Kamati hizi mbili na hasa nikilenga kwenye Kamati ya Viwanda, Biashara, Mifugo na Uvuvi. Kwanza nianze kwa kupongeza sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa kinara wa utekelezaji wa MKUMBI (Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Uwekezaji Nchi) ambao ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha sekta ya viwanda, biashara na uchumi kwa ujumla nchini unakua. Nami nichangie katika maeneo machache kulingana na maoni yaliyotolewa na Kamati pia na baadhi ya Wabunge ambao wamechangia kwenye Kamati hii ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kulikuwa na hoja ya Vituo vya pamoja vya mpakani *(OSBP)* ambavyo kuna changamoto chache mojawapo ikiwa ni kuhakikisha ukaguzi wa mizigo na bidhaa mbalimbali katika mipaka hiyo unaboreshwa kwa kuwa na *scanner* ili kupunguza ucheleweshwaji wa kusafirisha au kuingiza mizigo kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshafanyakazi kubwa na tunaendelea kuhakikisha katika vituo hivyo vya pamoja vya ukaguzi vinaendelea kupata *scanner*. Tayari kule Nakonde -

Tunduma tunayo *scanner* ambayo inasaidia sana kupunguza foleni na msongomano wa wafanyabiashara, kwa maana ya malori yanayopita katika mpaka ule na mipaka mingine. Zaidi Serikali itaendelea kuboresha, kuhakikisha hata mipaka mingine au vituo vya pamoja vya mipakani vinapata *scanner* kadri ambavyo fedha zitakapokuwa zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo hayana *scanner*. Moja ya kitu ambacho tunakifanya ni kuhakikisha kwa ile mizigo ambayo inakuwa imetoka bandarini, imekaguliwa pale bandarini, labda inaenda nchi za nje kupitia mipaka mingine basi tunakuwa na ule usindikizaji kuhakikisha hakuna kitu tofauti ambacho kitatokea katikati hapo kwa maana ya *either* mtu kukagua mizigo ndani ili kuhakikisha kwamba mizigo ile inatoka nje ili tupunguze ucheleweshwaji kwenye mipaka ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limechangiwa sana ni kuhusiana na changamoto ya wajasiliamari ambao wanafanya biashara au tuseme kwa ujumla wake wafanyabiashara wa ndani. Ushauri tunauchukua na nimhakikishie Kaka yangu Mheshimiwa Iddi Kassim na Wabunge wengine kwamba, Serikali tunaangali kwa ukaribu sana wafanyabiashara wa ndani lakini pia kulinda viwanda vya ndani, kwa sababu moja ya changamoto ambayo tunayo ni kuona baadhi yetu tunadhani bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi hazina ubora kama zile ambazo tunaingiza kutoka nje na hii imetuletea kuwa na urali hasi kwa maana ya kuingiza bidhaa zaidi kutoka nje *(import)* badala ya ku-*export* zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo moja tunahakikisha tunalinda viwanda vya ndani, pamoja na kuhakikisha tunawasaidia wafanyabiashara wa ndani kwa maana ya wajasiriamali wetu ambao wanasaidi kuuza bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vyetu lakini pia na mazao yanayozalishwa na wakulima. Kwa hiyo, hili tutaendelea kulifanya ili kwa kutoa moja taarifa ya bei za bidhaa mbalimbali.

**MHE. IDDI K. IDDI** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, kwa taarifa iwe fupi Mheshimiwa Mbunge.

**TAARIFA**

**MHE. IDDI K. IDDI** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninataka kumpa taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tunachohitaji hapa kwa wajasiriamali wetu ni namna gani Wizara sasa mtakuja na mwongozo, sera ama sheria ambayo itamlinda. Tunatambua kwamba bidhaa ni kweli zinazotengenezwa hapa zina ubora, lakini tunahitaji sasa kuwe na *restrictions* kwa hawa wageni wanaotoka nje kuja kuwekeza hapa ili kuweka usawa kwa wafanyabiashara.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, taarifa hiyo unaipokea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana napokea taarifa kwa sababu ni sehemu ya uboreshaji lakini tukizingatia sheria na taratibu za uwekezaji nchini, kwa sababu tunaboresha mazingira ya uwekezaji, kwa hiyo lazima tuzingatie sheria ili kuhakikisha wawekezaji wote wanahaki sawa, wawe kutoka nje au wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ambalo pia limeongelewa sana ni kuhusiana na viwanda vya mbolea au bidhaa mbalimbali muhimu ambavyo tunatakiwa kuhamasisha hapa nchini. Serikali inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda ikiwemo viwanda vya mbolea lakini pia hata viwanda vya bidhaa nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya mbolea kama walivyosema wachangiaji tuna viwanda vikubwa viwili ambavyo viko hapa nchini, lakini tuna viwanda na vingine vingi vya kuchanganya kwa maana ya *blending* na vingine vya kuzalisha mbolea aina ya *manure (composite manure)* lakini pia na *organic*. Kwa hiyo, tunachokifanya sasa ni kuona namna gani tutaenda pia kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda

vinavyotengeneza mbolea za kemikali kupitia gesi asilia kama ambavyo umesema kule Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunaliangalia sana ni kuona pia namna gani tunaweza kutumia madini tuliyonayo kama vile makaa ya mawe nayo pia yanaweza kutumika kutengeneza mbolea. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na mipango mbalimbali kuhakikisha gesi asilia tuliyonayo kule Kilwa tunaendelea kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge na Kamati wamechangia kwa karibu sana ni kuhusiana na kuhakikisha tunahuisha sera, sheria na kanuni mbalimbali ambazo zinasaidia sekta hii ya viwanda. Kwa taarifa yako tayari tumeshaanza kuhuisha sera zetu mbalimbali, tukiwa na Sera ya Taifa ya Viwanda lakini pia na Sera ya Biashara na sheria nyingine ambazo zinasaidia kuhakikisha tunatekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya kuona namna gani tunakuja na mkakati maalum wa kuwa na viwanda mahsusi kwenye maeneo mahsusi. Mheshimiwa Festo Sanga ametolea mfano wa kwamba kule Nyanda za Juu Kusini kwenye miti basi tuhamasishe ujenzi wa viwanda vya kutengeneza samani kwa mfano ambazo zinatumika shuleni. Kwa kweli tunachukua hoja hiyo na tayari Wizara kupitia taasisi zetu kama *SIDO* tuna mpango ule wa Wilaya moja, bidhaa moja kwa maana ya *one District*, *one product,* na hii tulilenga kuona bidhaa hizo zinazalishwa katika maeneo husika ziwe zinalingana na malighafi inayotokana na eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme kwa ujumla tunachukua hoja zote za Waheshimiwa Wabunge pia na Kamati na tutaendelea kuboresha kadri muda unavyoenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami ya kuchangia hoja zilizopo mbele ya Bunge lako Tukufu hoja za taarifa za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia zaidi Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo sisi Wizara yetu ndiyo wanatusimamia. Nitachangia baadhi ya maeneo hususani maeneo makubwa mawili ambayo nimeona na mimi naweza nikachangia nikiamini Bunge lako Tukufu litapata jambo ambalo litasaidia kuendelea kutushauri vizuri Serikali na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni mradi kwa maana ya Programu ya *BBT* (Jenga Kesho Iliyo Bora). *BBT* ni programu na programu hii ni ya muda wa miaka saba na siyo *project*, kwa hiyo hili ni vizuri Wajumbe wakalielewa na mwaka jana mwezi Machi, 2023 ndiyo mwaka ambao programu hii ilianza rasmi kwa kuzindua katika moja ya shamba la mfano la pale Chinangali lilopo katika Halmashauri ya Chamwino. Kwa hiyo *BBT* siyo *crash program* kwamba ni programu ama *project* ya muda mfupi ambayo inatakiwa kuisha, ndani ya *BBT* kuna *project* nne ambazo sisi tunakwenda kuzitekeleza. Miongoni mwa *project* hizo ni pamoja na *BBT block farms,* kwa maana mashamba makubwa ya pamoja. Mfano wa mashamba makubwa ya pamoja ndiyo kama tunavyoliona lile la Chinangali na vilevile tunavyoliona Shamba la Ndogowe na mingine ambayo tumeyapanga katika mwaka wa fedha huu hapa uliopo sasa mashamba mengine makubwa matano tutaenda nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BBT* ina-*project* ya *BBT financing*. Lengo la *BBT* tuliyonayo ni pamoja na kutoa mitaji na teknolojia kwa wakulima. Tumeanza kufanya hivyo na katika mwaka huu wa fedha mpaka muda huu tunavyozungumza tumeshatoa milioni 960 kwa vijana 118 vijijini huko ambako wako na wala siyo kama hawa ambao Wizara tumewa-*recruit* wanaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile programu ya *BBT* ina mradi mwingine wa *BBT borehole*. Maana yake tutachimba visima 67,000 ndani ya miaka saba kwa wakulima nchini kwa kila mkulima walau tutachimba kwa ekari 2.5 kwa wakulima ambao tutakuwa tumewakusudia. Lengo letu ni moja tu, kuongeza uzalishaji kwa mwaka mzima kwa hiyo hii ni programu ambayo tumesema tutaendelea nayo. Programu ya nne kwenye mradi wa *BBT* ni *BBT extension services,* kwa maana mradi wa kuajili vijana kutoa huduma za ugani kwa wakulima wetu hiyo ndiyo programu nzima ya *BBT*. Kwa hiyo, mtu mmoja akii-*passive BBT* kama ni Chinangali anakuwa hajaielewa kwa upana wake. Kwa hiyo hili niliona nilitolee ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa ambayo ni vizuri nikaiweka sawa. Kuna mchangiaji mmoja hapa alizungumza kwamba ile Chinangali peke yake tumetumia bilioni 40, ile ni taarifa ya uongo kabisa. Kwa sababu katika Bunge lako Tukufu mwaka huu wakati tunapitisha bajeti *BBT* ilipangiwa bilioni 10 pekee. Sasa mtu anaposema Chinangali imetumia bilioni 40 unashangaa Mbunge kabisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatoa taarifa za uwongo ndani ya Bunge lako Tukufu, *this is unfair* na vizuri tukaliweka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi wa pale kwa mfano alizungumzia mradi wa Chinangali pale zile ekari mia tatu ambazo zimelimwa zabibu. Zile siyo kwa vijana ambao walikuwa *recruited*, zile ni kwa ajili ya wanajamii wananchi wa eneo lile la Chinangali, na ndiyo ambao tulianza nao pale awali. Kwa hiyo *BBT* imekusudia kuongeza ajira za vijana kupitia kilimo milioni tatu ifikapo mwaka 2030. Kwa hiyo hilo niliona ni vizuri nikaliweka sawa ili Wabunge wanapokuwa wanatushauri sisi kama Serikali waweze kuona njia bora na sahihi zaidi ya kuendelea kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusudi hili ni kusudi la Mheshimiwa Rais na amekusudia tufanye *modern agriculture*, tusiendelee na ule utaratibu wa kizamani. Huwezi kuwa mpaka leo eti unashangaa kwa nini shamba lina fensi? Sisi tumekubaliana katika Wizara ya Kilimo, mashamba yetu yote ya mbegu tutazungusha fensi, mashamba yetu yote ya utafiti tutaweka fensi kuyalinda dhidi ya wavamiaji wote. Hiyo ni programu ambayo tumeiweka

na tuko *serious* katika jambo hili na niwathibitishie tu kwamba programu hii ya *BBT* haiwezi kufeli hata kidogo, kwa sababu tuna dhamira ya dhati na tunajua tunachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *with BBT*. Programu ya *BBT* imetusaidia sana, moja imesaidia ku-*solicit fund* kutoka katika *financial sectors*. Kwa mfano *AFDB* peke yake katika mwaka huu wame-*pledge* kutupa dola za Kimarekani milioni 100. Lakini katika ile mikutano mikubwa ambayo tuliiendesha *AGRF*, *COP* 28. *BBT* peke yake *pledges* tulizonazo ni dola za Kimarekani milioni 600! Unasemaje hiyo ni *failed program* wakati sisi tumedhamiria na kukusudia kuwasaidia Watanzania? Kwa hiyo, hili niliona ni vizuri nichangie na kuliweka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo la pili ni kuhusu sukari. Wizara tunatambua changamoto ambayo ilijitokeza. Mwaka jana katika Bunge lako Tukufu, Wizara ilieleza hapa Bunge kwamba matarajio ni uzalishaji wa sukari tani laki tano elfu hamsini na tano. Bahati mbaya kutokana na hali ya hewa mvua, *TMA* baada ya kutangaza, Bodi ya Sukari ika-*review* matarajio kwa maana ya lengo la sukari la uzalishaji kufikia tani laki nne arobaini na tano elfu. Kwa nini? ni kwa sababu mvua imekuwa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda na Kamati nafikiri ninyi wote mmeshuhudia. Tumeweka mikakati ya muda mfupi ambayo ni pamoja na kuagiza sukari tani laki moja na vibali vimetolewa na sukari inaendelea kuingia nchini mpaka sasa hivi karibu tani elfu saba tayari wanaendelea kushusha pale bandarini kuna meli zime-*dock* pale zitaendelea kushusha, ninaamini mpaka tunavyofika mwisho wa mwezi huu kila kitu kitakuwa kimekwenda sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona ni vizuri nikawaeleza Waheshimiwa Wabunge kwa nini tulifikia na tulitangaza kwamba malengo yatafikia kuzalisha tani laki tano na elfu tano? Tuna viwanda ambavyo nchini hapa vinazalisha sukari. Kwa mfano Kilombero *Sugar* wao walisema katika mwaka huu watazalisha tani 185,000, *TPC* walisema watazalisha tani 115,000, Kagera *Sugar* walisema watazalisha tani laki moja na hamsini, Mtibwa *Sugar* walisema tani elfu sabini, Manyara *Sugar* walisema tani elfu kumi,

Bagamoyo *Sugar* walitegemea kuzalisha tani elfu arobaini na Mkulazi tani elfu thelathini na tano, ndiyo ilikuwa inaleta tani laki tano na elfu hamsini na tano, lakini hali halisi ya uzalishaji mpaka sasa hivi Kilombero *Sugar* wamezalisha tani 84,000, *TPC* tani 98,000, Kagera *Sugar* tani laki moja na elfu tano, Mtibwa 58,000, Manyara 7,000, Bagamoyo 18,000 na Mkulazi 1,500, ambayo imeleta tani 334,357, Kwa hiyo unaona hapo panapatikana ile *sugar gap* ambayo imejitokeza. Niwathibitishie tu kwamba malengo ya Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Kilombero kinaongeza *extension* kutoka uzalishaji wa tani laki moja thelathini na tano kwenda tani laki mbili elfu sabini na moja kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *TPC* watatoka tani laki moja na kumi na tano kwenda laki moja na ishirini. Kagera *Sugar* watatoka tani laki moja na nusu kwenda laki moja na sabini, Mtibwa watatoka tani elfu sabini kwenda tani laki moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukiangalia *extension* zote utaona katika mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026 matarajio ya uzalishaji wa sukari *vis-a-vis* mahitaji ya ndani ambayo ni ya zile sukari za matumizi ya nyumbani ni tani laki tano elfu hamsini na mbili, tutakwenda kwenye tani laki saba na elfu sita…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani naomba nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwisho kabisa, kuna Wawekezaji wapya wa viwanda vya sukari nchini wakiwemo *Lake Agro* kule Rufiji watazalisha tani 30,000 *by* 2026/2027, Mufindi *Paper Mills* kule Kasulu watazalisha tani laki moja *by* 2026/2027. Kwa hiyo, ukija ukipiga *total* tutafika karibu tani laki tisa, *this is the projection* na ndiyo iko *actual* ndani katika Serikali na niwathibitishie tu Dkt. Samia amekusudia kumaliza hili tatizo kwa vitendo na siyo vitu vilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja za Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wetu wa Kilimo. Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, mtoa hoja namba moja Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na mimi niungane na wachangiaji waliopita kuipongeza sana Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya ya kuturatibu na kufuatilia shughuli mbalimbali katika sekta zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa kifupi sana kwa sababu ya muda nijikite kwenye mambo machache sana ambayo kama Serikali tumeyaona na tumesikia Waheshimiwa Wabunge wakijaribu kuyachangia. Nianze na hili la chombo cha kusimamia miundombinu ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mifugo yetu inapitia katika kipindi kigumu sana, hii ni kwa sababu Wizara inapomaliza kujenga majosho, inapojenga mabwawa hakuna anaekwenda kuyasimamia hayo mabwawa siyo Serikali za Mitaa, siyo Serikali za Vijiji, siyo mtu yeyote, kwa hiyo miundombinu hii kama majosho, mabwawa yanapokuwa yamekamilishwa kujengwa na Serikali Kuu maana yake yanatelekezwa Vijiji hakuna anaehangaika nayo. Hii ni kwa sababu unapotembelea majosho yaliyojengwa miaka minne, mitano iliyopita asilimia tisini ya majosho yetu hayafanyi kazi, kwa nini? unakuta ni kitu kidogo sana kimeharibika lakini hakuna anaepatikana kurudishia kile kitu, unakuta chuma ndogo imevunjika inahitaji shilingi laki moja, inahitaji elfu hamsini kuchomelea hakuna anayehangaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa mengi yamepasuka, mabwawa mengi yameharibika kule hakuna anaerudishia. Kwa hiyo sisi tukafikiri pengine kwa kushauriana tukafikiri kuna umuhimu wa kuanzisha chombo maalumu kitakachokuwa na wajibu wa

kurudishia kila kilichoharibika, kusimamia miundombinu yote ya mifugo ambayo pengine kwa namna moja ama nyingine inasaidia kuleta tija katika ufugaji wetu. Kwa hiyo, hili kwakweli tumelipokea na Waheshimiwa Wabunge wengi wamelisema, Kamati imelisema na sisi kama Wizara tumelichukua na tutakwenda kulifanyia kazi kwa haraka sana na tayari tumeishaanza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusiana na chanjo. Ngo'mbe zetu na Mifugo yetu mingi kwa asilimia kubwa haina chanjo na hii ndiyo maana kwa sababu kwamba sisi mifugo yetu kama ng'ombe ukimchinja ng'ombe Tanzania huwezi kumpatika soko lolote nje ya nchi, kwa sababu hatutibu ng'ombe zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mataifa yanayofanya biashara na mpaka leo cha kusikitisha ni kwamba bado tunaagiza nyama kutoka nje ya nchi kwa nini? kwa sababu kuna maeneo ambayo wao wanahitaji nyama ambayo imetibiwa, sisi bado hatutibu ng'ombe zetu, Serikali imeona hili jambo ni la muhimu na tunakwenda kuanzia mwezi wa saba, tunakwenda kutangaza rasmi chanjo sasa ni suala la lazima na siyo hiyari, na Serikali imekubali kuingia gharama ya kutoa gharama zote za chanjo. Chanjo itasimamiwa na Serikali na gharama ya yote ya chanjo itakuwa chini ya Serikali kupitia Wizara ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka niwahakikishie wafugaji wote popote walipo na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itasimamia jambo hili na tunakwenda kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusiana na *BBT*. Sisi Wizarani kwetu kwa sababu ni mifugo, mifugo huzaliwa, mifugo hukua na mifugo hufariki. Mifugo tayari imeshaanza kutengeneza faida, mwaka huu unaoisha wa fedha tayari tumeishatengeneza zaidi ya milioni mia moja kama faida kupitia vijana wetu wa *BBT* waliopo Mwabuki na maeneo mengine na kwakweli tunakwenda vizuri na *BBT* inafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine kwa haraka haraka ni kuhusiana na elimu, kuhusiana na mifugo. Tunaendelea kutoa elimu kwa wafugaji wetu, wafugaji wetu ni lazima wafike mahali wakubali kwamba ni lazima tuanze kufuga kisasa. Kuwa na wingi wa mifugo elfu moja, elfu mbili ambayo thamani yake ukifuga kisasa ni sawa sawa na ng'ombe mia moja, mia mbili kwa kweli huko lazima tutoke. Wafugaji wetu wakubali kwamba sasa ni lazima tuanze kufuga kileo, tufuge kisasa lakini kwa tija kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wafugaji wetu kwenye maeneo mbalimbali juu ya ufugaji bora kwa sababu pia tunapata shida sana hasa kwenye migogoro ya wakulima na wafugaji. Unakuta mfugaji ana ng'ombe 2,000 halafu hana mahali pa kuwalisha, kuwapa maji na kuwatibu. Kwa hiyo, tunachoshauri tunawaelimisaha kwamba ukipunguza mifugo, walau iwe 200 ili utafute sehemu ya malisho, sehemu ya kuwatibu na sehemu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wafugaji wetu wengi kwa asilimia kubwa wameweza kuelewa jambo hili na wanapokea kwa namna ambavyo inatakiwa. Hii itatusaidia sana kupunguza migogoro ya wafugaji na wakulima kwa sababu maeneo mengi tumeona wafugaji wetu wanavamia mashamba ya wakulima, wanakwenda wanalisha mifugo yao, kwa sababu ya wingi wa mifugo ambayo imemshinda na yeye kusimamia mifugo mpaka wanaingiza kwenye mashamba ya watu. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri na tunaendelea kupokea ushauri wa Kamati kadri ambavyo maelekezo yanakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na Mamlaka ya Uvuvi. Tayari tumeshafika kwenye hatua mbalimbali za uanzishaji wa Mamlaka ya Uvuvi Tanzania. Hiki chombo ndicho kitakuwa na jukumu la kuratibu shughuli zote zinazohusiana na masuala ya uvuvi ikiwemo uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wamekuwa wakifuatilia jambo hili, na kwa kweli mwarobaini wa uvuvi haramu ni uanzishwaji wa chombo hiki muhimu ambacho ndicho kitasimamia shughuli zote. Kama ni boti

za doria yatakuwa huko kwenye chombo hiki, kama ni wataalamu wa doria na operesheni mbalimbali kule ziwani, ndio watakuwa wanafanya shughuli hizi. Kwa sababu mpaka leo tukisema ni nani anasimamia uvuvi, tunashindwa kwa sababu hatuna chombo hiki. Sasa, chombo hiki kinakuja na tuko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha chombo hiki ili kiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta hii ya uvuvi, leo ukiuliza nani anajua nini kimevuliwa wapi, ni changamoto kubwa, kwa sababu Maafisa Uvuvi tulionao wengi wamejigeuza kuwa ni Maafisa Masuuli, Maafisa Wakatisha Kodi, Wakusanya Mapato wa Halmashauri. Ile kazi *professional* ya Maafisa Uvuvi ambayo Serikali imewatuma wakaifanye kwa kweli tuseme kabisa ukweli hawaifanyi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka kufanya nini? Tunataka tuondoke huko tuanzishe chombo ambacho kitakuwa na jukumu kikiamka asubuhi, kikilala jioni, kikishinda mchana kinashughulika na masuala yanayohusiana na uvuvi. Kwa hiyo, jambo hili limesemwa sana na Kamati, na pia Waheshimiwa Wabunge wamelisema sana kwa upana wake, nasi Wizara tumeshalichukua na tayari tupo kwenye hatua mbalimbali ya uanzishwaji wa Mamlaka hii ya Uvuvi Tanzania ili kuweza kuanzisha chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na elimu ya vizimba. Tumeshaanza, wataalamu wetu wanazunguka maeneo mbalimbali wanatoa elimu hii ya vizimba. Tumeanza Kigoma, baada ya hapo tutaenda Sumbawanga na Katavi na maeneo mengine. Tayari kule Mwanza (Kanda ya Ziwa), elimu imeshaingia na baadhi ya maeneo tayari wameshaanza kufuga samaki kwa njia ya vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, niwaambie kuwa hii ni fursa kwa Watanzania wote, wala siyo wavuvi tu, hata Waheshimiwa Wabunge wenye shida ya kutaka kufuga samaki kwa njia ya vizimba ruksa, unaweza kuomba Benki yetu ya Kilimo ipo tayari kuwakopesha Watanzania kwa sababu sisi tumechelewa. Mataifa yanayotuzunguka wanazalisha samaki

ambao sisi Tanzania hapa hatujawahi kuzalisha. Pamoja na kwamba sisi tuna eneo kubwa sana la ziwa kuliko wao, lakini wao wanazalisha samaki wengi na wanasambaza duniani kote, sisi hapa Tanzania hatujawahi kuwazalisha hao Samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumesemaje? Tumesema nasi lazima tuanze kuvua samaki, tuanze kufuga samaki kisasa ili kuendana na dunia ilipofika. Kwa hiyo, mnaruhusiwa ndugu Watanzania wote, milango iko wazi kuomba vizimba. Siku hizi dunia imehamia kwenye vizimba na ukifuga kwa vizimba utapata tija inayoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na kwamba mambo yalikuwa ni mengi sana yaliyoelezwa hapa, nasi Serikali tumesema tumeyapokea yote, kwa kweli tupo tayari kuyatekeleza na kuyafanyia kazi kadri Waheshimiwa Wabunge walivyokuwa wameelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, ambaye ni mtoa hoja namba moja. Wakati huo mtoa hoja namba mbili ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru, nianze kwa kupongeza Kamati yetu ya Kudumu ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Nampongeza Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Nyongo pamoja na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanafanya ya kuendelea kutushauri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, tunawashukuru na tunaanza kwa kuunga mkono hoja mambo ambayo yameletwa mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ilianza kwa kuipongeza Serikali, nasi tunapokea pongezi hizo, kwenye tisini na

tano tatu (95, 95, 95), kwenye mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI, Tanzania tumepiga hatua na niwape taarifa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba kwa upande wa nchi za *SADC,* Tanzania tupo kati ya nchi tano ambazo zinafanya vizuri kwenye mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI. Taarifa hii tumetajwa na *UNAIDS* kupitia *UNAIDS Global Updates* ambayo inatoka kila mwaka. Kwa hiyo, hii ni taarifa ya mwaka jana 2023. Nchi hizo ambazo tunaungana nazo kwenye mapambano ambayo tunafanya vizuri ni nchi ya Botswana, Eswatini, Rwanda, Zimbabwe pamoja na sisi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio makubwa ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nami niwaambie Watanzania na wana-CCM, tuko vizuri kwenye utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Ilani yetu ya CCM Ibara ya 88(a) – (i) kilitupa maelekezo mahususi Serikali kufanya kazi katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, kwenye hizi tisini na tano tatu, 95 ya kwanza, kupima na kujua hali; Tanzania tuko 82.7%. Hapa niseme kidogo kwenye kupima na kujua hali, wanawake wenzangu na mimi mwenyewe tunaongoza kwa kufanya vizuri kwenye eneo hili, kwamba tunapima vizuri, lakini akinababa (wanaume) nataka nitumie fursa hii kuendelea kuwahamasisha mpime mjue afya zenu. Wanaume wote kwa pamoja muungane mpime ili twende vizuri kwenye malengo haya tunapojitathmini mwaka kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 95 ya pili, waliopima na kuanza dawa; hapa ndiyo tupo 97.9% tumevuka lengo.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ummy, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tarimba Abbas.

**TAARIFA**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa mchango mzuri sana, lakini

kuwataka tu wanaume peke yao wapime, sidhani kama ni sawa. Tupime sote wanaume na wanawake na tuko tayari sisi wanaume. Je, wanawake mpo tayari? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, taarifa hiyo unaipokea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea kuelimisha kwamba twende tukapime. Kwa hiyo, naipokea taarifa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 95 ya tatu, waliofubaza; asilimia 94.3 ya Watanzania wamefubaza. Nataka kusema nini? Nataka kusema kwamba, kwenye mapambano haya dhidi ya virusi vya UKIMWI, sote lazima tuendelee kuungana na kushirikiana kuhakikisha kwamba tunakuwa mstari wa mbele. Jambo hili siyo la Serikali peke yake ni la kila Mtanzania. Kwa hiyo, tuendelee kuungana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetajwa hoja mbalimbali hapa hasa eneo la kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya mapambano dhidi ya virusi vya UKIMWI. Tumepokea maoni na ushauri wa Kamati. Ndani ya Serikali tayari tulishaanza mazungumzo na tutaendelea. Lazima niliambie Bunge lako Tukufu ili lisije likachukuliwa kama pengine hamna kinachofanyika, lakini Serikali tayari bajeti iliyopita na hii tuliyonayo sasa, tuna fedha zaidi ya kiasi cha shilingi 1,880,000,000 kwa ajili ya mapambano. Pia, tutaendelea kuongeza kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, tunalipokea kwa uzito Mwenyekiti wetu wa Kamati, jambo hili tutaenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, tunapataje hela ambazo ni *sustainable*? Tunawezaje? Kwa mfano, ikitokea leo wadau wamejitoa, tunafanya nini? Tumeanzisha *Sustainability Working Group* ya Tanzania ambayo itaendelea kutushauri na tunapokea mwongozo kutoka *UNAID* kuona namna ambavyo tutaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine tumechukua kufanya mapitio ya Sera ya UKIMWI. Tunaendelea kufanya tafiti kuona namna nzuri ya kufanya kwa kushirikiana na wenzetu wa upande wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni eneo la Vituo vya Maarifa. Hivi wanatumia madereva wetu wa masafa marefu. Tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI kuona namna ambavyo vituo hivi vinafanya kazi ile ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, tunaendelea kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa utayari wake, utashi wake na namna ambavyo anasaidia katika eneo hili. Pia nawapongeze sana na kuwashukuru wenzetu wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS),* kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zote na ushauri wa Kamati yetu tumeuchukua, tutaufanyia kazi, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkonio hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, ahitimishe hoja yake.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kukushukuru wewe, kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Uongozi wote wa Bunge kwa kutupatia nafasi sisi Wajumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kuweza kuwasilisha wasilisho letu. Vilevile nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mbalimbali waliyoitoa katika kuchangia Taarifa yetu hii ya Kamati ya Afya na Mausala ya UKIMWI. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango imetolewa mingi, lakini kwa sababu leo zilikuwa ni Kamati mbili zenye majukumu makubwa na mazito, Waheshimiwa Wabunge waliotoa maoni yao katika taarifa yetu ni watano, Waziri mmoja na Naibu Waziri mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunashukuru na tunaendelea kusisitiza, kwanza kabisa, tunaipongeza sana Serikali, tunampongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa anaoufanya katika Sekta ya Afya. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, Mama amefanya kazi kubwa sana katika Sekta ya Afya. Tumeona uwekezaji mkubwa uliofanyika katika Sekta ya Afya kwa ngazi ya msingi, kwa maana ya zahanati, vituo cha afya, Hospitali za Wilaya, tumeona uwekezaji mkubwa katika huduma za kati, Hospitali za Mkoa, Hospitali za Rufaa na vilevile katika hospitali za kibingwa na ubingwa bobezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jinsi alivyoweza kununua vifaa mbalimbali vya vipimo na sasa hivi utaona Majimbo mengi, Waheshimiwa Wabunge wamegawa magari ya kubebea wagonjwa *(ambulance)*. Hizi zote ni juhudi za Mheshimiwa Rais wetu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wamechangia na kwa kweli nashukuru wengi wamechangia na wamekubaliana na taarifa yetu ya Kamati hasa pale kwenye maazimio yetu ambayo tumeyatoa. Moja, ikiwa ni kutoa azimio la kuiomba Serikali kuendelea kutoa fedha za miradi ya maendeleo. Fedha zilizotoka mpaka sasa hivi ni 26% tu. Kwa hiyo, tunaona kwamba kidogo kwa mwaka huu kumekuwa na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha. Wasiwasi wetu, ile miradi iliyopangwa inaweza ikachelewa kutekelezeka ama kukamilika. Ikichelewa kukamilika maana yake ni kwamba Watanzania ndio wanaokosa huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamwomba sana Waziri wa Fedha, nia ya mama ni kubwa ya kuwekeza, atoe fedha kwenye miradi ya afya ili kusudi miradi hii iwe endelevu na iweze kujengwa na kukamilika kwa wakati uliopangwa. Vilevile,

namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, tumetoa azimio hapa kuona namna ya Serikali kupunguza *gap* ya upungufu wa wagonjwa wa Sekta ya Afya. Tunashukuru kwamba Serikali imetoa ajira, lakini tuna karibu 50% ya upungufu wa watumishi wa afya. Hawa watumishi wapo, wasomi wapo, Watoto wa Kitanzania wapo na wapo ambao wanajitolea. Tumesema wale wanaojitolea kwenye vituo vya afya wapewe kipaumbele kwa sababu wamekuwa ni wazalendo, wamejitoa na wanajitolea kufanya kazi za kutoa huduma kwa wananchi bila ajira. Tunaomba sana wanapokwenda ku-*recruit* kwa maana kuchukua vijana kuwaajiri, wale waliojitolea waangalie namna ya kuwapa kipaumbele waweze kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukosefu wa mtaji wa Bohari Kuu ya Madawa yaani shilingi bilioni 561, Mheshimiwa Waziri amesema na ametuahidi tusubiri Bunge la Bajeti linalofuata. Naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu, kwenye bajeti iliyopita tumepitisha kwamba *MSD* apewe mtaji. Leo tunapokwenda kwenye *budget execution* ni lazima wapewe kutokana na jinsi Bunge lilivyopitisha. Tukichelewa, atachelewa kufanya shughuli zake, atachelewa kununua dawa, tutarudi kwenye lile tatizo la Wabunge wanapokwenda kijijini wanakutana na tatizo la upungufu wa dawa, kwa sababu *MSD* anasubiri fedha kutoka kwenye vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali, hebu tunapopitisha bajeti katika Bunge letu Tukufu, mwendelee kutoa fedha kwa jinsi mlivyopanga. Tumekubaliana *MSD* apewe mtaji wa shilingi bilioni 561 ili afanye shughuli zake ambazo tumeiongezea ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa dawa. Hilo tumeomba kusisitia sana Bunge lako Tukufu tupitishe maamuzi haya ili Serikali ikatekeleze jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwekezaji mdogo wa viwanda vya dawa na vifaatiba nchini, wajasiriamali wanataka kuona usalama wa uwekezaji wao. Ili mtu aweze kuwekeza popote, anataka kuona ni jinsi gani atakapowekeza ataweza kupata faida. Tunaomba sana Serikali iweke kipaumbele katika uwekezaji wa viwanda vya vifaatiba na madawa, kwa sababu ukiwekeza huko utakuwa umemkomboa Mtanzania atakayekuwa

amepata ajira kwenye viwanda hivyo. Tutazalisha dawa kwa ajili ya mahitaji ya ndani ya nchi na tutaweza ku-*export* dawa hizi kwenda nje ya nchi, tutafanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho wanachokiongea Waheshimiwa Wabunge mambo ya *balance of trade,* mojawapo ya dawa ambazo tutazizalisha hapa nchini, mojawapo ya bidhaa ambazo tutaweza kutoa nje au ku-*export* na kuweza kupata fedha za nje ni kutengeneza madawa. *Geographical location* ya Tanzania inaruhusu kuwekeza kwenye *pharmaceutical industry* ili tuweze ku-*save purpose* ya kuwa na dawa zetu nchini na vilevile kupeleka dawa nchi jirani. Nchi yetu itakuwa imejiimarisha kiuchumi na wakati huo tutakuwa na uhakika wa kuwa na dawa zetu wenyewe. Naomba sana Serikali itekeleze hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la udhibiti wa chakula na vipodozi *(TMDA);* suala la *TMDA* kupewa jukumu la kusimamia dawa na vipodozi ni jambo la msingi. Ukimpa *TBS* anachoangalia ni *standard;* atakachotazama, ukisema kwamba chupa hii ya maji ina nusu lita, ataangalia ina nusu lita kweli? Ina uzito wa gramu kadhaa, ni kweli? Maji yanatakiwa yawe hivi, ni kweli? Ile *component* iliyomo ndani kwamba kuna *fluorine* kiasi gani na ina usalama gani, mpe mwenye uwezo wa kuweza kufanya hizo *analysis*. Mwenye uwezo huo ni *TMDA* ambaye sasa hivi tunaita ni *Tanzania Food and Drug Authority (TFDA)*. Yeye ndiyo ana maabara, ana wataalamu na hata *components* nyingine zinazokuwa ni hatarishi katika afya ya binadamu, yeye ndiyo mwenye kuzitambua kwamba hiki ni hatarishi na hiki ni kitu salama. Tumpe mwenye jukumu hilo. Kama ni mapato, mwacheni *TBS* achukue, lakini usalama wa Watanzania kiafya, yule ndiyo msimamizi, tumpe kazi hiyo aifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la changamoto ya uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, tumetoa mapendekezo yetu, tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuyapitishe haya. Usalama wa Mfuko, tumemwambia Mheshimiwa Waziri kwenye vikao vyetu, boresha *actuarial study* katika *NHIF* ili waweze kutoa hesabu inayokubalika. Unapolipa *premium* ndogo kuliko matibabu, mfuko utakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima zifanyike hesabu za uhakika ikiwa ni pamoja na *public facilities* zinazopokea bima, wanapopokea na kuwatibu wateja wao, lakini bima hiyo hiyo inakwenda kwenye *private facilities*. Wale nao wanalalamika sisi *payroll* yetu tunalipa wenyewe! Kodi zipo 32 tunalipa wenyewe, maji na *utilities* zote tunalipa wenyewe, lakini mteja huyu akienda kwenye Hospitali ya Taifa, *payroll* ni ya Serikali, madaktari wanalipwa na Serikali, Hospitali za Serikali hazilipi kodi. Sasa hapa hakuna *fairness* kwa sababu hili shirika la *NHIF* lilianzishwa kwa ajili ya watumishi wa Serikali, lakini vilevile wakapate huduma kwenye *public facilities.* Ukienda na *package* hiyo hiyo kwenye *public facilities,* hawa watu hawawezi kutengeneza faida, na tutawaonea. Kwa hiyo, tunaomba sana warekebishe…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa samahani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 34(5) nitaongeza muda wa nusu saa ili tumalize kazi iliyoko mbele yetu. Mwenyekiti endelea.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba basi wakae warekebishe sheria. Wakae pamoja waje na *package* zinazoeleweka na bei elekezi zinazoeleweka na upangaji wa bei elekezi ushirikishe wataalamu wote wa *private* pamoja na *public sector* ili tuwe na *fairness* na Watanzania wawe wazi waweze kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kufutwa kwa Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC)*. Imetangazwa mashirika 16 yameunganishwa, mashirika manne yamevunjwa. Tafsiri ya kuvunja ni kwamba, umevunja lile shirika na makujumu yake labda yaende sehemu nyingine. Tumekubalina majukumu yaende sehemu nyingine, lakini Shirika hili lilipoanzishwa mwaka 1932 kabla hata hatujapata uhuru, nia ilikuwa ni kuangalia afya ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikwambie, leo chumvi inawekewa *iodine* na *TBS* anahakikisha kwamba chumvi imewekewa *iodine*. Kwa nini waliweka *iodine* kwenye chumvi? Waligundua Tanzania inakabiliwa na upungufu wa madinijoto na ndiyo maana watu wanapata ugonjwa wa *goiter*. Leo tunavyozungumza, tuna *zero rate* ya *goiter* kwa sababu tunaweka *iodine* kwenye chumvi. Aliyeamua kuweka *iodine* kwenye chumvi lilikuwa ni hili shirika au taasisi iliyofanya *research* na kujua kuna upungufu wa *iodine* kwa Watanzania. Leo tunaifuta, Mheshimiwa Profesa Kitila anakwambia haya majukumu tunayapeleka kwenye Halmashauri, tunakwenda kuua sekta ya lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa ni kinara namba moja wa kuhakikisha kwamba, lishe iwe bora, tujiepushe na utapiamlo, tujiepushe na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza. Ni nani atakayesimama na kufanya *research* ya kujua tuna *deficiency* ya madini fulani katika sekta ya lishe? Ni huyu *TFNC,* leo unamfuta eti kwa sababu, sio shirika la umma, eti kwa sababu haleti faida, unataka faida ya *iodine deficiency*? Faida? Ni usalama na uzima wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IQ* ya Watoto wa Kitanzania inakuwa *built* na *components* nyingi mtoto anapoumbwa akiwa tumboni. Zile *nutrients* anayejua ni hawa *TFNC,* leo mama anakwenda *clinic* anapewa *iron* pamoja na *folic acid* kama *supplement* kwa sababu, walijua kuna upungufu wa *iron* kwa mama mjamzito. Waliotoa maamuzi haya ni *TFNC,* leo tunakwenda kuifuta, majukumu tunakwenda kuya-*dilute* kuyaingiza kwenye Wizara na maeneo mengine, tutapunguza *concentration* ya suala la lishe. Naomba Bunge lako liridhie tusikubali hili kwa sababu, tunakwenda kuua nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala jingine la udhibiti wa dawa za asili, tumetoa pendekezo, zidhibitiwe, pawe na *accreditation*. Dawa za asili zinazouzwa mtaani nyingine zina *ingredients* ambazo zinaleta uhatarishi katika mwili wa binadamu. Nyingine zinagawanywa katika *high dose,* nyingine zinakuwa *under dose*. Kuna dawa nyingine ukizitoa katika *high dose* unaenda kuua figo. Sasahivi kuna *high rate* ya *dialysis,* ni kwa

sababu ya matumizi mabaya ya dawa za asili na dawa nyingine. Serikali lazima isimamie tiba ya dawa asili na hili linawezekana na sisi tunaomba leo Bunge lako Tukufu lipitishe azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru, kwenye Tume ya Kudhibiti UKIMWI, namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Ummy Nderiananga, amezungumza vizuri, wamefanya kazi vizuri, *95, 95, 95,* hongereni, hongera kwa Mheshimiwa Rais, lakini bajeti ya mwaka bilioni 1.8 halafu wafadhili wanaleta bilioni 10 mpaka bilioni 20 tunaonekana sisi *we are not serious with this.* Tunaomba Serikali itenge fedha dhidi ya mapambano ya ugongwa wa UKIMWI, ili kusudi tuendelee kuimarisha na kuondoa ugonjwa huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Sera ya UKIMWI ni ya tangu mwaka 2001 leo miaka 23. Umefika wakati Serikali iangalie upya Sera ya UKIMWI, ili iweze kuendana na hali ya sasa hivi. Miaka 23 ni mingi, kuna *achievements* nyingi hapa katikati zimefanyika na mambo mengi yamefanyika kwa hiyo, *strategies* za mapambano dhidi ya UKIMWI lazima na zenyewe ziwe *modified.* Kwa hiyo, twende tubadilishe sera, ili tuweze kuja na namna nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, kabla sijatoa hoja naomba nimalizie, samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpina alisema tunaongeza maazimio. Katika Azimio analotaka tuliongeze Mheshimiwa Mpina, naomba nilisome, anasema; baada ya maelezo mengi kuhusiana na operations za kuongeza makalio na matiti akasema, pia, anaomba kuongeza azimio kwenye Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Kwamba, Bunge liazimie kwamba, "Huduma ya kuongeza makalio na matiti zipigwe marufuku nchini na ufanyike uchunguzi wa kina kubaini kilicho nyuma ya pazia na kujua tumefikaje hapa na kwamba, wote waliohusika kuruhusu hospitali za umma kutoa huduma ya kuongeza makalio na matiti wachukuliwe hatua kali kwa mujibu wa sheria za nchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mpina naomba nimueleze, Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo mazuri, hizi huduma zinazotolewa ni huduma bobezi. Katika huduma bobezi kuna *component* mbili, kuna *reconstructive surgery* pamoja na *cosmetic surgery*. Daktari anayesoma *reconstructive surgery* anasoma na *cosmetic surgery* na hata uwekezaji alioufanya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ngazi zote ikiwemo ya ubingwa na ubingwa bobezi, pamoja na kusomesha wataalam wapo waliosomea mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wimbi kubwa la Watanzania wanaokwenda Uturuki na nchi nyingine, China na maeneo mengine, wanakwenda kufanya kazi hizi au hizi *cosmetic surgery* kwa maana ya kutengeneza maumbo, lakini wengine wanakwenda kufanya *reconstructive*. Mtu ana uzito mkubwa anakwenda kuwekewa kitu kinaitwa *intra gastric balloon* kupunguza uzito; hii sio *cosmetic,* hii ni *reconstructive* kwa sababu, mtu akipunguza uzito anajiondoa katika hatari ya kupata magonjwa, sasa hizi *procedure* zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya kuongeza matiti na matako nadhani imekuwa ni maarufu, lakini naomba nikutaarifu pamoja na huyu Dkt. wa Mloganzila aliyetangaza kwamba, anawakaribisha wananchi waende wakafanye hizi *procedure* mpaka leo hajajitokeza hata mmoja na hata akijitokeza kama amekuja dola zake, kuna tatizo gani akifanyiwa kwa hela zake? Kwa sababu, hafanyiwi kwa kadi ya *NHIF,* amekuja na dola zake, badala ya kuzipeleka uturuki kwa nini asifanyiwe hapa na ikawa ni moja ya *source of income? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nadhani kwa sababu hizi *procedure* zinakuwa zinasimamiwa na *WHO* na zimekubalika duniani, niombe hili azimio tusiliingize katika maazimio yetu labda tuendelee kulifanyia kazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na baada ya kusema hayo, naomba sasa Kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI na kukubali maoni na mapendekezo yote kama yalivyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Toa Hoja.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA AFYA NA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hoja imeungwa mkono, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge wote mmeafiki, nichukue nafasi hii nikupongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Afya na UKIMWI kwa kazi nzuri, Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia tunawapongeza sana, hongereni sana.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo aje ahitimishe Hoja yake.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyowekwa Mezani leo asubuhi. Hoja hii imepata wachangiaji wa kuzungumza 18 wakiwemo Manaibu Waziri wawili. Naamini pia, kutakuwa na wachangiaji kwa njia ya maandishi na Mheshimiwa Mpina akiwa ni mmojawapo ambaye ameshawasilisha kwetu, baadhi ya maeneo ambayo wachangiaji wengi wamegusia, sitayasema yote, lakini machache nitayagusia:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wameongelea sana suala la uhaba wa sukari na upandaji wa bei, jambo hilo na kamati yenyewe ililiona na nitaliongelea, lakini vilevile wachangiaji wengi wameongelea kuhusu kilimo kuwa chanzo cha fedha za kigeni, ili kusaidia uchumi shindani na kilimo biashara. Wachangiaji wameongelea *concern* yao kubwa kuhusu tozo ambazo zimezidi au zimekithiri katika sekta mbalimbali na hasa sekta ya mifugo na uvuvi na vilevile katika muktadha wa ufungaji wa Ziwa Tanganyika kwamba, tozo zinaangaliwaje na gharama ambazo wananchi wameshaziingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbegu limeongelewa kwa kirefu sana. Umuhimu wa mbegu bora katika kuongeza tija, ili kukifanya kilimo chetu kiweze kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kulikuwa na suala la umuhimu wa Serikali kutoa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali, hasa miradi ya umwagiliaji, kutoa fedha hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengine walikwenda mbali na kusema labda sekta hii inahitaji kupewa fedha zaidi, katika sekta ya uvuvi na mifugo wachangiaji walio wengi walionesha umuhimu wa sekta hii kupewa mamlaka mahususi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, inaongeza mchango katika uchumi wa Taifa na inakuwa na udhibiti mzuri wa masuala yote yanayohusiana hasa na uvuvi ambao sio endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji hao wengi vilevile walimpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuiangalia sekta ya kilimo kwa namna tofauti na kuendelea kuipa bajeti kubwa ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo sekta ya kilimo ilisemekana kwamba, ni sekta ya muhimu katika uchumi wa nchi, lakini bado kwenye upande wa bajeti haikupata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu ninawashukuru sana wachangiaji wote waliojitokeza, kwani kwa kiasi kikubwa wamefafanua na kuifanya hoja ya kamati ieleweke vizuri Na hasa namshukuru kwa namna ya pekee Naibu Waziri wa

Kilimo, Mheshimiwa Silinde, kwa ufafafuzi wake katika hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, ambao nadhani kwa kiasi kikubwa imeondoa hofu waliyokuwanayo baadhi ya Wabunge na imejenga taswira ambayo kamati ilielezea katika Taarifa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Pastory Mnyeti, ambaye naye kwa nafasi yake ameweza kuongelea na kutolea maelezo hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge ambazo zilijitokeza kwenye sekta ya kilimo na sekta ya uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimisha hoja hii ningependa kuweka msisitizo kwenye mapendekezo ambayo kamati imeyatoa, ili hatimaye Bunge lako Tukufu liweze kuyaazimia na Serikali ikayatekeleze kwa manufaa ya Taifa letu na ustawi wa wananchi kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapendekezo 15 katika ripoti ambayo tulii-*table* hapa asubuhi, na mimi sitayaongelea yote, lakini nitayaongelea yale machache ambayo kwa kiasi kikubwa yameongelewa na Wabunge na wachangiaji walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa sukari nchini, ni kweli Waziri wa Kilimo alisimama Bungeni hapa na kutueleza Watanzania kwamba, kwa mara ya kwanza kuna mategemeo makubwa katika kipindi hiki cha fedha, nchi yetu itakuwa na ziada ya sukari au itakuwa na sukari itakayokidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uhalisia tumeona kwamba, sukari imekuwa na upungufu na kwa kiasi kikubwa taarifa ambazo tumezipata ni kwamba, imetokana na hali ya hewa na miundombinu ambayo iliharibiwa kwa kiasi kikubwa. Sisi kama kamati tulilichukua jambo hili kwa umuhimu mkubwa sana na tuliona ni vizuri tukafanya ziara ya kutembelea viwanda mbalimbali ambavyo vinazalisha sukari, ili tuweze kujionea sisi wenyewe kwamba, tatizo hasa lilikuwa ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nipende kukubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, ni kweli tulikuta hali ya

miundombinu katika viwanda vya sukari ilikuwa ni mbaya sana. Nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania ambao tuliwakuta katika viwanda vile ambao walituonesha jitihada walizofanya katika kujaribu kuendelea na uzalishaji au ukataji wa mazao ya miwa kutoka mashambani katika mazingira magumu mpaka pale ambapo ilionekana kwa kweli baadhi ya mashine, mitambo na magari hayakuweza kupita katika maeneo ambayo yalikuwa na maji mengi na mengine yalianguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuondoa tatizo hilo na tunaipongeza. Tunajua Serikali kitu cha kwanza iliagiza sukari ili kuweza kuondoa nakisi hiyo. Sukari hiyo, tunashukuru kwamba, tunaambiwa kwamba, sasa imeshapakuliwa na imeshaanza kusambazwa na kwa hiyo, kuna uwezekano mkubwa kwamba, bei ya sukari katika maeneo mengi ambayo bei ilikuwa mbaya imeanza kushuka polepole, inawezekana maeneo mengine bado hayajafikiwa na hiyo sukari kwa sababu, bado tunahitaji tani za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu Serikali vilevile ilichukua maamuzi ya kutoa bei elekezi. Sisi kama Kamati tuseme tu, maamuzi ya kutoa bei elekezi katika mazingira ambayo kuna uhaba wa sukari ni kwamba, hayawezi kuwa na tija na tumehakikisha na kushuhudia kwamba, bei elekezi imetolewa, lakini sukari imeendelea kuwa juu na sukari imeendelea sasa kuuzwa kwa kificho kwa kuhofia bei elekezi. Ni kwa sababu hiyo, sasa Kamati yetu kwa kuliona hilo iliona ni vizuri Serikali ikachukua hatua mahususi za kuhakikisha kwamba, inajipanga, ili kuhakikisha kwamba siku za mbele; moja, viwanda vyetu vinakuwa na miundombinu thabiti na vinaweza kufanya uzalishaji na pale ambapo itaonekana kwamba, pengine hali ya hewa inaweza kutishia *supply* ya sukari kwa walaji Serikali ichukue hatua za haraka za kuhakikisha kwamba, inaondoa *gape* hilo kwa kuagiza sukari kwa wakati na kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa malighafi za uzalishaji mafuta ya kula, tumesikia hapa na tunaendelea kutambua kwamba, sasa tuna nakisi ya mafuta ya kula kiasi cha tani 365,000 katika nchi yetu. Katika mazingira kama hayo tulitegemea bei zingekuwa zimepanda, tunamshukuru Mungu

kwamba, Serikali kwa jambo hili ilifanya kazi kwa haraka ikaagiza mafuta kutoka nje, ili kuondoa nakisi. Kwa hiyo, pamoja na uhaba na nakisi ya mafuta, lakini wananchi bado hawakupata zile athari ambazo walizipata kwenye sukari. Kwa hiyo, tunadhani kwamba, ni vizuri sasa Serikali ikachukua hatua mahususi za kuhakikisha kwamba, jambo hili siku za mbele linashugulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika maazimio yetu tumeiomba sana Serikali iendelee kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji wa mashamba, hasa ya mbegu ya *ASA,* ili upatikanaji wa alizeti uweze kuwa wa uhakika na viwanda vyetu viweze kuwa na malighafi ya kutosha. Hilo, liendane vilevile na kuongeza ruzuku katika mbegu kwa wakulima hata wale wa kawaida lakini la muhimu zaidi Serikali ihakikishe kwamba, inaihamasisha sekta binafsi kuendelea kuwekeza katika uzalishaji wa mashamba, kwanza na hata katika uzalishaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA),* katika uzalishaji wa mbegu. Ni wazi kwamba, mbegu ndio msingi mkubwa wa kuongeza tija kwenye kilimo kwa hiyo, kwanza tunaipongeza Serikali kwamba, imeweza kuchukua hatua mahususi kusaidia *ASA* na vilevile kuongeza vitendeakazi kwa Maafisa Ugani. Tunajua kuna pikipiki karibu 5,889 ambazo zilitolewa kwa Mikoa 26, ilitoa vipima udongo 143, imetoa mafunzo kwa Maafisa Ugani, imetoa mpaka vishikwambi kwa Maafisa Ugani kwenye Halmashauri karibu 166, vishikwambi 805.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi hatua zote ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba, *ASA* na uzalishaji wa mbegu unatiliwa mkazo na kwa kweli, ndio maana katika maazimio yetu tumeitaka Serikali ihakikishe kwamba, vilevile ili iweze kuwa na uendelevu kwenye suala la mbegu iweke mikakati ya kushirikisha sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu, lakini vilevile iwezeshe wakala wa mbegu ipasavyo na kuzifikisha kwa wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa mbolea nchini, hili limekuwa ni tatizo na tuanze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kuendelea kutoa mbolea ya ruzuku kwa wananchi wa Tanzania. Jambo hili limekuwa ni ahueni na nafuu

kubwa sana kwa wakulima wetu, lakini ukweli unabakia kwamba, bado uzalishaji wa mbolea katika nchi yetu haukidhi mahitaji. Tuna mahitaji ya karibu tani milioni moja za mbolea kwa mwaka na viwanda vyetu hapa nchini uwezo wake ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwa mwaka 2023/2024 viwanda vya ndani vilizalisha tani elfu 60 peke yake na karibu tani 411,000 ziliagizwa kutoka nje wakati tani 326,000 zilikuwa ni *carry over* kutoka mwaka uliopita kwa hiyo, utaona wazi kabisa kwamba, kuna tatizo kubwa sana katika mbolea. Tumeitaka Serikali katika maazimio yetu iweke mikakati ya kuanzishwa viwanda vya mbolea nchini pamoja na kuboresha uzalishaji katika viwanda vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi inapata uwekezaji katika maeneo ya gesi na tunaanza kupata gesi, Serikali ione hii kama ni chachu ya kusisimua viwanda katika eneo la mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchango mdogo wa tasnia ya umwagiliaji katika sekta ya kilimo, wachangiaji wengi wameliongea hili. Tupende kusema, pamoja na shukrani tunazotoa kwa Serikali na kwa Mheshimiwa Rais kuhusiana na fedha nyingi zilizokwenda katika umwagiliaji, bado tuna tatizo kubwa la fedha kufika katika miradi ya umwagiliaji kwa wakati. Jambo hili limekuwa ni changamoto kubwa, lakini sio hilo tu hata wataalamu katika eneo la sekta hii ndogo ya umwagiliaji imekuwa ni tatizo. Kwa hiyo, kamati yetu imeitaka Serikali ihakikishe inafikisha fedha hizi kwenye maeneo ya miradi ya umwagiliaji kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tija ndogo ya ufanisi usiokidhi wa Kampuni ya Mbolea, Kampuni ya Mbolea Tanzania ndio ina jukumu la usambazaji, na hasa kama kungekuwa hakuna mbolea ya ruzuku, kampuni hii iliundwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kunakuwa na utulivu wa bei katika mbolea, lakini kampuni hii imekuwa na changamoto nyingi na changamoto kubwa zimekuwa za kiuendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama kamati tumeliona hili na tunasema ingekuwa ni vema kwa vile shughuli ya mbolea

inafanywa na sekta binafsi na Serikali kwa kupitia kampuni hii ya mbegu, ingekuwa ni vizuri basi Serikali ingeangalia uwezekano wa kufanya mapitio ya taratibu za ununuzi wa umma, ili kuona namna ya kuruhusu *TFC* kumudu mazingira ya ushindani katika soko la mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema *TFC* ni lazima ipatiwe zana na vitendeakazi kwa ajili ya uendeshaji ikiwemo usambazaji wa mbolea. Tunaiomba Serikali iendelee kuzingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ambao wameutoa ndani ya Bunge lako na leo baadhi ya Wabunge wameutoa wa kuona kwamba, vifungashio vya ujazo wa mbolea viwe katika ujazo tofauti, ili kuwasaidia wananchi wetu wakulima ambao ndio wengi na wengine hawawezi kuchukua mbolea katika ujazo mkubwa.

Kuhusu changamoto ya uvuvi na ufugaji wa samaki, sekta hii wote tumesikia wachangiaji wengi wamesema. Sekta hii inaendelea kuwa na changamoto kubwa sana ya kutokuwa na tija katika utekelezaji wake, vilevile tumeona kwa kiasi kikubwa sana malalamiko mengi yanayotokana na aidha, kwa sababu ya kukosa ufahamu wa watu walio wengi ambao wanajihusisha na sekta hii ambao ni wananchi wa kawaida, lakini sekta hii vilevile imekumbwa na tatizo kubwa sana la kuwa na tozo nyingi ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, tatizo jingine katika sekta hii ni nyenzo za kisasa za uvuvi ambazo tunazihitaji katika Bahari, mito, maziwa na maeneo mbalimbali. Tunaipongeza Serikali imeanza kutekeleza suala hilo la kuwasaidia wavuvi wetu wadogowadogo, ili waweze kufanya uvuvi ambao una tija, lakini tumeendelea kusisitiza utoaji wa elimu, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri ameliongelea kwa kina suala hilo, nadhani sitapenda kuendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sekta ambayo ingeweza kuwa na mchango mkubwa sana kwenye uchumi wetu, lakini kwa kiasi kikubwa sekta hii ina changamoto kubwa, sekta hii bado kwa kiasi kikubwa ina uzalishaji ambao hauna viwango ambao hauna viwango ambavyo kama nia ya Serikali ni kuwa na uchumi shindanishi na shirikishi ni wazi kwamba, sekta hii bado iko nyuma

sana. Kwa kiasi kikubwa tuna mifugo mingi, lakini suala la kuongeza thamani kwenye sekta ya mifugo bado liko nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyama tunayozalizalisha, pamoja na Mheshimiwa Rais kufungua masoko, pamoja na Wizara kufungua masoko, kufungua soko katika biashara ni jambo moja, lakini kuhakikisha tunabaki na soko ni jambo jingine. Kwa hiyo, tuna mazao ambayo hatuwezi kuongeza thamani kwenye viwango ambavyo tunaweza kushindanishwa Kimataifa, lakini hata katika eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika maazimio tuliyoyasema tumeitaka Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuiwezesha sekta hii kuchangia ipasavyo katika Pato la Taifa na kuwawezesha wafugaji kunufaika na rasilimali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni lile linalohusiana na vituo vya pamoja mipakani, tulipata nafasi ya kutembelea kituo cha mpakani kimoja na tulichojifunza ni kwamba, pamoja na Serikali kuwa na *scan machine* kwenye maeneo mengi, bado kulikuwa na vituo ambavyo vilikuwa hazina *scan machine*. Tunaongelea nia na kiu ya kuhakikisha tunakuwa na ukaguzi wa uhakika, madhubuti, katika mipaka yetu yote. Kwa hiyo, Kamati iliona kuwa kuna uwezekano mkubwa kukawa na upotevu wa mapato na kuna uwezekano kukawa na udhibiti ambao haukidhi haja ya kuhakikisha kwamba, tunapata mapato katika baadhi ya vituo na hatuzungumzii vituo vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana Kamati yetu kwa kuliona hilo, iliazimia na imelitaka Bunge lipitishe azimio la kuitaka Serikali kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya 2024/2025 ili kununua *scanner machine* za kusambaza katika vituo vya mipakani, na kituo hasa ambacho tulikiona kwamba, kina tatizo ni kituo cha Mpaka ule wa Mutukula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata vilevile mchango wa Mheshimiwa Mpina ambao umeandikwa katika kurasa 17, na kwa vile katika uchangiaji wake hakufikia kuongea au kuongelea sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi nimeona niuchukue kama

mchango na tuu-*treat* kama michango mingine ambayo tumeipokea kwa sababu, hatujapata muda wa kuutathmini na nilitegemea labda ametoa, ame-*suggest resolutions,* lakini ni maelezo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyaongea haya yote na kutoa maelezo mbalimbali na nikitathmini au ku-*appreciate* michango ya wachangiaji mbalimbali. Naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, pamoja na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono, sasa kwa mujibu wa kanuni zetu nitawahoji, wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Kilimo na Mifugo, Makamu Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri mliyofanya; lakini niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge mliopata nafasi ya kuchangia katika Kamati hii yetu. Pia, niipongeze Serikali kwa ufafanuzi mzuri mlioutoa kwenye hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati, na tuwaombe mchukue Maazimio haya ya Bunge na mkayafanyie kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo machache, basi niwatakie jioni njema na ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.05 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 13 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*